

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 13 Mei, 2019**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tono, leo ni Kikao cha Ishirini na Sita.

Katibu!

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:**

#### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2019/2010.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Viwanda na Biashara kwa kutuletea hiyo Randama mezani. Katibu!

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali, swali la kwanza litaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Kondoa Mjini, Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda.

Na. 210

**Posho za Vikao vya Madiwani Nchini**

**MHE. EDWIN M. SANNDA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu tumepigania kuboreshwa kwa maslahi ya Madiwani ikiwepo posho za vikao na Serikali imekuwa ikisitiza kuongeza mapato ili halmashauri ziweze kuwalipa Madiwani vizuri kadri ya uwezo, wito ambao umeitikiwa vizuri, mwezi Februari, 2019 tumepokea barua toka TAMISEMI ikielekeza Madiwani walipwe posho za vikao shilingi 40,000 na si vinginevyo.

Je, kwa nini Serikali isiache halmashauri kulipa posho kadri ya uwezo kama ambavyo msisitizo umekuwa toka awali?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda, Mbunge wa Kondoa Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imetoa ufanuzi kupitia barua Kumb. Na. CCB. 215/443/01 ya tarehe 02 Januari, 2019 juu ya ulipaji wa posho mbalimbali za Madiwani

ikiwemo posho za kuhudhuria vikao. Sheria ya Serikali za Mitaa Sura Namba 288 Kifungu cha 42 na Sura ya 287 Kifungu cha 70, inamtaka Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kuitisha viwango vya posho za Madiwani. Hivyo posho hizo zinapaswa kulipwa kwa kuzingatia miongozo na maelekezo ya Waziri mwenye dhamana wa Serikali za Mitaa. Maelekezo yanayotolewa yanasakiwa kuweka usawa wa viwango vya posho za Madiwani katika halmashauri zetu nchini, hivyo kuondoa malalamiko kutoka wa Waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na udhibiti wa mapato na itendelea kuongeza posho na maslahi ya Madiwani kulingana na kuimarika kwa uwezo wa halmashauri kwa kukusanya mapato yake ya ndani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sannda nilikuona, swalii la nyongeza.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na nashukuru kwa majibu ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza, kwanza fursa za vyanzo vya mapato na uwezekano wa kuongeza mapato inatofautiana baina ya halmashauri na halmashauri. Hili suala la malalamiko lina kosa msingi linabaki kuwa dhana.

Sasa je, Serikali huwezi kulinganisha kati ya Kondo au Geita au hata Dar es Salaam fursa za mapato zilizopo, na Madiwani ni sehemu ya wanaoweka nguvu ya kukusanya mapato na kuongeza mapato. Serikali haioni umuhimu wa kuwaruhusu walipe kadiri ya uwezo wa halmashauri zao ili pia iwe sehemu ya motisha? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, lini sasa maana tulipata Waraka wa kutuambia tulipe 40,000 na hapa tunazungumzia posho za vikao peke yake, lini sasa maslahi mengine tunaendelea kuruhusu kadiri ambavyo inafanya kazi. Lini sasa tutapata Waraka wa kufafanua ili ule Waraka uliotolewa mwezi Januari uweze kupitwa maana Serikali inafanya kazi kwa maandishi?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Waheshimiwa Madiwani wanafanya kazi kubwa sana ya kusimamia mapato, kwa kukusanya lakini pia na ndiyo maana fedha nyingi hapa tunapeleka halmashauri Waheshimiwa Madini kupitia vikao vyao na Kamati mbalimbali ndiyo wanapaswa kusimamia na kwa kweli tunawashukuru sana wamekuwa wakifanya hivyo. Majibu yangu ni kwamba ni kweli Mheshimiwa Waziri wa Nchi wakati anamalizia hoja yetu hii ya bajeti ya TAMISEMI, aliahidi mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba jambo hili linafanyiwa kazi na naomba niwaahidi kwamba, Waheshimiwa Wabunge wote na Waheshimiwa Madiwani popote walipo wavute subira ndani ya wiki hii Mheshimiwa Waziri atatoa maelekezo na jambo hili litafikia mwisho ambapo tunaamini kwamba utakuwa ni mwisho mwema, ahsante.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, suala linaloulizwa na Mheshimiwa Sannda na sisi pia watu wa halmashauri ya Masasi linatuletea shida. Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ilipanga kulipa posho Madiwani na stahiki zao nyingine kutokana na makusanya yaliyokuwa yanakusanya kutoka kwenye ushuru wa korosho ambaa Mheshimiwa Rais amesema hatapeleka tena. Sasa swali langu, ni je, Serikali haioni umuhimu wa kuwalipa Madiwani hawa posho moja kwa moja kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo moja Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza kwenye majibu yangu ya

msingi kwamba suala la posho za Madiwani, kwanza kimsingi yanatokana na mapato ya ndani na suala lingine ni uwezo wa halmashauri yenye we na Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo kwa Wilaya hizi ambazo zilikuwa zinakusanya mapato kupitia korosho wajipange kwa msimu mwagine wa korosho wafanye kazi vizuri ili waweze kupata mapato hayo. Sisi maelekezo yetu ni kwamba tutaoa maelekezo na halmashauri italipa Madiwani kulinga na uwezo wao wa ndani, ahsante.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa halmashauri ambazo zinalima korosho maamuzi yanayohusiana na ununuzi wa korosho ndiyo yaliyopelekea wao kupoteza mapato. Kuna halmashauri ambazo makusanyo yake sasa hivi ni 6% tu kwa sababu fedha zake zote walikuwa wanategemea korosho, Serikali haioni ni busara kufanya *compensation* ya fedha hizi ili halmashauri hizi ziweze kuendelea na shughuli zao kama kawaida ikiwemo kuwalipa Madiwani? (*Makof!*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la *compensation*, *compensation* yenye we siyo kwa korosho tu hata wengine wana....

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, nadhani jambo hili kila halmashauri inapanga mipango yao na kilichofanyika na Serikali ni kwamba ilikuwa ni lazima tuchukue hatua kuwawezesha watu wetu waweze kuuza korosho zao, lakini halmashauri zenyewe maelekezo ya Serikali ni kwamba kwa kuwa hiki kilikuwa ni kipindi cha mpito tunaamini kwamba msimu ujao watajipanga vizuri waweze kukusanya kwa kuzingatia Sheria na miongozo yao. Kwa sasa suala la *compensation* halitakuwepo kwa sababu hiyo bajeti hatuna, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, nawaona Waheshimiwa Wabunge swali hili ni gumu, tuokoe muda

tuende mahali pengine, ndiyo Waheshimiwa halmashauri nyingi sana mapato yake ya ndani si makubwa kihivyo. Hayo mapato yakishapatikana utoe asilimia 40 iende kwenye maendeleo, utoe asilimia 20 irudi kwenye vijiji, utoe asilimia 10 ya lishe tayari hapo sijui imeshakuwa asilimia ngapi, utoe *running* ya halmashari, huwezi ukawa na fedha ya kulipa Madiwani, *Never*, huwezi. Kwa hiyo, inatakiwa iangaliwe vizuri kabisa, hii posho ya Madiwani labda iwe *pledged* Serikali Kuu au la sivyo sijui nini kifanyike lakini ni *disaster*, ndiyo maana nikasema ni swali gumu. (*Makof*)

Mheshimiwa Khatib Said Haji wa Konde, Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Sijui ni namba ngapi.

**SPIKA:** Swali namba 211.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba swali langu namba tatu lipatiwe majibu. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Swali namba tatu halipo tunaendelea na swali lingine.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, namba 213 samahani, 211, samahani. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Khatib leo sijui ameamkia wapi leo, inaelekea ameamkia Mtera. (*Kicheko*)

Na. 211

### **Kuungeza Fedha za Mfuko wa Jimbo**

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Fedha za kuchochaea Maendeleo ya Jimbo (*CDCF*), zimekuwa msaada mkubwa katika kusaidia Maendeleo Majimboni.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza viwango vya fedha hizi ili kuleta ufanisi zaidi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge Konde kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Kuchochera Maendeleo ya Jimbo yaani *Constituency Development Catalyst Fund*, ulianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 16 ya Mwaka 2009 yaani *The Constituency Development Catalyst Fund Act, 2009*. Lengo la Mfuko ni kuhakikisha miradi ambayo ni vipaumbele vya wananchi katika Jimbo husika na ambayo haikupata fedha katika bajeti inapata fedha za utekelezaji. Kwa tafsiri ya Sheria iliyoanzisha Mfuko, fedha za Jimbo ni kwa ajili ya Majimbo ya uchaguzi ambayo yameanzishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia Ibara ya 75 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungao wa Tanzania. Vigezo vinavyotumika kugawa fedha ni ukubwa wa eneo, idadi ya watu na kiwango cha umasikini katika Jimbo husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiongeza fedha hizi kwa kadri ya upatikanaji wa fedha ambapo mwaka 2018/2019, Serikali iliongeza kiasi kinachotolewa kutoka shilingi bilioni 10 zilizokuwa zikitolewa kipindi cha nyuma mpaka shilingi bilioni 12.5 na Serikali itaendelea kuongeza kiwango cha fedha kinachotolewa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutumia fedha za Mfuko wa Jimbo umeainishwa katika Sheria ya Mfuko Kifungu Na. 10(1) kwamba kutakuwa na Kamati ya Mfuko wa Kuchochera Maendeleo ya Jimbo katika kila halmashauri ambayo Mwenyekiti wake ni Mbunge wa Jimbo husika. Miiongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati hii ni kuchambua miradi inayowasilishwa kutoka kwenye jamii na kuidhinisha miradi itayotekelze na jukumu la Mkurugenzi

Mtendaji ni kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Kamati hii. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khatib.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kuna baadhi ya halmashauri hufanya matumizi ya fedha hizi bila kumshirikisha Mheshimiwa Mbunge, na hayo yako hasa kwa upande wa Zanzibar. Je, Serikali inatoa kauli gani ili waache tabia hiyo mbaya na kujuu kama Mbunge ndiyo mhusika mkuu na msimamizi wa Mfuko huo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, sijui huku Bara lakini kwa upande wa Zanzibar Mheshimiwa Mbunge baada ya kupitisha matumizi ya fedha hizi, halmashauri inakuwa haimshirikishi katika suala lolote tena. Je, mamlaka ya Mbunge katika kusimamia fedha zile kwa upande wa Zanzibar ni ya halmashauri au ni Mbunge anahuksika mwanzo hadi mwisho? Ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, anataka kujuu kama fedha hii inaweza ikatumika bila Mbunge kuhusika. Kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu langu la msingi ni kwamba Mwenyekiti wa fedha hii ya Mfuko wa Jimbo ni Mbunge mwenyewe na wametajwa vizuri wajumbe wa Mfuko wa Jimbo, Madiwani wawili kwa kuzingatia jinsia, Watendaji wawili wa Kata au Viti Maalum lakini na mtu mmoja ambaye anakuwa ni kutokana na *NG’O* katika Jimbo husika, halafu anaongeza na Katibu wa Mfuko huu anakuwa ni Mchumi katika halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama kuna fedha inataka kutumika, kwa vyovyote vile hata kama Mbunge hatakuwa Jimboni ni lazima Mkurugenzi wa halmashauri hiyo afanye *consultation* na Mbunge wa Jimbo kama Mwenyekiti na kama hatakuwepo maana yake Mbunge ataridhia labda

Diwani miongoni mwa wale Madiwani kwa sababu shughuli haziwezi kusimama ili aweze kufanya kazi hiyo. Miradi inapopitishwa Mkurugenzi kazi yake ni kwenda kupitisha fedha ikatumike na siyo kupanga kwamba ongeza, punguza hiyo hairuhusiwi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili linafanana na la kwanza, kama nilivyosema na naomba nirudie tumepata malalamiko kwa kweli karibu Wabunge wengi hapa wanalamika. Wakurugenzi wa halmashauri hawana maamuzi katika fedha hizi, hizi fedha zinaenda kwenye vikao na Wabunge ambaao ni Wenyeviti wenyewe wanajadili, na inawezekana Mbunge akaenda kwenye eneo A au Kijiji B akasikiliza kero za wananchi au Mwenyekiti wa Mtaa au Mheshimiwa Diwani au wananchi wa kawaida wakalalamika, Mbunge anaweza akasema napeleka shilingi laki tano hapa. Kwa hiyo Mkurugenzi hawezi kubadilisha haya maelekezo ya Mbunge kwa sababu ndiyo uwezo wake. Ndiyo maana inaitwa Fedha ya Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, kwa hiyo, wale Wakurugenzi ambaao wana tabia ya kutumia fedha bila Mbunge tunaomba majina yao tutawashuhulikia kwa sababu Sheria imetaja vizuri namna ambavyo wanapaswa kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumeelekeza, ukishapitisha fedha hizi kwenda kutumika ni lazima Kamati ya Mfuko wa Jimbo iende kufanya ziara ikakague hiyo miradi kama kweli ipo na kama imetekelizwa na anayetajwa pale ni Mbunge. Hii ni fedha ya Serikali, lazima isimamiwe vizuri na Sheria imeelekeza kwamba Mbunge inawezekana hana fedha mfukoni kutoa lakini kupitia Mfuko huu unaweza ukatamka neno kwa wananchi na roho za wananchi zikapona, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Wabunge mkumbuke neno moja tu, kuna Kamati ambayo wewe ni Mwenyekiti usije ukafikiri wewe Mbunge ndiyo Kamati. Ukaanza tu *dish out* na fedha unavyotaka, lazima Kamati ipitishe maana yake ni Sheria. Waziri wa Nchi nimekuona Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, makofi kwa majibu ya Serikali kutoka kwa Wabunge yanaashiria kwamba yako matatizo katika uendeshaji na matumizi na usimamizi wa Mfuko wa Jimbo ambao lengo lake mahsusni kuhakikisha kwamba Wabunge wanachochea shughuli za maendeleo katika Majimbo yao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali sisi mtuachie pia twende tukashauriane na Waziri mwenye dhamana ikiwezekana Serikali itoe waraka wa maelekezo tena kusudi kila halmashauri iweze kusimamia utekelezaji wa kisheria wa mfuko huo, lakini vilevile tuwaombe Waheshimiwa Wabunge kama Wenyeviti wa Mifuko hiyo, waone kwamba wana wajibu pia wa kuhakikisha kwamba matumizi ya fedha ya Mfuko wa Jimbo yanafanya kwa kuzingatia Sheria. (Makofi)

**SPIKA:** Hilo litasaidia sana, litasaidia sana ukitoa hiyo nanii. Mheshimiwa Neema William Mgaya, uliza swali lako tafadhali.

Na. 212

**Fedha za “*On call Allowance*” kwa Madaktari Hospitali za Wilaya**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italeta fedha za *on call allowance* kwa madaktari wanaofanya zamu hasa katika hospitali za Wilaya na vituo vyaya ambavyo mapato yake ni madogo kwani sasa ni zaidi ya miaka miwili fedha hiyo hajaletwa na Serikali?

**SPIKA:** Bado tuko TAMISEMI, majibu ya swali hilo Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Naibu Waziri TAMISEMI tafadhali. *On call allowance* ya madaktari.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hapo awali Serikali iliweka utaratibu wa kulipa fedha za *on call allowance* kuitia Hazina, ambapo halmashauri ziliwasilisha orodha za madaktari na wataalamu wote wanaostahili kulipwa fedha za *on call allowance*. Ofisi ya Rais TAMISEMI ambayo hupeleka madai hayo Wizara ya Fedha na Mpipango. Hata hivyo utaratibu huo ulipelekea baadhi ya wataalam wasiyo waaminifu kutoa taarifa ambazo siyo sahihi na hivyo kusababisha madeni makubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na hali ya kuwa na madeni makubwa yasiyo na uhalisia, halmashauri zilielekezwa utaratibu wa kuweka fedha za *on call allowance* kwenye mipango na bajeti zao ili kuweza kulipa stahiki hizi. Pamoja na kuweka fedha za *on call allowance* kwenye mipango na bajeti, ilibainika kuwa zipo halmashauri zenye uwezo mdogo wa kimapato hivyo maelekezo yaliyotolewa hospitali na vituo vya afya kutenga asilimia 15 kutoka kwenye mapato yatokanayo na uchangiaji wa huduma za afya kwa ajili ya kulipa motisha kwa wataalam ikiwa ni pamoja na *on call allowance*.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Neema Mgaya.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuweza kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha ya Serikali. Lakini Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba mmeelekeza ile asilimia 15 ya mapato kutoka kwenye hospitali na vituo vya afya ziende kulipa *on call allowance* kwa madaktari hawa, lakini bado kuna changamoto kwa sababu kuna halmashauri ambazo ni nyingi zina mapato madogo sana.

Sasa je, nyie kama Wizara mmejipangaje kuhakikisha kwamba zile halmashauri ambazo mapato yake ni madogo mtumie njia gani nyingine ambayo itakuwa muafaka ili kuweza kuhakikisha kwamba madaktari hawa wanapata stahiki zao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa bado kumekuwa na changamoto za kupandishwa vyeo kwa mfano kutoka *clinical officer* kwenda kuwa daktari lakini vile vile kutoka mkunga kwenda kuwa muuguzi na vile vile *promotion* zao bado tumeziona zikiwa zina suasua. Je, nyie kama Wizara mmejipanga vipi kuhakikisha kwamba mnatatua changamoto hii pia? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba uniruhusu kipekee nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Neema, amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Mkoa wa Njombe wanapata huduma nzuri ya afya. Binafsi ameonekana akichangia mifuko ya saruji lakini pia nikimuona amepeleka mashuka kwa ajili ya kusaidia wagonjwa wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, katika swali lake la kwanza anaongelea namna ambavyo uwezekano mdogo kwa baadhi ya halmashauri. Kwanza katika kuimarisha tumeajiri wahasibu zaidi ya 350 ambao katika vituo vya afya wameenda kusimamia na mapato yameongezeka. Hakika fedha hii ikiweza kusimamiwa vizuri hakuna uwezekano wa kwamba madaktari na wauguzi wanaweza wasilipwe *on call allowance*. Nilienda kituo cha afya Kisosora pale Tanga nimekuta katika fedha ambazo zinapatikana mpaka wanafanya na ukarabati katika vituo vya afya. Kwa hiyo, ni suala tu la kusimamia vizuri na hakika maeneo yote ambayo yanasihamiwa vizuri, fedha inatosha na hatujapata malalamiko hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili anaongelea suala zima la kuwapandisha vyeo. Hizi nafasi zinategemeana na ujuzi kwa hiyo si rahisi kwamba mtu atapanda bila kwenda kuongeza ujuzi na ni matarajio ya Mheshimiwa Mbunge kwamba asingependa akapandishwa cheo mtu ambaye hana ujuzi mahsusini na ndiyo maana zimekuwa zikitolewa fursa za wao kuijendeleza na pale anapojiendeleza na kuhitimu akirudi huwa anapandishwa cheo.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza. Mheshimiwa Ussi tafadhali.

Na. 213

**Viongozi wa Kimataifa Wanaotembelea Nchini  
Kutokufika Zanzibar**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Viongozi wa Kitaifa wanaofanya ziara Tanzania walikuwa wakifika Zanzibar na kuonana na Rais wa Zanzibar:-

(a) Je, kwa nini katika siku za karibuni viongozi hao wamekuwa wakiishia Tanzania Bara?

(b) Je, ni viongozi wangapi wa Kimataifa ikiwemo Marais ambao wamefanya ziara Tanzania katika kipindi cha 2016/2017 na nchi wanazotoka?

(c) Je, kati ya viongozi hao wangapi wamefika Zanzibar na wangapi hawakufika na kwa sababu gani?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa William Tate Olenesha, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza Mbunge wa Chumbuni lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida viongozi wa Kitaifa wanapokuja nchini wanakuwa na ratiba ya maeneo ambayo wameyaainisha kuyatembelea kulingana na muda waliopanga kuwepo nchini. Pamoja na hilo Wizara imekuwa ikiwashauri viongozi hao kuzuru maeneo m balimbali ya nchi hususan Zanzibar ili pamoja na mambo mengine kukutana na kufanya mazungumzo rasmi na viongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii vilivypo Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi Aprili, 2019 jumla ya viongozi 21 wa Kimataifa walitembelea Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Viongozi hawa walitoka katika nchi za Afrika Kusini, Burundi, Chad, Cuba, Ethopia, India, Jamhuri ya Democrasia Congo, Jamhuri ya Korea, Msumbuji, Morocco, Mauritius, Misri, Malawi, Rwanda, Uturuki, Uganda, Vietnam, Sudan Kusini, Sri Lanka, Switzerland, Zambia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, kati ya viongozi hao wa Kimataifa walitembelea Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tisa walifika Zanzibar na 12 kati yao hawakufika Zanzibar. Sababu zinazopelekea kutofika kwao ni kutokana na aina ya ziara, ratiba ya ziara husika na ufinyu wa muda katika ziara. Sababu nyingine ni vipaumbele na malengo ya ziara za viongozi hao pamoja na utashi wa kiongozi husika. Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeendelea kushauri viongozi wa Kitaifa kutoka nchi za kigeni wanaozuru nchini kutembelea Zanzibar katika ratiba zao. Aidha, Wizara kupitia Idara ya Mambo ya Nje Zanzibar imekuwa ikifanya maandalizi stahiki ya kiitifikasi ili kurahisisha viongozi hao kutembelea Zanzibar.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru sana kwa majibu hayo mazuri ya

Mheshimiwa Waziri lakini je, Serikali ya Muungano au Wizara hii ya Mambo ya Nje inazishauri zile nchi wakati zina mpango wa kuja kutembelea Tanzania kuziarifu kuwa nchi yetu ya Tanzania ina sehemu mbili za Muungano na kila sehemu ina mahitaji yake ya kiuchumi. Hivyo basi, Wizara ingekuwa inazishauri kwa sababu ukiangalia nchi tisa tu ambazo zimekuja Zanzibar naamini zingekuja na hizi nchi nyingine 12 kuna fursa nyingi ambazo ziko Zanzibar ambazo bara hakuna na kuna fursa ambazo ziko bara ambazo Zanzibar hakuna.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Wizara iweze kuzishawishi wakati nchi za nje zinapoweza ku-*engage* kuja Zanzibar kuja kutembelea Tanzania. Basi iziambie kuwa Tanzania ina nchi mbili na nchi hizo mbili kila upande una vipaumbele vyake vya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, swali la pilli ambalo nataka niliseme, Wizara inafanya jitihada gani kuwashawishi wale viongozi ambao hawakuja Zanzibar kutembelea wakati wa ziara zao lakini kufanya ushawishi wakutane na viongozi wa Zanzibar huku Tanzania Barai ili wale viongozi wa Zanzibar waweze kutoa haja zao na kuweza kutoa ushahwishi wao wa kuiona Zanzibar nayo inanufaika na ugeni ule. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Hivi Mheshimiwa Ussi ungependa kazi hiyo wewe, watu wametoka nchi za nje wanakuja halafu unaanza kuwaambia Tanzania ina nchi mbili, watakuelewa kweli? Wataelewaje? Haya matatizo yenu wenyewe bwana hayo! Wao wanakuja kwenye nchi moja inaitwa Tanzania wewe unaanza tena kusema Tanzania ina nchi mbili unamwambia mtu wa nje, majibu tafadhali. Tanzania ni nchi moja bwana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni nchi moja kwa mujibu wa Ibara ya 1 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Na masuala ya nje ni sualala Muungano kwa m ujibu wa Ibara ya 4 nyongeza ya kwanza ya Katiba. Kwa hiyo, uhusiano wetu na mambo ya nchi za nje unachukulia maanani suala la kwamba ni nchi moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mahusiano yetu mara nyingi tukwasiliana wanafahamu kwamba kuna nchi moja inaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na hayo, Serikali na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje imekuwa ikifanya jitihada kubwa sana kuhakikisha kwamba kwa sababu ya historia ya Muungano wetu na hali halisi kwamba ni Muungano ambao umetokana na nchi mbili tunahakikisha ya kwamba wakati viongozi hao wanapokuja nchini, tunajenga ushawishi mkubwa ili watembelee Zanzibar na ndiyo maana kuanzia 2015 mpaka sasa viongozi 21 walio tembelea nchini kwetu. Tisa kati yao wametembelea Zanzibar, vile vile ifahamike kwamba kuna wengine vile vile ambao wametembelea Zanzibar tu wala hawajatembelea upande mwingine wa Jamhuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kati ya masuala ambayo yanapewa kipaumbele sana katika uhusiano wa Kimataifa ni Muungano wetu ndiyo maana hata kwenye Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje kuna Idara maalum inahusika na mambo ya Zanzibar. Mualiko wowote au kiongozi ye yote akija ushawishi mkubwa unafanyika ili aweze kutembelea pande zote mbili za Muungano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa mara nyingi kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi mara nyingine linakuwa ni suala la utashi wa kiongozi mwenyewe na hauwezi kumlazimisha. Kwa hiyo, nimueleze tu kwanmba kwa kweli Serikali inajitahidi sana kuhakikisha kwamba viongozi hawa wanapata fursa ya kutembelea maeneo yote na hasa kujaribu vile vile kuelezea kuhusu fursa za kiuchumi na za kitalii zilizopo Zanzibar.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Ally Saleh, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nchi hizi zilipoungana tulikubaliana kwamba tutakuwa na Serikali mbili na tutakuwa na nchi mbili, Taifa ndiyo moja, Tanzania lakini nchi ziko mbili na hali hii ya viongozi wa nje

kwenda ina historia ndefu kwenda Zanzibar kama Abdul Nassor, Nelson Mandela, Fidel Castro, Indira Gandhi na wengine wengi wamekwenda.

Mheshimiwa Spika, lakini hivi karibuni miaka kama 10 nyuma ulizuka utata kwa sababu wanapigiwa mizinga na ikaja hoja kwanini wapigwe mizinga Dar es Salaam na kisha wapigwe mizinga Zanzibar.

Swali langu linakuja hapa, je, hamuoni kwamba kwa kutowaambia wageni wanaokuja hapa kwamba kuna Taifa moja na kuna nchi mbili kunaleta mzozo na kunaleta sintofahamu kubwa kwamba kunaonekana Zanzibar hawapewi hadhi ambayo inastahiki? (*Makofi!*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Saleh kabla hujakaa, tupe *reference* ya Katiba hilo unalolisema. Mahali gani kwenye Katiba imeandikwa Taifa moja nchi mbili.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba kutakuwa na Serikali mbili na Zanzibar ni nchi ndani ya Tanzania hata katika Katiba ya Warioba ilisema kwamba...

**SPIKA:** Nimesema tupe *reference* ya Katiba iliyoko sasa wapi maneno haya yanasesemwa, ili swalilako liwe swalil, vinginevyo sio swalil.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, hakuna mtu yeoyote aliambiwa atoe *reference* akiuliza swalil.

**MBUNGE FULANI:** Ally acha uchochezi huo bwana.

**SPIKA:** Hakuna swalil, huo ni uchochezi, tunaendelea! Huwezi kuzua mambo tu ya kichwani kwako ukafanya ndiyo sera za nchi. Wewe ni Mwanasheria bwana, tupe Katiba wapi inasema haya maneno, haya ni maneno ya mtaani haya.

Wizara ya Maji, swalil la Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande, Tanzania ni nchi moja, Taifa moja.

Na. 214

### **Mradi wa Maji Liwale**

**MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y MHE. LATHIFAH H. CHANDE)** aliuliza:-

Serikali iliahidi Mji wa Liwale Kufanyiwa usanifu wa mradi wa maji:-

(a) Je, ni lini mradi huo uliofanyiwa usanifu utakamilika na kuanza kutoa huduma ya maji kwa wananchi wa Liwale?

(b) Je, ni kata zipi zilizopo katika Wilaya ya Liwale ambazo zitanufaika na mradi huo wa maji?

### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa ruksa yako kwanza naomba nitoe pole kwa wananchi wa Pangani na Chama cha Mapinduzi na wanaCCM wote kwa kuondokewa na Mzee wetu ndugu Hamis Mnegerwa ambaye ni Mwenyekiti wa chama chetu Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Pangani. Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lathifah Chande, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Liwale ili kutatua changamoto hiyo, Serikali inatekeleza mipango ya muda mrefu na muda mfupi. Kwa upande wa muda mfupi katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imekamilisha mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji katika Mji wa Liwale.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelzewa katika mradi huo ni ukarabati wa kituo cha kusukuma maji, ununuzi na ufungaji wa pampu, ununuzi na ulazaji wa mabomba,

usambazaji maji umbali wa kilometra 16 pamoja na ununuzi wa dira za maji 200 kwa gharama ya shilingi milioni 264. Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka masaa matano kwa siku hadi masaa 12 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa muda mrefu, Serikali imepanga kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa vitabu vya zabuni ambazo kazi hiyo imepangwa kufanyaika mwaka wa fedha 2019/2020. Kukamilika kwa kazi hiyo kutatoa gharama halisi ya utekelezaji wa mradi mkubwa katika Mji wa Liwale pamoja na kuainisha kata zitakazonufaika na mradi huo.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka wakati Mheshimiwa Rais, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli analihutubia Bunge hili wakati wa ufunguzi wake alisema asingependa tena kusikia tena hili neno la upembuzi yakinifu likiendelea kutumika kwa sababu linaonesha ni ambalo limekuwa *liki-roll on* mambo yaani ni utaratibu tu wa kutaka kuchelewesha. Sasa tunafahamu Serikali ina mipango yake na hapa unasema *specifically* kwamba itafanyaika kwenye Mwaka wa Fedha 2019/2020. Sasa je, Serikali iko tayari kutueleza ni lini *specifically* mradi huu utaanza kufanyaika ili kuondoa kero ya watu wa Liwale? Swali langu la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, ni kwamba matatizo yaliyoko Liwale yanafanana kabisa na matatizo yaliyoko Jimbo la Ndanda hasa kwenye Kata ya Nanganga. Kata ya Nanganga kuna mradi ambaao ulikusudiwa upeleke maji kwenye vijiji vya Chinyanya, Nanganga A na B, Mkwera moja na Mbili pamoja na Mumburu 1 na 2 pamoja na vijiji vya Chipite. Mpaka sasa hivi tunaonge ahapa mradi ule ulitekelezwa chini ya kiwango na inasemekana kwamba mkandarasi amekimbia hajaukamilisha na hajaukabidhi kufanya *commissioning* kama ambavyo ilikusudiwa.

Sasa nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, yuko tayari kupeleka wataalam wake kutoka Makao Makuu ya Wizara ya Maji wakauchunguze mradi huu na kutoa majibu stahiki kwa wananchi wale?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge, moja; Wizara yetu ya Maji jukumu lake ni kuhakikisha Watanzania wanapata maji safi na salama lakini katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji katika Mji huu wa Liwale, kuna miradi ambayo inaendelea. Moja, mradi wa Kipure pamoja na Mangilikiti na Nanyungu yote ni katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji na hata katika bajeti hii yetu ya 2019/2020 tumetenga zaidi ya 699,000,000 katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji. Kubwa, Mhandisi wa Mkoa, wahandisi wa wilaya wahakikishe fedha hizi zinatumika kuweza kutatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu mradi ambao ameuelezea nataka nimhakikishuie, sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo kutuma wataalam kwenda kuukagua mradi huo na mimi kama Naibu Waziri niko tayari kuongozana na wewe katika kuhakikisha tunaenda kuchukua hatua nzitio. Ahsante.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Chatanda na Mheshimiwa Mbunge wa Liwale.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naomba kuuliza swali la nyongeza, Korogwe Mji tuna kijiji kinaitwa Mahenge, kiko nje kabisa ya Mji wa Korogwe na katika mpango wa miji 28, sina hakika kama kinawenza kikafikiwa na ule mradi wa maji.

Je, mtakuwa tayari kukipatia maji kijiji hicho kwa kuwapa kisima cha maji kirefu? (*Makof*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo ni majirani zako hawa natumaini unapafahamu Mahenge.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge anafanya kazi kubwa sana katika Jimbo lake wala haina haja ya kulalamika sana kwa sababu ukimuona mtu mzima ujue kuna jambo. Labda tuwaagize watu wa *DDCI* waende kuchimba kisima haraka pale ili wananchi wake waweze kupata maji safi na salama. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika mradi wa kutafuta chanzo cha pili cha mbadala cha maji ya Wilaya ya Liwale palitolewa shilingi milioni 300 na *DDCIA* walishaanza kufanya kazi hiyo lakini wamechimba visima viwili ambavyo vina uwezo wa kutoa maji lita 5,000 lakini visima vile vimetelekezwa mpaka leo.

Je, Serikali iko tayari kutoa fedha kwa ajili ya kwenda kufanya uendelezaji wa visima vile ambavyo viko katika Kijiji cha Makata na kijiji na Mikunya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Visima hivyo vya Makata na Mikunya.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza labda kwa nia njema kaisa katika kuhakikisha visima hivi vinakuwa endelevu labda baada ya saa saba nikutane na Mheshimiwa Mbunge na tuweze kufanya mawasiliano na wenzetu ili tangalie ni namna gani tunaweza tukasaidiana naye. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Kwa sababu ya muda Waheshimiwa Wabunge tuvumialne. Bado tupo Wizara ya Maji. Swali la Mheshimiwa Methusalah Mbunge wa Kilolo.

Na. 215

### **Ujenzi wa Mabwawa Kilolo**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO** aliuliza:-

Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani ya ujenzi wa mabwawa ya maji ili kupunguza matatizo ya maji katika Wilaya ya Kilolo.

### **NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Jimbo la Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Halmashauri ya Kilolo kwao aupande wa Vijiji ni asilimia 71. Kilolo Mjini ni asilimia 80 na Ilula ni asilimia 47.5. Aidha, halmashauri ya Wilaya ya Kilolo imekamilisha ujenzi wa miradi ya vijiji 10 kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji pamoja na Ujenzi wa vijiji vitano kupitia ufadhilli wa Taasisi isiyo ya Kiserikali ya WARIDI.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo inatekeleza miradi ya maji katika vijiji vitatu vya Lundamatwe, Kitelewasi na Ilambo. Pia miradi miwili katika miji midogo ya Kilolo na Ilula. Aidha, Halmashauri ya Kilolo kwa kutumia fedha za ndani inakarabati mabwawa matatu yaliyopo katika vijiji vya Uhambingeto, Image na Mgowelo kwa ajili ya binadamu na mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya uhaba wa maji kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Kilolo imepokea jumla ya shilingi bilioni 1.7 ili kuhakikisha miradi ya maji inatekelezwa na kukamilika na kuwapunguzia keri ya maji wananchi wa wilaya hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Kilolo nilikuona tafadhalii.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alifanya ziara katika Mji wa Ruaha Mbuyuni baada ya kuonekana kuna shida kubwa sana ya maji na kipindupindu kinatokea kila mara na akaahidi pale kwamba kichimbwe kisima kwa tahadhari ili wananchi waanze kupata maji. Lakini kwa masikitiko makubwa wale wataalam wamepuuzwa hakuna aliyefika pale. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atakubali tena kwenda kuona hali ilivyo na wananchi wanazidi kuteseka?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali kuna wahisani ambao huwa wanansaidia Serikali, kuna tatizo kubwa katika Kijiji cha Udekwu na Mlafu, tayari Serikali ya Italy, kuititia Shirika linaitwa WAMAKI liko tayari kusaidia, lakini linataka *commitment* ya Serikali, yenye we litasaidia kiasi gani, ili na wao waweze kusaidia fedha. Je, Serikali sasa itakuwa tayari kusaidia ili WAMAKI waweze kutoa maji safi na salama kwa kata mbili. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Jumaa Aweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kabisa nilifika Kilolo na nimeona kazi nzuri ambayo inafanywa na Mheshimiwa Mbunge Venance Mwamoto katika Jimbo lake. Lakini kikubwa tulifika kweli Ruaha Mbuyuni na tukaona changamoto ile na tukatoa agizo, watu wa Bonde walikwenda walishafanya tafiti ya upatikanaji wa maji. Labda nimuagize sasa Mhandisi wa Mkoa, ahakikishe kabisa kile kisima kinachimbwa ili wananchi wale waweze kupata maji na anipatie taarifa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu suala lake la pili, pamoja Serikali imekuwa ikitatua tatizo la maji, imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Serikali tupo

tayari kukaa nao, tuangalie ni namna gani tunaweza tukashirikiana katika kuhakikisha tunatatua changamoto hii. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana, tunahamia Fedha na Mipango, swali la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu.

Na. 216

### **Malengo ya Benki ya TPB**

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA** Aliuliza:-

Miongoni mwa malengo ya Benki ya *TPB* ni kupeleka huduma ya kibenki kwenye maeneo ya vijijini na pembezoni ambayo hayafikiwi na huduma hizo:-

Je, ni kwa kiasi gani lengo hilo limefikiwa mpaka kufikia mwaka 2018?

**SPIKA:** Ahsante sana Juma, majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa malengo ya Benki ya *TPB* ni kupeleka huduma za kibenki na pembezoni mwa miji, kuongeza wigo na mtadao wa biashara ya benki ya kutumia teknolojia ya kisasa.

Katika kutekeleza malengo haya, Benki ya *TPB* imefanikiwa kuboresha huduma za kibenki kuititia mtandao wa ofisi 200 za Shirika la Posta Tanzania zilizopo katika kila wilaya na baadhi ya tarafa na kutumia teknolojia ya habari

na mifumo ya kisasa kutoa huduma za kibenki ikiwemo simu za kiganjani (*TPB POPOTE*), mawakala wa kampuni za simu, mashine za *POS* pamoja na *ATM* katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Benki ya *TPB* imefanikiwa pia kuongeza idadi ya matawi makubwa kutoka 30 kwa mwaka 2017 hadi 36 mwaka 2018 na matawi madogo yaliyoongezeka kutoka 37 mwaka 2017 hadi kufikia 40 mwaka 2018. Idadi hii ya matawi inahusisha matawi ya iliyokuwa Benki ya Twiga na Benki ya Wanawake Tanzania. Matawi yote yameunganishwa kwenye mfumo wa *TEHAMA* unaowawezesha wateja kupata huduma za kibenki bila kutembelea matawi walipofungulia akaunti zao.

Mheshimiwa Spika, vituo vya huduma ndani ya Ofisi za Shirika la Posta viliiongezeka kutoa 40 mwaka 2017 hadi kufikia 45 mwaka 2018. Aidha mashine za *ATM* zilliongezeka kutoka 51 mwaka 2017 hadi kufikia 72 mwaka 2018. Vilevile, mawakala wa *SELCOM POS* waliongezeka kutoka 225 kwa mwaka 2017 na kufikia 670 Desemba, 2018. Vituo vyote vua huduma ndani ya Ofisi za Shirika la Posta vimeunganishwa pia kwenye mtandao na mfumo wa *TEHAMA* wa benki na hivyo kutoa fursa kwa wateja wa vijiji na pembezoni mwa miji kupata huduma kwa wakati kama ilivyo kwa wateja wengine wanaohudumiwa na matawi makubwa na madogo.

Mheshimiwa Spika, jumla ya akaunti 227,052 zilifunguliwa na wananchi wa vijiji na pembezoni mwa miji kwa kutumia mfumo wa kutoa huduma za kibenki kwa njia ya simu za kiganjani, ujulikanao kama *TPB POPOTE*. Mfumo huu wa *TPB POPOTE* unasaidia wananchi kufanya malipo mbalimbali kama kuhamisha salio, kutuma fedha, kulipa ankala za maji, kununua umeme wa luku na kununua vocha za simu bila kulazimika kwenda katika matawi ya benki ya *TPB*. Wateja wanawea pia kuhamisha salio kwenda katika akaunti nyingine, kuhamisha fedha kwenda katika akaunti zao za *M-Pesa*, *Tigo Pesa*, *Airtel Money* na *Halopesa* na hatimaye kuchukua fedha kuititia mawakala.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Tumbatu nilikuona, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kutoshereza kabisa, lakini nina swali moja la nyongeza.

Majibu yake yamejikita sana kwenye maeneo ya miji, swali langu ni kwamba Serikali ina mpango gani, huduma hizi kuzipeleka katika visiwa vidogovidogo kama vile Tumbatu? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Benki ya Posta Tumbatu kule inafika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema huduma zetu za *TPB* zimeongezeka kwa kiwango kikubwa na tumeweza kuwafikia wananchi walio wengi na kwa visiwa vyetu kwa Zanzibar tumeshafungua matawi tayari na sasa tunajipanga kwenda kufungua katika visiwa hivi vidogo, wakati huo tukiendelea kuwashudumia kwa kupitia mfumo wa kidigitali.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata, bado tuko Wizara hiyohiyo, swali la Mheshimiwa Asha Abdullah.

Na. 217

#### **Kuwasaidia Waliokuwa Wateja wa FBME Bank**

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA (K.n.y. MHE. ASHA ABDULLAH JUMA)** aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kuwasadia wananchi walioweka amana zao katika Benki ya *FBME*.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo bado tuko Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji tafadhali.

## **NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge Vitib Maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 kifungu cha 39(2) na (3), amana au akiba za wateja katika benki au taasisi ya fedha, zina kinga ya bima ya amana ya kiasi kisichozidi shilingi za kitanzania 1,500,000 tu. Endapo mteja hana salio la amana la kiasi kilichozidi shilingi 1,500,000 atapata fidia ya asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, wateja walio na amana zaidi ya shilingi 1,500,000, wanalipwa shilingi 1,500,000 kama fidia ya bima ya amana, na kiasi kinachobakia kinalipwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za ufirisi. Aidha malipo kwa mujibu wa sheria na taratibu za ufirisi yanategemea makusanyo ya fedha kutoka kwenye mauzo ya mali pamoja na fedha zilizowekezwa na benki katika taasisi mbalimbali za fedha za ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kukusanya mali na fedha zilizokuwa zimewekezwa na za benki ya *FBME* katika taasisi mbalimbali za fedha, hususan nje ya nchi, limekumbwa na changamoto za kisheria kati ya Tanzania na nchi ya Cyprus ambako benki ya *FBME* ilikuwa na tawi lililokuwa linaendesha sehemu kubwa ya biashara zake, na hivyo kusababisha ucheleweshaji wa ukusanyaji na ugawaji wa fedha za ufilisi. Hivyo basi tarehe ya kuanza kulipa fedha zinazotokana na ufilisi haijulikani kwa sasa kutoptaka na uwepo wa kesi zinazokwamisha zoezi la ukusanyaji mali na madeni ya benki ya *FBME*. Serikali kupitia Bodi ya Bima ya Amana, Benki Kuu ya Tanzania pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ipo katika mazungumzo na Serikali ya Cyprus ili kulipatia suala hili ufumbuzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa muuliza swali Mheshimiwa Asha Jecha.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tatizo hili sio mara ya kwanza kutokea hapa nchini, je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi kuzuia jambo hili lisitokee tena kupunguza usumbufu kwa wananchi wetu? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Fedha na Mipango, Dkt. Ashatu Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, Serikali mikakati iliyanayo ni kusimamia sheria ya mabenki na taasisi za fedha ya mwaka 2006 kama inavyoelekeza kuhusu unazishwa na usimamiaji wa uanziswaji wa taasisi za kifedha ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, na Serikali mmeona kwa sasa imekuwa, imeweka udhibiti wa hali ya juu kuhakikisha taasisi zote za kifedha zinafanya kazi kulingana na sheria ili kuzuia changamoto hizi wanazozipata wateja wetu.

**SPIKA:** Ahsante sana, nilikuona Mheshimiwa Nape, swali la nyongeza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na majibu ya Serikali, kuna mkanganyiko mkubwa na mlolongo mrefu kwa watu hawa kupata haki zao.

Sasa kwa kuwa Benki Kuu ndiyo *guarantor* wa hizi benki, kwa nini Serikali isimalizane na hawa wateja kwa niaba ya hii benki halafu Serikali sasa ibaki ikishughulika na benki hii wakati wananchi wakiwa wanaendelea na shughuli zao, hasa ikizingatiwa kuwa ziko taarifa kwamba, wamiliki wa benki hii wametushitaki, wameishitaki Serikali kutokana na hatua walizochukua?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, benki inapofilisika, benki inaponyang'anywa leseni yake ya kufanya kazi, hatua zote za ulipaji wa wateja wa beki hiyo au taasisi hiyo ya kifedha, imetajwa katika sheria ya mabeki na taasisi za fedha kifungu cha 39(2) na (3), ambako kuna maeneo mawili.

Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao wana amana zilizo chini ya 1,500,000 hulipwa fedha zao zote, kwa wale ambao amana zao ni zaidi ya hiyo, hulipwa kwa kutumia sasa sheria ya ufilisi baada ya kujiridhisha na madeni na mali halisi ya benki hiyo au taasisi ya kifedha kama ilivyoelezwa.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niliambia Bunge lako Tukufu kwamba, siyo kwamba wamiliki wa benki ndiyo walioishitaki Serikali, hapana, wallostopisha mchakato huu ni *Central Bank ya Cyprus*, ambayo wao wanaona wana *mandate* ya kuweza kulipa wateja wote wa benki hii, wakisahau kwamba kulingana na sheria ya uanzishwaji wa mabenki, wanaotakiwa kulipa ni kule ambako benki hiyo ilikuwa na makao makuu, na makao makuu ya benki hii ya *FBME* yalikuwa Dar es Salaam lakini shughuli zake nyingi zilikuwa zinafanyika nchini Cyprus.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, mwezi wa nne tarehe 5 mwaka 2019, Serikali mbili zimekutana nchini Cyprus na tayari makubaliano yamefikiwa ya jinsi gani ya kuhakikisha wateja wote wa iliyokuwa benki ya *FBME Tanzania* na *FBME Cyprus* wanapata haki zao bila kupoteza chochote katika mchakato huu.

**SPIKA:** Hiyo ni habari njema, Waheshimiwa bado mna maswali! Uliza swali lako Mheshimiwa.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, wananchi wengi wameathirika kwa kukosa fedha zao ambazo waliziweka katika benki hii na Benki Kuu inapotoa leseni au kibali kwa ajili ya kufungua benki, wao wanakuwa ndiyo dhamana.

Mheshimiwa Spika, na kuna methali inasema dhamana ndiyo milipaji, lakini hata mahakamani unapomchukulia mtu dhamana, akikimbia wewe ndiyo unakamatwa unahusika na suala lile. Kwa nini Benki Kuu isiwali pe hawa watu fedha zao, halafu wao wakaendelea na huo, kwa sababu watanzania wanaathirika na hili. (*Makofi*)

Sasa maana ya ninyi kuwa dhamana ni nini?

**SPIKA:** Swali zito hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango, Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, ninyi ndiyo *guarantor*.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nimesema kwenye majibu yangu ya msingi, uendeshaji wa taasisi za kifedha yakiwemo mabenki imeelezwa wazi kwenye sheria ya mabenki na taasisi za kifedha ya mwaka 2006. Benki Kuu haiwezi kuwa dhamana na kuchukua jukumu la kulipa wateja wote ndiyo maana ikaanzishwa Bodi ya Amana, kama nilivyoeleza, ambayo ina dhamana kubwa ya kuwalipa wateja ambao wanamiliki amana chini ya 1,500,000.

Mheshimiwa Spika, na niseme kwamba, asema wateja wengi wamepoteza, kwa *experience* tuliyonayo ndani ya Taifa letu, iknafungiwa benki yoyote au taasisi yoyote ya kifedha, zaidi ya asilimia 90 ya wateja wa benki au taasisi husika ya kifedha, huwa ni wale wenye amana ya 1,500,000 kurudi chini.

Kwa hiyo, hawa asilimia 10 iliyobaki, ndiyo nimesema kwamba, Serikali mbili zimeshakutana, mwezi Aprili, tarehe 5, 2019 na tayari tumeshakubaliana jinsi ya kuliendeja jambo hili ili wateja wote sasa waliobaki ambao ni zaidi, waliokuwa na amana ya zaidi ya 1,500,000, waweze kulipwa amana zao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Turky, nilikuona, swali la mwisho la nyongeza eneo hili.

**MHE. SALIM HASSAN ABDULLAH TURKY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Ukiangalia juhudzi za Serikali ya kukuza uchumi huu, sasa hivi jinsi hizi benki zinavyokwenda tunaanza kupata mshituko kidogo. *FBME* imezama, *M Bank* nayo imezama, *M Bank* kama ninafahamu ni benki ya Tanzania hatuwahitaji *Ma-Cyprus* kuja kutujibu, lakini bado zile dhamana ambazo ni za Serikali, naomba sana kwamba Serikali itoe tamko rasmi kwa sababu wateja ni wengi ambao wanahangaika na Serikali iko hapahapa na hii benki iko hapahapa, na sasa hivi imechukuliwa na benki nyiningine ya Serikali yetu.

Kwa hiyo, tunaomba sana tujulishwe hii hatma ya kudai fedha za *M Bank*, tunazipata vipi kwa uharaka wake? Ili watu waamini kuweka fedha benki maana sasa hivi sasa watu kuweka fedha benki tunaanza kuogopa, tunaona hizooo, zinazama. (*Makof*)

**SPIKA:** Na ukiweka benki maana yake usiweke zaidi ya milioni moja na nusu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango tuge *re-assurance*, kuna usalama nchini hapa kuweka fedha benki zaidi ya 1,500,000! *M Benk.* (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kuna usalama mkubwa sana ndani ya Taifa letu, kwenye taasisi zetu za kifedha kwa sababu Benki Kuuu ya Tanzania iko macho na iko makini kusimamia sheria ya kuazisha benki hizi na taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Spika, na niliombe sana Bunge lako Tukufu, tunapokuja na sheria ya kusimamaia hizi taasisi za kifedha, muwe mnatuunga mkono, ni kwa sababu tunaona wengi wa wateja wetu wanapoteza fedha kwa kuingia katika mifumo ambayo siyo sahihi na nilishukuru Bunge lako Tukufu kwa kuturuhusu kwenye Bunge letu la mwezi wa 11 kuitisha sheria ya huduma ndogo za fedha na sasa tunawafikia wote kule walipo ili kuhakikisha wateja wetu wote wanakuwa salama.

Mheshimiwa Spika, na niseme, hili la *M Bank*, kama alivyosema muuliza swali, *M Bank* imechukuliwa na benki nyingine. Kwa maana hiyo, *M Bank* siyo kwanza wataja wake wanatakiwa kusubiri mchakato kwa sheria ya ufilisi, hapana. Benki iliyoichukua *M Bank*, ina jukumu na dhamana kubwa ya kuhakikisha wateja wote wanalipwa na wanalipwa amana zao zote pale wanapozihitaji.

Mheshimiwa Spika, lakini niwaambie watanzania kwamba, kuweka fedha zao kwenye benki zetu ni salama na benki ambayo *M Bank* imeunganishwa inafanya vizuri na niwaombe waendelee kuacha amana zao huko kwa sababu faida ni kubwa ya kuacha fedha zao kwenyeakaunti zao.

**SPIKA:** Tunahamia Wizara ya Nishati, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha kwa majibu mazuri sana. Swali la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mheshimiwa Mary.

Na. 218

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Ujenzi wa Njia ya Umeme Pwani**

**MHE. MARY D. MURO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia Wananchi wa Kiluvya, Madukani, Mwanalugali na Mikongeni ambao wamepisha ujenzi wa njia ya umeme?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mbunge wa Viti Maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* inatekeleza mradi wa kujenga njia ya kusafirisha umeme wa

msongo wa kilovot 400 kutoka Kinyerezi (Dar es Salaam) na Rufiji (Pwani) kupitia Chalinze hadi Dodoma kupitia maeneo ya Kiluvya, Madukani na Mwanalugali. Mradi huu unalenga kuongeza upatikanaji wa umeme katika ukanda wa Mashariki, Kati na Kaskazini mwa nchi kutoka katika mitambo ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi na mradi wa Rufiji.

Mheshimiwa Spika, upimaji wa njia na uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi ulikamilika mwaka 2018. Jumla ya shilingi bilioni 21 na milioni 600 zinatakiwa kulipwa kama fidia kwa wananchi katika maeneo ya Halmashauri za Kisarawe, Kibaha Mjini na Kibaha Vijiji ikiwemo wananchi wa Vijiji vya Chalinze, Kiluvya madukani na Mwanalugali. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali imetenga fedha shilingi bilioni 50 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi wa maeneo hayo baada ya kukamilisha uhakiki wa madai hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inawaomba wananchi wavute subira wakati Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za malipo haya, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mary nimekuona swali la nyongeza.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuiliza swali la nyongeza, swali la kwanza kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Pwani especially sehemu hizo zilizotajwa, walisitishiwa tangu 2014 wakati wa Awamu ya Nne, na anasema kwamba watalipa fidia kwa uthamini wa 2018 watu hawa walikuwa wanajenga wakaacha ujenzi na gharama zimepanda.

Je, Serikali iko tayari kulipa hasara ambayo maongezeko ya gharama za ujenzi watakapokuwa wanalipa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa Serikali imekaa kimya muda wote huu.

Je Waziri yuko tayari kufuatana na mimi baada ya Bunge ili akaweze kuongea hayo ambayo ameyaeleza hapa wananchi waweze kumuelewa kwa urahisi? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Nishati, Mheshimiwa Subira Hamisi Mgali tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru kwa kufuatilia ili suala hili ni swali lake la pili, lakini pamoa naye niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo ya Kibaha Mjini, Kibaha Vijijini na Chalinze kwa kufuatilia hili swali kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nimueleze Mheshimiwa Mbunge na na wananchi wa Mkoa wa Pwani wakati wa mwaka 2014/2015 Serikali ilipo *design* mradi huu wa Kinyerezi, Chalinze, Segera Tanga ulikuwa kabla haujafanywa maamuzi ya ujenzi wa mradi mkubwa wa Rufiji *Hydro Power*.

Kwa hiyo, Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani na kuamua kutekeleza mradi huu kwa nia ya kufanya nchi iwe na umeme wa kutosha ilibidi ifanye utaratibu wa kuuisha upembuzi yakinifu kwa sababu mradi huu sasa wa Rufiji *Hydro Power* kuna njia mpya ambayo itajengwa ya KV400 kutoka Rufiji, Chalinze ambayo inaelekea Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndio suala ambalo limepelekea fidia hii kuchelewa kwa sababu lazima iuishwe, lakini tunatambua fidia inalipwa kwa mujibu Sheria na Kanuni. Kwa hiyo, malipo ya fidia hii kwa wananchi wa Mkoa wa Pwani yatazingatia Sheria na Kanuni za nchi ambazo zinapeleka malipo haya ya fidia.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili amesema je, nipo tayari?, nataka nimualifu Mheshimiwa Mbunge na mimi pia ni mdau ni Mbunge wa Mkoa wa Pwani hivi karibuni tu nilifanya ziara Kata ya Pera Jimbo la Chalinze na niliongea na wananchi suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo namkubalia kwamba baada ya Bunge hili au wakati wowote tunaweza tukafanya ziara katika maeneo ya Kibaha, maeneo ya Jimbo la Segerea, maeneo ya Kibaha Vijijini, maeneo ya Chalinze kuzungumza na wananchi na kwamba kwa kweli kama nilivyosema wakati wa bajeti yetu wataona tumedhamilia kabisa kulipa hii fidia kwa sababu mradi huu unaanza mapema Julai, 2020 na kukamilika Desemba, 2022, ahsante sana.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Salm Kikwete swal la nyongeza tafadhali.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swal la nyongeza, mradi wa kuchakata gesi wa *LNG* Likong'o Lindi. Ni muda mrefu sana wananchi wa eneo la Likong'o hawafanyishughuli zao za kilimo ili kujipatia mahitaji yao ya msingi na kuongeza uchumi wao binafsi na mradi huu ni muhimu sana kwa wananchi wa Lindi kwa ajili ya kuongeza uchumi wao, lakini si hilo tu bali ni Taifa kwa ujumla kwa sababu ni mradi mkubwa sana, Mheshimiwa Waziri.

Je, ni lini wananchi hawa wa Lindi hasa Likong'o watalipwa fidia zao kwa ajili ya kuinua vipato vyao na kuacha eneo hilo liendelee na kazi iliyokusudiwa? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swal hilo zuri la wananchi wa Lindi, eneo la Likong'o Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati Mheshimiwa Subira Hamis Mgusu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati nakushukuru kwa kunipa fursa ya kujibu swal la Mheshimiwa mama Salma Kikwete Mbunge wa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais juu ya suala la fidia la eneo la Likong'o ambalo tunatarajia kutekeleza mradi mkubwa wa kujenga kiwanga cha kuchakata gesi asilia ambayo imegundulika kwa wingi katika Mikoa ya Mtwara kwa kiasi cha triliioni *cubic feet* 55.

Mheshimiwa Spika, nataka nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge mama Salma na wananchi wa Mkoa wa Lindi Serikali inatambua umuhimu wa mradi huu na ndio maana Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo ya kukwamua mkwamo ambao uliokuwepo kwa Wabia wale wa mradi wa kutaka kila mmoja tuzungumze naye kwa wakati tofauti na mazungumzo hayo yameanza kati ya kampuni ya *BP SHELL* pamoja na *STATOIL* ambayo kwa sasa hivi inajulikana kama *equinor*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mazungumzo haya yameanza kwa kwa kuwa sasa hivi kuna kila dalili ya mradi huu kufanyika na taratibu zinaendelea na Kamati ya Wataalam wameshakaa suala la fidia kwa eneo hili limeshafanyiwa kazi na naomba nimualike Mheshimiwa Mama Salma Kikwete na Wabunge wote wa Mkoa wa Lindi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwenye mukutano wa tarehe 21 mwezi huu wa 5 wa *ku-raise awareness* ya mradi huu na ambapo pia taarifa na uhakika wa ulipaji wafidia baada ya tathimini kukamilika itatolewa.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru wananchi wa Mkoa wa Lindi kwa uvumilivu wao tunakuja tarehe 21 na kwamba kila kitu Serikali imekiweka vizuri, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, swali la mwisho kwa siku la leo linaulizwa na Mheshimiwa Agness Mathew Marwa, Mbunge wa Viti Maalum, Kwa niaba yake Mheshimiwa Chacha.

Na.219

### **Nyumba Ambazo Bado Hazijapata Umeme wa REA**

**MHE. MARWA R. CHACHA (K.n.y. MHE. AGNESS M. MARWA)** aliuliza:-

Nyumba nyingi za Vijijini hazikuwekewa umeme wakati wa usambazaji japo baada ya kuweka umeme kumekuwa na ongezeko la ujenzi wa nyumba na uzalishaji mali kama ujasiriamali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha nyumba zote zilizobaki zinapata umeme kabla mradi wa *REA* haujamaliza muda wake?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati na Madini, Mheshimiwa Subira Hamis Mgusu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijiji (*REA*) ni kupeleka umeme katika Vijiji vyote Tanzania Bara ifikapo Juni, 2021. Ili kutekeleza azma hiyo, Serikali imeweka kipaumbele kwa kusambaza miundombinu ya umeme katika maeneo ambayo hayajafikiwa na miundombinu ya umeme na katika Taasisi zinazotoa huduma za kijamii kama vile Shule, Zahanati, Makanisa, Misikiti, Vituo vya Afya, Nyumba za Makazi na Biashara na Miradi ya Maji. Utekelezaji wa Mradi wa *REA* Awamu ya III mzunguko wa kwanza ulianza kutekelezwa mwezi Julai, 2018 na unaendelea katika maeneo yote nchini ambapo utekelezaji wake utakamilika ifikapo mwezi Juni, 2019. Maeneo yatakayobaki ikiwa ni pamoja na nyumba za makazi, Taasisi, miradi ya maji na biashara yatapelekewa umeme kupitia mradi wa *REA* III Mzunguko wa pili utakaoanza kutekelezwa mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mpango huo, Serikali imebuni miradi ya ujazilizi (*Densification*) kwa lengo la kujaziliza katika mapungufu kwa miradi iliyo tangulia. Miradi hii ya ujazilizi inalenga hasa kuhakikisha nyumba zote katika kila Kijiji na Kitongoji zinaendelea kupata umeme. Shirika la Umeme nchini (*TANESCO*) nalo linaendelea kusambaza na kuunganisha wateja mara kwa baada ya miradi ya *REA* kukamilika. Ili kuhakikisha wananchi wote wa Vijiji wanaunganishiwa umeme kwa gharama nafuu ya shilingi 27,000, ahsante sana.

**SPIKA:** Mhehsimiwa Mbunge wa Serengeti nilikuona.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kwanza nichukue nafasi, nimshukuru Mheshimiwa Waziri, na Naibu wake Waziri wanafanya kazi nzuri sana, na ni kazi ambayo itaisaidia sana CCM 2020 tunakoenda kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza, swali la kwanza Mheshimiwa Waziri wa Nishati alipokuja Serengeti mwaka huu mwanzoni alihaidi maeneo ya yafuatayo yatapa umeme; shule ya Sekondari Inagusi ilipo Kata ya Isenye, Kijiji cha Nyamatoke na Mosongo viliwyopo Kata ya Mosongo pamoja na Kiyakabari Kata ya Stendi Kuu. (Makofii)

Ni lini maeneo haya yatapata umeme ambao ulihaidiwa na Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni lini *TANESCO* au *REA* watapeleka umeme Kata ya Morotonga katika Vitongoji vya Mutukura na Romakendo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Morotonga iko Mugumu Mjini pale pale.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza tupokee pongezi zake, lakini naamini pongezi ni kuhitaji zaidi huduma. Kwa hiyo, tumepokea kwa ahadi kwamba tutaendelea kufuatilia hiyo miradi. La pili pia nimpongeze ye Mheshimiwa kwa namna ambavyo anavyofuatilia masuala ya nishati katika Jimbo lake na sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini masuala yake mawili yamejielekeza kwanza kwenye ziara ambayo imefanywa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati katika Jimbo la Serengeti na ahadi aliyoitoa katika shule ya Sekondari Nagusi na maeneo ya Kiyabakari. Nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nishati alipotoa ahadi hii alikuwa na uhakika wa utekelezaji wa mradi wa REA Awamu

ya III mzunguko wa kwanza unaoendelea na kwamba mkandarasi Derm wa Mkoa wa Mara ni mionganini mwa wakandarasi wanaofanya vizuri tulivyo wa-rank na kwamba inatarajiwani itakamilisha kazi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maeneo aliyojataja mara tu Julai 2019 mradi wa REA Awamu ya III unaanza na kazi ndiyo itafanyika. Kwa hiyo nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwa kipindi hiki cha kuendelea 2019 maeneo haya yote ataiona kazi inaanza na nguzo zitapelekwa na ninaomba nimuelekeze mkandarasi Derm azingatia maelekezo ya Mheshimiwa Waziri pamoja na Meneja wa TANESCO wa Mkoa wa Mara na msimamizi wa mradi wa REA katika Mkoa wa huo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mheshimiwa Mbunge ameulizia masuala la kwa mfano Marotonga na eneo ambalo umelitaja Mgumu Mjini, yanaonyesha haya maeneo ni ya ujazilizi. Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi Mheshimiwa Agnes Serikali baada ya kuona pana changamoto baada ya miradi ya REA kukamilika na kwa kuwa lengo lake Serikali ni kusambaza umeme palikuwa na changamoto ya *gap* ya usambazaji wa umeme. Na ndiyo maana ikabuni mradi wa ujazilizi na bahati nzuri Mkoa wa Mara ulikuwemo katika ujazilizi Awamu ya kwanza ambao ulikuwa kama mradi wa majaribio.

Mheshimiwa Spika, na Serikali imekuja na mradi wa ujazilizi Awamu ya pili, Awamu ya II(a) ambayo itakuwa na Mikoa tisa na Awamu ya II(b) itakuwa na Mikoa 16, ikiwemo Mkoa wa Mara na kwa kweli tunauhakika Awamu ya II(a) utafadhiliwa na Serikali za Norway, Sweden na Umoja wa Ulaya na hela zake tunazo bilioni 197 na Awamu ya II ya ujazilizi *two* (b) utafadhiliwa na Serikali ya Ufaransa mpaka sasa tunauhakika wa kiasi cha bilioni 270 kati ya bilioni 400 ambazo zitaanzia kazi na mchakato tupo hatua ya manunuzi na mradi huu utaanza 2019/20 kwa ajili ya kufikisha umeme katika maeneo ya Vitongoji ili kuweza kusambaza umeme, nikushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa sababu ya muda Waheshimiwa Wabunge inabidi tuendelee, lakini mradi huo wa ujazilizi ni mradi muhimu mno ili kusahihisha makosa yote yale yaliyofanyika kule nyuma, tunasubiri sana kwa hamu hiyo *Densification*.

Wageni waliopo katika Jukwaa la Spika leo asubuhi ni viongozi wa Benki ya *DCB* ambaao ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Profesa Lucia Msambichaka, Profesa Msambichaka, Mkurugenzi wa Benki Godfrey Ndalama, Mkurugenzi wa Blashara James Ngaluko, Mkuu wa Kitengo cha Masoko Rahma Ngasa huyo hapo, Meneja wa Tawi Joseph Njile na Afisa Uhusiano Nuru Ashraf, ahsante sana karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Wahaeshimiwa Wabunge wageni nane wa Mheshimiwa Stella Ikupa Nalbu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Watu Wenye Ulemavu ambaao ni viongozi wa shirikisho la Vyama vyta wenye Ulemavu (*SHIVYAWATA*) wakiongزوا na Katibu wao ndugu Ramadhan Mrisho, (*SHIVYAWATA*) karibuni sana wale pale.

Wageni nne wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa Naibu Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ambaao ni familia yake wakiongozwa na mke wake Dkt. Marcelina Mumbee, karibu sana, karibuni sana.

Pia kuna wageni wengine 24 wa Mheshimiwa Kwandikwa ambaao ni Viongozi wa CCM na Madiwani kutoka Ushetu Mkoani Shinyanga wakiongozwa na Katibu Mwenezi wa CCM wa Wilaya ya Kahama ndugu Joachim Simbila, wale wa kutoka Kahama wale haya karibuni sana Wasukuma wote Dodoma ni Jiji muwe munaangalia magari barabarani huko. (*Makofi*)

Wageni 29 wa Mheshimiwa Daimu Mpakate ambaao ni Viongozi wa Vyama vyta ushirika msingi kutoka Tunduru Mkoa wa Ruvuma wakiongozwa na Katibu wa Chama cha Msingi ndugu Ally Jafari Ally, karibuni sana wageni wetu

kutoka Tunduru, mmesafiri masafa marefu karibuni sana Dodoma.

Wageni tatu wa Mhehsimiwa Joseph Haule ambaao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake Mikumi wakiongozwa na Ndugu Philemon Nyalusai, karibuni sana wako pale. Mgeni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salam ndugu Kwezi Mwakapala, karibu sana Kwezi yule kule. (*Makofi*)

Kuna wageni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 24 toka Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) ambaao wamelitembelea Bunge kujifunza namna linavyofanya kazi, wageni wa kutoka (*UDOM*) wengi wao watakuja mchana taarifa nillizonazo, ahsante sana.

Tangazo ni moja tu kutoka kwa Idara ya Utawala na Rasilimali watu hapa Bungeni wanawaomba niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge wote kwamba zoezi la usajili wa kadi za simu kwa kutumia alama za vidole linatarajiwa kuhitimishwa leo kwa upande wa hapa Bungeni.

Hivyo Waheshimiwa Wabunge wote ambaao bado hamjasajili kadi zenu za simu kwa kutumia mfumo huu mnakumbushwa kukamilisha usajili huo.

Aidha, Waheshimiwa Wabunge wote mnatakiwa kupatiwa chanjo ya homa ya ini kwa awamu ya tatu, pia mnakumbushwa kuwa zoezi hilo bado linaendelea na linatarajiwa kuhitimishwa wiki hii.

Hivyo Waheshimiwa Wabunge wote ambaao mlikuwa mmepata chanjo hiyo inatakiwa iendelezwe kwa maana ya Awamu ya III mnapaswa kufika pale kituo cha afya ili kuweza kupata huduma hiyo, Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi,  
Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea, atakayetufungulia ni Mheshimiwa Peter Serukamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Secil Mwambe na Mheshimiwa Andrew Chenge ajiandae, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Saleh. Mheshimiwa Serukamba tafadhali!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru wka kunipa nafasi niwe wa kwanza leo, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na wafanyakazi wa wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya. Naanza, nina mambo matatu kwa kweli, moja ni suala la barabara ya kwangu kule Mwandiga kwenda Kabunga ni barabara mpya barabara ambayo Mheshimiwa Rais aliahidi kwenye kampeni, ningetamani sana tutakapoenda kwenye kampeni mwaka kesho hilo lisiwe swali, naomba sana waziri tujitahidi barabara hii tuweze kuimaliza na barabara hii ina faida zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ikiisha maana yake Gombe watu hawataenda kwa njia ya boti; barabara hii ikiisha *TPA* wamejenga bandari kule Kagunda ili bandari ile iwe na maana lazima barabara hii iishe *TPA* na halmashauri wanajenga soko Kagunga ili soko lile liwe na maana kwa biashara ya Burundi na Uvira, lazima barabara hii iishe, niombe sana Wizara tujitahidi barabara hii iishe kwa kweli ni barabara ya kiuchumi ni barabara ya kiulinzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la *PPP*. Nimesoma kitabu hiki cha Waziri sijaona popote tunapoongelea barabara za *PPP* au mradi wowote mkubwa wa *PPP*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hili ningeomba sana watu wa Serikali watusaidie. Mimi naamini tunapoongelea barabara Tanzania, Rais Nyerere alijenga barabara, Mwinyi alijenga barabara, Mkapa alijenga barabara, Kikwete alijenga barabara, Magufuli anajenga barabara. Mimi leo nataka tumtenganishe Magufuli na Marais wote waliopita kwenye barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kumtenganisha lazima tuje na mawazo mapya. Umefika wakati barabara za nchi hii tuanzishe *super high way* ambazo hatutumii fedha zetu. Tutajenga barabara ambazo totalipa kwa *road toll*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wako watu fulani Serikalini wanasema kwa kujenga *standard gauge* barabara haina maana, siyo kweli.

**MBUNGE FULANI:** Siyo kweli.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Dodoma Jiji, ili Dodoma iwe *accessible* lazima tujenge *super high way from Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Arusha*. Maana yake ni nini? Kama kuja Dodoma ni saa nane, maana yake Dodoma haiwezi kukua kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nasema reli hata ikiisha kazi yake ni mizigo. Kama mnadhani tunajenga reli kwa ajili ya kusafirisha watu nadhani siyo sahihi. Kwa hiyo, tunasema tujenge barabara na hizi barabra duniani kote wanatumia hela za *PPP*, Malaysia, Marekani na China wanatumia *PPP*, tatizo letu ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi na wewe tulikwenda kwenye mkutano wa *IPU*, Urusi. *International Airport* ya Urusi (Moscow) ni ya mtu amejenga, siyo Serikali lakini *service* zinapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najua sana mambo ya barabara kwa sababu na mimi nimekulia humo ndani, naombeni tumfanye Magufuli awe tofauti na wenzake. Namna bora

ya kuwa tofauti ni moja tu: Amekuwa tofauti kwenye reli, wote hawakujenga reli ye ye anajenga reli; amekuwa tofauti kwenye umeme wa *Stiegler's* wote hawakufanya ye ye anafanya, naombeni tumpe na utofauti wa barabara, tujenge *super high way* nchi nzima ambazo watu watakuja kwa kulipa. *Chalinze high way* tumeiondoa, *why?* Ukiwauliza watu wa Serikali wanasema Chalinze *high way* tumeiondoa kwa sababu kuna *standard gauge*, hapana, havina mahusiano hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siyo lazima watu wote watapanda reli. Haiwezekani kilometra 100 tunakwenda saa tatu, kiuchumi siyo sawa. Kwa sababu *infrastructure* ndiyo inayoleta uchumi, ndiyo *enabler* wa *economy*. Sasa kama *infrastructure* ndiyo *enabler* wa *economy* lazima tufanye vitu ambavyo vitasababisha *goods* zifike mapema, tuweze kwenda kwenye maeneo yetu mapema, twende kwenye biashara tuwahi kurudi. Sielewi kwa nini Serikali haitaki miradi ya *PPP*. Naamini kama tunataka twende haraka lazima twende kwenye *PPP*. Wenzetu wote wanatumia fedha za watu, hii kwamba lazima tufanye wenyewe siyo sawa.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kufanya wenyewe ni haya yafuatayo. Barabara ya kutoka Nyakanazi kwenda Kabingo Kilometra 50 tunajenga huu mwaka wa 10. Barabara ya kutoka pale Kidahwe - Kasulu huu mwaka wa 10. Maana yake ni nini? Tuna shida nyngi sana tunataka kufanya yote. Namna bora ili tuweze kwenda kwa kasi, maeneo mengine tuwaachie wengine wafanye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naamini Watanzania hawawezi kushindwa kulipa *road toll*, hawawezi. Kama natoka na basi Kigoma saa 12.00 asubuhi, nina uhakika nitakuwa Dar es Salaam saa 10.00 kuna shida gani ya kuweka *toll*? Nani atakataa kulipa *toll*? Sielewi kuna nini Serikalini. Sielewi *why* Serikali hawataki miradi ya *PPP*, sielewi.

Mheshimiwa Spika, napenda Waziri atakapokuja atuambie hivi sisi ni tofauti na watu wengine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo ukienda Marekani hata uki-google, mtu pekee anayekumbukwa kwenye barabara Marekani ni Rais Franklin Roosevelt? Kwa sababu gani? Baada ya vita kuu ya pili ya Dunia aliamua kuunganisha *states* zote 50 kwa *super high way* na watu wanalipa kwenye *toll*. Kwa nini hatutaki kufanya hivyo? Kwa hiyo, mimi ningeomba sana Serikali, najua jambo hili linawawia ugumu lakini sioni ugumu wake ni nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni viwanja vya ndege. Mimi hili naleta ushauri Serikali mlitafakari upya, nadhani umefika wakati viwanja vya ndege viachiwe kazi ya kujenga na kuendesha. Habari ya kuchukua viwanja vya ndege unapeleka *TANROADS*, inawezekana ni nia ya kudhibiti lakini kuna ucheleweshaji. *TANROADS* wana kazi kubwa, wana madaraja, barabara na kila kitu. Ningeomba suala la viwanja vya ndege tuvirudishe. Pale tumepeleka *CEO* mzuri sana, *Engineer* Ndyamkama *is one of the best*, tumpe kazi hii ataifanya na kwa haraka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuweke taa kwenye viwanja vyetu. Tumenunua ndege lakini ili ziweze kufanya kazi mara nyingi tunahitaji taa. Hii kusubiri juu tu maana yake ndege zetu hazifanyi kazi *at its capacity*. Kwa hiyo, naomba sana hili nalo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la bandari. Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana viongozi wa bandari kwa kazi kubwa wanayofanya. Hata hivyo, kazi kubwa inayofanyika bandarini naomba tuwasaidie tuondoe vizingiti barabarani.

Mheshimiwa Spika, kwenye *transit trade*, biashara hii tupo na wenzetu sasa kama kila baada ya dakika tano kuna Polisi, tunaifanya bandari yetu isiwe *attractive*. Kwa sababu gani? Bandari itafanya kazi vizuri, inatoa mizigo kwa wakati lakini lori likishaingia mpaka kufika Tunduma ni shughuli ya siku nne au tano. Wafanyabiashara wanataka waende haraka warudi, hii ndiyo maana ya biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hapa kwetu kuna *point* nyingi za kukaguliwa unapotoka Dar es Salaam mpaka Kigoma na unapokwenda kwenye mipaka yetu nawahurumia wale wanaoendesha haya malori kwa sababu wanasimamishwa kila baada ya kilometra 3 au 4, trafiki wapo. Rais amesema jamani eeh, Polisi haiwezekani mkasema kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro kuna *point* mbili za kukagua, huku kwagine kote wanasimamishwa, biashara haiwezi kutusubiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana sasa bandari yetu inapambana na ushindani wa Mombasa na Beira kwa sababu bandari ina-*perform* lakini kama wale wengine hatuisaidii itaonekana imeelemewa. Kwa hiyo, naomba sana watu wa Serikali tuwasaidie sana watu wa bandari kwa maana ya ku-*enable* ili kazi yao iweze kufanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni suala la fedha za barabara hasa za *GOT*. Naomba sana Serikali, ukiangalia *trend* yetu, barabara ambazo zinajengwa na *GOT*zinatumia muda mrefu sana. Maana yake ni nini? Zikitumia muda mrefu, *interest rate*, *idle time*, kwa barabara ambayo ungeijenga kwa shilingi bilioni 50 unaijenga kwa shilingi bilioni 100, siyo sawa. Atakuja mtu siku moja tutapata shida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba na mimi niunge mkono hoja, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba. Nilikuwa nimeshakutaja Mheshimiwa Cecil Mwambe na Mheshimiwa Andrew Chenge ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, nataka tu niongee mambo matatu, kwanza, ni suala linalohusiana na Reli ya Kusini kwa maana ya Mtwara-Mbambabay. Pili, ni suala linalohusiana na masuala ya barabara ya uchumi ya Mtwara

- Newala - Masasi - Nachingwea lakini tunaomba ikiwezekana iongezwe Liwale -Morogoro kwa sababu tunafahamu sasa hivi Makao Makuu ya nchi yetu yamehamishiwa Dodoma. Sisi wakazi wa Mtwara tunakwenda Dar es Salaam kufauata huduma na siyo lazima tufike pale, tungeweza moja kwa moja kutokea huko tunakokutaja tukaja hapa Dodoma *straight*. Kwa hiyo, tunataka na hii Serikali nayo tuishauri.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho kabisa, nitapenda pia niihoji Serikali kwa sababu mpaka sasa kwenye Wizara hii na idara zake mbalimbali wameshatengewa na pesa zimeshatumika *almost* triliioni 18 lakini hatujaona kimsingi athari yake kiuchumi ndani ya nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la barabara hii niliyoitaja ya Mtwara – Mnivata -Newala – Masasi. Ukisoma kwenye hotuba ya Waziri, ukurasa wa 278, kipengele cha tano, wanasesma: "Ujenzi wa barabaraya Mtwara -Newala -Masasi".

Mheshimiwa Spika, barabara hii ina jumla ya kilometa 221. Kama ambavyo Mheshimiwa Serukamba pale amesema tuangalie *value for money*. Barabara yenye urefu wa kilometa 221 imetengewa shilingi bilioni 3.4 tu. Kwa wastani wa sasa wa kilometa 1 ya barabara kutengenezwa kwa shilingi bilioni 1, wanatuambia kwamba katika mwaka huu wa fedha watakwenda kujenga barabara hii kwa kilometa 3 tu. Sasa tunampa mkandarasi barabara ya kilometa 221.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameikagua barabara hii akasema tunaomba hii barabara ijengwe kwa haraka sana kwa sababu ni barabara ya uchumi lakini katika hali ya kushangaza Wizara wanatenga shilingi bilioni 3.4 pekee yake, wanamkwamisha sana Mheshimiwa Rais. Hawa wasaidizi wake wakati fulani wanashindwa labda kumpa ushauri unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kimsingi barabara hii ni ya uchumi na ni ndefu, hauwezi kutenga shilingi bilioni 3.4 pekee kwenye

barabara yenyе urefu wa kilometra 221. Kwa hiyo, tuiombе Wizara ikiwezekana warekebishe fungu hili au waone namna ya kufanya ili kuweza kutekeleza ile ahadi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, Rais alipokuja alisema barabara hii atahakikisha wanawekwa wakandarasi watatu mpaka wanne kwa urefu wa kilometra hamsini hamsini kila mmoja. Mpaka sasa barabara inayojengwa ni Mtwara -Mnivata lakini ni asilimia 36 tu ambazo zimeshatekelezwa na sasa ni mwaka wa tatu. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara itusaidie, kero ya barabara hii ni kubwa sana na nia yetu sisi ni kusafirisha watu. (*Makofі*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine hapa, suala la Reli ya Kusini. Kwa muda mrefu sana tumeongea na maeneo mengi watu wanadai fidia ikiwemo maeneo ya Mtama, Ndanda, Masasi na sehemu kubwa sana ya Jimbo la Mtwara Vijijini kwa maana ya kule anapotokea Mheshimiwa Mama Hawa Ghasia.

Mheshimiwa Spika, tatizo lilitopo kwenye mradi huu, mpaka sasa haueleweki kwamba ni lini utaanza au Serikali nao wameamua kujiondoa kwenye huu mradi kama walivyofanya miradi ya barabara ya kutoka Dar es Salaam *high way*mpaka kufikia Chalinze. Kama ni hivyo basi waseme wazi ili wale wananchi waendelee kufanya shughuli zao za kiuchumi kwenye maeneo yao. (*Makofі*)

Mheshimiwa Spika, katika miradi mikubwa ambayo Serikali ilikuwa inaipangilia ni pamoja na mradi wa Liganga na Mchuchuma. Hakuna mwekezaji ye yote atakayekuju hapa kama hatujaboresha hii miuondombinu.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani chuma kisafirishwe kutoka Liganga kuletwa Bandari ya Mtwara kwa kutumia barabara, siyo *reliable* na hasara ni kubwa na hii mizigo ni mizito. Barabara hizi tuache watumie watu kama ambavyo wengine wamesema lakini hii miradi mikubwa ya kipaumbele itekelezwe tuweze kuona sasa manufaa ya chuma tulichonacho sisi. (*Makofі*)

Mheshimiwa Spika, sisi tulishauri Serikali hata kwenye Kamati yetu ya Viwanda Biashara, kwa nini wasifanye uwekezaji mkubwa pale ili kuokoa *forex*? Pesa ambayo ingepatikana Mchuchuma ingekwenda kujenga hiyo Reli ya Kati ya *Standard Gauge*. Chuma ambacho kingepatikana Mchuchuma ingekwenda kusaidia kujenga kwenye reli hiyo pia lakini matokeo yake tunaagiza chuma, tuna viwanda vyetu hapa vya nondo vinaweza kutengeneza lakini bidhaa karibia asilimia 90 zinazotumika kwenye *standard gauge* ni imported. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, huko ndiko tunakomalizia pesa zetu za kigeni na tunashindwa kufanya miradi midogo midogo hii ya kuwasaidia wananchi. Tunaona Wizara ya Maji wanalamika lakini mpaka sasa hivi nguvu kubwa sana inapelekwa kwenye hii miradi mikubwa ambayo utekelezaji wake nao ni wenyе kutia shaka kwa sababu hakujafanyika *due diligence* wala kuonyesha *impact assessment* kwenye hii miradi mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli hii ni muhimu sana kwa watu wa Kusini kama ilivyo kwa watu wa upande wa Magharibi na kwingine kwenye reli hii ya *standard gauge*. Sasa Serikali ituambie hapa wazi, wana mpango wowote wa kufanya kazi hapa kwa sababu kwenye hivi vitabu hawaonyeshi waziwazi wanataka kwenda kufanya nini. Kwa hiyo, waje watueleze kama kuna mpango huo na kama haupo basi tuwaeleze wananchi wetu waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi kwenye maeneo haya. Hii itakuwa ni *failure* kubwa sana kwa sababu hakuna mwekezaji atakayekuja kufanya kazi Liganga kama miundombinu hii wezeshi hatujaitekeleza na tunajinasibu kwamba sisi ni nchi ya viwanda na mambo mengine. Kwa hiyo, tuanze kwanza na msingi wa usafirishaji kutoka kule Liganga kuja kuleta Bandarini Mtwara ambayo ni Reli ya Kusini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kusini ilijengwa mwaka 1949, mwaka 1963/1964 ilindolewa, kwa vyovyote vile inatakiwa pale kufanyike uwekezaji mkubwa. Ni jambo jema kujenga hii *standar gauge railway* lakini malengo ya Reli ya

Kusini iwe ndiyo ya kipaumbele na malengo yake ni makubwa kwa sababu ni sehemu ambako tutakwenda kuongeza uchumi wa nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mweyekiti, nigosie kidogo suala la barabara, tukitaja barabara inayoishia Masasi. Ukisoma pia kwenye hiki kitabu, barabara inayotokea Masasi kuelekea Nachingwea na yenyewe ina kilometra 45 wametenga shilingi bilioni 1.3 tu. Tuiombe Wizara itueleze, tunapotenga shilingi bilioni 1.3 kwenye barabara yenyе urefu wa kilometra 45 tunakwenda kufanya kazi gani na pesa hizi? Pale Masasi sasa hivi kuna ajali nyingi sana kwa sababu kuna *round about* kubwa, barabara inayounganisha kwenda Songea, Newala, Nachingwea na kurudi Mtwara Mjini, tunaomba pale katikati ikiwezekana ziwekwe taa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hili jambo sisi tumelijadili hata kwenye vikao vyetu ya *RCC* na *Road Board* kwamba tunahitaji pale kupata taa kwa sabbau ni *junction* kubwa na watu wengi sana wamekuwa akiwemo Afisa Mkuu wa Maji wa Wilaya yetu sisi ya Msasi, alifia pale na ajali nyingi zinatokea, tunaziona. Kwa hiyo, tunaomba pale ziwekwe taa.

Mheshimiwa Spika, hii barabara tunayoitaja inayokwenda Nachingwea pamoja na pesa ndogo mlizozitenga tuishauri sasa Serikali, tunaomba Mkoa wa Mtwara kuititia Wilaya ya Masasi ifunguliwe sasa isiishie Nachingwea peke yake iende mpaka Liwale, ikitoka Liwale iende mpaka upande wa Morogoro, Malinyi. Safari hii ni fupi sana kutoka Masasi mpaka kufika Morogoro, Malinyi siyo zaidi ya kilometra 300 lakini tunalazimika kutembea kilometra 600 kwanza kufika Dar es Salaam ili tuweze kuondoka Dar es Salaam tuje Makao Makuu ya nchi na wakati mwingine unalazimika kusafiri siku mbili mfululizo. Kwa hiyo, niombi Wizara hii wakafanye kazi kwenye barabara hii waone namna ya kuunganisha Wilaya hizi mbili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine niligusia kidogo kuhusiana na uwekezaji mkubwa uliofanyika kwenye Wizara hii. Mpaka sasa hivi Wizara hii na Idara zake wametumia

*almost 18 trillion* kwa maana ya kununua ndege, kutengeneza hivyo viwanja vya ndege na kufanya shughuli mbalimbali zinazohusiana na miundombihu ya hivyo vitu nihavyovisema.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana sisi tulikuja hapa tukasema tunataka tuone manufaa ya moja kwa moja yanayopatikana kwa wananchi kutohana na miradi hii mikubwa inayofanywa na Wizara hii. Sasa utakapokuja Mheshimiwa Waziri tueleze ni namna gani uwekezaji huu mkubwa mlioufanya umenufaisha wakulima wa maeneo yetu wakiwemo wakulima wa korosho na wengine? Ni namna gani uwekezaji huu mkubwa uliofanywa kwenye Wizara hiyo umenufaisha uwekezaji nchini kwetu? Ni namna gani tumewavutia wawekezaji kwa kununua ndege na ni namna gani tumewavutia wawekezaji kwa kufanya huo uwekezaji mkubwa tunaoutaja hapa, Mheshimiwa Waziri uje hapa utueleze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini mtueleze ni namna gani sekta ya kilimo imenufaika na uwekezaji huu mkubwa unaofanywa. *Otherwise* na yenyewe tutakuwa tunasema *bad timing, hatuna proper value for money*. Tuiombe Serikali mwisho kabisa ikubali kufanya utafiti wa kina (*impact assessment*) ili kuweza kujua uwekezaji huu mkubwa uliofanyika pale umenufaisha wananchi kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa tumewekeza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa idadi ya Wabunge nilionao na hasa upande wa Chama Tawala hatuwezi kupata

dakika 10, baadhi itakuwa dakika tano watakaopata nyingi ni dakika saba kwa sababu nina wachangiaji wengi na kwa kweli haiwezekani. Kwa hiyo, ukipata nafasi yaani nenda moja kwa moja unachotakiwa useme.

Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Chenge dakika saba atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Saleh dakika saba.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, nikishukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami nichangie kwa ufupi tu.

Mheshimiwa Spika nipongeze kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii kwenye maeneo muhimu ya ujenzi wa barabara, mawasiliano na uchukuzi. Hongereni sana, naelewa rasilimali fedha ndiyo zinatusumbua. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jana nimetoka Bariadi kuja Dodoma nimeona kazi nzuri inayofanywa kati ya Bariadi na Maswa, mkandarasi anaendelea na pesa imetengwa tena. Tungependa tukamilishe barabara hii ikiwezekana mapema mwaka huu au mwaka kesho tuweze kutoka moja kwa moja Dar es Salaam – Dodoma – Shinyanga – Mwigumbi –Bariadi – Lamadi – Musoma – Sirari - Nairobi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Bariadi imekaa katikati kwa ukanda wa Kaskazini Mashariki mwa Tanzania na ndiyo maana tunasema sana barabara, tulitegemea katika Mwaka huu ujao wa fedha angalau kipande cha Bariadi kuja Moboko-Mwanuzi mpaka Sibiti Kingeliweza kufanyiwa *feasibility study* yaani upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Lakini naona sioni kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri hata kwenye majedwali yale ya kipande hiki hakipo, tunaendelea kuiomba Serikali kwamba tuunganishwe na mikoa jirani ya Singida na Arusha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lingine mkisoma hotuba za Wizara hii kwa miaka mitatu iliyopita barabara ya Kolandoto, Munze, Lalago mpaka Thibiti ilikuwa inaenda mpaka Matala - Mang'ola na Odiang Junction. Sasa hivi tunaongelea

kasehemu kadogo tu, tumeanzisha mradi mzuri tu huu wa kutoka Karatu, Mbulu, Haydom, Sibiti, Lalago Maswa. Ningependa Serikali ituambie kwa kazi iliyofanyika kwa kipande cha kutoka Sibiti, Mataala, Mang'ola na Odiang Junction ile sehemu tunaiacha au tunaendelea nayo? Ningependa nipewe majibu na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije kwenye upande wa barabara, mimi kuna barabara nasema kwa sababu tunajua hali ya Tanzania iliyvyo kuna maeneo mengine ni ukame, mengine yana hali nzuri ya barabara, naendelea nashukuru Serikali nimeona upande wa barabara ya Kidatu - Ifakara - Tupilo kuelekea Malinyi - Londo mpaka Lumecha Songea nashukuru sana kwa sababu tukiweza kukamilisha barabara hii tunafungua njia ambayo eneo lenye utajiri mkubwa sana wa chakula na hali nzuri ya hewa. Lakini ningependa tuangalie plia uwezekano wa kutoka Ifakara twende Kihansi, twende Mlimba, twende Taweta, twende mpaka Madeke, twende mpaka Lupembe maana tukiyabeba haya yote unaifungua sehemu hiyo yenye utajiri na kuweza kupeleka chakula kwa haraka katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho naomba tunafanya kazi nzuri katika kupanua Bandari ya Dar es Salaam, napongeza Serikali lakini nasema mwaka jana nilishauri reli yetu ya katii hii tunayojenga sasa hivi ni afadhali tukachukua mkopo wa muda mrefu kuliko hii ya mikopo ya masharti ya muda mfupi ambayo yatakuja kutuumiza, maana hata kabla hatujaanza kuitumia reli hii tutaanza kulipa madeni haya. Lakini tukichukua madeni ya muda mrefu na kwa masharti nafuu tunajenga reli hii tukamilisha yote kwa wakati mmoja ili tuweze kupata faida ya uamuzi mzuri huu unaofanywa na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa bandari ya Dar es Salaam itatusaidia kwa muda mfupi tu. Duban na Bellair na sasa Nakala lakini upande wa Lam na Mombasa wenzetu hawa wanaangalia mbali sana, tungependa na sisi Bandari hizi Mungu ametupa nafasi nzuri sana, Bandari ya Mtwara, Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Bagamoyo Mbegani

narudia kuishauri Serikali na Mwambani hizi kwa upande wetu wa Tanzania zikiweza hizi zikajengwa, hii ndio *future* ya Tanzania kuunganisha na nchi za Maziwa Makuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa sana Bunge lako tuendelee kuishauri Serikali waone faida ya haya. Najua muda wangu ndio huo lakini nikushukuru sana kwa nafasi uliyonipa, naishukuru Serikali kwa haya wanayoyafanya, niungane na Mheshimiwa Serukamba kwamba tuangalie kwa haraka na sio kupoteza muda, sekta binafsi ishirikiane na sekta ya Umma kwa PPP katika kuyafanya mengi haya na tusiogope. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Chenge huo ndio uchangiaji wa *masenetorsio* unachangia Jimboni kwako tu ohoo kataja Bariadi, kataja Malinyi huko, Ifakara, Bandari nakadhalika tunachangia kama nchi inakuwa inasaidia zaidi kuisaidia Wizara kuwa na uono wa mbali na kapigia mstari bandari ya Bagamoyo, kwa kweli Bandari ya Bagamoyo ni ukombozi mkubwa sana tungeipata ile ingefungua nchi yetu. Mheshimiwa Ally Saleh dakika saba anaafuata na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba dakika saba. (*Makofi*)

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kweli sehemu yangu kubwa ya mchango wangu utakuwa ni kuhusu bandari ya Bagamoyo ambayo umeitaja hapo. Lakini kwanza nitapitia *in passing* tu. Kuhusiana na ATCL nakubaliana 100 kwa 100 na mchango wa Mheshimiwa Kapteni Abbas Mwinyi wa wiki iliyopita ametusemea wengi na amesema mengi na amesitiza yale ambayo *opposition* tumekuwa tukisema lakini Serikali ilikuwa haitusikilizi naamini kwa kuwa yametoka kwao sasa labda pengine utasikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusiana na reli nakubaliana na wengi ambao wanaosema kwamba reli ni muhimu lakini haiondoshi kuwepo na taratibu nyingine za usafiri. Marekani mizigo mingi inasafirishwa kwa magari

makubwa hata kuliko reli, reli ni ya pili, pia kutegemea reli kwa abiria ni makosa makubwa sana, reli ni mizigo, yupo mtu alisema hapa kuna haja ya kuwa na *drive ports* kila baada ya eneo ili kurahisisha mizigo kuwa *collected* ili kwenda sehemu nyingine ya nchi au nchi jirani. Kwa mfano kuwa na *drive port* Dodoma au kuwa na *drive port* Morogoro ili mizigo inatuliwa pale kisha reli inabeba. India mizigo ni *80 percent* ya reli inatia faida kwa *80 percent*. Abiria ni *less* labda *15 percent*, mizigo mingine midogo ndio *percent* ili yobakia, kwa hiyo tusijidanganye reli ni mizigo bila mizigo hakuna reli itakuwa hasara tupu.

Mheshimiwa Spika, la tatu nataka kuzungumzia juu ya suala la mabaharia, nchi yetu mwaka jana tuliridhia mikataba miwili *Maritime Convention* na *Seafarers ID*. Lakini hatukwenda mbali zaidi kuleta sheria kuibaidilisha ile sheria ya meli ili iweze kufaidika. Kwa hivyo kwa maana nyingine tumeridhia *conventional* lakini hali ya mabaharia wetu 5,276, iko mbovu vilevile bila kitambulisho, bila sheria ya kupitishwa hapa haiwezekani mabaharia wetu wakafaidi malipo mazuri ambayo wanaweza kulipwa na wanaendelea kupunjwa kwa sababu tu kwamba sheria haikufuatiilia *domestication* *I mean* mkataba wa Kimataifa hawakufuatiilia *domestication* ya sheria ili mabaharia wetu wawe na hadhi kamili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo nakwenda kwenye *Special economic zone* ya Bagamoyo, na naanza kwa kusema kwamba tunafanya makosa kama Bunge na kama nchi kuachia mradi mikubwa kama hii ikafutwa bila kuwepo na *public discussion*. Vilevile nataka nikushawishi hata wewe kwa nafasi yako unaweza kuunda vyombo au kuunda namna ambayo ya kuweza kuchunguza kwa nini kama nchi tunaacha mradi huu ambaeo tutauelezea leo hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mradi huu kwanza tunaondokane na dhana kwamba ni bandari, ni zaidi ya bandari ni mji, ni ajira ni kufunguka kwa uchumi wa Tanzania. Kutakuwa au kungekuwa na viwanda 800 ambavyo tayari viko pale pale

katika eneo kwa hivyo mzigo unachukuliwa unatiwa katika meli unapelekwa nje au mwingine unatoka pale unakwenda Silama unaunganishwa na reli hii mpya ya *SGR* inakwenda kwagine inakwenda kuuzwa. Pia utajenga Mji wa Kisasa Bagamoyo kwa maana mbili, kwa maana ya kupata watu kuishi lakini pia Dar es Salaam itapumua, Dar es Salaam ikipumua watu wanakwenda kule kuishi Bagamoyo kwa hivyo nchi inatononoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la tatu kutakuwa na *logistic la tan trade* ambayo itafanyika itakuwa kubwa sana bandari ya Bagamoyo kama ingejengwa au kama itajengwa itaweza kuchukua makontena milioni 420 kwa mwaka. Sasa hivi bandari kubwa duniani *Rotterdam* inachukua milioni 11.87, kwa maana nydingine bandari ya Bagamoyo ingebakia kuwa kubwa pengine kwa miaka 100 ijayo kwa Dunia nzima. *Rotterdam* wanaingiza meli 3,613,315 kwa mwaka kwa maana ya meli 110, hapa ndipo unaweza kuona suala la *locally country* linawenza kuwa pana. *Imagine* meli 100 zinakuja kwa siku wanataka maji, wanataka matunda, wanataka *toilet paper*, sijui wanataka kitu gani *imagine* faida ambayo ingepatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia Bandari hii au eneo hili lingeweza kuzalisha ajira zaidi ya 120,000. Eneo la Dar es Salaam kusema una *forfeit* kule ambako mkopo unatoka China na Oman marafiki zetu wakubwa tuseme pia suala la demokrasia katika hili wanatuunga mkono katika mambo mengi lakini unasema na kuna Dar es Salaam, tayari kuna Banana unatka uje na *fourth generation* meli ambazo ni kubwa zinashusha zinapakia wenyewe haziwezi tena kuingia Dar es Salaam, pengine kina cha bandari cha Dar es Salaam kitagoma kupokea meli hizo za *fourth generation* na tukaenda itakuja *fifth* na *sixth generation*. Meli moja ya sasa inaweza kuwa na tani milioni 100 inaleta mzigo wa tani pengine milioni mbili, pengine Dar es Salaam isiweze kubeba tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa pale Dar es Salaam pameshajaa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Saleh bahati mbaya dakika saba zimeisha, lakini kwa hatua hii kwa alichokuwa anakichangia Mheshimiwa Ally Saleh, niongeze sentensi mbili kwa dakika moja tu. Sielewi binafsi sielewi nini kimekwamisha mradi huu wa Bagamoyo labda Mheshimiwa Waziri kama atapata muda anaweza akatufafanulia vizuri ye ye yuko kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuelezea jambo hili. (*Makofi*)

Lakini niliwahi kwenda China mwaka juzi kwa jambo jingine kabisa katika Jiji la Shenzhen, nikiwa na baadhi ya ujumbe wa baadhi ya Wabunge humu ndani na kumbe bahati nzuri Makao Makuu ya wale China *Merchants* amba walikuwa wajenge bandari ya Bagamoyo yako Shenzhen pale. Kwa hiyo, baada ya ziara yangu kuisha Mheshimiwa Balozi wetu akasema ni vizuri tukawapitia hawa jamaa tukasikia kidogo wanachokisema, wakatufanyia *presentation* kubwa nzuri sana, ndio maana nasema sijui upande wa Serikali kuna nini. Lakini ukisikiliza ile *presentation* huwezi kuacha kuunga mkono ujenzi wa bandari ya Bagamoyo. (*Makofi*)

Ni mradi mkubwa mno na wale jirani zetu wanatukuba pale juu sitaki kuwataja majina mnawaelewa tutakuwa tumewabana vizuri, kwa kifupi Wachina walisema tunawashangaeni sana Watanzania nyinyi rafiki zetu ndugu zetu sijui kwa nini inapofika mambo mazuri makubwa kama haya mnavuta miguu, hamuamui na wakasema kwenye kampuni yao ile bodi wameshabadilika sana ile *turnover* yao ni kubwa, hasa waliobakia amba ni watu wazima na *soft touch* na Tanzania katika ile bodi yao walikuwa ni wawili tu na wenyewe walikuwa kama wana miaka miwili nao wataondoka, kinakuja kizazi ambacho hakijui hii maneno. Wakati nasema msipo- *take advantage* ya sisi tunaoondoka sasa hivi mkafanya maamuzi shauri yenu. (*Makofi*)

Lakini mwisho akasema nimwambie Mheshimiwa Waziri, tunakushangaeni eti mjenga reli ya kisasa SGR, kwa maoni yao wao ni marafiki zetu wanasema kama rafiki *over lounge* wanasema ni kama kugeuza mkokoteni si kuna ng'ombe na lile nani... wanasema mnachofanya mnaweka

ule mkokoteni mbela halafu ehee! Wanasema kwa sababu unaanza kujenga bandari ndio unajenga reli, nyinyi mnaanza reli kabla ya bandari wanasema kwa hiyo, tunakuangalieni marafiki zetu, kwa kweli sijui kinachokwamisha labda kuna vitu viwili lakini si mradi wa kuacha jamani chonde chonde na hawa wafanya maamuzi wakae waamue yaani *is grand project* bandari kubwa ya kisasa hakuna Afrika Mashariki hapa mpaka Msumbiji hakuna, viwanda kama alivyosema yule bwana vingi ni Mji wa viwanda yaani ni halafu karibu hela zote wanatoa wao. (*Makofi*)

Kwa hiyo narudia tena sijui kulichoko serikalini inawezekana kuna mambo ya msingi sana wa kuyatazama lakini ni kitu ambacho ni vizuri tukakipa macho mawili tukaacha mambo mengine yote mradi kama huu ni uchumi mkubwa tukafungua uchumi mkubwa sana tukambana jirani yetu yule anatukaba kila wakti yule jiarni yule. Mheshimiwa Lolesia nilishakutaja dakika saba. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, hongera sana kwa kuchangia.

**MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu kabisa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri pamoja na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya tunashuhudia jinsi ambavyo kazi kubwa inafanyika katika Taifa hili, barabara zinajengwa, *flyover* zinajengwa lakini barabara mbalimbali za mikoa zinajengwa. Nichukue nafasi hii kipekee kupongeza kwa kazi nzuri inayofanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze na barabara muhimu kabisa katika Mkoa wetu wa Geita barabara ya kutoka Kahama kwenda Bukoli mpaka Geita, ni barabara muhimu sana kiuchumi, kumbuka katika Mkoa wa Geita na Mkoa wa Shinyanga ni mikoa ambayo imebobea katika masuala mazima ya madini, na kwa sababu hiyo tunahitaji barabara hii iwe ya lami ili iwezeshe shughuli za uchiumbaji wa madini

ziende vizuri zaidi usafirishaji wa mizigo mbalimbali. Kwa hiyo niseme tu kwamba barabara hii ni muhimu sana na kila bajeti barabara hii huwa inakuwepo kwenye bajeti lakini kwenye utekelezaji sijawahi kuiona. Kwa hiyo nitumie fursa hii kuiomba Serikali iwekeze fedha sasa nimeona kwenye bajeti imeweka fedha kiasi fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaomba barabara hii ianze kujengwa sasa kwa kiwango cha lami, barabara hii ni barabara ya kiuchumi, barabara hii imekuwepo kwenye bajeti kuanzia wakati wa Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Rais Kikwete katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi barabara hii imekuwepo kila Ilani inakuwepo barabara hii kuwekewa kiwango cha lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Serikali awamu hii barabara hii ianze kujengwa kwa kiwango cha lami kwa kuanzia Geita kwenda Bukoli mpaka Kahama. Kwa kuwa tunafahamu kuna mradi mkubwa mgodi mkubwa wa Geita lakini pia kuna mradi mkubwa mgodi wa Bulyang'huru, ambao wote hawa wanafanya shughuli za uchumbaji wa madini katika mikoa yetu, kwa hiyo, tukiimarisha barabara hizi nina uhakika shughuli hizi za uchimbaji zitawenza kunufaisha Taifa letu kwa kiwango kikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna barabara muhimu kabisa ya kutokea Katoro - Bukombe ambapo barabara hii pia ni muhimu sana kiuchumi katika Mkoa wetu wa Geita niombe Serikali pia iangalie uwezekano wa kuiwekea barabara hii lami ili kuwezesha uchumi ndani ya Mkoa kuwa mchumi mzuri. Ninafahamu sera yetu ya Taifa inasema kwamba mikoa yote itaunganishwa kwa kiwango cha lami, jambo ambalo ni la msingi sana na ndio maana ninatolea msisitizo kwamba tuunganishe Mkoa wa Geita na Mkoa wa Shinyanga ili hatimaye uchumi wetu uweze kwenda vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile katika upande wa barabara ziko barabara ambazo zimekuwa ni muhimu sana kuchumi kwa mfano, kuna barabara ya kutokea Katoro

kwenda Nyang'wale kuititia Kamena - Nyalwanzaja-Busanda ni barabara ambayo kwa muda mrefu tumeiomba iwe barabara ya mkoa imekuwa ni barabara ya halmashauri lakini sasa hivi naiombea iwe barabara ya mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na kwa bahati nzuri mwaka jana kuna watu walitoka Wizara ya Ujenzi walikuja kuikagua barabara hii lakini kwenye bajeti sijaweza kuiona hajapandishwa hadhi mpaka sasa. Niombe barabara hii pia kwa umuhimu wake niombe ipandishwe hadhi iwe barabara ya Mkoa ili hatimaye iweze kuwashudumia wananchi waliowengi kwa sababu tunatambua kabisa vijijini wananchi tunahitaji barabara nzuri ambazo ziwezeshe katika kuimarisha uchumi wa wananchi katika maeneo yote kwa ajili ya usafirishaji wa mizigo mbalimbali, mazao, kupeleka katika viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba sana Serikali iangalie barabara hii ni muhimu kuweza kuipandisha kutoka halmashauri kwenda kwenye kuwa barabara ya Mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna barabara zingine ambazo tunaishukuru Serikali kwamba imeweza kupandisha hadhi barabara ya kutokea Mbogwe kuititia Bukoli kwenda mpaka Bujula kuwa barabara ya Mkoa ninaishukuru sana Serikali na naipongeza kwa hatua hiyo niombe sasa mwaka huu barabara hii ianze kutengenezwa vizuri ili wananchi waweze kunufaika zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusiana na suala la mawasiliano. Mawasiliano ni jambo la msingi na ni suala muhimu sana kwa ajili ya wananchi hasa waishio vijijini. Nitumie fursa hii kuiomba Wizara iangalie sana maeneo ya vijijini. Natambua kwamba Mheshimiwa Waziri alituambia tupeleke majina ya kata zote ambazo hazina mawasiliano ya simu. Na mimi nilipeleka majina ya kata mbalimbali ikiwemo Kata ya Nyamalimbe, ikiwemo Kata ya Bujura ambazo zina matatizo makubwa sana ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitumie fursa hii kuiomba Serikali iangalie maeneo haya. Najua kibashara pengine hayalipi sana, lakini kwa kuwa kuna Mfuko ule wa *UCAF* naiomba Serikali iwekeze zaidi vijiji kupeleka mawasiliano ili hatimaye kuimarisha zaidi wananchi waweze kufanya kazi zao kwa mawasiliano. Tunatambua mawasiliano ni kitu muhimu. Kupitia mawasiliano tunarahisisha biashara mbalimbali na zinaweza kufanyika bila shida yoyote. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie sana katika suala hili la mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ziko kata mbalimbali ambazo zinahitaji mawasiliano kama ambavyo nimezitaja kwenye Jimbo la Busanda, lakini pia na maeneo mengine ya vijiji, kwani maeneo ya vijiji mengi yanahitaji mawasiliano ya simu ili kuweza kuimarisha na kuwezesha kustawisha zaidi hali ya uchumi katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natumia fursa hii kuiomba Serikali iwekeze zaidi katika Mfuko wa *UCSAF* ili hatimaye kuweza kuyafikia maeneo mengi ya vijiji ambayo yamekuwa na changamoto kubwa sana ya mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile katika upande huo wa mawasiliano napenda kuomba Serikali iangalie minara. Minara mingi ambayo imesimikwa katika maeneo mengi wanakuwa hawalipi kwenye vijiji wanapochukua yale maeneo kwa ajili ya kusimika minara. Kuna changamoto kubwa, watu wengi wanafuatilia sana, lakini hawapati haki zao. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie pia suala hili hasa wananchi ambao ni wanyonge ambao wame... (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lolesia Bukwimba. Mheshimiwa...

**MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Nashukuru sana kwa nafasi hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Bashe.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia katika hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Waziri. Nitaenda moja kwa moja katika hoja ya Bandari ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa uwekezaji umeorodheshwa na Serikali katika bajeti ya mwaka huu ambayo inamalizika 2018/2019 ikiwa ni mradi mkuu wa kielelezo ambao Serikali mlitaka kuutekeleza kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii. Mradi huu unajumuisha ujenzi wa bandari, lakini pia unajumuisha ujenzi wa viwanda. Eneo hili maalum la uwekezaji ni kichocheo kikubwa sana cha maendeleo ya nchi yetu, maendeleo ya viwanda na maendeleo ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa yale ambayo umeyasema kwa maana kwamba, umeendana kabisa na mawazo ambayo nilikuwanayo mimi kama Mbunge wa Bagamoyo. Imekuwa faraja sana kupata hao wawekezaji; China na Serikali ya Oman, marafiki zetu kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema. Lazima tutumie fursa hizi za marafiki ambao tumehangaika nao sana kwa miaka mingi ambapo sasa fursa hizi wanatumia watu wengine sisi hatuzitumii, ni muhimu sana tutumie fursa hizi.

Mheshimiwa Spika, China na Oman wamekubali kuwekeza jumla ya dola bilioni 10 ama takribani trillioni 23 za Kitanzania kwa ajili ya ujenzi wa bandari na ujenzi wa viwanda. Mwanzoni wamekubali kwamba watajenga viwanda vikubwa 190 vya kuanzia. Maana yake kwa ajili ya ujenzi huu, vitatoa fursa za ajira takribani 270,000.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa imefanyika na viongozi wetu na wataalam katika nchi hii, kwa miaka mingi iliyopita, tumeanza na mwaka 2012 ambapo *MOU* ilisainiwa, Machi, 2013 *Framework Agreement* imesainiwa; Desemba, 2013 *Implementation Agreement* imesainiwa; Oktoba, 2015

*Tripartite MOU imesainiwa; na Septemba, 2015 jiwe la msingi la ujenzi wa bandari limewekwa na Rais Mstaafu. (Makof)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Pande na Mlingotini wamejitolea ardhi yao kwa ajili ya maendeleo haya ya ujenzi wa bandari pamoja na viwanda katika hali ngumu sana, lakini wakasema potelea mbali acha tutoe maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana kwamba inavyoelekea sasa juhudhi hizi zote hazikuzaa matunda. Nimesoma ukurasa wa 99, aya ya 136 ya Hotuba ya Waziri, inaelekea kwamba bandari hii sasa haipo.

Mheshimiwa Spika, *China Merchant* wakati tunasaini *MoU* ya 2012 wamesaini pia *MoU* na nchi ya Djibout kwa ajili ya ujenzi wa bandari. Hivi sasa wameshajenga *multipurpose port* inayoltwa Doraleh kule Djibout. Bandari hii sasa inafanya kazi. Kama vile haitoshi mwezi Machi mwaka huu wamesaini tena na *China Merchant* ujenzi wa *Special Economic Zone* Djibout kwa mtaji wa dola bilioni tatu na nusu, takribani shilingi za Tanzania trillioni nane; kwamba, 2012 wamesaini kama sisi na wameongeza tena sasa hivi wanajenga *Special Economic Zone*.

Mheshimiwa Spika, kama vile haitoshi, katika kipindi hiki sisi tunaongea tangu 2012, *China Merchant* weamesaini na kujenga bandari Nigeria, Tin Can Ireland; wamejenga Lome, Togo; wamejenga Abidjan, Ivory Coast, wamejenga Colombo – Sri-Lanka.

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki cha miaka hii karibu saba sisi tunafanya maongezi, nchi tano nilizozitaja zimekamilisha maongezi. Djibout imekamilisha maongezi na wamejenga bandari, Nigeria wamekamilisha maongezi na wamejenga bandari, Togo wamekamilisha maongezi, Ivory Coast wamekamilisha maongezi, Sri-Lanka wamekamilisha maongezi na wamejenga bandari isipokuwa Tanzania tumeshindwa kwa muda wote huu kukamilisha maongezi. Tuna tatizo gani? Tuna shida gani? (Makof)

Mheshimiwa Spika, wataalam wa nchi hizi tano nilizotolea mfano ni bora zaidi wanaweza wakakamilisha maongezi isipokuwa sisi nchi yetu ya Tanzania haina wataalam wa kuweza kukamilisha maongezi.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani 2025 nchi hii kuwa nchi ya uchumi wa kati ni miaka sita ijayo. Hatuna muda tena hata kidogo wa kusubiri katika jambo hili. Mtaji wenyewe una wakati, kwa sababu sasa hivi China wanatekeleza mradi wao wa *Belt and Road Initiative* nao uko *time bound*, tukiuchacha huo maana yake watakwenda kuwekeza mahali pengine. Huwezi kupata mtaji mkubwa kama huu unashiriki nchi moja tu ifanye maongezi miaka saba haikamiliki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, atakapokuja Mheshimiwa Waziri, kama ulivyoweka msisitizo, atuambie kwa kina. Tanzania tuna wataalam, Watanzania ni mahodari, Watanzania hatuna fani ambayo iko nyuma. Haiwezekani nchi hizi zikaweza kukamilisha, bandari zikajengwa, sisi tunaendelea kuzungumza kila siku. China wana usemi wao, maneno matupu ni hatari kwa Taifa. Na sisi tunataka kukumbatia kuzungumza tu na kuzungumza tu na kuzungumza tu kila siku, tutaliangamiza Taifa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Hussein Bashe, utafuatiwa na Mheshimiwa Charles Tizeba na Mheshimiwa Saada Mkuya atafuata, dakika saba saba.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa na vilevile nikushukuru kwa dhati kabisa kwa maamuzi uliyofanya ya kuchangia kuhusu Bagamoyo. Ni jambo muhimu sana. *Investiment ya Special Economic Zone ya Bagamoyo ilikuwa inatuletea inflowya 10 billion US Dollars* kwenye uchumi wetu na ni jambo ambalo ni vizuri Serikali wakati Waziri anakuja kufanya *wind-up* watueleze kinagaubaga kwa nini mradi huu unashimama?

Mheshimiwa Spika, nataka niongelee *SGR*. Kumekuwa na mjadala mkubwa sana na *last week* kulikuwa kuna mjadala mkubwa hapa ndani ya Bunge kwamba mradi wetu wa *SGR* kwa nini hauonekani kama unatuletea *impact* na mzunguko wa fedha kwenye uchumi?

Mheshimiwa Spika, nilitaka nije niombe kwamba wakati Waziri anakuja kufanya *wind-up* na hasa Waziri wa Fedha, *the financing model* ya *SGR* ya Dar es Salaam – Makutupora: Je, itaendelea kuwa hiyo hiyo *model* ya *financing* kutoka Makutupora kwenda Tabora; Tabora – Mwanza, Tabora – Kigoma, Uvinza – Msongati? Kwa nini nasema hivyo?

Mheshimiwa Spika, *the financing model/tunayofanya, which is very good*, mimi sipingani nayo katika hatua hii ya awali, kwamba tunatumla fedha zetu kujenga reli hii. Sioni kama tukiendelea hivi mpaka mwisho itatusaidia ndani ya uchumi wetu. Kwa sababu tunakusanya shilingi na tunapomlipa huyu Mkandarasi ni *ratio* ya 65:35. 35% ya fedha zake analipwa kwa shilingi. 65% analipwa kwa dola.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kinachotokea ni kwamba shilingi inakuwa *converted into dollar*, halafu dola analipwa Yapi nje, halafu Yapi anarudisha ndani dola ai-*convert into shilling* kuwalipa *local contractors*. Kinachotokea ile process ya kuhamisha shilingi kwenda kwenye dola *there is a cost*, kwa sababu *we are losing money in that process*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili kuna tatizo kubwa la Mkandarasi wa Yapi kulipa *local contractors*. Hili nalo ni tatizo, ni vizuri Wizara ikaliangalia. Hili ni jambo muhimu sana. Tuangalie *financial model* ya ku-*finance* mradi wa *SGR* kuanzia Makutupora kwenda mbele ubadilike. Bila hivyo, uchumi utaendelea ku-suffocate.

Mheshimiwa Spika, sitaki kujadili takwimu za *IMF*, hizo ni kazi za zao, lakini ninachotaka niwaulize, ukiangalia *trend*, toka mwaka 2014 *construction sector in general*, 2014/2015

ili-grow by 16.8%, leo ina-grow katika wastani wa asilimia 13. *What is the problem?* Shida ni nini wakati tunapeleka fedha nyingi sana za *development budget* kwenye *construction sector*? Kuna nini? Hili ni jambo ambalo lazima tuijulize Serikalini.

Mheshimiwa Spika, tuangalie *2014 to date, average growth* yetu ya *GDP* ni asilimia sita *point something*, imekuwa namna hiyo mpaka leo. Kuna nini wakati tunapeleka fedha nyingi sana kwenye *construction*? Hili ni jambo moja.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka nitoe ushauri, Mheshimiwa Waziri Kamwelwe, *TRC* wako pale, washauriane hili. Sisi tunajenga *SGR* kwenda Mwanza. *Our cash cow* kwenye reli ni mizigo na ni nchi ya Uganda, Congo, Zambia na Malawi.

Mheshimiwa Spika, nashauri, *TAZARA* inasuasua, *TRC* ikodi *infrastructure* ya *TAZARA* halafu wanunue *wagon* kwa ajili ya kuhudumia Zambia na Malawi. Wakati huo tutakuwa tunalipa *fee* kwa kutumia *infrastructure* hiyo, *TRC* wanunue mabehewa na vichwa ambavyo vinaweza kupita kwenye reli ya *TAZARA* ili wabebe mizigo ya Zambia na Malawi, tutapata *revenue*.

Mheshimiwa Spika, la pili, leo sisi tunataka kumpelekea huduma Mganda ambaye ana-*constitute* asilimia 30 ya mizigo wetu. Tujenge kipande cha *Port Bell* kwenda Kampala ambacho ni kilometra 11, tuweke meli kubwa, mizigo utoke Dar es Salaam mpaka Mwanza, uingie kwenye hiyo meli kubwa ibebe mizigo tipeleke *Port Bell*. Tutakuwa na *competitive age*. Kinachotokea, tunaye-*compete* naye leo ambaye ni Mombasa anamjengea bandari kavu Mganda, Naivasha ili kupunguza *distance* iliyoko ambayo sisi kwetu ni *competitive age*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la tatu, kwenda Msongati ni kilometra 200, ninawashauri achachenii na reli ya kwenda Rwanda, wekeni fedha kujenga Msongati kuja Uvinza. Tujenge kwa *SGR*. Tukijenga kwa *SGR* kutoka Msongati kuja

Uvinza mzigo utabebwa kutoka Msongati kuja Uvinza kwa *Standard Gauge*. Kutokea pale tutatumia *meter gauge* kuja Dar es Salaam. Kwa hiyo, tutaanza kupata fedha kabra ya reli kufika Mwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la nne, *we only have 30 kilometers* kuhudumia *Eastern Congo* ambayo ina *population* ya *22 million people*. Ushauri, shaurianeni na Serikali ya Congo tufanye *joint effort* tujenge gati upande wa Congo tuweze kubeba mizigo kutokea Kigoma kwenye meli kubwa tuvushe kwenda Kalemie ili tuanze kuwahudumia hawa wakati tunasubiri *ku-generate revenue*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *this is a question of where to get money*. Kwa nini nasema hivi? Leo Mozambique wamejenga reli kwenda Zambia, ill...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Bahati mbaya dakika saba ndiyo hizo.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Spika, naomba Serikali waangalie maeneo ambayo wanaweza kupata fedha. Ahsante, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mjadala huu unaisaidia sana Serikali katika kupata mawazo mbalimbali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge ni wajibu wetu kushauri. Kwa hiyo, tutumie fursa hii vizuri.

Mheshimiwa Spika, nilimtaja Mheshimiwa Saada Mkuya na Mheshimiwa Tizeba. Tuanze na Mheshimiwa Saada. Baada ya Mheshimiwa Tizeba, Mheshimiwa Turky.

**MHE. SAADA SALUM MKUYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Naunga mkono hoja na nitakwenda kwenye maeneo mawili matatu *specifically*.

Mheshimiwa Spika, kwanza naanza na Shirika letu la Ndege, *Air Tanzania*. Naipongeza sana Serikali kwa uamuzi huu ambao umekuja kuwa *implemented* katika awamu hii, lakini tumeanza mazungumzo muda mrefu na tumeanza mipango ya kufufua hili shirika katika awamu zilizopita. Mkurugenzi Mkuu wa shirika anafanya kazi nzuri, lakini tunaomba aangalie utaratibu mzuri zaidi wa kupunguza *unnecessary delays*, hususan katika safari ambayo tunafanya kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ukipanda ndege mara saba, nadhani mara tano tunapata *delays*; na tunaambiwa mara nyingi kwamba kunakuwa kuna *operational problems*, lakini kunakuwa kuna *delays*. Kwa hiyo, hiyo kidogo inapunguza ufanisi wa shirika letu la ndege. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kiukweli ni kwamba shirika hili ni la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini toka kuanzishwa shirika hili hatujawahi kuwa na Mjumbe wa Bodii anayetoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maana ya Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, asije akaniambia napandikiza, namwambia kwamba hakujawahi kuwa na Mjumbe wa Bodii na hili ni shirika letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nataka tu anijibu kwa nini hakujawahi kuwa na huyo Mjumbe wa Bodii na kuna matatizo gani hasa? Kwa nini asikuwepo? Lini atakuwepo Mjumbe huyu wa Bodii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, tunaipongeza sana Mamlaka ya *TCRA* kwa kuendesha zoezi hili la usajili wa *line* za simu. Hoja yangu kubwa hapa ni kwamba hili ni zoezi zuri na litatusaidia kama Taifa, hususan kupunguza uhalifu kwa njia ya mitandao, lakini wakati zoezi hili linaendelea, kitambulisho kikanachotakiwa ni kitambulisho cha *NIDA*. Kule Zanzibar wengi tuna vitambulisho vya Mzanzibari (*Zan ID*), hivi kwa nini *TCRA* haikubali mtu asajili *line* yake kwa kutumia *Zan ID* ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetumia pesa nyingi sana kuwekeza? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kule Zanzibar sisi huwezi kuishi, maisha yako hayatakwenda kama huna *Zan ID*. Sasa tukija kwenye *TCRA* ambayo tunajua ni Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa nini haitambui *Zan ID* kwa mtu ambaye hana kitambulisho cha *NIDA?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba atakapokuja Mheshimiwa Waziri atuambie ni kwa sababu gani *TCRA* haikubali mtu asajili *lineyake* kwa kutumia kitambulisho chake cha Mzanzibari ambacho kwetu katika miamala yote, katika matukio yote, katika kila unalofanya *Zan ID* lazima iwepo? Kwa hiyo, naomba hilo lizingatiwe na tuje kupata majibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, tunapongeza Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) kwa kuendelea kabisa kuona kwamba inatekeleza kazi zake kwa ufansisi. Kuna maeneo kadhaa ambayo katika mwaka 2019/2020 itaendelea kutekeleza ikiwa ni pamoja na kuendelea kutekeleza mradi wa kuanzisha vituo 10 vya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atakapokuja atuambie hivi huu mradi wa vituo 10 vya TEHAMA, wapi na wapi utatekelezwa na tuone kwamba kwa upande wa Zanzibar vituo hivyo vitajengwa wapi au vitatekelezwa wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusiana na ndege zetu hizi ndogo. Mara nydingi sisi wa visiwani tunatumia sana ndege hizi ndogo, lakini tunachokiona mara nydingi ni kwamba, badala ya kuwepo marubani wawili kunakuwa kuna rubani mmoja.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018 au mwaka 2017 wakati lilitokea tatizo kupitia ndege hii ya *Coast Airline*, nakumbuka Serikali ilitoa tamko kwamba, ni lazima tuhakikishe kwamba ndege zetu hizi ziwe na marubani wawili, lakini umekuwa utaratibu wa kawaida, hata kama tunapanda hizo ndege, tunatoka Dar es Salaam tunakuja Dodoma, rubani anakuwa mmoja.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaomba Serikali i-/literate yale mazungumzo yake ama tamko lake, tuone kwamba hizi ndege ndogo zinapunguza sana matokeo ambayo hatutarajii, lakini sababu isiwe kwamba kunakuwa kuna rubani mmoja. Hili jambo lipo na limezungumzwa, lakini sasa hivi naona linatoweka na halipewi msisitizo ambao unahitajika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *otherwise nashukuru sana kwa kupata nafasi hii*. Naomba sana Bodi ya Shirika la *Air Tanzania* tuone Zanzibar na yenyewe inakuwepo. Nashukuru. (*Makof*)

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi nami ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwa sababu ya muda, mengine niliyopanga kusema nitaya-*skip* na nijikite katika mambo matatu hivi ambayo naamini kwamba yana umuhimu mkubwa Serikali kuyapima na kuona kama inaweza kuyafanya kazi kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, moja, ume-*pre-empty* mazungumzo niliyotaka kufanya ya Bandari ya Bagamoyo, lakini kwa vile na wewe uliamua kuchangia siyo mbaya. Bandari hii ndiyo itakayokuwa pekee ya kupokea mzigo utakaosafirishwa na *SGR*, Dar es Salaam haina huo uwezo. Amesema vizuri sana Mheshimiwa Ally Saleh kule, Bandari ya Dar es Salaam tutake, tusitake, hata tuki-*dredge* namna gani pale Magogoni, *turning base inayoweza kupatikana haiwezi ku-accommodate post panamasna forth na fifth generation* ya meli zinazotengenezwa sasa, lakini Bagamoyo ndiyo ilikuwa jibu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, haya mambo yaangaliwe upya tu, yaani tusifike mahali tukalikatia tamaa hili jambo. Naishauri Serikali yangu na naipenda, wafanye kuangalia upya suala la Bagamoyo haraka iwezekanavyo kwa sababu tutakamilisha ile *SGR*, hatutakuwa na mahali pa kushushia mzigo, tutaonekana kituko. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni Mfuko wa Barabara; Mfuko wa Barabara wameusema wengi katika kuchangia hotuba ya TAMISEMI, lakin mahali penyewe ni hapa kwa sababu *Act* ya Mfuko wa Barabara ipo chini ya Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na ule mgawanyo wa 70 kwa 30 umepitwa na wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitasema neno moja tu, mtu akiwa na matatizo ya mishipa ya damu, mishipa mikubwa huwa *hai-clot/haipati obstructions*, inayopata *obstructions* ni mishipa midogo midogo (*arteries*) na hiyo ndiyo husababisha kifo. Sasa sisi tuki-concentrate sana na barabara kuu tukasahau kwamba barabara kuu hazina maana kama barabara ndogo hazifikishi watu na mizigo kwenye barabara kuu na lenyewe hili tunakosea. langaliwe upya tu, waangalie kwamba kama sasa ni 50 au 60, 40 lakin kuna kila haja ya kuongeza fedha kwa upande wa *TARURA*; sasa hivi ilivyo *TARURA* haiwezi ku-function. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, nataka kuzungumzia watoa huduma wanaitwa *DSTV*. *DSTV* hawa wanatoa huduma kama ving'amuzi vingine, wanatoa huduma kama kampuni za simu, kama umeme na kadhalika. *Software* ya kumfanya mtu aliyelipia atumie kadiri anavyolipia zipo lakini ndugu zetu hawa wao wana-charge kwa mwezi, ukishalipia ile *subscription* hata ukafunga king'amuzi, baada ya mwezi ukienda kimekwisha unatakiwa ulipe tena. Sasa mimi sitaki kuuita wizi kwa sababu tunalipa kwa halali, lakin huo ni wizi. Hizi simu tuna-recharge vocha, mbona wao hawatuambii uki-recharge baada ya siku 5 imekwisha automatically, wao kitu gani kinashindikana kwamba nikiwa nimezima king'amuzi maana yake mita haisomi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nimemaliza hayo, naomba nizungumzie jimbo langu kidogo. Ukurasa wa 300 katika kitabu cha hotuba ya Waziri, imetajwa barabara ya Sengerema-Nyehunge-Kahunda. Hii barabara natarajia inapaswa kufanyiwa *upgrading* na siyo *feasibility study* na *detailed design*, namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie hayo maneno yaliyo kwenye mabano yanatofautiana na uhalsia

uliopo kwa sababu hiyo hatua ya *feasibility study* na *detailed design* imekwishapita na huku ameweka katika miradi kwa hiyo, hawawezi kurudia mradi huo ambao tayari umekwishakamilika. Naamini ni *typo* tu, kinachotakiwa hapa kuwepo na naomba hili katika kuhitimisha anifafanulie yaani anihakikishie kwamba ni *upgrading* na siyo habari ya *feasibility study* na *detail design*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho; naomba kuzungumzia vivuko; nimesoma kitabu viro vivuko vinajengwa, lakini kuna kivuko cha Kome – Nyakalilo, zimeenda tume mbalimbali pale. Sitaki na mimi kubashiri vifo, ndugu yangu Mheshimiwa Mkundi alibashiri ajali kule Ukara na ikatokea, sasa mimi hayo maneno sitaki kuyasema, itoshe tu kusema kwamba hicho kivuko hakitoshi watu ni wengi. Kome leo ina watu karibia 120,000 wanavushwa na kivuko cha tani 35, ukiuliza kwa nini kivuko kingine hakijengwi? Fedha hakuna, fedha tunayozungumzia ni shilingi bilioni mbili au tatu, watu pale wakiteketea sijui nani ataulizwa.

Mheshimiwa Spika, nilimweleza Mheshimiwa Kamwelwe tulipokuwa Ukara kwamba hicho kivuko hakifai, Mheshimiwa Kwandikwa amefika mwenyewe; tume iliyoundwa na Serikali baada ya MV Nyerere kuzama imefika pale Nyakalilo, nimeshangaa kweli kwamba humu ndani hakuna mazungumzo ya eneo hilo, halafu nikisimama kupinga bajeti nionekane mkorof? (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana, usipinge bajeti inakutosha Dkt. Tizeba, Mheshimiwa Waziri ataangalia hayo maneno. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Salim Turky atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Magereli, Mheshimiwa Mlinga na Mheshimiwa Zungu mjiandae.

**MHE. SALIM HASSAN TURKY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu hasa kwa kufikiria vitu vikubwa na katika vitu hivyo, hivi viwili ni vya kiuchumi kabisa na leo hapa mimi na

Mheshimiwa Bashe tunakaa pamoja lakini fikra zetu tofauti kabisa. Mimi nasema uchumi wetu tunatoka kwenye reli na kwenye ndege, tujipangeni; tunajipanga namna gani? Naomba sana, pesa ziko nje nje kwa kuendesha reli hii na ndege. Naomba Serikali itazame namna ya *ku-float bonds* katika *national* na *international market*. Tukitoa share hizi tukaziweka katika stock exchange yetu, tayari watu watanunua *shares* *shareholders* ndio pesa unazipata haraka haraka. Tena hili litakuwa na nguvu zaidi hata kesho Mheshimiwa Rais akimaliza muda wake maana yake sasa tunaingia *partnership* ya *private* na *Government*, tupo pamoja sasa. Kwa hivyo, hata ile *management* kesho itasimamiwa vizuri sana, mambo haya makubwa hayatofeli maisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, naomba sana hili tulipokee kwa nguvu zote Mheshimiwa Waziri alifanyile kazi. Halafu reli ni moja ambayo haina hata mshindani, *Government* peke yake, ni *monopoly* yao, hakuna mtu anayeweza akajenga reli. Kwa hivyo, hii naamini akisema kesho tu atawapata *shareholders* sisi wengine wote humu tutanunua *shares* na watu wa nje wengine watakuja watajiunga pesa nje nje, hilo tumemaliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili; nashukuru sana bandari inafanya kazi vizuri sana hasa ninavyozungumza Bandari ya Dar es Salaam pale, lakini kuna kitu ambacho kinatakiwa kiboreshwé, nacho ni mizigo inayotoka Zanzíbar. Bainá ya Bara na Zanzíbar ni biashara ya tangu mababu na mababu, japo siku hizi imepewa majina ya ajabu ajabu lakini huwezi ukaamini ukweli kwamba Zanzíbar ni kisiwa cha biashara na biashara hii itadumu sisi kama tupo hata tukiondoka naamini biashara hii itaendelea.

Mheshimiwa Spika, pale Dar es Salaam sasa hivi kuna *congestion* kubwa sana sana ya mizigo ya Zanzíbar, nashukuru kwamba tumetoa ushauri kwa bandari kulikuwa na banda lilijengwa ukuta, namshukuru sana pale *Port Director* tumempa ushauri na ameufanyia kazi mara moja na jana nimepigiwa simu kwamba upo ukuta wa batí pale

wa kuweka magari ya godauni umeshaondoshwa na watu wanashusha mizigo yao. Hata hivyo, bado kuna ukiritimba mmoja mkubwa sana ambao unafanyakia; nao ni kwamba kuna ZFA, TBS na TRA wanagongana pale, mizigo haitoki ndani ya *warehouse*. Naomba hili lisimamiwe kwa nguvu sana chini ya bandari yake kwa sababu hawa wote hawana ofisi isipokuwa yeye mwenye bandari ndiyo anawakaribisha mle. Kwa hivyo, wakubwa wa bandari waangalie hilo na walismamie kwa nguvu zote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, la tatu; Mheshimiwa Rais wetu anataka nchi hii ikue kiuchumi, mimi nashangaa sana mnapokuja na mawazo ya kudumaza uchumi kwa kusema mtu mmoja awe na *line* moja ya simu au *line* mbili za simu, akitaka ya pili apate kibali; vitu hivi vya ajabu vinatoka wapi jamani? Huu uchumi leo sisi tunao *mobile operators* karibu watano kwa sita, kila mmoja anataka aingle sokoni; hapa kuna ajenda gani? Tunataka kumpandisha mtu mmoja, kama ilikuwa wana nia kila mtu awe na simu moja, basi hawa *operators* ilikuwa tuwanyime leseni hizo. Leo kila mmoja anataka soko, kwa nini anatubana tusiwe na simu?

Leo mimi nataka simu ya jimboni kwangu na ya ofisini kwangu; hizi ni simu lazima kila mmoja apewe uhuru wake, huwezi ukanibania mimi ooh uwe na laini moja, kwa nini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi uchumi huu unatakiwa ukue kwa kasi, huwezi ukabana hizi simu; simu nyininge mimi napokea simu za nje tu, sasa leo unaniambia aah usiwe. Hiyo nazungumza mimi kama Mbunge lakini kuna wafanyabiashara nje, wakulima na watu wote wanataka simu. Naomba hii sera ya kusema kwamba mtu mmoja laini moja, akitaka laini ya pili *special pass* sijui iende wapi, hiyo kitu inadumaza uchumi wa nchi hii. Naamini Rais akilisikia hili, hawezi akalikubali hata siku moja, tutakuja kuumbuliwa hapa bora tujumbueni wenyewe, tujivekeni sawa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, baada ya haya, sina la zaidi ila naipongeza sana Wizara na naunga mkono hoja na pia

maendeleo yote yanatofanyika katika nchi hii nayapongeza kwa nguvu sana na naamini 2020 CCM itatisha sana. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Turky. Nilishakutaja Mheshimiwa Lucy Magereli.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi ya kuchangia. Naomba nianze kwa kueleza tatizo la kwanza kabisa la nchi hii kwamba ni matatizo yanayohusiana na sera na mipango. Tuna changamoto ya kupanga nini tunataka, tuna changamoto ya kuamua nini tutekeleze na tunapoamua kutekeleza basi ni kwa manufaa ya nani na kwa kipindi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali tuwe waangalifu sana nini tunapanga, nini tunatekeleza, kwa wakati gani na kwa maslahi ya nani. Tuangalie mipango yetu ya maendeleo na vipaumbele tuvipange kadri tunavyoweza kutekeleza. Tumekuwa na vipaumbele vingi kuliko uwezo wetu wa kutekeleza, badala yake tunakuwa na orodha ndefu sana ya miradi ambayo hatuwezi kui-fund, tunatumia mikopo kutoka nje, pesa zinaingia kwenye miradi mikubwa, hiyo miradi haikamiliki, haiondoki ilipo wala haitunufaishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni huu wa Bandari ya Bagamoyo ambayo watu wengi wamezungumzia, ukurasa wa 99. Ziko kazi nydingi sana ambazo zimeshafanyika pale na pesa nydingi sana za walipa kodi zimeingia pale, leo yanakuja maelezo mepesi kweli kweli yanayosema eti wameshindwa kuelewana majadiliano na wawekezaji, ukurasa wa 99, naomba ninukuu inasema:

*"Mradi umeshindwa kwa sababu wawekezaji hao kuweka masharti yasiyokuwa na maslahi kwa Taifa, masharti hayo ni pamoja na wawekezaji hao kudai kuachiwa jukumu la kupanga viwango vyta tozo na kutoruhusu wawekezaji wengine katika eneo la kati ya Bagamoyo na Tanga."*

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ambayo yangeweza kujadiliwa, haya ni maelezo ya kitoto kabisa kwamba eti tumeahirisha utekelezaji wa mradi wa Bagamoyo kwa sababu eti wawekezaji wameweka masharti, hatuna wataalam wa kujadili mambo hayo? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nishangae pia kwamba sasa Serikali inarudi kushika hatamu za huduma za kimiundombinu wakati ni kati ya eneo ambalo lingeweza kuvutia wawekezaji na ni miradi ambayo ingeweza kutekelezwa kwa mfumo kama alivyosema Mheshimiwa Turkey hapa aidha wa hisa ama kupata wadau na wachangiaji wengine katika maeneo hayo ili kuboresha huduma zetu za kimiundombinu ili moja, tuweze kutanuka, lakini pili, tutoe huduma, tatu, tuweze kutoa ajira. Kwa nini Serikali sasa ndiyo mmiliki wa *SGR*, ndege za Serikali, Serikali ndiye sasa hivi mjenga *Stiegler's Gorge*, kwa nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye danadana za *ATCL*. Mwaka jana nilisimama nikashauri, nikasema miaka michache ijayo *of course* nilitaja mitano, nafurahi kwamba hata hatufiki mitano tunakaa tena hapa leo kujadiliana namna ambavyo *ATCL* haisaidii nchi hii, haipigi hatua na imeshindwa kabisa ku-perform. Nilishauri kwamba tuanje kwanza na kuimarisha mtandao wa ndani wa ndege, mpaka sasa hivi hatua zilizochukuliwa ni dhaifu mno. Tunang'ang'ana kufikiria kwenda Uchina kuchukua abiria katika mipango ambayo siyo ya kudumu, si endelevu na wala haitaisaidia nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ndege ambazo tumezinunua tulizinunua kwa maana ya lengo la kufufua *ATCL*, lakini kwa bahati mbaya hizo ndege zilipewa Wakala wa Serikali na sasa hivi tunavyozungumza kwa bahati mbaya nyingine tena, ndege hizo zimehamishiwa Ikulu. Sasa sielewi kwamba Ikulu imedhamiria kufanya biashara na bahati mbaya nyingine zaidi ni kwamba bado suala la ndege za Serikali tunazipa fedha kuitia bajeti ya *Vote 62* lakini zinakwenda kuhudumiwa na *Vote 20*; pana kizungumkuti hapo tunaomba Waziri mhusika atatusaidia kuchambua jambo hilo ni kitu gani.

Mheshimiwa Spika, nirudi Dar es Salaam; suala la msongamano wa Dar es Salaam ni mkubwa, imekuwa shida na tabu. Sasa hivi Dar es Salaam mvua inanyesha ninyi nyote ni mashahidi, ule mji hautembe. Mradi wa mwendokasi tuliofikiria kwamba ungetupa suluhisho nao umekuwa shida, umekuwa tatizo sugu; mwendokasi hau-*perform*, lakini kibaya kuliko vyote kumekuwa na changamoto ya ununuzi na uuzaaji wa tiketi. *Scanner za pale hazifanyi kazi kwa hiyo, pesa zinatolewa na kuhifadhiwa kiholela na sijui zinakuwa reported namna gani.* (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kingine kibaya kuliko vyote, sasa hivi pale kwenye mradi wa mwendokasi hakuna chenji, ukidai chenji ya 200, 150 hupati. Kwa hiyo, kuna makusanyo mengine ya mapato yamezaliwa pale katika mradi wa mwendokasi na kuwanyang'anya wananchi na abiria wa Dar es Salaam fedha zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ujenzi wa gati na maegesho eneo la abiria *Ferry* ya Kigamboni. Mwaka 2016/2017 na mwaka 2017/2018 tulizungumza, tukalipangia fedha na 2018/2019 vilevile, lakini mpaka ninavyozungumza hadi leo pale *Ferry* ya Kigamboni hakuna kinachoendelea, abiria wetu bado wanarundikana kama mizigo, utaratibu wa huduma kama vyoo na huduma nyingine pale bado haujakamilika, utaratibu wa utoaji magari ndani ya vivuko na kuondosha eneo la *ferry* na kuingia bado ni changamoto.

Mheshimiwa Spika, kibaya kingine sawa kama ilivyo kwenye mwendokasi na zile *scanner* za tiketi pale *ferry* nazo hazifanyi kazi, kwa hiyo, sasa hivi tiketi unanunua inapita bure ikiwezekana yule anayekusanya akaamua kuzirudisha tena kule zikauzwa upya, zinauzwa upya; hicho ni chanzo kingine cha wizi wa fedha za Watanzania kupitia ule mradi wa malipo ya *ferry* pale Kigamboni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Mwaka 2016/2017 tuliwapa jumla ya asilimia 40.3 ya fedha zote za maendeleo sawa na shilingi triliioni 11.8, mwaka 2017/2018 tumewapa asilimia 40.8, mwaka 2018/2019

tumewapa asilimia 34.8, lakini bado unaweza kuona kabisa kwamba Wizara hii hajaleta matokeo tarajiwa ukilinganisha na kiasi cha bajeti kubwa ya maendeleo tunayowapatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante ingawa nilikuwa na dakika kumi, umenipa pungufu ya hapo. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana, mbio mbio kidogo; Mheshimiwa Mlinga atafatiwa na Mheshimiwa Zungu dakika tano tano.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nianze na barabara ya Kidatu – Ifakara; barabara hii ilizinduliwa tarehe 5/5/2018, tulizindua nikiwemo na mimi na Mheshimiwa Waziri na Wabunge wote wa Morogoro. Rais alizindua ujenzi na barabara ikaanza kujengwa, lakini baada ya muda mfupi mkandarasi akaondoa vitu *site*; mpaka sasa hivi ninavyoongea ni mwaka mmoja sasa barabara hii hajawekwa hata kilometra moja ya lami.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alitoa mwongozo kwa Wizara ya Fedha na Wizara ya Ujenzi watatue tatizo la mgogoro wa kikodi wa VAT lakini mpaka leo hii Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Ujenzi wanaogopana kama mtu na baba mkwe wake. Mheshimiwa Rais ameshawaambia wakae watatue huu mgogoro lakini wanaogopana; kama wameoleana si wamwambie Mheshimiwa Rais awahamishe Wizara waje Mawaziri wengine watatue huo mgogoro kama wao wanashindwa? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la pili, ni barabara ya Ifakara – Mahenge. Barabara hii ina urefu wa kilometra 74. Sasa hivi Ulanga tuna *deposit* kubwa ya *graphite* na kuna kampuni kubwa tatu tayari zimeshaanza uwekezaji na kwa mwaka tutatoa tani zaidi ya laki tano.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya barabara ile hii biashara haiwezi ikafanyika. Endapo barabara hii itakuwa tayari Serikali ina uwezo wa kuingiza zaidi ya shilingi bilioni

400 kwa mwaka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wakati ana-*wind up* atuambie mkakati uliofikiwa kwa ajili ya barabara hii.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ni ya Liwale – Ulanga. Ukiacha ahadi ya Mheshimiwa Rais, ni mkakati wa Serikali kuunganisha barabara za mikoa na ni muhimu sana katika uchumi wa Wanaulanga. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atuambie amefikia wapi kuhusiana na ujenzi wa barabara hii umefikia.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la viwanja vya ndege. Naipongeza Serikali kwa umalizaji wa *Terminal* / / / lakini wasisahau na viwanja vingine kwa vifaa, maana tumeshuhudia ndege zikisukumwa na watu. Bahati mbaya ikatokea wafanyakazi wa *airport* wakawa na miili kama mimi watasukumaje hizo ndege? (*Kicheko*)

Suala lingine ni uhalifu wa mitandaoni, hii naongelea kuhusu *TCRA*. Uhalifu wa mitandaoni umegawanyika katika sehemu tatu: Udhgilishaji, wizi na upotoshaji.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia udhalilishaji mkubwa na *TCRA* wamekuwa wakikaa kimya. Wameanzia kwa viongozi wa siasa sasa hivi wamekuwa wakitengeneza picha za ngoni za viongozi wa dini. Hali imekuwa mbaya na *TCRA* wamekaa kimya.

Mheshimiwa Sika, suala lingine ni la wizi wa mitandao. Wizi huu makampuni ya simu yanahuksika. Tumeona meseji za tafadhali tuma pesa kwenye namba hii, waganga feki, unaweza ukatumiwa meseji ukaambiwa mtoto wako ameanguka shulenii, hizo meseji ni za uongo. Meseji nydingi zinatoka Kampuni ya Vodacom na baada ya uchunguzi wangu nikakuta wafanyakazi wanahuksika.

Kwa hiyo, makampuni ya simu walipeni vizuri wafanyakazi wenu na wekeni mfumo ambao mtaangalia hawa wafanyakazi wasiwe wanashiriki katika wizi wa mitandaoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na taarifa nyingi za upotoshaji. Taarifa hizi nyingine zinatolewa na Wabunge wakiwa wanapotosha taarifa za Serikali katika mitandao na wanafahamika lakini *TCRA* wanashindwa kuwachukulia hatua. Naomba suala hili lishughulikiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la *ATCL* na nitaongelea kwenye nauli. Nauli za *ATCL* zimekuwa kubwa tofauti na matarajio ya Watanzania. Kwa mfano, kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam nauli hadi Sh.600,000. Sasa mimi nakuwa nimepanda nalipa nauli au nimekodisha ndege? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, napenda kuongelea usafiri wa Noah. Enzi zenu kipindi hicho kulikuwa na mabasi tu, sasa hivi kuna usafiri wa Noah ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa. Sasa hivi kuna Noah zaidi ya 16,000 zinasafirisha Watanzania zaidi ya milioni 115 kwa mwaka. Hizo Noah 16,000 zimeajiri makondakta na madereva 32,000. Ukichukulia kila kondakta mmoja na dereva mmoja akiwa anahudumia watu wanne, kuna wananchi zaidi ya 128,000 wanahudumiwa na watu hawa. Bado wanalipa kodi, *TRA*, *SUMATRA*, bima na wanatumia mafuta lakini kumekuwa na sintofahamu ya hawa madereva wa Noah na huu usafiri wa Noah Serikali imekuwa ikiwasumbua hasa *SUMATRA*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, siungi mkono mpaka niambiwe suala la *VAT* linaishaje.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Zungu, dakika tano.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa dakika hizo.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajielekeza kwenye masuala ya *infrastructure* na hasa Bagamoyo kama ulivyosema wewe na baadhi ya Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwako, sasa hivi lazima tuwe na *new thinking* kwenye *economic corridor* nchini Tanzania. Bila kuweka *new thinking* tutaendelea kuwa waoga wa kufanya maamuzi, kutoa ushauri na kuirudisha nyumba hii. Uzalendo haimaanishi kukataa kila kitu, lazima tuwe na *calculated risk*. *Risks* hizi zinapimwa na zinaweza zika-work Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwako; *negotiating team* hii ya Tanzania ipate fursa ya kuja kwenye Bunge lako, ikae na Wabunge wajaribu ku-*brainstorm* na kusaidia nchi yetu iweze kwenda mbele na hasa kwenye mradi huu wa Bagamoyo. *Infrastructure* za nchi nydingi sana zimeendeshwa na *gold backed currency*; *deposit* ya *gold* na baadhi ya madini nchini mwetu yanaweza kutumika ku-*fund infrastructure* katika nchi yetu. Naomba wataalam wa nchi yetu watazame suala la *gold backed currency* ili kuweza kujenga taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napongeza watendaji wa Serikali, nampongeza Waziri, naipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mchango wangu ulikuwa ni huo tu, Bunge lipate nafasi kukaa na *team inay-negotiate* Bandari ya Bagamoyo ili tupeane taarifa mbalimbali na *tu-move this country forward*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa kuchangia kwa kifupi kabisa, ni mchango mzuri sana.

Tunaendelea na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, dakika saba, ajiandae Mheshimiwa Charles Mwijage.

**MHE. MOHAMED O. MCHENERWA:** Mheshimiwa Spika, ni aibu kubwa sana kwa taifa hili kuwa na wanasheria ambao wanafanya *negotiation* kwa miaka saba. Hii inadhalilisha sana wanasheria hapa nchini au wale wote ambao wapo katika tume ya kufanya *negotiation* kuhusu ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi, uliunda Kamati ya Tanzanite hapa pamoja na Kamati ya Almasi. Wabunge walitumia miezi mitatu tu kuishauri Serikali na kufanya marekebisho katika mikataba ambayo ilikuwa ni mibovu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia matakwa ya Ibara ya 63 ya Katiba na marekebisho ya sheria tuliyoyafanya mwaka jana ambayo yanalipa mamlaka Bunge kupitia mikataba mbalimbali, nikuombe unda Kamati. Kama tatizo ni mkataba kwenye suala zima la Bandari ya Bagamoyo, unda Kamati, Wabunge wako vizuri, hatutatumia miaka saba. Tunahitaji miezi miwili, miezi mitatu na tutaishauri Serikali na pengine tutawaita wahusika. Kama mkandarasi anayejenga hana uwezo, basi tutafute mkandarasi mwagine ambaye atahusika na ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo ikizingatiwa kwamba bandari hii ni muhimu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, anguko kubwa la kiuchumi la watu wa Pwani limetokana na ubovu wa miundombinu. Wewe ni shahidi, Pwani ya Kusini, kuanzia Mkuranga, Kibiti, Rufiji na Kilwa miaka 700 iliyopita walikuwa na uwezo wa kutengeneza *coin* yao. Juzi katika Pwani ya Australia wameokota *coin* ambayo ilitengenezwa Kilwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi, tumekwenda pamoja Russia, tumekutana na wananchi wa Fiji, wao wanasema walitokea Rufiji, Pwani ya Tanganyika ambako ndiko kunatokea Nyamisati na maeneo mengine. Wewe ni shahidi tulikuwa pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Pwani siyo goigoi bali tatizo kubwa tulilonalo ni miundombinu mibovu. Iwapo

miundombinu itaboreshwa, Pwani ya Kusini tutaweza kulisha Tanzania hii.

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi ulikuwa Kingupila na Ngarambe, Rufiji kuna viwanja vya ndege vitatu, ndiyo wilaya pekee hapa nchini ambayo ina viwanja vya ndege vya kutosha. Mkoloni asingejenga viwanja vya ndege kama eneo hili lilikuwa halifai kiuchumi. Kule Ngarambe kuna vipepeo mamilioni ambavyo duniani hakuna lakini watalii watafikaje Ngarambe, ubovu wa miundombinu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hali ya miundombinu imefanya Warufiji washindwe kuzalisha. Tunaona ni bora tulime vyakula vitakavyotufaa wenyewe kuliko kulima vyakula vingi ambavyo inatugharimu kusafirisha kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Machi, 2017, Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa barabara ya Nyamwage – Utete. Sitakuwa na mchango wowote iwapo nitashindwa kutaja barabara ya Nyamwage – Utete ambayo Mheshimiwa Rais aliahidi.

Mheshimiwa Spika, sisi wanasheria tunatambua, zipo ahadi wakati wa kampeni, ahadi hizi wakati mwingine zinaweza zisitekelezeke kwa sababu ni ahadi ambayo mtu anaahidi ili aweze kupata. Mheshimiwa Rais aliahidi 4 Machi 2017 kwamba barabara hii itajengwa. Mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, anakuwa Rais wa kwanza kujenga barabara hii. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi kwa kuridhia barabara hii ijengwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Warufiji wamechoka na maneno, tumebadilisha Wabunge zaidi ya tisa, mimi ni Mbunge wa tisa ukianzia Bibi Titi Mohamed, kule ni miaka mitano mitano na Wabunge wamehukumiwa kwa sababu ya barabara hii ya Nyamwage – Utete. Unaweza ukawa ni Mbunge mzuri sana, ukawa na mchango mzuri sana kama mimi lakini kama tutashindwa kujenga barabara ya Nyamwage – Utete, hatutoki. Katika sehemu ambayo kuna siasa, kule mtu

hajasoma darasa hata moja lakini ni profesa kwenye siasa, anayajua tusiyoyajua. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nimpongeze Waziri kwa kuridhia lakini kusema peke yake Warufiji wamechoka na maneno. Nimesema sana, Waziri anajua, nimekwenda sana ofisini kwake na ye ye ameridhia barabara hii sasa inakwenda kujengwa, Warufiji wanaomba kuona vitendo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameridhia sasa kufungua Pwani ya Kusini, tunakwenda kwenye utalii wa picha, tunakwenda kwenye mradi wa umeme wa *Stiegler's* lakini huko kote hatuwezi kufika kama barabara zetu hazitaboreshw. Barabara ya kutoka Kibiti - Mloka kama haitajengwa kiwango cha lami mradi wa *Stiegler's* utachelewa sana, pengine utachukua miaka kumi kukamilika. Kwa sababu ukarabati uliofanywa ambao Mheshimiwa Waziri ameuzungumzia kwenye kitabu chake hiki, ukurasa wa 15, ukarabati ule sasa hivi kutoka Kibiti - Mkongo unatumia saa nne, kilometra 15, niombe Serikali ukarabati barabara hii.

Mheshimiwa Spika, zipo barabara ambazo iwapo zitafunguliwa Pwani kutakuwa kuchele kwelikweli. Nikuombe barabara ya Kisiju - Mkuranga; Vikindu - Vianzi; Nyamwage - Utete nimeshaisema; Ikwiriri - Mloka, Mloka - Kisarawe, Mloka - Kisaki, Utete - Ngarambe, Kibiti - Mloka pamoja na Bungu - Nyamisati. Barabara hizi zikifunguliwa Pwani tutazalisha na tutailisha nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuna bonde kubwa lenye ekari zaidi ya laki tano ambazo hazijalimwa; watalimaje? Kutoa mazao kutoka shambani kupeleka sokoni tunatumia saa nane au kumi. Niiombe Serikali, kwa kuwa Mheshimiwa Rais amedhamiria kuifungua pwani, tuifungue pwani kwa kuboresha miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, katika ukurasa wa 15 amezungumzia barabara ya Chalinze,

*express way.* Mheshimiwa ndugu yangu, Mheshimiwa Serukamba, amesema sana, nimuombe Mheshimiwa Waziri...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa  
Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchengerwa. Nakushukuru sana kwa mchango wako, umenikumbusha mbali, kweli nayaelewa maeneo haya.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nikiwa kijana mdogo niko huko, asubuhi unafungua mlango saa 11.00, 12.00, unakuta mama mjamzito amewekwa hapo nje kwa sababu hawana usafiri wamehangaika naye tangu juzi, imeshindikana kujifungua na mimi peke yangu ndio niliyekuwa na *Defender*. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, unachukua watu wako mnaanza kumsafirisha yule mama kutoka Ngarambe kwenda Utete, mnatembea mnachimbua, hiyo gari inakwama kila mahali, mna sepetu, sululu, majembe mpaka mkimfikisha huyu mama basi Mungu amependa. Kwa hiyo, barabara ya Nyamwage kwenda Utete ukivuka Ikwiriri tu pale inakwenda *parallel* na Mto Rufiji, hiyo kweli ndiyo inang'oa Wabunge. Hii ya Mloka wala huna haja ya kuhangaika nayo maana lazima itawekwa lami tu kwa sababu ndiyo inayoelekea *Stiegler's*, kwa hiyo, tuombe Mungu, yote yanawezekana. (*Makofi*)

Nilishakutaja Mheshimiwa Charles Mwijage dakika tano, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu dakika tano.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia kidogo Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nikushukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake. Kipekee niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu ya Ijumaa na leo.

Mheshimiwa Spika, itoshe mimi leo kuchangia kwamba safari yetu ni kwenda kwenye uchumi wa kati, ulio jumuishi na ili kufika hapo lazima tujenge uchumi wa viwanda, siyo viwanda. Kuweza kujenga uchumi wa viwanda ni lazima tuwe na miundombinu wezeshi na saidizi. Kwa hiyo, Wizara hii ndiyo inayojenga miundombinu wezeshi na saidizi. Twaweza tusione leo hayo tunayoyataka lakini tunapokwenda kwenye uchumi wa kati nina imani hayo tutayaona. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo nalotaka kuzungumzia ni bandari. Watu wa bandari, sitzungumzia suala la Bagamoyo ila Mheshimiwa Ally Saleh, nikukosoe kidogo au nikupe taarifa, *Bagamoyo Special Economic Zone* itazalisha viwanda 1,000 na watu laki tano watapata ajira. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, watu wa bandari, kuna kiwanda cha Hengia cha Tanga kinachotaka kuzalisha tani milioni saba, nawaomba tukubaliane na wazo la kiwanda kile cha kupata access. Alipokuja Dangote akazalisha tani milioni tatu nchi nzima bei ilishuka, akiingia wa tani milioni saba mambo yatakuwa mazuri. Kama walivyosema wenzangu, twende kasi kwenye maamuzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, watu wa *TPA* niwaeleze kuhusu kitu kinaitwa *Port Community*. Tunafanya vizuri sana ndani ya bandari lakini wale wanaotusaidia, kwa mfano *TRA*, *TANROADS*, hawafanyi kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, nimewaeleza kwa maandishi kwamba ya nini kuweka mzani wa *TANROADS* Kurasini wakati unaweza kuweka mzani huohuo bandarini na wote wako chini ya Wizara moja? Ndiyo maana kunakuwa na foleni. Niwaombe watu wa bandari tuongeze kasi, tunafanya vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda nirudie tena; sisi Nacala na Beira si washindani wetu katika bandari, Durban si mshindani, tunatengeneza washindani sisi wenyewe. Yaani ni kama mtu unatengeneza mke mwenza, unashindwa kumhudumia uliyenaye mpaka analazimika kwenda nje kutafuta ushindani. Wanaokwenda Beira na Durban wamelazimika kwenda kule. Tukisawazisha *ease of doing business*, Nchi za Maziwa Makuu wanapenda kuja hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na rafiki yangu mmoja kwenye Serikali ya Kongo iliyomaliza muda, aliniambia wanaweza kutupa robo ya shehena walijonayo, Bandari ya Dar es Salaam haitapokea mzigo wa Tanzania au nchi nyiningine. Kama walivyozungumza tuitumie njia ya Kigoma tuweze kuvuta huu mzigo wa Mashariki ili uweze kuja lakini na Kigoma iweze kuchangamka ili hawa ndugu zangu waache mambo ya kulalamika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie *ATCL*, niwashauri watu wa Wizara hii tafadhalii Uwanja wa Ndege wa Bukoba uangaliwe. Bukoba tunahitaji uwanja mkubwa, hatuhitaji ndege nydingi, sisi shida yetu ni kupakia bidhaa za kwenda kwenye masoko makubwa. Mkoaa wa Kagera unamiliki sehemu kubwa ya Ziwa Victoria lakini viwanda vya samaki haviwezi kwenda pale kwa sababu ndege za mizigo haziwezi kuja pale Bukoba.

Mheshimiwa Spika, lakini niwapongeze *ATCL* hapo mlipofikia, mnachopaswa kufikia sasa ni kutengeneza soko kubwa, kuchangamsha soko na mimi nawaona Watanzania wanakwenda kule. Mnakumbuka kuanzia tarehe 19 Desemba mpaka Januari Bukoba mlikuwa mnapiga *trip mbili* kwa siku na ilikuwa inajaa.

Sasa ninachowashauri *ATCL*, nimekuwa nikiwaambia muende kwenye utamaduni, mtu akipanda ndege unamkaribisha kwamba karibu kahawa, unampa kahawa, unampa senene ili watu wapande ndege waweze kuzoea ndege. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sisi hatufanyi mambo ya *profit and loss*, hii siyo biashara ya maandazi, wazoeshe Watanzania ndege hata kwa kuwapa *free ride*, wapande ndege na wazipende ili tutengeneze soko kubwa. Haya mambo ya kuongeza *destination* watu wakishapanda ndege wakazizoea watapanda ndege.

Mheshimiwa Spika, kama alivyozungumza Mheshimiwa Kepteni Abbas, sitaki kuchangia, *competitive advantage* ya *Air Tanzania* ni soko la ndani.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa muda huo, mengine ntaleta kwa maandishi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, dakika tano.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, bila kupoteza muda, dakika tano ni chache sana, naomba nianze na suala la barabara ya Mogitu – Haydom – Sibiti. Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba itaiwekwa barabara hii lami kwa sababu tuna Hospitali ya Rufaa kule na watu wengi wa maeneo ya Hanang, Mkalama na hata Sibiti yenyewe wanakuja pale Haydom kupata huduma ya afya.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, kuna maeneo ambayo wakati mvua ya El-Nino iliponyesha, makorongo makubwa yalitokea na yakitenganisha shule na watoto au zahanati na wagonjwa. Kwa hiyo, naomba wasiachie Halmashauri tu, Wizara hii ya Ujezi nayo isaidie na namwambia Waziri kila siku.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, naomba ni-*declare interest* kwamba aliyesaini mkataba ule kuhusu Bandari ya Bagamoyo ni mimi wakati nikiwa Waziri wa Uwekezaji. Nataka niwaambie tulifanya hivyo kwa sababu ilionekana Afrika nzima Ukanda wa Pwani *the best place* ya kuweka bandari ni Bagamoyo lakini Bagamoyo si bandari tu, Bagamoyo ni *Economic Special Zone* ambapo kutakuwa na viwanda na miradi mingine minge ambayo itainua uchumi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana na mimi nisingesemea, mimi natoka Hanang huko hakuna bandari, lakini naisemea Bagamoyo kwa sababu kwa kweli ni mahali ambapo itasaidia sana na hii *SGR* itumike vizuri kuleta *economic change* kwenye Tanzania yetu na kwa kweli naombeni sana muangalie hilo na sisi Wabunge nimeshukuru sana Spika mwenyewe alivyosema na sisi wote tuwe pamoja, lakini sidhani kama hii Serikali wala inakataa, ina sababu labda kuchelewesha, lakini wajuje ya kwamba kwa kweli hapa ni mahali ambapo tukipapuuza tunapuuza kukuza uchumi wa nchi hii ulingane na tunachotaka baadaye.

Mheshimiwa Spika, ya mwisho Rufiji si mahali padogo ni mahali pa kubwa, babu yangu mimi alikuwa akipingana sana na wakoloni wakampeleka Rufiji wakamzika huko alipokufa, sasa na mimi nashindwa kwenda kuona lile kaburi la babu yangu, kwa hiyo tumsaidie Mchengerwa na yeye tuone umuhimu wa kuona eneo ambalo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaunga bajeti hii mkono na nina imani na Serikali hii kwamba wala haina shida na Bagamoyo, lakini wataona umuhimu wake na kutoa kipaumbele, ahsante sana, sana na Mungu akubariki. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mary Nagu kwa kweli ukweli ni huo *Bagamoyo is the grand, grand project*, si rahisi kupata *project* kama hiyo kirahisi. Mheshimiwa Elibariki Kingu kwa dakika tano, Mheshimiwa Hawa Ghasia tafadhali.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa dakika hizo tano, lakini mimi pia ninaona tu kwamba ninamshukuru Mungu kwa sababu ili la Bagamoyo mionganoni mwa nondo ambazo pia ambazo nilikuwa nimeziandaa nilikuwa nimejiandaa sana kuja kuchangia katika hii *project* ya Bagamoyo kwanza nikushukuru wewe binafsi kwa uzalendo mkubwa ambao umeuonyesha kulizungumzia hilo, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, mimi nakumbuka mwaka 2012 alipokuja Rais wa China kabla ya hapo Serikali hii ya Chama cha chetu cha Mapinduzi mwaka 2008 ili *hire consultant* ambaye alifanya kazi ya kufanya *feasibility study* wakaja na *recommendation* za ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo, lakini kama alivyosema mama yangu Nagu kipindi hicho mimi nilikuwa chini ya Wizara ya Viwanda nilikuwa nikifanya *fair competition*, Mama Nagu alikuwa bosi wangu, nataka nikuambie kitu kimoja *not only* kwamba hii Bandari ya Bagamoyo tunaizungumza hapa kwamba ilikuwa ina muhimu, lakini ilikuwa inakwenda kuwa the *biggest port in Africa*.

Mheshimiwa Spika, namba mbili Bandari hii ya Bagamoyo ilikuwa inakwenda kufanya *circulation*ya kuingiza makontena zaidi ya millioni 22 kwa mwaka ukilinganisha na Bandari ya Dar es Salaam, kwa wachumi waliokuwa wamefanya *feasibility study* pamoja na *consultant*, bandari hii ilikuwa inakwenda kuwa *hub* ya kuzifungua nchi ambazo ni *land locked* na mradi huu, nataka nikwambie ulikuwa unakwenda kuongezwa, wawekezaji hawa walikuwa wanakwenda kujenga *Standard Railway Gauge* ambayo ilikuwa inakwenda ku-connect kutoka Bagamoyo mpaka kwenye Reli ya TAZARA.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nikwambie ndugu zangu wa Serikali mimi ninawaomba hapa sisi kama Wabunge ni wawakilishi wa wananchi kwa maslahi ya hili Taifa, hatuwezi tukaja hapa Bungeni tukazungumza kwa lengo la kuikwamisha Serikali, nimesoma kitabu hichi, kinachozungumzwa ni kwamba inaonekana kwamba

mkandarasi sijui kuna mambo hayako kwa maslahi ya nchi, hatuwezi tukaishia hapo tu, tuangalie vipengele ambavyo vinakwamisha tuviondoe, mradi huu ukatekelezwe kwa maslahi ya hili Taifa.

Mheshimiwa Spika, leo Rais tayari Serikali yetu imeanza kujenga *Standard Gauge Railway* kutoka Morogoro - Dar es Salam kuja Dodoma, kama tutafanikisha mradi huu tayari hii Reli ya *Standard Gauge* itawenza kupata *access* ya kuwa *fade* na mizigo ambayo tutaichukuwa kutoka Bandari ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi kwa unyenyekevu mkubwa ninaungana na Wabunge wengine kuisisitiza Serikali *this is the grand project* kama Spika ulivyosema, tunaishauri Serikali ikakae iangalie wapi tumekwama mradi huu uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, la pili naomba niende jimboni. Katika jimbo langu la Singida Magharibi na Mheshimiwa Waziri nimeshakuona zaidi ya mara tatu mwaka jana watu wangu wa Kata ya lyumbu walivamiwa na majambazi saa tisa mchana, maduka yakaporwa kila kitu, watu wakakosa *access* ya kufanya mawasiliano hata polisi kuja kuwasaidia, hakuna minara ya mawasiliano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tumeletewa kitabu hapa na hili lazima tuliseme, Serikali Watanzania pia wanaona, msiwe manakuja hapa jamani wakati mwiningine mnatupiga longolongo tunapata shida huko, tuliletewa vitabu hapa vinavyoonesha takwimu za minara itakayokwenda kujengwa na makampuni ikiwemo *TTCL*, mpaka leo tunapozungumza, wale wananchi wangu mimi kutoka makao makuu ya Wilaya mpaka ufile Kiyumbu ni zaidi ya kilometra 190 hawana minara ya mawasiliano, makampuni ya *private* mmeyazuia, sasa tunataka *TTCL* ikuwe lakini *it must be competitive* ili tuweze kuwasaidia watu wetu.

Mheshimiwa Spika, la pili kwenye kitabu nimeangalia barabara inayojengwa kutoka Sepuka - Mlandala kwenda

Mgugila, ninaomba nimalizie hili kwa uchache sana, barabara hii nimeanza kuiona toka nikiwa Mkuu wa Wilaya ya Igunga mwaka 2012/2013; imejengwa madaraja yasiyopungua 40, ni mwaka wa kumi hii barabara Serikali wameshindwa kuipandisha/kujengea tuta la moramu, leo naangalia kwenye kitabu imeombewa milioni 90.

Mheshimiwa Spika, mimi naiomba Serikali wananchi hawa wa lyumbu, Mheshimiwa Waziri nimeshakufuata zaidi ya mara mbili.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ikungi asilimia 90 ya revenue inapata revenue kutokana na wakulima wanaotoka kwenye Jimbo langu Singida Magharibi kwa sababu tunazalisha mpunga na mchele kwa kiwango kikubwa, lakini wananchi hawa tumeshindwa kuwakamilishia ujenzi wa hii barabara *for ten years* madaraja yamejengwa. Mimi nasema safari hii sitaingua mkono bajeti ya Wizara hii kama sita pata majibu ya ujenzi wa barabara ya watu wangu kwa sababu watu hawa wamekuwa wakipata shida, nimekwenda *personal/kulizungumza* nimefanya njuhudi na sijapata majibu yoyote nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kingu, ahsante sana, nakushukuru sana na mimi sikusema yote kuhusu *China merchants*, lakini tutaendelea kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri na na kadhalika, hilo likampuni kwanzza ni likampuni la Serikali wala siyo *private company sorry to say*, ni Serikali ya China inaunda mashirika na hili ni shirika mojawapo na zile bandari kubwa tatu duniani ambazo zote ziko, China wana nne; tatu *Mainland China* na Hongkong; hizi tatu hizi ni *China Merchants plus the other* zinazoendelea.

Kwa hiyo, kupata uwekezaji wa bandari wa trilioni 23 iko maneno, hapa *negotiation team* yetu inabidi kwa kweli kama watakuwa hawa hawa kwenye miradi mingine haya. Mama Hawa Ghasia *please* atafuatiwa na Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa *Engineer Christopher Chiza ajiandae.*

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi nashukuru.

**SPIKA:** Dakika tano tano.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** ...kwa kunipa dakika tano nitajaribukukimbia kimbia.

Mheshimiwa Spika, ahsante niipongeze Wizara kwa kazi kubwa wanaofanya katika kuhakikisha kwamba miundombinu ya nchi yetu inaboreshwu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianzie jimboni kwangu ambako kwanza ningependa suala la barabara ya Mtwara - Msimbati - Madimba - Kilambo ambazo ni barabara zinazounganisha nchi yaani Tanzania na Mozambique ambayo ni sera yetu kuhakikisha kwamba barabara zinazounganisha nchi zinajengwa kwa kiwango cha lami, Mheshimiwa Waziri naomba utakapokuja kunijibu basi uniambie imefikia wapi suala la kujenga barabara ya Mtwara - Msimbati - Madimba - Kilambo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala la barabara ya kutoka Hiari -Nanguruwe ambayo ni mchepuko, sasa hivi kutokana na kiwanda cha saruji ambacho ni kikubwa sana magari yote yanayokwenda Newala hayapiti tena Mtwara yanatumia barabara hii tumeiomba Serikali, nimekuja kwako Mheshimiwa Waziri nimezungumza na Meneja wa *TANROADS* kuomba barabara hii ichukuliwe na Wizara kwa sababu inapitisha malori makubwa ambapo *TARURA* peke yake hawawezi kuijenga barabara hii ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri yangu tulikuwa tunajenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Kivukoni pale Msemo kwenda Msanga Mkuu, lakini barabara hii imekuwa na changamoto kubwa sana watu wa bandari wa Mtwara hawataki barabara ipite katika maeneo yao, sasa maeneo yote hata Dar es Salaam kuna barabara ambazo zinapita ndani ya eneo ya bandari na kule Msanga Mkuu ni

lazima upite katika bandari ndipo uweze kufika katika vijiji vyetu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aingilie kati kwa sababu barabara hii ilikuwa inajengwa sasa hivi imesimama kwa eti tu kwamba hatuwezi kujenga barabara ya lami kupita eneo la bandari eneo ambalo hata kuendelezwa bado alijaendelezwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba uingilie kati suala hilo.

Mheshimiwa Spika, tunayo barabara yetu ya kutoka Mpapura kwenda Kitere mpaka Mkwichi kule Mtama, naomba hii barabara inaunganisha mikoa, Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Mtwara kama kawaida tunaomba barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami kwa sababu ndiyo sera kuziunganisha kwa kiwango cha lami barabara zote ambazo zinaunganisha mikoa.

Mheshimiwa Spika, na mimi niungane na wenzangu kuzungumzia suala la Bandari ya Bagamoyo, hata wenzetu China walivyotaka kuendeleza nchi yao, walivyotaka kuanzisha maeneo ya *special economic zone* walianzia na China ya Mashariki ambako ndiko ambako wanapakana na bahari. Sasa kuanzia Djibouti mpaka tunafika kule *South Africa*, sisi hapa tulikuwa na nafasi kubwa sana ya kuwa na bandari kubwa ambayo itachukuwa meli za *four generation* ambazo zingeweza kuleta mizigo baada ya kufika pale ile mizigo sasa ndiyo ikawa inaenda kwenye bandari zingine za Beira, Mombasa, Dar es Salaam na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali yetu suala hili waliangalie kwa mtizamo mpana zaidi na hasa wakisikiliza na Wabunge michango yao pamoja na mchango wako.

Mheshimiwa Spika, na suala la mwisho ni suala la Reli kutoka Mtwara kwenda Mbambabay na matawi la kwenda Liganga na Mchuchuma. Tunategemea kuchimba chuma, kuchimba makaa ya mawe na alivyokuja Waziri wa Ujenzi alisema kuna *tender* ya kupeleka...

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia. Nilishakutaja Mheshimiwa Venance Mwamoto na Mheshimiwa Christopher Chiza ajiandae, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, kwa dakika tano tano.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niunge mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ndoto ya uchumi na viwanda haitawezekana bila kuwa na barabara, reli, mawasiliano, bandari na viwanja vya ndege na ndege zenyewe. Kwa hiyo mimi nishukuru, Mheshimiwa Waziri ujue kwamba unadhamana kubwa ya kututoa tulipo ya kutupeleka kwenye nchi ya uchumi ya viwanda, kama hutofanya vizuri kwenye Wizara hii/hamtofanya vizuri mjue kwenye hiyo ndoto ya kwenda kwenye uchumi wa viwanda itakuwa haiwezekani, kwahiylo mnatakiwa mfanye kazi kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, mimi niwapongeze baadhi ya sekta ambazo zimekuwa zikifanya vizuri, lakini sitaki kuchukuwa muda mwingsi kuchanganua hii kwa sababu muda nilliopewa ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, nirudi jimboni kwangu, ninapozungumza sasa hivi mvua zinanyesha, barabara zote zote zinakufa. Kwa hiyo, mimi niombe kitu kimoja kwamba kwa kuwa tunakubali na tumepitisha Sheria ya TAKUKURU wenyewe, sasa basi tuangalie uwezekano wa kutusaidia, kuna maeneo, kuna Wilaya na Mikoa ambayo ni ya kiuchumi, mikoa ambayo inachangia pato la Taifa kwenye nchi mojawapo ikiwa ni Kilolo.

Mimi nishukuru sana Mheshimiwa Rais alifika Kilolo mwaka jana, akaahidi kutujengea barabara na ninashukuru Mheshimiwa Kamwelwe tumekuwa tukiongea kila siku na umenihakikishia kwamba barabara hiyo itajengwa ya kuanzia Iringa Mjini kwenda Kilolo na bahati nzuri kwa heshima ya pekee tumeipa jina la *Engineer Mfugale* kama vile ambavyo

Mheshimiwa Rais ametoa daraja na sisi tumempa heshima ndugu yetu Mfugale kwanza anatoka Kilolo, lakini pia huwezi kuwa daraja bila kuwa na barabara, kwa hiyo, tumempa na barabara, kwa hiyo najua itajengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo na Mheshimiwa Kamwelwe pia kuna barabara tunategemea kukupa, kwa hiyo na wewe umeolea kule Iringa, kwa hiyo kwa heshima ya pekee lazima uhakikishe kwamba barabara ya Kilolo zinapatikana.

Mheshimiwa Spika, barabara za kiuchumi ni pamoja na Kongwa. Kongwa ni sehemu ambayo tumesema tutaweka maazimisho yote kule, kwa hiyo lazima ijengwe kama vile itajengwa Kilolo, kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa ile ahadi ya Rais usimwangshe na barabara ambazo ni barabara ya Mkoa kutoka Iringa - Dabaga - Edete inaunganika na barabara ya kwenda Mlimba; kwa kuwa barabara ile mmeipeleka *TARURA*, lakini *TARURA* awana fedha naomba hiyo barabara muikamilishe wenyewe kwa sababu Wilaya ya Kilolo kama nilivyosema safari hii kitaifa kuchangia pato tumekuwa watu wanne na kutohana na kuchangia vizuri tumeinua Mkoa wa Iringa umekuwa Mkoa wa kwanza kuchangia pato la Taifa na Mkoa wa pili umekuwa Geita, kwa hiyo niombe msituangushe.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ya kuanzia Kitoo - Pomerini - Kihesa - Mgagao - Mwatasi sasa hivi haipitika, mimi nikuombe Mheshimiwa jungu kuu halikosi ukoko, toa fedha hizo za tahadhari au za *emergence* ziweze kwenda kuwasaidia wananchi kule wanapata taabu. Wilaya ya Kilolo ndiko ambako nguzo za barabarani za umeme zinatoka, Wilaya ya Kilolo ndiko mbao nyingi zinatoka sasa hivi zinazojenga Makao Makuu, Wilaya ya Kilolo ndiko ambako tunazalisha pareto kwa wingi, inakuwaje mnaisahau?

Mheshimiwa Spika, mimi niombe mfanye kila jitihada ili zile barabara zijengwe na niombe pia barabara ile ambayo inaunganisha kama nilivyosema mkoa kwa mkoa na iko kwenye ilani ijengwe, na nimshukuru sana *Engineerwa Mkoa*

Bwana Kindole ni mtu ambaye anatupa ushirikiano mzuri, kwa hiyo nishukuru sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna barabara ya Busega - Nyasuga - Ngasamo kwa ndugu yangu Chegeni, mimi naomba mumsaidie kwa sababu huyu ni mkongwe mwenzangu, tulitoka kwa ajili ya kukosa hizo barabara, sasa mmetupa matumaini tumerudi, sasa msituondoe tena kwa sababu bado tunapenda kuwatumikia Watanzania na wananchi wa majimbo yetu, ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwamoto sijui barabara ya Busega itasafirisha nini maana hawana kitu hawa jamaa. (*Kicheko*)

Hawa Wanyantuzu watasafirisha nini hawa! Ahsante sana bado natafakari mchango wa Mheshimiwa Charles Mwijage bado ndiyo unaongoza hapa anasema kuna baadhi ya matendo mtu ukiyafanya ni kama unatengeneza mke mweza wewe mwenyewe. Nikawa nafikiria hivi kuna mtu anaweza kutengeneza mke mwenza yeye mwenyewe kabisa kwa kukusudia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa *Engineer Chiza jiandae* kwa dakika tano, tano.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na napenda kuzungumzia kuhusu ujenzi wa barabara kama Serikali ilivyosema kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam nimejaribu kujenga barabara, lakini sasa barabara hizo ambazo zinatokea Ardhi - Makongo - Goba, mpaka kufika Kimara na Mbezi kwa kweli kwenye kitabu imeeleza kwamba barabara ya kutoka Ardhi mpaka Makongo tayari imeshakamilika kwa kiwango cha lami. Napenda kuiarifu Serikali kwamba barabara hii bado haijakamilika kwa kiwango cha lami, bado barabara hii ni changarawe kutoka Ardhi hadi Makongo, kwa hiyo naiomba Serikali ihakikishe hizi kilometra nne zinazotoka Ardhi mpaka Makongo zijengwe katika kiwango cha lami ili kupunguza msongamano kwa sababu eneo la kutoka Ardhi mpaka

Makongo kuna kuwa na msongamano na magari kutokana na mashimo mashimo.

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia kuhusu barabara ya Tanga - Pangani, Tanga - Pangani siku zote tunaambiwa itajengwa kwa kiwango cha lami, lakini hapa sioni, sasa hivi ninaona kwenye kitabu imeandikwa kwamba tutajengwa kiwango cha changarawe kuanzia Mabanda ya Papa hadi Boza Buyuni, sasa Mabanda ya Papa pale ni katikati ya jiji pale, kuna lami mpaka sehemu ya Mwang'ombe ambayo ni kilometra nne kutoka Mabanda ya Papa, kwa hiyo, pale pana lami, changarawe inaanzia pale Mabanda ya Papa mpaka inafika huko Boza Buyuni. Sasa Serikali iangalie uwezekano wa kuifanya barabara ile iwe katika kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyikiti, na kwa taarifa yenu ni kwamba sasa hivi mvua zinazonyesha barabara kutoka Pangani mpaka Tanga haipitiki tena, inabidi sasa hivi wapitimeneo jingine linaloitwa Tongoni, wapiti Tongoni waende Lumbwa waingie Kisima Tui - Pongwe ndiyo warudi tena Tanga kwa sababu kuna daraja linaitwa Neema limearibika, gari haziwezi kupita.

Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iangalie uwezekano wa hizi barabara ikamilike kwa kiwango cha lami badala ya kutengeneza tena changarawe maana yake hapa inaonesha kuwa barabara itawekwa changarawe kuanzia Mabanda Papa hadi Buyuni Boza.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuzungumzia kuhusu mabasi haya ya mwendokasi. Mabasi ya mwendokasi yametusaidia sana lakini *yard* ya mwendokasi kwa kweli inasikitisha. Imejengwa mahali ambapo mvua zikinyesha panajaa maji kiasi cha kuharibu miundombinu yote. Kwa hiyo, Serikali iangalie uwezekano wa kujenga tena upya na kufanya *drainage system* ili maji yaweze kupita chini na ile *yard* ikaweza kutumika au vinginevyo ile *yard* ya mwendokasi ihamishwe pale iwekwe mahali pengine, kwa sababu maji

pale jangwani yanajaa kiasi cha kuyafanya mabasi tena hayafanyi kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikzungumzia kuhusu reli ya Tanga hadi Arusha, kwa kweli reli hiyo imeshaanzwa kutengenezwa Tanga hadi Same. Cha kusikitisha ile reli pia inatakiwa ifanyiwe usafi. Kwa sababu kuna nyasi zimeota. Sasa mtu mwingine anaweza kung'oa reli, bila mtu kujuu reli pale imeng'olewa. Kwa hiyo, Serikali ihakikishe kwamba maeneo yale ambayo tayari yameshatengenezwa na ile reli vile vile inakuwa safi, inalimiwa vizuri ili kama kutakuwa na uharibifu wowote utakaotokea inaweza ikajua.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuzungumzia kuhusu viwanja vya ndege. Kwa kweli Serikali inajitahidi kujenga viwanja mbalimbali vya ndege lakini tatizo linakuja, kuna baadhi ya viwanja vya ndege vinakosa taa na kusababisha usiku ndege haziwezi kutua. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali katika viwanja vyote vile ambavyo havina taa za ndege ihakikishe taa zinawekwa ili kuwezesha ndege kutua wakati wa usiku.

Mheshimiwa Spika, mwisho...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nuru. Ahsante sana. Mheshimiwa *Engineer Chiza*, dakika tano.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Nitaongelea mambo mawili tu. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na viongozi wote wa Wizara hiyo kwa kuleta hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, nataka niongelee mambo mawili tu; moja ni Mfuko wa Barabara; la pili ni kasi ya ujenzi wa barabara za lami hususan katika Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, kabla hatujaingia kwenye uchumi wa kati na uchumi wa viwanda bado Watanzania tunategemea kilimo na tutaendelea kutegemea kilimo kama ndio mhimili wa uchumi wetu. Wataalam wanasema asilimia 60 ya upotevu wa mazao hutokea katika *level* ile ya *postharvest*, yaani miundombinu hafifu ya kuhifadhi mazao, lakini pia miundombinu hafifu ya kusafirisha mazao kutoka shambani kwenda sokoni (*farm to market roads*). Hapa ndipo ninapotaka kusisitiza umuhimu wa Mfuko huu wa Barabara. Nikitazama kwa mfano mkoa wangu wa Kigoma wote kwa pamoja tumetengewa shlingi milioni 694 ndizo ninazoziona kwenye kitabu hiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, barabara hizi ambazo ndizo zinatarajiwa zinategemewa na wakulima watoe mazao yao wasafirishe sasa waje kwenye *truck road* tunazojinga, kupeleka sokoni, bado bado sana. Kwa kweli tunahitaji mfuko huu upate pesa, *TARURA* wapate pesa tuwajengee wakulima miundombinu ya barabara waweze kutoa mazao yao kwenda shambani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka niunganishe hapa hapa kwamba katika Jimbo langu kule tumejenga soko la kisasa, la Kimataifa katika Kijiji cha Muhange, soko ambalo litatufanya sisi tuunganishe tufanye biashara na wenzetu wa Burundi. Soko hili ili liweze kufanya kazi vizuri sasa, ni muhimu barabara ile inayojengwa kutoka Nyakanazi kwenda mpaka Kigoma ipate barabara ya kiungo kutoka Kakonko kupita Kinonko, kwenda Gwarama, kwenda mpaka Muhange sokoni ili sasa wananchi wetu waweze kufanya biashara na ndugu zao wa Burundi kwa kutumia barabara nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakwenda haraka kidogo. Miundombinu hii tunayojenga sisi watu tunaotoka Kigoma; kuufungua Mkoa wa Kigoma tunahitaji sasa miundombinu hii ijengwe kwa kasi kubwa ili mkoa huu uweze kuwa *hub* ya biashara hususan katika baadhi ya nchi za maziwa makuu. Tatizo tulilonalo kama nilivyosema awali ni usimamizi au ucheleweshaji wa ujenzi wa barabara hizi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Nyakanazi, mpaka Kabingo pale kijiji ni kwangu mpaka hivi tunavyozungumza tangu mwaka 2014 ni asilimia 60 tu ambazo zimeletekelezwa tangu 2014. Tumeikagua tukiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu tukakuta hata Mkandarasi mwenyewe yuko nje ya mkataba (*out of contract*) kwa siku 986. Naiomba Wizara isimamie kwa karibu Mkandarasi anayejenga barabara hii Nyakanazi mpaka pale Kabingo ili aweze kuongeza kasi ya utekelezaji. 2014 - 2019 asilimia 60, kwa kweli tunaendelea kuchelewa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba tu nimalizie kwa kuishukuru Serikali. Nimeona katika kitabu sasa, mmesema kutoka Kabingo kwenda Kasulu kwenda Kibondo Kasulu hadi Manyovu, Benki ya Maendeleo ya Afrika imetutengea shilingi bilioni 15 ili tuweze kujenga kilomita hizi 260 za barabara hii. Huu ndio mwendo ambao kwa kweli kama tutatekeleza, hii itapelekea kufungua...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Wa kutufungia mjadala wetu awe ni Mheshimiwa *Engineer* Edwin Ngonyani ndio atakuwa mchangiaji wa mwisho. Mheshimiwa Ngonyani ndio atakuwa mchangiaji wa mwisho. Kama hayupo nimtaje mwingine. Karibu *Engineer*, ooh nimekuona.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Kwa kweli nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii ya kuwa hai na kuchangia leo hii. Kwa sababu muda ni mfupi, naomba sana nianze na suala moja la taasisi mbili za *TARURA* na *TANROADS*. Kwa hivi sasa kwa mfumo tulionao, *TARURA* iko chini ya *TAMISEMI* na *TANROADS* iko chini ya Wizara hii tunayoiongelea leo.

Mheshimiwa Spika, hawa wote wanapata fedha kutoka Mfuko wa Barabara unaosimamiwa na Bodi ambapo mgawanyo wake *TANROADS* wanapata asilimia 62.46, *TARURA* wanapata asilimia 26.77, Ujenzi wanapata asilimia 6.94, TAMISEMI wanapata asilimia 2.97 na mfuko wenyewe wa barabara kwa maana ya taasisi inayosimamia inapata asilimia 0.86.

Mheshimiwa Spika, wajibu wa *road fundboard* ni pamoa na kusimamia au kufuatilia utekelezaji au matumizi ya fedha zinazokwenda katika taasisi ya *TARURA*, Ujenzi na *TANROADS*. Wakati huo huo TAMISEMI wanapata hiyo asilimia 2.97 kwa ajili ya ufuatiliaji wa miradi hiyo hiyo na Ujenzi wanapata asilimia 6.94 kwa ajili ya ufuatiliaji wa ujenzi wa barabara hizo hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine Ujenzi, TAMISEMI na mfuko wa barabara wote wanasi mamia barabara zinazoshughulikiwa na *TANROADS* na *TARURA*. Naomba, ni mawazo yangu kwamba *TANROADS*na *TARURA* wawe chini ya Wizara moja na kwa sababu Wizara inayohusika na barabara ni Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, basi ningependa *TARURA* maadam imeshaundwa chombo kinachojitegemea, basi sasa isimamiwe na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano badala ya TAMISEMI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii haina maana kwamba *D by D* itakuwa imekufa, hapana. Bado watu wa TAMISEMI suala la *eyes on, hands off* tabakia pale pale, linaendelea. Ni kama ilivyo katika barabara za *TANROADS*, nazo zinasimamiwa na TAMISEMI hata kama hawapati fedha na wala hawawajibiki, kuisimamia lakini wana *eyes on* katika shughuli zote zinazofanywa na *TANROADS*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba vilevile *eyes on* iendelee na watu wa TAMISEMI kwa maana ya Wizarani pamoa na mkoani katika barabara za *TANROADS* wanavyofanya sasa na wafanye sasa na *TARURA*, lakini suala la usimamizi lirudishwe liwe chini ya Wizara moja, chini ya

Waziri mmoja ambaye ni Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Hii itasaidia mambo mengi. Kwanza hizi hela zote za usimamizi asilimia 6.94, 2.97 na 0.86 zote zitaungana zitafanya kazi kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halafu na mgawanyo wa bajeti hiyo suala la asilimia 70 kwa 30 halitakuwa na mvutano tena na wala hatutakuwa na mvutano tena wa kusema kupandisha barabara hadhi lakini sababu tu ni kutaka hizo barabara zishughulikiwe na *TANROADS*. Mvutano huo hautakuwa tena kama taasisi zote hizo mbili zitasimamiwa na Wizara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuliongea hilo, naomba tena upande wa mawasiliano *TTCL*, Mkongo wa Taifa, Tume ya TEHAMA, pamoja na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Taasisi hizi nimeangalia kwenye vitabu vya Mheshimiwa Waziri, sijaona kama amezipa mtaji wowote. Tatizo la taasisi hizo ni mtaji. mimi nina uhakika taasisi hizi zina wataalam wa kutosha, lakini hawafanyi kazi yoyote kwa sababu hawana mtaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeona katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri, ni vizuri kutoa zile trillioni kwa upande wa uchukuzi pamoja na ujenzi lakini upande wa mawasiliano hajapewa fedha ya kutosha au hajaomba fedha ya kutosha. Ni fedha ndogo sana na kwa hiyo, haiwezi kufanya kazi kubwa inayotakiwa katika kutuimarishtia mawasiliano na tunashida kubwa katika uimarishtaji wa mawasiliano pande zote; mawasiliano ya simu pamoja na *data*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana taasisi hizo zipate fedha za kutosha, zipate mtaji ili ziweze kujiendesha na kushindana na taasisi nyingine.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumejitahidi mno kujaribu *to accommodate*, lakini bado wengi hamkupata nafasi, tusameheane sana, wakati mwingine. Natumaini mmechangia kwa maandishi, ilikuwa siyo rahisi kwamba kila mtu aweze kupata nafasi kwenye Wizara hii muhimu, lakini wengi mmeweza kuongea. Tumejitahidi mpaka asilimia tisini na kitu hivi, katika waliojiantikisha mmeputa nafasi. Kwa hiyo, kwa maana ya Serikali kupata ushauri, kwa kweli wameputa ushauri wa kutosha kabisa.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja ya Waziri na nampongeza sana Waziri, Naibu Mawaziri na vviongozi wote wa Wizara hii kwa hotuba yenye kuleta mabadiliko makubwa katika kujenga miundombinu itakayotufikisha kwenye uchumi wa kati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, naomba Waziri arejee kwenye barabara ya Njombe (Ramadhani) – Igwachanya – Iyayi ambayo ni barabara muhimu kwani inaunganisha Makao Makuu ya Mkoa na Makao Makuu ya Wilaya ya Waging’ombe (Igwachanya). Pia inapita maeneo muhimu ya utalii ya msitu wa asili wa Nyumbanantu na Hifadhi ya Pori la Akiba la Mpanga/Kipangele pale Ludunga na kuunganisha na TANZAM Highway pale Igando. Barabara hii ilishafanyiwa upembuzi na usanifu wa kina toka mwaka 2014 ilipokamilika na ipo kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM ya 2015.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Wizara ione uwezekano wa kuongeza kiwango cha lami pale Igwachanya ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya. Nimeona imepangwa kujengwa mita 100 tu kwa bajeti hii 2019/20.

Kumleta mkandarasi kuja kujenga mita 100 itagharimu pesa kubwa kwani kuleta mitambo ya kujenga mita 100 haina tofauti na ile ya kujenga kilomita 5. Naomba tupate angalau kilomita 2.

Mheshimiwa Spika, sijaona mpango mahsus na kuboresha Uwanja wa Ndege wa Njombe. Mkoa wa Njombe unahitaji kupata uwanja mkubwa wa ndege. Huu ulipo ni mdogo na pengine itakuwa vigumu kuupanua kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri toka bajeti ya 2018/2019 kuwa Wizara ijaribu kwenda pale llembula Hospitali tunao uwanja wa ndege na ardhi ya kutosha ambapo ingeweza kujenga uwanja mkubwa wa ndege kwa kiwango cha uwanja wa ndege wa mkoa. Hakutakuwa na gharama kubwa ya fidia kama kupanua ule Uwanja wa Njombe Mjini ambapo majengo mengi ya kudumu yamejengwa.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, Mji wa Geita ulipewa ahadi na Mheshimiwa Rais kujengewa kilomita 10 za lami. Mwaka jana nilipoongea na Waziri aliahidi kuziweka kwenye bajeti ya mwaka huu wa 2019/2020. Nimeangalia kwenye kitabu lakini hakuna barabara zangu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri anionee huruma hii ni ahadi ya Rais ambayo kwa miaka yote minne imekuwa inaonyeshwa kwenye vitabu lakini barabara hazijengwi. Kwa heshima kubwa, naomba jambo hili Waziri aliipe umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawawiliano.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru kwa ujenzi wa Gati la Nyamisati lililogharimu shilingi bilioni 14 na kazi inaenda vizuri sana. Nina kila sababu ya kujivunia Serikali yangu ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John

Pombe Joseph Magufuli kwa kazi yake nzuri. Kweli huyu ni mzalendo namba moja kwa kujali wananchi wa hali ya chini, wanyonge, kwani gati hili likikamilika litatua changamoto za usafiri kwa wananchi wa Wilaya ya Mafia na Kibiti.

Mheshimiwa Spika, Iakini kila penye mafanikio hapakosi kuwa na changamoto. Barabara yetu ya Bungu-Nyamisati, naomba ijengwe kwa kiwango cha lami kwani kipindi cha mvua huwa haipitiki kabisa kwa hiyo huwaletaa usumbufu wananchi hasa wa Wilaya ya Mafia na Kibiti. Naiomba Serikali yangu sikivu ituangalie kwa jicho la huruma. Vilevile, barabara ya kutoka Muhoro - Mbweria nayo ifanyiwe ukarabati wa kiwango cha changarawe kwani ina manufaa makubwa ukizingatia sasa kuna ujenzi mkubwa wa Kituo cha Afya-Mbweria.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kibiti lina jumla ya kata 16, vijiji 58 na vitongoji 272. Kati ya hivyo, baadhi yake viro kwenye visima/delta au pembezoni mwa Bahari ya Hindi ambavyo vina jumla ya kata 5, vijiji 17 na vitongoji 42. Moja ya changamoto ya maeneo hayo ni kutokufikika kwa urahisi, miundombinu yake ya barabara siyo mzuri kabisa kama maeneo ya Kata za Msala, Mbuchi, Kiongoroni, Salale na Maparoni. Naiomba Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ituangalie kwa jicho la pekee ili tupate magati madogo madogo sambamba na barabara zake ili kufikike kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya jambo lenye manufaa kwa wananchi waishio vijijini kwa kuunda chombo ambacho kinakwenda kutatua kero za wananchi waishio vijijini cha *TARURA*. Naomba sasa chombo hiki kiongezewe nguvu za kifedha na ikama ya watumishi ili wakatekeleze wajibu wao bila ya kupata kikwazo cha aina yoyote sambamba na kuongezewa vitendea kazi kama magari na maboti ya kuendea *site*.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali yangu sikivu ituongezee fedha katika Jimbo langu la Kibiti ili tuweze kukamilisha baadhi ya barabara zetu za lami kama kutoka

Kibiti kwenda Makao Makuu ya Wilaya. Kazi imeshaanza lakini inasuasua kutokana na uhaba wa fedha.

Mheshimiwa Spika, naomba barabara za mitaa zichongwe ikiwa ni pamoja na kujengwa kwa mifereji. Mfano barabara ya Kibiti Mjini, Bungu Mjini, Jaribu Mpakani Mjini, Nyamisati Mjini, barabara hizi za mitaa miundombinu yake siyo rafiki kipitika wakati wote na ukizingatia miji hii inakua kwa kasi na ina wakazi wengi sana. Barabara ya kwenda Makima ambayo ina jumla ya kilomita 32 tayari kilomita 17 zimeshachongwa bado kilomita 15. Tunaomba chombo chetu cha *TARURA* kipewa fedha za kutosha ili kutatua changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo yenyе mito ambayo kipindi cha mvua huwa hayapitiki kwa urahisi. Maeneo hayo ni kama Kibanga Hodi, Mkelele Mkumbwa, Kipoka, Nyafeda na Daraja la Mbwera Mjini. Naomba maeneo haya yaangaliwe kwa jicho la pekee.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Kibiti hadi leo kuna maeneo hayana mawasiliano ambapo ni jumla ya vijiji 24 kwenye maeneo ya nchi kavu. Vijiji hivyo ni Nyambunda, Nyambili, Majawa, Nyamatanga, Mchukwi A&B, Ngondae, Machepe, Nyamwimbe, Nyakinyo, Tomoni, Kingunguri, Mkenda, Kivinja A&B, Msindaji, Muyunu, Ruaruke, Mbawa na Kilolatambwe. Kwenye visiwa (Delta – Rufiji) vijiji ambavyo havina mawasiliano ya simu ni Kiomboni, Mfisini, Salale, Mchinga, Ruma, Kiomboni, Pombwe, Jafa, Mbuchi, Mbwera Magharibi na Mbwera Mashariki, Maparoni, Kechulu, Msala, Tuwasalie na Kiasi. Upatikanaji wa mawasiliano utaongeza kipato kwa wanafamilia, kutoa taarifa kwa haraka pindi majanga yanapotokea kama ya wahalifu na mauaji ya watu wasiojulikana.

**MHE. OMARI A. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niipongeze Wizara na Mawaziri wake kwa kazi bora.

Mheshimiwa Spika, kipande kilichobaki cha Mziha - Handeni kwenye majibu ya Waziri kilitengewa shilingi bilioni

2, katika kitabu cha hotuba ya Waziri ukurasa wa 29-30 ameeleza Serikali bado inatafuta hela. Naomba kwenye majumuisho nipate ufanuzi wa suala hili hasa akizingatia wananchi wa Handeni na Tanga kwa ujumla wamepata faraja baada ya kusikia imeshatengwa shilingi bilioni 2 kutohama na majibu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine yenye umuhimu mkubwa ni ile ya Handeni – Kiberashi. Hii barabara ndiyo litakapopita bomba la mafuta. Naomba ufanuzi wa Serikali kuhusu barabara hii kujengwa kwa kiwango cha lami hata tukianza kwa vipande vipande itasaidia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia kwa maandishi hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa ununuzi wa ndege sita, ujenzi wa reli ya mwendo kasi na mambo mengi sana ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusu barabara ya Bigwa – Mvuha – Kisaki (Morogoro Vijijini) kwa kiwango cha lami. Wabunge wa Morogoro tumekuwa tunachangia mara kwa mara na kuambiwa kuwa itatengenezwa lakini kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri sikuweza kuiona kama kweli imetengewa fedha. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze wananchi wa Morogoro Vijijini ni lini barabara hii ya Bigwa – Mvuha - Kisaki itajengwa kwa kiwango cha lami na ikakamilika?

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa kutengewa fedha kiasi cha shilingi milioni 2,020.00 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Dumila – Kilosa – Mikumi sehemu ya Rudewa – Kilosa (km 24). Barabara hii nimekuwa nikiizungumzia mara kwa mara na hasa kipande cha Kilosa – Mikumi. Kipande hiki wakati wa mvua kinakuwa

kibaya sana na kuitikika kwa shida. Maelezo ya mara kwa mara ni kuwa wafadhili hawajapatiakana. Je, ni lini kipande hiki kitatengewa fedha na Serikali au kitapata wafadhili kwa ujenzi wa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, napongeza kwa fedha zilizotengwa shilingi 12,135.00 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidatu-Ifakara (Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha – Songea). Nashauri fedha zilizotengwa 2019/2020 zitolewe zote na kwa wakati kwani mpaka sasa ujenzi huu unafanyika polepole au unasuasua.

Mheshimiwa Spika, Serikali chini ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano, imefanya mambo mengi mazuri. Hata hivyo, nakumbushia barabara muhimu sana ya Lupiro – Mahenge – Mwaya kwa ujenzi wa kiwango cha lami. Kwenye hotuba hii sijaona kuwa barabara hii imetengewa fedha. Barabara hii nimekuwa nikiisemea pamoja na Mbunge wa Jimbo la Ulanga kwani kuna faida zinazopatiakana Ulanga kama madini, utalii pamoja na mazao mbalimbali kama mpunga. Naomba maelezo ni lini barabara hii itaanza kuongelewa, kutengewa na kupatiwa fedha na ujenzi wa lami kuanza?

Mheshimiwa Spika, barabara ya Magole – Turiani – Mziha – Handeni. Nianze kwa kutoa pongezi kwa barabara hii, ujenzi wake unaenda vizuri na wananchi wa Wilaya ya Mvomero wanaipenda na kuishukuru Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali kwani mradi huu umetengewa shiling milioni 1,170.00 katika mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya barabara ya Turiani – Mziha – Handeni (km104). Naamini kuna wakati barabara hii itakamilika na wananchi wa Mvomero na Handeni watafurahi zaidi kwani miundombinu itakuwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa ujenzi wa reli ya mwendokasi. Wananchi wanaisubiri kwa hamu ikamilike,

hasa wa Mkoa wa Morogoro Vijijini, Morogoro Mjini, Kilosa na Mkoa mzima wa Morogoro kwa ujumla. Wananchi waliopisha umeme wa reli hii ya mwendokasi wanaulizia ni lini watalipwa fidia yao? Ni vyema wakaelezwa kwani ni muda sasa umepita tangu *evaluation* imefanyika.

Mheshimiwa Spika, natoa hongera kwa Mheshimiwa Rais kwa ununuzi wa ndege sita na ukarabati wa viwanja vyta ndege unaoendelea. Tuliahidiwa ujenzi wa viwanja vyta ndege sehemu za utalii, Mkoa wa Morogoro ujenzi wa kiwanja cha watalii Selou Kisaki (Morogoro Vijijini). Kwa kushirikiana na Wizara husika ya Utalii, nashauri uwanja huu ujengwe.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano. Kuna orodha ya vijiji na kata vyta wilaya ya Mkoa wa Morogoro ambavyo amepewa Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba wakajengewe minara illi waweze kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, usalama wa usafiri kwenye barabara ya Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma. Kuna magari makubwa/malori mengi na baadhi ya ajali husababishwa na magari haya. Nashauri mwenendo wao barabarani udhibitiwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nianze na kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa namna ambavyo imeimarisha mitandao ya kiuchumi katika ujenzi wa barabara, madaraja, gati, reli, viwanja vyta ndege na bandari. Uwekezaji huu kwenye miundombinu itafanya wawekezaji/uwekezaji kukua kwa kasi na kuongeza mapato ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kufuatilia ukarabati wa barabara za lami unaonDELETEA. Wahandisi wahakikishe wanawashauri wakandarasi kuweka viraka vyta lami vinavyofanana na uhalisia wa lami ya zamani. Sasa hivi

barabara zetu ziko kama zimechorwa rangi, viraka vyeusi na lami yenewe nyeupe. Sura ya barabara inaonekana kama ni michoro ya rangi. Taifa letu ni kubwa, nchi yetu tuipe heshima na kuiweka katika sura nzuri inayopendeza.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina umuhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu. Hakuna nchi ilioendelea duniani bila uwepo wa mawasiliano ya barabara, reli, anga na majini. Katika nchi inayoendelea kama Tanzania ambayo uchumi wake unategemea kilimo kwa asilimia 75 ni muhimu sana usafiri wa reli na barabara ukawepo ili kufikisha mazao sokoni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ujenzi unaondelea ni muhimu sana barabara zijengwe kwa kiwango kinachostahilli. Ikumbukwe kuwa zaidi ya 40% ya fedha za miradi yote imewekezwa kwa Wizara hii, hivyo, ni muhimu sana fedha hizi zikatumika ipasavyo. Kibaya zaidi fedha hizi zinanunua malighafi za ujenzi kutoka nje huku tukiwa na malighafi hizi kutoka nchini kama vile chuma cha Liganga ambacho kingesaidia mataruma ya reli na pia makaa ya mawe na madini mengineyo.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la ajabu kuona kuwa ATCL haina sera madhubuti na mpango mkakati, jambo linalosababisha shirika kuendelea kupata hasara kubwa. Pamoja na mpango wa biashara bado tumeshindwa kushika soko la utalii kutoka nchi mbalimbali kutokana na kutokuwa na uwanja wa ndege maeneo ya karibu na mbuga kama Serengeti hivyo, watalii hao kwenda Kenya na baadaye kusafirishwa na magari hadi mbugani, jambo linalotukosesha mapato mengi. Nashauri uwanja wa ndege wa Seronera ukarabatiwe ili watalii watue hapo na iwe rahisi kwenda kutilii.

Mheshimiwa Spika, kuna kilio kikubwa cha wananchi wa Dar es Salaam, hasa Ubungo - Kibamba, waliovunjiwa nyumba na cha ajabu tunaelezwa barabara ya Dar es

Salaam – Chalinze (*Express Way*), haitajengwa kwa sasa. Jambo hili limetonesha vidonda kwa wale waliovunjiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Uwanja wa Ndege wa Msalato umekuwa ukizungumziwa lakini cha ajabu pamoja na Makao Makuu kuhamia Dodoma uwanja umekuwa ni huu ulio katikati ya Jiji na ni mdogo. Mwanzoni tuliambiwa ni wa muda tu lakini tumeshuhudia ukiendelea kupanuliwa na watu wakivunjiwa nyumba zao. Hivyo, nataka kujua ile ahadi ya Uwanja wa Msalato ni lini itatimia?

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa nayo imekuwa na shida kubwa sana. Sielewi ni vifaa vyta kizamani au ni utaalam hafifu. Inashangaza tunapopewa *forecasts* ambazo haziendani na uhalsia. Mfano kile Kimbunga Kenneth Kilivytangazwa na hali ilikuwa sivyo kabisa, matokeo yake madhara yakawa mikaoani na si kule Mtwara. Ni albu kubwa sana katika ulimwengu huu wa digitali bado *forecasts* zinakuwa hazieleweki. Iko siku tutaambiwa kutakuwa na juu kali ghafla mnnapata mvua za mafuriko, hivyo inakuwa janga kubwa na vifo.

Mheshimiwa Spika, kule Marangu kuna barabara kutoka Mtoni – Kirua, ujenzi ni kama umesimama lakini cha ajabu hata zile sehemu ambapo ujenzi umekamilika madaraja hayajengwa. Hali hii ni hatari sana kwa kuwa barabara ni pana lakini kwenye madaraja ni nyembamba kuweza kuitisha gari moja tu, hivyo kwa madereva wageni kuna hatari ya kupata ajali. Mfano Mto Ghona/Wona, Mto Makoa, kwa kifupi mito yote toka Marangu Mtoni mpaka Kilema madaraja yake ni tishio kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa Dar es Salaam ni jiji kubwa kuliko majiji yote na lenye kuiingizia nchi pato kubwa sana. Hali ya msongamano Dar-es-Salaam inapoteza kwa kiasi kikubwa pato hilo. Haiwezekani gari kutoka Ubungo hadi Kibaha kilometra 30 litumie saa 2 – 3 wakati kwa hali ya kawaida ni dakika 30 – 45. Hali hii imekuwa mbaya zaidi kutokana na ujenzi wa barabara unaoendelea. Hivyo basi, ni muhimu sana malori ambayo ndiyo chanzo kikubwa cha

foleni kutokana na ama kuharibika na ukubwa wake yatafutiwe njia mbadala au *dry port* eneo la Mlandizi au Ruvu kupunguza adha hii kubwa ili kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, suala la mawasiliano ya simu ni muhimu sana. Hivyo ni muhimu miundombinu ya minara iboreshwe ili kupata usikivu mzuri. Imekuwa ni kilio kikubwa kwa tatizo la usikivu wa simu kutoka eneo moja kwenda lingine.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mgawo wa bajeti ya maendeleo kwa Wizara ya Ujenzi mwaka 2016/2017 ulikuwa shilingi trillioni 4.8, mwaka 2017/2018 shilingi trillioni 4.9, mwaka 2018/2019 shillingi trillioni 4.1 ambayo ni 34.5% ya bajeti yote ya maendeleo. Mpaka mwaka huu wa fedha unaisha Bunge litakuwa limeidhinisha jumla ya shilingi trillioni 13.8 kwa miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, napenda kujuu ni sekta zipe nyingine za uchumi zimechochewa kutokana na uwekezaji huu kama viwanda, ni vingapi vimeanzishwa? Watanzania wangapi wameondokana na umasikini? Pato la Taifa limeongezeka kwa kiasi gani kutokana na uwekezaji huu?

Mheshimiwa Spika, sekta ya ujenzi. Kumekuwa na changamoto kwa wakandarasi Watanzania kutopata kazi za kufanya ndani hata nje ya nchi. Serikali ina mkakati gani wa kufanya wakandarasi hawa waweze kupata angalau asilimia 50 ya kazi za ndani ya nchi na hata za nje ya nchi?

Mheshimiwa Spika, *TBA* wanapewa kandarasi za Serikali na mara nyingi hawashindanishwi. Hii imefanya kazi zao kuwa chini ya kiwango na malalamiko yamekuwa mengi, Serikali ifanyie kazi suala hili.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingi zimekuwa hazikamiliki kwa sababu fedha nyingi zinaenda kwenye

upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambao unachukua muda mrefu sana. Wananchi wanaathirika kwa kutosafirisha mazao yao kwa wakati na uchumi kususua.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna ahadi za Mheshimiwa Rais kutekeleza ujenzi wa barabara za Mkoa wa Iringa, nikitaja chache barabara ya Rujewa - Madibira, Iringa Mjini - Hifadhi ya Taifa ya Ruaha (kilometra 14) na Ipogolo - Kilolo (kilometra 133). Barabara zote hizi fedha za ujenzi bado hazijafika, kinachofanyika ni usanifu tu. Pamoja na utengaji huu wa fedha mnaouainisha, naitaka Serikali hii itekeleze ahadi hizi mapema ili wananchi wasipate adha.

Mheshimiwa Spika, bado nasisitiza uendeshaji wa Shirika la Ndege la ATCL ni wa hasara. Serikali iangalie suala hili kwa makini kwani kodi za wananchi zinazidi kuteketetea.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *SGR* vifaa vinavyotumika vinatoka nje ya nchi. Nashauri Serikali itumie malighafi kutoka hapa nchini. Kwa mfano, makaa ya mawe ambayo yapo Mchuchuma yangetumika katika mradi huu.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza Mheshimiwa Waziri Kamwelwe na Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Kwandikwa na Mheshimiwa Nditiye kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuna shida kubwa ya kukosa minara ya mawasiliano Kata za Shitage, Igulungu na Makazi. Naomba minara katika kata hizo.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tabora - Mrambali - Ishitimulwa - Mhulidede ni muhimu kuwa na lami. Barabara hii muhimu kwani inaunganisha Mikoa ya Shinyanga na Tabora.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mamlaka ya Mawasiliano *TCRA*. *TCRA* wamefanya kazi kubwa ya kubadili mawasiliano na matangazo ya *TV* kutoka analogia na kuwa digitali na kuwa moja ya nchi za kwanza Barani Afrika na ya

kwanza EAC. Vilevile wanasmamia mgawanyo wa masafa (*frequency monitoring*) na ugawaji bora wa leseni za redio na televisheni. *TCRA* wamefanya kazi kwa weledi sana kusimamia mashirika ya huduma za simu na kuhakikisha wanalipa kodi za Serikali kwa kutumia mtambo wa *TTMS*.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Waziri, tunaomba sanasana tuenze kujenga kwa lami barabara ya Kongwa – Arusha kupitia Olkesmet (Simanjiro). Tuanze hata kama ni kilometra 15 tu.

Mheshimiwa Waziri, Kongwa Mjini tunahitaji lami angalau tupate hata kilometra 5 tu.

Mheshimiwa Waziri, Daraja kubwa la Njoge kwenye barabara itokayo Pandambili ni muhimu mno kujengwa. *TARURA* wapewe bajeti.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Wizara hii na Mheshimiwa Waziri kipekee na Naibu Mawaziri wake kwa kazi nzuri wanayofanya ili kuunganisha nchi yetu kwa barabara, reli na kimawasiliano, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, barabara yangu ya lkungu - Malampaka ilitengewa bajeti ya shilingi milioni 800 ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami mwaka wa fedha 2018/2019 lakini ujenzi huu haujaanza mpaka leo. Katika bajeti ya 2019/2020, Wizara imetenga shilingi milioni 300 kwa ajili ya barabara hii. Je, ni lini sasa barabara hii itaanza kujengwa ikiwa tumebakia na mwezi mmoja tu mwaka wa fedha 2018/2019 uishe? Barabara hii ni muhimu sana kwa ajili ya kuunganisha na bandari kavu ya Malampaka ambayo itakuwa ni lango la bidhaa na biashara kwa Mikoa ya Simiyu, Mara na maeneo ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ulilenga kuboreshwa kwa barabara na kurahisisha

usafiri ili uwe wa haraka zaidi na kufanya watu na usafirishaji mizigo ifike mapema zaidi na hatimaye kuchochaea shughuli za uchumi ziende kwa kasi zaidi. Cha kushangaza muda wa kusafiri kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza umebakvi kuwa ni uleule kama wakati ule ambapo barabara hazikuwa za lami. Mabasi yalikuwa yanatoka saa 11.00 alfajiri Dar es Salaam kabla ya lami na kufika Mwanza saa 5.00 au saa 6.00 usiku. Sasa tuna barabara za lami lakini muda unaotumika kwa mabasi kusafiri bado ni uleule na wakati mwingine ni zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa barabara za lami zimetusaidiaje ikiwa hazijapunguza muda tuliokuwa tunapoteza barabarani? Ni shughuli ngapi za kiuchumi zinachelewa? Ni fedha kiasi gani zinapotea kwa kupoteza muda barabarani? Wizara hii inafanya kazi nzuri lakini tafuteni ufumbuzi wa tatizo hilli.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100 na niombе yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mkongo wa Taifa. *TTCL* na Tume ya TEHAMA iimarishe kwa kuwekeza mtaji wa kutosha ili sekta ya mawasiliano ichangie zaidi katika uchumi wa Taifa na ukuaji wa sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya yangu ya Namtumbo kuna maeneo yenye wakazi wengi lakini hayana mitandao ya mawasiliano ya simu. Ni maeneo yote ya Kata za Msindo, Mgombasi na Lisimonji.

Aidha, vijiji vya Mtewamwachi, Likusanguse, Limamu na Mtakuja navyo havina usikivu wa mawasiliano ya simu. Naomba Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote utusaidie kukamilisha na kufungua mawasiliano ya simu na data katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuisemea barabara ya kuunganisha Mikoa ya Ruvuma na Morogoro ya Lumecha - Kitanda-Londo - Kilosa Kwa Mpepo - Lupiro - Ifakara - Mikumi. Mheshimiwa Rais ameliisemea barabara hii wakati akifungua Daraja la Kilombero na Kituo cha Mabasi cha VETA cha Namtumbo au tuseme alipokuwa kwenye ziara Mkoani Ruvuma kuanzia tarehe 4 hadi 09 Aprili, 2019 lakini katika kitabu naona shilingi milioni 80 tu ambazo haziwezi kujenga barabara kati ya Lupilo-Kilosa Kwa Mpepo-Londo - Lumecha kupitia Kitanda. Hii ni sawa kweli? Namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa wana Ruvuma barabara ya kuunganisha Mikoa hii inaanzia Kilosa Kwa Mpepo - Londo - Kitanda. Kipande hiki cha kilometra 121.5 hivi ndiyo inaweza kuitwa kiungo cha mikoa hiyo miwili. Naomba fedha zilizotengwa zishughulikie kipande hiki cha barabara vinginevyo tafsiri ya bajeti hii ni kujenga barabara ya Mikumi - Ifakara - Mlimba na kuelekea Njombe badala ya barabara yetu wana Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kutufikiria wana Namtumbo kwa barabara zetu za kutoka Naikesi - Mkonga na Namtumbo - Likuyu -Namabengo - Mbimbi - Libango - Namtumbo na nyinginezo kwa kuzitengea fedha za matengenezo hususani lami nyepesi ya mita 100 katika barabara ya Naikesi - Mtanya.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia Waziri, nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wetu mpendwa kwa kuitengeta fedha ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara ya Mtwarapachani - Likusanguse - Nalasi jumla ya shilingi milioni 450 na hivyo kumfanya Mhandisi Mshauri aendeleze na kukamilisha kazi iliyoanza.

Mheshimiwa Spika, *TARURA* na *TANROADS*, taasisi hizi mbili zinapata fedha kutoka Hazina na *Road Fund Board (RFB)*

kwa kuwa taasisi hizi ni za kushughulikia barabara. Naomba taasisi zote za *TANROADS*, *RFB* na *TARURA* ziwe chini ya usimamizi wa mamlaka moja ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Kuziweka taasisi hizo katika Wizara mbili tofauti inaongeza ghamama za utawala na uendeshaji na kugawana wataalam hususani Wahandisi wa sekta ya barabara wachache tulionao nchini. Hoja za kupandisha hadhi barabara pamoja na kuiongeza *TARURA* mgao wa fedha za Mfuko wa Barabara zitaondoka ikiwa taasisi hizi za *TARURA* na *TANROADS* zitawekwa chini ya Wizara moja yenye wajibu wa kujenga na kukarabati barabara.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa pumzi. Aidha, nimpongeze Waziri na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiwezesha mihimili ya utawala na Bunge kufanyakazi kwa umakini na kwa umoja kwa kiwango cha kutuwezesha wana Namtumbo kuanza kuona maendeleo katika sekta mbalimbali hususani barabara, mawasiliano ya simu, umeme na kadhalika. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100 na naomba kuwasilisha.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri pamoja na timu yake yote kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Wilaya ya Lushoto hasa katika Jimbo la Lushoto, barabara za Lushoto siyo siasa tu, ni zaidi ya maisha ya watu hasa barabara ya Mlalo – Ngweloo – Mlola – Makanya - Mlingano - Mashewa yenye kilometra 57. Barabara hii nimeizungumzia kwa muda mrefu sana kuwa ni barabara ya kiuchumi yenye wakulima wengi wanaozalisha mazao ya kibashara.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, barabara hii inapigwa danadana na *TARURA* wanasema ipo *TANROADS* nao *TANROADS* wanasema ipo *TARURA*. Naomba Mheshimiwa Waziri barabara hii muichukue iwe ya *TANROADS*

ili wananchi wa maeneo hayo niliyotaja waweze kunufaika. Kama hili Mheshimiwa Waziri haliamini, atume timu yake iende ili ajue ukweli wa haya niliyoyaandika.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kuna barabara ya kuanzia Doch - Ngulwi – Mombo. Kama unavyofahamu Lushoto kuna barabara moja kubwa tu na barabara hii ni nyembamba na imejaa mawe yanayoning'inia juu ya barabara na ndiyo sababu mvua ikinyesha mawe yanaporomoka na kuziba barabara.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017, barabara hii iliziba kwa siku zaidi ya 21 (wiki tatu) hali iliyosababisha usumbufu mkubwa sana na kupelekeea wakulima wa mboga mboga na matunda kupata hasara kubwa sana pamoja na huduma za jamii kukosekana. Niiombe Serikali yangu Tukufu, kwa kuna kuna barabara hii ya Doch - Mombo kilometra 16 tu itengenezwe ili iwe barabara mbadala lakini siyo kwa kupidika tu ila pia ni barabara yenye mazao mengi na pia kuna wananchi wengi wanaoishi katika maeneo hayo na kwa sasa wanakosa huduma za afya pamoja na za kijamii. Pamoja na hayo, barabara zote hizi mbili siyo lazima ziwe na lami. Wananchi wanataka zipitike tu kwa mwaka mzima yaani ziwe za changarawe tu.

Mheshimiwa Spika, pia kuna barabara ya *TANROADS* inayoanzia Nyasa – Mshizi - Gare - Magamba. Barabara hii kwa kweli nimshukuru Meneja wa *TANROADS* Ndugu Ndumbali kwa kazi kubwa. Barabara hii ina maeneo ya kujenga madaraja mawili; Daraja la Mshizi na Daraja la Kongei pamoja na kuweka zege maeneo hatarishi kama vile Mlima wa Yamba. Hili nalo niiombe Serikali yangu itengeta fedha ili barabara hii iweze kurekebishwa na kujenga hayo madaraja mawili.

Mheshimiwa Spika, pia niendelee kuipongeza Serikali yangu tukufu kwa kutupatia kilometra 1 kila mwaka kwa barabara iliyoanzia Magamba kwenda Mlolo na Magamba kwenda Mlalo. Niiombe Serikali yangu ituongezee angalau

kilometra 3 ili ziwe 4 ili kuharakisha maendeleo ya Wilaya ya Lushoto na huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu kuwa Tanga ni Jiji lakini tunayo changamoto za uwanja wa ndege. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu iupanue Uwanja wa Ndege wa Tanga ili ndege kubwa ziweze kutua.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, mwaka jana tuliomba Bombardier iweze kutua Tanga na Waziri alikubali lakini mpaka leo ndege hajatua. Naomba nikumbushie tena kuwa Bombardier itue Tanga sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa ndege nchini. Serikali iliagiza ndege kubwa (*Dreamliner*) iko wapi? Mbona hatuoni ikifanya kazi? Inanunuliwa ndege ya maonyesho kwa *cash money*, kodi za wananchi halafu hatuoni ikifanya kazi kwa kuinua uchumi wa nchi kama ilivyoelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, zipo taarifa kuwa ndege hiyo imekodishwa Kenya. Kama ndivyo, hayo ndiyo tunayolalamikia kuwa Serikali ina tatizo katika kusimamia na kupanga *priorities*. Hivi kulikuwa na sababu gani kukimbilia Dreamliner, *ku-invest* kwenye ndege ambayo *return* zake haziwezi kuonekana kwa haraka? Ni bora Serikali ingewekeza kwenye *project* kama za afya, maji na kadhalika, ndege bora ingetumia *PPP*.

Mheshimiwa Spika, matengenezo ya ndege ndogo tatu (*Bombardier*) zaidi ya shilingi bilioni 14, hivi kweli ndege zinajidesha kwa faida? Kwa nini Serikali isingeachia *private sector* au nchi zenye uzoefu wa biashara za ndege mfano Ethiopia na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, *SGR*, kwa sasa ajira kwa Watanzania ni asilimia 20 na asilimia 80 ni Waturuki. Hiyo siyo

sawa, Serikali ilipaswa kuandaa watu wetu kuingia kwenye ajira kabla ya kuanzisha mradi wa *SGR*. Kazi ambazo ni *professional/technical skills* zingefanywa na Watanzania kuliko hivi sasa Watanzania wanaishia kwenye kazi ndogo ndogo.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na pia kuwataktakia Waislamu wote Tanzania na duniani kwa ujumla, Mfungo mwema wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhanii.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Pangani ni miongoni mwa barabara za kimkakati na ni miongoni mwa barabara inayounganisha Mikoa na Wilaya. Pangani *road* inaanza Mkao wa Tanga na kupitia Wilaya za Muheza, Pangani na Chalinze Mkao wa Pwani na Dar es Salaam. Pia barabara hii inaunganisha nchi za Afrika Mashariki kwa barabara kuu itokayo Mombasa - Kenya kupitia Tanzania na hadi Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, barabara hii imewekewa ahadi na Marais wanenye ambaa sasa ni wastaafu ambaa Julius K. Nyerere, Mzee Ally Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa na Jakaya Kikwete. Pamoja na fedha kupatikana (bajeti) upumbuzi yakinifu tayari na mkandarasi ameshapatikana, naionomba Serikali itoe tamko ni lini barabara ya Pangani itaanza kujengwa rasmi?

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara kwa changarawe. Barabara zifuatazo katika kitabu cha bajeti na sijaziona, naomba zitengewe fedha:-

- (i) Barabara ya Mabokweni-Maramba-Daluni-Korogwe;
- (ii) Barabara ya Kirare-Mapojoni-Mkembe;
- (iii) Barabara ya Amboni-Mleni-Rubawa-Pangarawe;
- (iv) Barabara ya Pongwe-Marungu-Geza; na
- (v) Barabara ya Fuweni-Mondura-Mwarongo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iongeze fedha katika bajeti hii ili barabara hizi ziweze kuitikana wakati wote wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Tanga ni miongoni mwa bandari za kihistoria duniani. Kama tunavyoja, bandari ni langoo kuu la biashara lakini haitumiki ipasavyo pamoja na kufanyiwa ukarabati wa shilingi bilioni 1.8 na *crane* ya 40Ft mpya bado kuna upungufu wa vifaa vingi.

Mheshimiwa Spika, nashauri bandari hii ipatiwe fedha za kutosha kwa ajili ya vifaa bora na vya kisasa. Serikali na Mamlaka ya *TPA* ifanye utaratibu wa kupanga aina za mizigo (*categories*) kwa kila mandarin. Bandari ya Tanga ichukue mizigo ya Tanga, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Musoma na Bukoba bila kusahau mizigo ya Uganda, Rwanda na Burundi. Bandari ya Mtwara (*Mtwara Corridor*) ichukue mizigo ya Mtwara, Mbeya, Sumbawanga, Katavi, Kigoma, Iringa bila kusahau mizigo ya Zambia, Malawi na Congo *DRC*. Bandari ya Dar es Salaam ni kuipa mizigo mikubwa sana. Dar es Salaam Port kwa kuifanya ishughulikie mizigo yote inayotoka nchi za nje matokeo yake meli zinasubiri muda mrefu sana na kuwa ni sababu ya baadhi ya makampuni ya meli kuikimbia Bandari ya Dar es Salaam na kushushia mizigo Mombasa *port*, Beira na Maputo. Hivyo, naiomba Serikali ifanye *categories* za mizigo na Bandari zote za Tanga, Zanzibar, Dar es Salaam na Mtwara zifanye kazi kwa faida.

Mheshimiwa Spika, Bandari Bubu ziboreshwani. Bandari Bubu Tanzania ni jambo lisiloepukika kwa kuwa Watanzania wanafanya kazi za usafirishaji kuitia maji (bahari, mito, maziwa). Bila kuathiri huduma hii kwa wananchi ni vyema Bandari Bubu zikafanyiwa tathmini na zinazokidhi vigezo zikarasimishwa (kuboreshwa) na kuwa chanzo cha mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tanga tunazo Bandari Bubu katika maeneo ya Moa, Jasini, Monga, Tongoni, Mwarongo, Marungu (Tanga *Mjini*), Kigombe (Muheza), Kipumbwi na Mkwaja. Nashauri Bandari Bubu za Kigombe

(Muheza) na Kipumbwi (Pangani) ziboreshwwe kwa kujengewa majengo bora ya *TRA*, *TPA* kwa ajili ya kukusanya mapato ya Serikali ya forodha na kodi mbalimbali. Bandari hizi zikiboreshwra zitaongeza mapato ya Serikali na pia itaongeza ajira na kuongeza mzunguko wa fedha kwa wananchi (wafanyabiashara) wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, minara ya simu/mawasiliano. Moja ya vigezo vya maendeleo ni mwasiliano ya uhakika. Yapo maeneo katika Jimbo/Jiji la Tanga hakuna mawasiliano ya uhakika. Unapotaka kuongea na simu lazima upande ju ya mti, kichuguu au katika maeneo maalum hali inayopelekea wananchi kupata shida ya mawasiliano hususani katika kipindi cha dharura yoyote inapotokea au hata katika shughuli za biashara. Maeneo hayo baadhi ni Kata za Marungu, Tongoni, Mzizima, Mabokweni, Kiomoni na Maweni. Naishauri Serikali kwa kushirikiana na Makampuni ya simu (Tigo, Airtel, Zantel, TTCL na Vodacom) kuongeza minara.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Spika, naomba sana ahadi ya barabara ya kutoka Njombe – Makete - Mbeya ifanyike. Kutoka Makete ni barabara ya kutoka Makete - Bulongwa – Mbeya na Makete- Ivalalila - Ujuni kuunganisha barabara ya kutoka Bulongwa.

Mheshimiwa Spika, pia kwa ajili ya kuwezesha Hifadhi ya Kitulo ni muhimu barabara ya kutoka Chimale- Matemba au Mfumbi kuja Matamba ijengwe kwa lami. Pia ili kuboresha ujenzi wa barabara za Ludewa, Kipengele- Mbalache - Lupila kwenda Ludewa ijengwe kwa lami.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano Kata za Mang'ota, Ikuwo, Kigala, Lupila na Ukwama zipewe mawasiliano ya Voda, Airtel, Halotel na Tigo. Hili likifanyika litasaidia sana kutupa mawasiliano.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia ujenzi wa barabara ya Kigoma – Nyakanazi. Barabara hii imechukua muda mrefu sana lakini mpaka leo haijakamilika. Nomba Serikali iweze kusimamia ili iweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kipo kipande cha kutoka Uvinza – Malagalasi, nacho ni tatizo. Tunaomba kipande hiki nacho kiweze kujengwa. Kipo kipande cha Chagu - Kazilambura nacho tunaomba kiweze kujengwa ili wananchi waweze kuondokana na adha ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nishukuru Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuweza kukubali barabara ya kutoka Kabingo-Kibundo- Kasulu - Bulingwe kujengwa kwa lami kuititia fedha za AfDB.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na naunga mkono hoja.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuishukuru Serikali kwa kutuungezea kilomita 50 za barabara ya lami kutoka Mnivati – Tandahimba. Ombi langu kwa Serikali ni kwamba kwa kuwa barabara hii ni muhimu kwa uchumi wa Mkoa wa Mtwara ambao unategemea sana zao la korosho huku asilimia 47% ya korosho zote Tanzania zikiwa zinatoka maeneo hayo, Serikali iwave wakandarasi zaidi ya mmoja ili tupate matokeo ya haraka sana.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe tu kuwa tunazo kilomita 50 za awali za kutokea Mtwara kuelekea Mnivati lakini barabara hii ambayo mkataba wake ilikuwa uwe umekamilika ndani ya miezi kumi na saba mpaka sasa ni kilomita 8 tu ndiyo zimewewka lami. Hii ndiyo kusema kwa kusuasua huku tutahitaji miaka 10 kukamilisha barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba maeneo yafuatayo yapate minara ya simu; Kata za Mdimiba, Michenjele, Nganja, Mkwiti, Mkoreha na Chaume. Kata hizi hazina mawasiliano ya simu, naomba suala hili lishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, niombe kuzungumzia suala la reli ya kutoka Mtwara - Mbambabay - Mchuchuma - Liganga. Reli hii kama itejengwa italeta fursa za kibashara Kusini mwa Tanzania na nchi za Malawi, Zambia na Msumbiji.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Watendaji na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mawasiliano, katika Jiji la Dodoma eneo la pembezoni Kata ya Mbalawala, Kijiji cha Lugala - Matangizi hakuna mawasiliano ya simu hali ambayo inasababisha wagonjwa kutopata huduma kwa haraka kutokana na umbali wa eneo hilo. Naomba wananchi hawa wapatiwe mawasiliano ya simu ili waondokane na changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Seminari, mnamo mwaka 2015 wakati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli akiwa mgombea wa Urais aliwaahidi wananchi wa Jimbo la Segerea kuwa barabara ya Segerea - Seminari - Majumbasita (km 3) itajengwa kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, barabara hiyo haina hata dalili ya kutengenezwa kwa kiwango cha lami. Naomba Serikali itekeleze ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nirudie kuwashukuru sana watendaji wote kwa kazi nzuri wanayofanya.

**MHE. WILLIAM T. OLENASHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuishukuru Wizara ya Ujenzi na Serikali ya Awamu ya Tano kwa miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara katika jimbo la Ngorongoro, hususani barabara ya Loliondo - Mto wa Mbu inayojengwa kwa kiwago cha lami.

Mheshimiwa Spika baada ya pongezi hizo, naomba nieleze changamoto zilizopo katika Jimbo la Ngorongoro. Kwanza, ni kusimama kwa ujenzi wa barabara ya Loliondo – Mto wa Mbu. Ujenzi wa barabara hii unasuasua kutokana na ukosefu wa fedha na uchelewashaji wa malipo kwa mkandarasi. Kwa sasa mkandarasi anadai zaidi ya shilingi bilioni 13. Kwa sababu *cashflow* isiyo nzuri, mkandarasi amelazimika kusimamisha ujenzi kwa kiasi kikubwa kuanzia tarehe 19/4/2019. Mkandarasi amelazimika pia kupunguza wafanyakazi 300 kwa sababu ya kukosa fedha za kuendelea na ujenzi. Ucheleweshaji huu wa malipo utaendelea kufanya mradi kucheleva kukamilika. Tunaomba Wizara ifanye malipo mapema ili ujenzi uweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, pili, kukwama kwa miradi ya mawasiliano ya simu za mkononi, Tarafa ya Ngorongoro. Tunashukuru sana Wizara kupitia Mpango wa Mawasiliano kwa Wote kwa kutuletea miradi ya mawasiliano katika Wilaya ya Ngorongoro ikiwemo ile inayotekelawa ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro, eneo la matumizi mseto ya ardhi lenye vijiji 25 na wakaazi wapatao 95,000.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupatikana msaada huu wa Serikali, ujenzi wa minara umekwama kwa muda mrefu kutokana na vikwazo vya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, ikiwepo taratibu za Tahmini ya Mazingira (*EIA*) inayochukua muda mrefu kukamilika. Baadhi ya miradi ambayo imeshindwa kuendelea kwa wakati ni pamoja na ile ya Embakaay (Naiyobi), Sendui (Alaililai) na Nainokaroka inayojengwa na kampuni ya Halotel.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itupie jicho miradi ya mawasiliano ndani ya hifadhi ya Ngorongoro kwani wananchi wanakosa huduma muhimu inayotolewa na Serikali. Wizara iangalie usahihi wa miradi midogo kama miradi kufanyiwa tathmini kubwa ya mazingira (*EIA*) na katika njia inayochukua muda mrefu.

Mhe Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kuniwezesha kufika mahali hapa nami niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kama inavyojieleza, hotuba hii inakwenda kutatua changamoto mbalimbali na kutekeleza miradi ya kimaendeleo inayogusa sekta husika za ujenzi, uchukuzi na mawasiliano. Aidha, inakwenda kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi kama ilivyoainishwa. Pia nichukue fursa hii kumpungeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri yenye malengo chanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kuchangia kwa kuipongeza Serikali katika jithada zake za kuendelea kuhakikisha nchi yetu inakua na barabara nzuri zinazopitika wakati wote. Lengo kuu la Serikali ni kuunganisha mikoa yote kwa barabara za lami ili kuimarisha na kurahisisha mawasiliano ya usafiri na usafirishaji wa watu, bidhaa na mazao mbalimbali. Ni jambo la kujivunia sana kwani hadi kufikia Februari 2019, jumla ya kilomita 266.78 za barabara kuu za mikoa zimekamilika na kilomita 392.2 zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. Vilevile katika jithada zilezile Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja matano katika Mto Lukuledi (Lindi), Mara (Mara), Sibiti (Singida), Mombasa (Rukwa na Songwe) na Mlalakuwa (Dar es Salaam) na ujenzi wa madaraja 8 unaendelea katika sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miradi hii, utatoa fursa mbalimbali kwa wananchi kupata ajira pamoja na kupata soko kwa bidhaa na mazao yao. Aidha, utasaidia sana kuvutia wawekezaji kuja kuwekeza nchini ikizingatiwa miundombinu yetu ni mizuri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado naendelea kuipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza ujenzi wa miradi ya barabara inayolenga kufungua fursa za kiuchumi kwa wananchi. Miradi hiyo inahusisha ujenzi wa barabara

kuwezesha mradi wa kuzalisha umeme wa *Stigler's Gorge* kwa kiwango cha changarawe kutoka Ubena Zomozi mpaka Selous kilomita 177.6 na ukarabati wa barabara ya kutoka Kibiti - Mloka - Selous - Mpenda (Km 370), Makutano - Natta - Magumu - Liliondo (Km 239) na Loliondo - Lumecha (Km 464). Haya yote kwa ujumla yamefanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi yenye viongozi imara wenye kutekeleza yale yote yaliyomo kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM, ikiongozwa na Rais wetu shupavu na mpenda maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa awamu ya kwanza wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro kwa asilimia 42.8 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Novemba, 2019. Hali kadhalika, ujenzi wa awamu ya pili wa reli hiyo ya kisasa kutoka Morogoro - Makutupora Jijini Dodoma umefikia asilimia 6.07. Hadi sasa mradi kutoka Dar es Salaam - Makutupora umeshaajiri wafanyakazi wazawa wapatao 6,335 sawa na asilimia 90 ya wafanyakazi wote. Ni jambo la kupongezwa kwani limezalisha ajira kwa watu wetu na kuna faida kubwa mradi husika utakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ujenzi wa reli mpya ya kisasa, Serikali katika mwaka 2018/2019 imeendelea na kazi ya kuboresha, kujenga na kukarabati miundombinu ya reli ya kati kwa kuondoa reli zote nyepesi na kuweka reli mpya zenye uzani wa paundi 80 kwa yadi kati ya stesheni ya Dar es Salaam na Isaka. Aidha, kazi ya ukarabati wa reli ya Tanga-Arusha imekamilika kwa sehemu ya Tanga - Same (Km 199). Hata hivyo, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea na kazi ya ujenzi wa reli ya kisasa, ukarabati wa ujenzi wa reli ya kati na nyingine ikiwemo ya Tanga - Arusha ili kuimarisha huduma za usafirishaji na biashara kwa ujumla. Miradi hii inatekelezwa chini ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ikiongozwa na Rais wetu anayetekeliza llani ya Chama.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kuwa na changamoto ya msongamano katika Jiji letu la Dar es Salaam na imejitokeza pia katika baadhi ya miji, lakini Serikali imefanya na inaendelea kufanya jitihada kubwa kutekeleza

miradi ya kuondoa msongamano wa magari kwenye Jiji la Dar es Salaam ili kurahisisha usafiri na usafirishaji na kuchochaea shughuli za kiuchumi kwani Jiji hili lina bandari kuu ambayo huchangia pato la nchi kwa kiasi kikubwa. Hivyo, jitihada hizi zinafanyika kulingana na hali halisi iliyopo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa mradi wa barabara ya juu ya Mfugale na miradi mingine inayoendelea. Miradi ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano ya Ubungo (*Ubungo Interchange*), upanuzi wa barabara ya Kimara Mwishi - Kiluvya (Km 19.2) kutoka njia mbili kuwa nane. Katika mradi huu upanuzi wa hii barabara ya njia nane, naishauri Serikali mradi huu uweze kuishia mizani ya Vigwaza. Kwa kufanya hivyo kutasaidia sana kupunguza msongamano ambao sasa pia umeanza kujitokeza katika Mkoa wetu wa Pwani hasa Kibaha.

Mheshimiwa Spika, aidha, pongezi hizi pia zinakwenda katika mradi mpya wa daraja jipyaa la Salender na miundombini ya mabasi yaendayo haraka awamu ya II na III. Hata hivyo, katika mradi wa mabasi yaendayo haraka kwa awamu ya kwanza kumejitokeza changamoto mbalimbali na za muda mrefu ambazo wananchi wamekuwa wakizilalamikia za uhaba wa mabasi, abiria kujaa kwa wingi na kwa muda mrefu kwenye vituo vya mabasi hayo. Pia changamoto ya uwepo wa baadhi ya mabasi ya *express*, mabasi haya ya *express* hayana tija kwa kuwa miundombini ya mabasi haya yenyewe yanajitosheleza kufika kwa haraka. Kero ya mabasi haya ni pale yanapoacha abiria vituoni ili hali kuna uhitaji, athari zake ni abiria kuzidi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kama ifuatavyo, mabasi yote ya *express* yarudishwe katika hali ya kawaida ili kukidhi mahitaji kwa sababu hivi sasa mradi unakabiliwa na uhaba wa mabasi. Kufanya hivyo, kutasaidia kupunguza mlundikano wa abiria katika vituo vya mabasi. Aidha, naishauri Serikali katika mradi huu wa mabasi yaendayo haraka awamu ya pili ufike mpaka Kibaha. Kuleta mradi mpaka Kibaha kutarahisisha usafiri kwa wananchi kwani

mkoa wetu sasa umekua hasa Kibaha tunaongezeko kubwa la watu wanaokuja kuishi na kufanya shughuli zao mbalimbali, pia ni eneo ambalo linakua kwa kiwango kikubwa katika ukuaji wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuanzisha treni ya moja kwa moja kutoka Posta hadi Mlandizi. Uwepo wa treni hii utakuwa na tija kwani treni inabeba abiria wengi kwa wakati mmoja ukilinganisha na usafiri mwingine. Mfano tumeona mabasi yetu yanayotumika katika mradi wa mabasi yaendayo haraka, mabasi haya ni ya gharama kubwa, utunzaji wake pia ni ya gharama pamoja na vipuri vyake. Hali hiyo inapelekea mabasi haya yanapoharibika kuchukua muda mrefu kukarabatiwa na hivyo kupunguza ufanisi wa mradi huu lakini tutakapokuja na treni itatusaidia sana kupunguza adha hii ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, aidha katika mradi huo wa treni, naishauri Serikali kwenye kila kituo treni itakaposimama kujengwe maegesho ya magari ya kulipia ili wananchi wanapotoka katika maeneo yao wanaacha magari yao hapo na kupanda treni. Hii itasaidia kuingiza kipato katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine inayotukabili wana Kibaha Vijijini ni kukosekana kwa mawasiliano ya uhakika. Kuna maeneo hakuna minara na hivyo kuifanya dhana nzima ya uchumi wa viwanda kuwa ngumu, kwani mawasiliano ya simu ni muhimu, yanakwenda sawia na dhana nzima ya uchumi wa viwanda. Maeneo hayo ni *Ruvu Station*, Ruvu kwa Dosa, Kipangege, Miande, Dutuni, Madege, Lukunga, Videte, Boko Mpiji, Kwala, Mperamumbi Msua na Waya.

Mheshimiwa Spika, hapana shaka yoyote juu ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya barabara kama nilivyokwishapongeza hapo awali. Katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa mikoa ambayo haijaunganishwa na barabara kuu za lami. Kibaha Vijijini tuna

changamoto kubwa ya miundombinu ya barabara, tuna bandari kavu Kwala ambayo kwa kiasi kikubwa inakwenda kuleta mapinduzi makubwa sana lakini barabara zake haziridhishi. Naiomba Serikali kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Vigwaza- Kwala kwani ikiwa katika kiwango cha lami itavutia wawekezaji kuja kuwekeza eneo hili na kurahisisha uchukuaji wa mizigo.

Mheshimiwa Spika, aidha, tuna changamoto ya barabara za Chalinze – Magindu, tunaomba ijengwe kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, kuna mradi mkubwa wa ujenzi wa miundombinu ya reli ya kisasa *SGR* lakini barabara hii inayoelekea katika mradi huo kuanzia Kongowe – Soga ilipo karakana tunaomba ijengwe kwa kiwango cha lami. Kwa sasa maeneo yale kutokana na mradi huu shughuli za kiuchumi zimekua kwa kiasi kikubwa, kujengwa njia hii kwa kiwango cha lami kutazidisha kasi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Makofia- Mlandizi - Mzenga ni ya muda mrefu. Barabara hii imeongelewa hapa Bungeni tangu Mbunge wa kwanza hadi awamu yangu nimekuwa nikiisema hapa Bungeni ijengwe kwa kiwango cha lami lakini hadi leo hatujapata majibu ya kuridhisha ama utekelezaji. Barabara hii ina umuhimu mkubwa kwani inaunganisha Majimbo takribani manne ya Bagamoyo, Mkuranga, Kibaha Vijijini na Kibaha Mji. Kwa umuhimu wake, hakika barabara hii inahitaji ijengwe kwa kiwango cha lami hasa ikizingatiwa kila Mbunge aliywahi kuongoza Jimbo hili amewahi kuizungumzia.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kipindi cha kampeni mgombea wa nafasi ya Urais wakati huo ambaye hivi sasa ndio Rais wetu, alituahidi wana Kibaha Vijijini kujengewa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita 10. Hii ni ahadi ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambapo mpaka leo hii tumebakiza takribani mwaka na nusu wa kumaliza kipindi cha miaka mitano haijatekelezwa. Ni aibu kwa Chama kwani tukirudi tena kuomba ridhaa kwa wananchi hawa tutawaambia nini? Ni vema ahadi zote za Mheshimiwa Rais alizoahidi kutekelezwa kwa wakati kabla

hajamaliza muda wake. Namuomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho atupatie majibu ya hoja hizi ili nasi wana Kibaha Vijijiini tuwe na matumaini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano, hususan Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ya ujenzi wa miundombinu katika maeneo mbalimbali nchini. Naomba kusema, naunga mkono bajeti hii kama sehemu ya kuunga mkono juhudhi hizi za Mheshimiwa Rais na Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ujenzi wa barabara ya Kahama - Geita uanze. Kwa miaka mitatu mfululizo tumekuwa tunatenga bajeti lakini fedha hazitolewi na ujenzi hauanzi. Hii ni bajeti ya mwisho kabla ya uchaguzi mwakani, hatuna cha kuwaambia wananchi. Mheshimiwa Rais pamoja na llani kuahidi, pia aliahidi wakati wa kampeni mwaka 2015 na alipofanya ziara Shinyanga mwaka 2017, bado ujenzi hauanzi. Naomba sana, tuanze ujenzi hata kidogo ili tupate cha kusema mwakani.

Mheshimiwa Spika, pili, usanifu wa barabara za Kahama - Bulige - Solwe - Mwanangwa, Kahama - Nyang'hwale - Busisi, Kahama - Kaliua - Mpanda na Kagongwa - Itobo - Bukene - Tabora. Ukamilishwe haraka ili ujenzi uanze kama llani yetu ya CCM ya mwaka 2015/2020 ilivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, tatu, ujenzi wa reli kwa *SGR* kati ya Dodoma - Tabora - Isaka - Mwanza utaanza lini?

Mheshimiwa Spika, nne, ujenzi wa reli ya kisasa Isaka - Kigali umefikia hatua gani?

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa nia ya kifufua reli yetu ya Tanga Moshi ambayo ni mwokozi mkubwa sana kwa wananchi wa kanda nzima ya Kaskazini, kwani kwenye suala la usafirishaji mizigo na imleepusha barabara yetu kuharibika mara kwa mara kutokana na mizigo mingi kupita kwa njia ya barabara. Tunaomba mradi huu uwekewe mkazo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, naiomba Wizara ione umuhimu wa kupanua barabara ya Dodoma inayoenda Dar es Salaam, maana kwa sasa hasa wakazi wa njia hiyo wameshaanza kukumbana na tatizo la foleni hasa kipindi cha jioni na asubuhi.

Mheshimiwa Spika, pia bado matumizi mabaya ya mitandao yanaendelea. Watu wamekuwa wakitapeliwa na hata kutuma vitu visivyoofaa kwa jamii yetu na hivyo kupelekea mmomonyoko wa maadili kwa vitendo vyta ukatili. Naiomba Wizara itoe adhabu kali na ziwe hadharani ili watu waogope kutenda mambo yasiyofaa. Anayeadhibiwa itangazwe na wengine wasikie waogope na wao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri tunaomba ukarabati ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani kwa kiwango cha lami. Barabara hii imekuwa ni kero ya muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, pia barabara ya Bagamoyo – Msata, matuta yamezidi, yapunguzwe kama zilivyo barabara za *highway* nyingine.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Tanga vitendea kazi vyake ni chakavu sana na ni bandari muhimu sana kwa ustawi wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia kuliko mizigo kulundikana bandari ya Dar es Salaam, Bandari za Tanga na Mtwara ziimarishwe na mizigo igawanywe kikanda ili kuzijengea uwezo Bandari za Tanga na Mtwara na kupunguza mlundikano sehemu moja.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, tunaomba mtujengee uwanja wa ndege Manyara Babati pale eneo la Magugu. Pia tunaomba mawasiliano ya simu Kijiji cha Himiti, Chemchem, Imbilili na Babati Mjini.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunaomba mwalipe fidia wananchi walio pembezoni mwa barabara za lami mita 12.5 zilizoongezeka. *All the best.*

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuleta bajeti yenyε vipaumbele vya miundombinu inayochochea ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwenye utekelezaji, kipande cha barabara ya Kidahwe - Kibondo - Nyakanazi kinachotekelzwa kutoka Nyakanazi ni Nyakanazi - Kabingo kilometra 50, siyo Nyakanazi - Kibondo. Nashauri Wizara isahihishe kwa sababu kati ya Kabingo na Kibondo kuna kilometra 50 ambazo hazina Mkandarasi, ndiyo maana kwenye mradi utakaofadhiliwa na AFDB zinaonekana kilometra 260 za Kabingo – Kibondo – Kasulu – Manyovu. (*I stand to be corrected*)

Mheshimiwa Spika, wakazi wa Mkoa wa Kigoma katika wilaya zote za Kigoma, Uvinza, Kasulu, Buhigwe, Kibondo na Kakonko wanafanya biashara zao nyingi katika Kanda ya Ziwa, hususan Mwanza na Shinyanga. Naishukuru Wizara kwa kuliona hili na kutenga fedha za kujenga barabara yote ya Nyakanazi – Kabingo – Kibondo – Kasulu - Manyovu ili kuunganisha Mkoa wa Kigoma na mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kama ufuatao:-

(i) Mkandarasi wa Nyakanazi - Kabingo asimamiwe kwa ukaribu, *he is very slow*. Tulipokagua utekelezaji na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mkandarasi alikuwa ametekeleza asilimia 60 tu na tayari alikuwa na siku 986 nje ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwa kipande cha Kabingo - Manyovu AFDB utaratibu wa fidia uanze mapema.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itekeleze ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli ya 2015 ya kujenga kilometra tatu za barabara za lami Mjini Kakonko. Kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri, *RC* wa Kigoma, kupitia *TANROADS* ameshatuma Wizara ya Ujenzi makisio ya gharama ya kujenga kilometra tatu za Mjini Kakonko. Chonde chonde, hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mkinga – Maramba – Mng’aro, Mlalo hadi Lushoto ipo chini ya Wakala wa Barabara ya Mkoa. Barabara hii inaunganisha Wilaya za Mkinga na Lushoto, lakini pia na pacha ya kwenda Korogwe na wilaya jirani ya Same Mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, mara zote kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo barabara hii tumekuwa tukiipitisha katika vikao vyetu vya *RCC* ili itengewe fedha kwa ajili ya upembuzi na usanifu wa kina (*detailed design*) mara zote inapofika katika ngazi ya Taifa, *budgets* inakatwa. Tunataka kujua kulikoni? Tanga - Lushoto tunakosea wapi? Barabara hii Lushoto - Mlalo yenye kilometra 45 ni muhimu sana na kiungo kikubwa cha uchumi kwa wananchi wa Usambara. Tunataka kujua kwa nini?

Mheshimiwa Spika, sisi tunaipanga barabara hii katika mipango yetu kwa kuzingatia vipaumbele. Tunapenda kupata taarifa rasmi kutoka Serikali. Hivyo Serikali itoe umuhimu wa kipekee kwa barabara hii angalau hata ijengwe kwa kiwango cha lami hata kwa awamu za kilomita 10 kwa kila mwaka. Vinginevyo kutokana na jiografia ya Lushoto ilivyo, ikibaki kwa kiwango cha changarawe, Serikali inapoteza pesa nyingi sana katika *periodic maintenance*.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina viwanda 14 vinavyochakata samaki katika Mikoa ya Mara, Mwanza na Kagera, lakini kwa bahati mbaya kutokana na kutokuwa na ndege za mizigo, minofu hii inasafirishwa kwenda Nairobi na Entebbe hata Kigali ambako wenzetu wanapata mapato ya *export*.

Mheshimiwa Spika, hivyo, nashauri, pamoja na ndege za abiria, Serikali iweke mkazo kuanzisha mchakato wa kununua ndege za mizigo ili pia viwanja mbalimbali vinavyoboreshwa viweze kutumika kusafirisha mazao mbalimbali kwenda nje ya nchi kwa masoko.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itazame upya gharama zetu za viwanja vya ndege ili viweze kuvutia hata ndege za mizigo kuweza kutua katika viwanja yetu.

Mheshimiwa Spika, shirika letu la ndege *ATCL* linafanya vizuri sana lakini bado linakumbana na ushindani mkubwa kutoka mashirika ya ndege ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana hata wenzetu katika Kanda ya Afrika Mashariki miradi hii wanaichukulia kama miradi ya kimkakati, hivyo kusimamiwa na Serikali nzima tofauti na hapa kwetu ambapo jukumu hilo imeachwa kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pekee.

Mheshimiwa Spika, Mashirika kama *Emirates, Turkish, RwandAir* ni sehemu ya kukuza utalii na biashara ya Kimataifa katika nchi zao. Mfano, *RwandAir* inatumika kuitangaza Kigali kuwa kituo cha utalii wa mikutano ya Kimataifa. *Ethiopian Airways* inajulikana kwa kuchangia pato la nchi hiyo kupitia sekta hii ya usafirishaji. *Turkish Airline* inasifika kwa kuifanya Uturuki kuwa kituo kikubwa cha biashara katika Bara la Ulaya na Bara la Asia. *Qatar Airways* imeubadili mji wa Doha na kuwa kituo kikubwa cha biashara cha Asia na kuhakikisha kuwa mji wa Doha unakuwa kiunganishi muhimu cha ndege zote za Kimataifa kwenda maeneo tofauti duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo na mifano hiyo, *ATCL* inawezaje kuhimili ushindani na mashirika haya ikiwa huko kwao yana misamaha ya kodi, hayalipi gharama za kutua viwanjani na uongozaji wa ndege yanaendesha au ni sehemu ya mfumo wa uendeshaji ya viwanja vikubwa vyta ndege (mfano, Dubai Kigali, Doha na Addis Ababa) yanamiliki kampuni za kutoa huduma viwanjani (*ground handling company*), yanamiliki kampuni za kutayarisha vyakula vinavyotumika ndani ya ndege (*inflight catering*) na hata kumiliki shule za kutayarisha wafanyakazi wa karakana za utengenezaji wa ndege kwa mashirika mengine ya ndege. Kwa bahati mbaya gharama zote hizi hapa kwetu zimeachwa chini ya Shirika la *ATCL*.

Mheshimiwa Spika, gharama za uendeshaji wa *ATCL* ambazo zinatokana na utoaji wa huduma zinazotolewa na mashirika ya Serikali ambazo zinaweza kutazamwa kama walivyofanya wenzetu kwa mashirika yao.

Mheshimiwa Spika, tusipoitazama *ATCL* kama uwekezaji wa kimkakati wa Kitaifa wenyewe nia ya kuwezesha sekta nyingine, hapo baadaye tutakwama, suala linaweza kuchukuliwa kwamba ni biashara ya muda mfupi, lakini tukilipa mtizamo wa Kitaifa litakuwa na tija ambayo ndiyo dhumi kubwa ya kulifufua Shirika hili.

Mheshimiwa Spika, hivyo, badala ya kung'ang'ania tozo la għarama za kutua uwanjani na uongozaji ndege (*landing and air navigation charges*) ni vyema kuitazama *ATCL* kama sehemu ya utoaji huduma hizo isiyohitaj kulinpiwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, uwanja wa ndege wa Tanga unapaswa kufanyiwa ukarabati ili nasi tuweze kusafiri na kusafirisha bidhaa zetu kwenda kwenye masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa

Waziri, Naibu Mawaziri na timu yote ya Wizara katika utekelezaji wa majukumu yao kwa ufanisi pamoja na changamoto za ufinyu wa fedha (bajeti).

Mheshimiwa Spika, katika mradi na ujenzi na reli ya *SGR*ni muhimu katika vituo vikubwa kama vile Morogoro, Dar es Salaam na Dodoma kungejengwa maeneo makubwa ya kuegesha magari (*car parking*) ili kuwezesha abiria wanaotoka Dodoma kwenda Dar es Salaam kwa usafiri binafsi, wanapofika Morogoro wanaweza kuegesha magari yao kwenye maengesho hayo, kisha kupanda *SGR*kwa safari ya Dar es Salaam na hivyo hivyo wanaporudi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Londo – Lumecha – Songea inapitia katika maeneo muhimu kwa uchumi wa nchi pamoja na mradi *SAGCOT* (kilimo cha biashara) lakini barabara hii bado haijapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, barabara kipande ya Kidatu – Ifakara, ujenzi wa kiwango cha lami unasuasua sana. Sababu ni uzembe wa Mkandarasi. Tunaiomba Serikali itafakari kama kweli Mkandarasi anao uwezo wa kumaliza kazi katika muda muafaka. Aidha, Serikali ilete taarifa ni mkakati gani utafanya katika kumsukuma Mkandarasi kumaliza kazi ndani ya muda.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ifakara – Lupiro – Malinyi – Londo – Lumecha – Songea imefunguka toka mwaka 2017, lakini haipitiki kabisa kipande cha Mpepo - Londo kutokana na milima haijachongwa. Tunaiomba Serikali irekebishe maeneo korofi yote ili barabara hii itumike kwa kuwaunganisha wakazi wa Mikoa ya Morogoro na Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ifaka – Lupiro – Malinyi – Londo imetolewa ahadi na Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli katika kampeni zake za uchaguzi mwaka 2015, lakini pia alirudia ahadi hiyo katika ziara yake mkoani Morogoro Mei, 2018 kuanza kujenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika majumuisho, naomba itoe maelezo katika kutekeleza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais kwa wakazi wa Morogoro/Ruvuma. Ahsante.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Mafinga – Mgololo, barabara ya Mgololo – Mtwango, barabara ya Kasanga – Mtambula – Nyigo ni za muhimu sana katika kuinua uchumi kwa wananchi wa Mufindi. Kuna viwanda vya Chai, Mbao na Karatasi (*MPM*). Naomba Serikali ianze kujenga kiwango cha lami ili ziweze kupidika kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali isimamie ujenzi wa barabara za vijiji ambazo zinatengenezwa na Wakala wa Barabara Vijiji na Mijini (*TARURA*). Barabara ya Maguvani, Mtambale, Kilolo imeharibika sana wananchi wanashindwa kusafirisha mazao yao. Barabara ya Nyanyembe hadi Idunda, barabara ya Malangali hadi Idunda, barabara ya Sawala hadi Iyegeya, barabara ya Maduma hadi Makugali zipo chini ya *TARURA*, zimeharibika sana. Naomba Serikali itengeneze barabara hii ili wananchi waweze kusafirisha mizigo yao, pia kurahisisha shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ijenje minara katika Kata ya Idete, Ihowanza, Idunda na Kiyowela. Maeneo haya hakuna mawasiliano kabisa, wananchi wanashindwa kupata mawasiliano kiurahisi.

Mhesimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja.

**MHE. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu Waziri nawapongeza kwa kazi nzuri mnayoifanya. Nashukuru kwa miradi inayoendelea kujengwa *Airport* ya Mwanza, ujenzi wa jumba la wasafiri ufanyike haraka kuondoa adha ya wasafiri iliyopo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa ndege Dodoma – Mwanza ni vyema ukaanza kutokana na ukweli usiofichika

kuwa Kanda ya Ziwa ina abiria wengi sana wanaotumia usafiri wa anga. Nashukuru nimeona fedha imetengwa kwa ajili ya fidia kwa wananchi wanaotakiwa kuondolewa eneo la viwanja. Ombi langu ni kwamba zoezi lisichukue muda mrefu ili kuondoa kero iliyopo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nimeona fedha kidogo zimetengwa katika baadhi ya barabara. Ombi langu ni kwamba barabara ya Nyakato Veta – Igombe TX kilomita 18 ina miaka mitatu; inajengwa kila mwaka kilomita moja. Naomba angalau ikamilishwe ili kuondoa mgongamano.

Aidha, barabara ya *Airport* – Kayenze – Nyanguge Kilomita 45 ijengwe kwa kiwango cha lami ili kurahisisha wasafiri wanaoshuka uwanja wa ndege waendao Musoma waweze kutumia barabara hii badala ya kupita mjini ambako msongamano unakuwa mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kivuko cha Kayenze – Baze unaendelea vizuri isipokuwa wasiwasi wangu ujenzi wa maegesho ya kivuko bado hawajaanza kujenga. Naomba angalau kivuko kinapokamilika kujengwa kiende sambamba na ujenzi na ukamilishaji wa maegesho hayo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi alitembelea Jimboni na kujionea adha kubwa ya wananchi wa Kigala Kata ya Buswelu kuwa na korongo kubwa ambalo limekuwa mto, limekosa daraja na tayari watoto walishachukuliwa na maji eneo hilo. Naomba ujenzi wa daraja hilo ufanyike.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano alitembelea Jimboni tukampeleka maeneo yenye kero ya mawasiliano, hakuna mawasiliano kabisa. Orodha ya maeneo tayari nilishakabidhi. Naomba utekelezaji ufanyike ili kuondoa adha ya mawasiliano. Ahsante.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya bajeti ya Wizara hii ya Ujenzi na Mawasiliano.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Timu yake kwa hotuba na ripoti nzuri.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kongwa (Hogoro) – Kibaya – Orkesimet – Oljoro – Arusha, ina mpango gani? Tunaomba tujengewe kwa awamu, Kongwa – Kibaya. Sababu ya barabara hii ni kusafirisha mazao toka Chemba, Kiteto, Kilindi na Handeni kwenda Dodoma na Dar es Salaam. Kwa kurahisisha barabara ya Babati – Kibaya – Dar es Salaam, Kondo – Kibaya – Dar es Salaam, Kilindi – Kibaya – Dar es Salaam, Kilindi – Kibaya – Dodoma, Chemba – Kibaya – Dodoma.

Mheshimiwa Spika, mizigo mingi toka Dar es Salaam kwenda Babati, Simanjiro, Chemba, Kiteto, Kilindi, Kondo yote inapita hapa. Tusaidieni kwa sababu hii ni *too economical*.

Mheshimiwa Spika, pia tunaomba kujua barabara ya Handeni – Kiberashi – Kibaya – Chemba – Kondo – Singida itajengwa lini kwa kiwango cha lami? Umuhimu wa barabara hii ni bomba la mafuta, bandari ya Tanga kwenda Kanda ya Ziwa, kuunganisha Mikoa ya Tanga, Manyara Dodoma na Singida.

Mheshimiwa Spika, naomba Mawasiliano, tupatiwe minara katika Kijiji cha Raiseli, Songambele, Kijunge, Rengatei, Sunya, Dongo, Mangungu na Namelok. Shahidi ni Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii muhimu kwa uchumi wa nchi yetu, hasa kwenye *transport economy*. Muda umefika sasa Serikali kuhakikisha inajenga ama kukarabati viwanja vya ndege katika Wilaya zote nchini. Kama bajeti hairuhusu, lazima ihakikishe basi mikoa yote ya nchi yetu ina viwanja vya ndege ambavyo vina hadhi za kupokea ndege za abiria ili kuweza kuharakisha safari toka sehemu moja ya nchi kwenda nyingine.

Mheshimiwa Spika, mfano, Mkoa wa Mara ni mkoa wenyewe fursa nyingi za kibiashara kama vile samaki toka Ziwa Victoria, biashara ya utalii maana tuna mbuga pale, tuna migodi na zaidi tuna kumbukumbu ya Baba wa Taida ambapo Mataifa mbalimbali wangependa kutembelea na kuweza kuingiza fedha kwenye mkoa wetu pamoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni aibu kwa kweli kuona mkoa ambao ametoka Baba wa Taifa hili na Rais wa Kwanza hadi leo hatuna uwanja wa ndege wenye hadhi na ambao ungepitika kwa maana ya ndege kutua muda wote. Nakumbuka kuna mwaka tulishashindwa kutua pale sababu ya mvua na uwanja ule *runway* yake siyo ya lami na ilikuwa ni Kumbukumbu ya Kifo cha Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikiongelea huu uwanja tangu Bunge la Kumi. Tunaomba sasa fedha ziende ili wale wananchi walipwe fidia na hatimaye uwanja ukarabatiwe na kupanuliwa ili wananchi wa Mara waweze kurahisishiwa usafiri wa kutoka sehemu mbalimbali za nchi kama ndege za *Precision Bombadierna* hata *Dream Liner* kutua. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho atueleze wananchi wa Mara juu ya hatua ya uwanja wa Mara, Musoma.

Mheshimiwa Spika, noamba pia kuzungumzia kuhusu usikivu hafifu wa mawasiliano kwenye baadhi ya maeneo Wilaya ya Tanze na hasa Jimbo la Tarime Mjini maeneo ya Mofabiri, Nkende ambapo Mheshimiwa Naibu Waziri alifika na kuahidi kushughulikia hasa Kata ya Ketave, Nbende, Ngendoto na Kuyananyori. Vilevile Jimbo la Tarime Vijijini hasa maeneo ya Mpabani, Sirari na kule Nyamundu, ni muhimu sasa hili lishughulikiwe maana tunapata Safaricom ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu *round about* iliyopo Tarime Mjini ambayo ni *junction* ya kwenda Sirari, Nyamagana, Mwanza na Soko Kuu. *Ille round about* inasababisha ajali nyingi sana na hasa kwa wageni maana sehemu ni finyu sana kuweza kuruhusu mzunguko wa magari

hasa makubwa (kama lori na mabasi). Pia ukifika unashindwa kujua unaanza wapi wala unaelekeea wapi. Tumeshazungumzia sana hili kwenye *Road Board* tangu mwaka 2017 na *TANROADS* Mara iliahidi kulishughulikia.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuondolewa ile *round about* na kuwekwa taa za barabarani ili ziweze kuongoza magari pale kama ile ya Mwenge inavyoruhusu magari ya kutoka Kawe/Lugalo, Mikocheni kwenda Ubungo na kwenda Posta (hiijunction ndiyo mfano). Hizi taa zitasaidia kuondoa ajali nyingi sana zinazopoteza maisha ya Watanzania lakini pia zitasaidia kupandisha hadhi Mji wa Tarime ambao unakua kwa kasi sana na upo jirani na nchi ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunaendelea kupata adha ya mtaro hasa kwenye barabara ya Nyamwaga kujaa hasa mvua inaponyesha, mitaro midogo haikidhi haja kabisa. Vilevile, maungio ya barabara za *TANROADS* kuingia kwenye mitaa zinaachwa bila maingilio kwa barabara nyingine, kukatika kwa mawasiliano kati ya barabara za *TANROADS* na zile za *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kujengewa daraja la Nyandogo linalounanisha watu wa Kata ya Nyandogo na Bunera pamoja na ukarabati au upanuzi wa daraja la Movi linaloenda uwanja wa ndege wa Magena.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu *ATCL*. Kwanza kabisa ielewewe kuwa naunga mkono uboreshaji wa Shirika la Ndege, ambapo kimekuwa ni kilio changu cha muda mrefu na tunatumia fedha za walipa kodi kulifufua. Naishauri Serikali kuiacha Menejimenti ya *ATCL* iwe huru kujiedhesha kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imeshauri vyema. Ili Shirika liwe na ufanisi, Serikali haina budi kuwaacha menejimenti waweze kupanga na kulisimamia Shirika, maana wao ndiyo wana utaalam wa biashara hii ya ndege kuliko sasa wanavyoingiliwa kibiashara, hili Shirika kuendeshwa

kisiasa na siyo kibashara. Ona wenzetu wa KQ, Ethiopia, Emirate, Shirika lolote la *operation*, mawasiliano na mengineyo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nimesoma hotuba yako vizuri sana, lakini nasikitika miradi ya Jimbo na mkoa wangu hazipo. Mradi wa lami Makao Makuu ya Jimbo la kisasa (Mwandoya); kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa barabara ya lami kutoka Bariadi – Kisesa Mwandoya – Mwanhanzi, Bukundi (Sibiti) - Egiguno.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ni wa kimkakati hasa baada ya ujenzi wa daraja la Sibiti kukamilika. Mradi huu utafungua uchumi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa Mara, Kagera, Mwanza, Simiyu na Shinyanga pamoja na nchi jirani za Kenya na Uganda.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, naungana na wote waliotangulia kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mimi ni shahidi wa kazi inayoendelea barabara ya Sanya Juu - Kamwanga.

Mheshimiwa Spika, naomba baada ya mkataba wa Ujenzi wa barabara ya Kiboriloni –Kikarara, Tsuduni – Kidia kusainiwa, tunaomba sasa ujenzi uanze kwa kasi kabisa baada ya subira ya miaka zaidi ya saba.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunaomba sehemu ya barabara ya kutoka Chuo cha Wanyamapori – Mweka hadi lango la Mlima Kilimanjaro ijengwe kwa kiwango cha lami ili kuondoa kero kwa watalii, kwani ni ya charangawe na ni nyembamba sana. Bahati nzuri mvua nazo katika eneo hilo ni nytingi, hivyo kupelekea watalii kusukuma magari badala ya ku-*enjoysafari*.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa kazi nzuri iliyofanywa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Marangu na Machame kuelekea Mlima Kilimanjaro, imesaidia kuboresha mazingira ya utalii.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara ni jambo kubwa na zuri. Ni vizuri ushirikishwaji huu ufanyike kwenye Wilaya zote nchini. Kuna kazi za ujenzi wa barabara katika wilaya zetu zinazoweza kutekelezwa na wanawake. Nashauri mwongozo wa Wizara kuhusu suala hili uelekeze kila Wilaya kutoa mafunzo kwa wanawake na kuweka asilimia ya kazi ambazo lazima zifanywe na wanawake.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha agusie mafunzo ya utunzaji barabara kwa jamii. *TANROAD* na *TARURA* watoe mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, kero kwa wale walioipa barabara ya Arusha - Moshi siku za karibuni watakulaliana nami kuwa hii ni moja ya barabara yenye msongamano mkubwa wa magari. Inachukua muda wa saa tatu kusafiri umbali wa kilometra 85 Tengeru - Himo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba mazungumzo kati ya Serikali na *JICA* yakamilike mapema ili hatimaye upanuzi wa barabara kutoka Tengeru hadi Himo ufanyike kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze na kumpongeza Waziri Mheshimiwa Eng. Kamwelwe, Manaibu Mawaziri Mheshimiwa Kwandikwa, Mheshimiwa Eng. Nditiye, Makatibu Wakuu na Watendaji wa taasisi zote kwa kazi nzuri sana zilizofanywa na kwa kuwasilisha hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu ujenzi wa viwanja vya ndege. Naishukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa ahadi ya ujenzi wa viwanja kikiwepo kiwanja cha Nduli Iringa. Nilikuwa naomba Serikali ijitahidi pia kutoa

fidia kwa wakati kwa wananchi walioguswa na upanuzi wa kiwanja hicho.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu Shirika la Ndege ATCL. Niungane na wote walioipongeza Serikali kwa ununuzi wa ndege sita. Napongeza pia kwa kuanzisha mfuko wa ndege katika kiwanja chetu cha Iringa, tunaamini sasa hata uchumi wetu kupitia utalii utaongezeka.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwa na *connection* ya kiwanja cha Dodoma angalau kuwa na miruko mfano Mwanza – Dodoma, Mbeya – Iringa, Dodoma – Songea, Dodoma – Dar es Salaam ili kuwe na urahisi wa Makao Makuu kufikika kwa urahisi na abiria ni wengi. Vilevile bei za nauli za ndege ziangaliwe ili abiria wapande wengi.

Mheshimiwa Spika, Sekta hii ya Ujenzi inafanya kazi nzuri sana hapa nchini. Napongeza sana kazi nzuri ya ujenzi wa barabara nchini ikiwepo na mkoa wetu wa Iringa. Katika Mkoa wa Iringa naomba Serikali iangalie na kujenga barabara ya mchepuo itakayosaidia kuchepusha magari makubwa sana kupitia katikati ya mji.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya magari makubwa kupita katikati ya mji, kwanza yanaweza kusababisha ajali na hatari kubwa mno. Barabara ni finyu na kuna maduka hoteli na biashara ambazo zinafanya wananchi kuegesha magari na vyombo vya moto katika barabara hiyo. Pia changamoto ni kwamba wafanyabiashara wanashindwa kufanya biashara. Ni lini sasa barabara hiyo ya mchepuo itajengwa ili kuchepusha hayo magari kupita katikati ya Mji wa Iringa?

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dodoma – Iringa, ukipita katika kona za Nyangoro, kuna maporomoko ya mawe na wakati wa mvua yanaongezeka. Nimeshauliza sana maswali kuhusiana na changamoto hiyo: Je, ni mkakati gani unawekwa ili kuondoa changamoto hiyo?

Mheshimiwa Spika, lingine ni ujenzi wa reli. Naipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa inayofanywa ya kwa ujenzi wa reli hiyo. Ukitamiliwa utasaidia hata uharibifu wa barabara zetu ambazo zinaharibika kwa kubeba mizigo mizito. Ujenzi huo mpaka sasa umefikia asilimia 50 *phase one* Dar es Salaam – Morogoro. Mradi huu ukitamiliwa, utaleta ajira 10,000,000. Ni kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa maboresho makubwa mbalimbali ya sheria na elimu kwa bodaboda na bajaji. Pongezi kwa mtambo wa *VTS*, umesaidia kupunguza ajali barabarani. Changamoto kubwa ni abiria, wakipata ajali wanapata taabu sana. Ni lini Serikali italeta sheria ya kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu?

Mheshimiwa Spika, *TTCL* wanafanya kazi nzuri sana. Je, yale madeni wanayodai katika taasisi za Serikali watalipwa kwa utaratibu gani?

Mheshimiwa Spika, *UCSAF* inafanya kazi nzuri sana, maeneo mengi yameweza kupata mawasiliano, lakini kuna maeneo bado hayajapata mawasiliano. Kwa mfano, Mafinga ni Kata ya Ideta, Ihowanza – Ipimo – Ihowasa – Kilolo – Kata ya Ihimbo.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kuititia njia ya maandishi nichangie bajeti ya Wizara hii muhimu katika ujenzi wa Taifa imara. Rejea ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwa sekta zote inaonyesha dhahiri kuwa ujenzi wa uchumi wa viwanda uko kwenye uelekeo sahihi na kasi inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba na kushauri *TPA* wakamilishe ujenzi wa mradi wa gati la Kyamkwikwi. Ukamilishaji wa mradi huu utawezesha sekta binafsi kujua mipaka ya mradi na kuweza kuendeleza eneo lilllobaki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Tano, kuititia Wizara hii kwa uwekezaji katika

vivuko. Naomba Wizara ifikirie maombi ya kupatiwa vivuko (*pantoni/ferry*).

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2012 nimekuwa nikiomba kivuko kwa ajili ya visiwa nya Bumbiile, Kelebe na Goziba. Kutokana na jitihada na mafanikio ya *TPA* kukamilisha ujenzi wa gati Kyamkwikwi, ni busara kijamii na kiuchumi kuweka vivuko ili tusaidie na kuokoa wananchi wanaosafiri ziwani.

Mheshimiwa Spika, Tanzania upande wa Mkoa wa Kagera tunayo mahitaji ya uwanja wa ndege mkubwa. Tunaomba na kushauri Serikali kwa njia zote isaidie uchumi wa mkoa huu kwa kuwekeza katika upanuzi wa uwanja wa ndege wa Bukoba au tujenge uwanja mpya sehemu ya Omukajunguti. Hoja hapa ni kuwa na uwanja wa ndege ambaao utawezesha ndege za mizigo kutua. Kagera lna fursa ya kuvutia; viwanda nya samaki na uzalishaji wa matunda na mboga kiurahisi kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi na maombi kwa *TANROADS* kupitia kwa Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote. Barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Muleba ujenzi unaendelea, hasa sehemu hii ya Muhutwe – Kamachumu. Naomba sehemu hii ya Muhutwe mpaka Kamachumu isimamiwe ili ikamilike kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile kipande cha Kamachumu/Ibuga mpaka Rutenge tunaomba kipigwe lami hasa ile sehemu ya Kamachumu *Islamic School* ambacho ni eneo korofii.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwaomba *TANROADS* kupitia Wizara kuboresha barabara za *TANROADS* za Rutenge – Bulyakashaju – Rubale – Izimbya – Kara. Barabara hii ni muhimu kwa kuwa inaunga Wilaya ya Muleba, Bukoba na Karagwe. Eneo ipitapo barabara hii ni mkanda muhimu kiuchumi kwani inalengwa kuwekeza ufugaji wa ng'ombe wa kisasa na kilimo.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuipongeza *TPA* kwa utendaji wa bandari wa sasa. Bandari hii kwa sasa inafanya kazi masaa 24 kwa siku, siku saba za juma. Ushauri ni Serikali kuhakikisha jamii yote za bandari (*Port Community*) kushirikiana ili kuongeza ufanisi mkubwa. Eneo moja dogo la kutolea mfano ni ukosefu wa ushirikiano wa *TPA* na *TANROAD* katika kupima mizigo, hali inayopelekea foleni eneo la Kurasini.

Mheshimiwa Spika, ni rahisi magari yanayotoka bandarini yapimwe yote uzito ndani ya eneo la bandari. Kazi hii inaweza kufanyika chini ya wadau wote wenye maslahi ikiwemo *TANROADS* na baada ya hapo magari yasipimwe au kusimamishwa mpaka yatoke eneo la jiji. Faida moja kubwa ni kuondoa foleni hali ambayo itaongeza kasi.

Mheshimiwa Spika, yapo madai kuwa bandari za Nakura, Beira, Durban na hata njia za Angola ni washindani wa bandari za Tanzania hasa Dar es Salaam. Kimsingi wateja wote wanaopita njia hizo wamelazimika kuititia huko baada ya njia ya Tanzania kuwa na vikwazo. Nashauri Serikali ziangalie maslahi mapana na kwa pamoja naomba vikwazo hivyo ili kuchangamka kwa biashara ya *TPA* kulete neema kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali inachelewesha miradi ya maendeleo ya miundombinu ya Mkoa wa Kigoma?

Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa kuendelea kuamini katika maendeleo ya Mkoa wa Kigoma na hususan Mji wa Kigoma kwa kuwekeza katika ujenzi wa Bandari Kavu ya Katoshu pamoja na ujenzi wa Bandari ndogo za Kibirizi na Ujiji.

Mheshimiwa Spika, miradi hii mitatu ikikamilika itawezesha uwepo wa gati katika eneo la mji wa asili wa

kibiashara wa Ujiji na kuwezesha ndoto yetu ya kurejesha hadhi ya Ujiji katika maendeleo ya nchi yetu. Miradi wa Bandari kavu ya Katosho utawezesha mizigo ya nchi za *DRC*, Zambia na Burundi inayopitia bandari ya Dar es Salaam kuchukuliwa Kigoma na hivyo kurahisisha biashara na hichi hizo jirani. Mamlaka ya Bandari pia wanajenga jengo la *OSBC* (*One Stop Center*) ambayo itarahisisha shughuli za ukusanyaji kodi, biashara na uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yetu kuwa *TRC* wanajiandaa nao ili ukamilikaji wa miradi hii uende sambamba na uwepo wa reli ya kusafirisha kwa urahisi mizigo ya Zambia, *DRC* na Burundi. Mambo haya yataingiza fedha kwenye mzunguko wa uchumi wa Mkoa wa Kigoma na kutoa ajira kwa wananchi wenzangu wa Manispaa ya Kigoma Ujiji.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mkurugenzi Mkuu wa *TPA* kwa kuendeleza miradi hii na hii ni ishara ya imani yake kwa ukuaji na maendeleo ya mji wetu na mkoa wetu wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kumpongeza Meneja wa *TANROADS* Kigoma kwa kuwezesha mikataba ya Barabara ya Manyovu - Kasulu - Kibondo (mpaka Nyakanazi) kupitia ufadhili wa *AFDB* na barabara ya Uvinza - Darajani kupitia *Kuwait Fund*. Miradi hii ni muhimu kwa Mkoa wa Kigoma kwa kuwa itauunganisha Mkoa wa Kigoma na Mikoa mingine na kurahisisha usafirishaji wa mazao na bidhaa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizo kwa watu wa *TPA* na *TANROADS* bado watu wa Kigoma wanalia kwa kuwa ipo miradi yao ya msingi inayokwamishwa na Serikali. Licha ya Jumuia ya Kimataifa kuelewa umuhimu wa Mkoa wa Kigoma kijografia na kiuchumi na hivyo kutoa fedha za miradi ya maendeleo itakayochochea shughuli za kiuchumi, Serikali ya CCM imekuwa inavuta miguu kutekeleza miradi hiyo. Nitawapa mifano michache ya namna Serikali ya CCM inavyohujumu Mkoa wetu wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, moja, Serikali ya Japan imeidhinisha mradi mkubwa wa kuboresha Bandari ya Kigoma wenyе thamani ya dola za Marekani milioni 40 (karibu shilingi za Kitanzania bilioni 100), lakini kwa mwaka mzima sasa Wizara ya Fedha haitaki kusaini mkataba ili zabuni itangazwe na kazi ianze. Fedha hizi ni msaada, siyo mkopo.

Mheshimiwa Spika, pili, hoja ya Serikali ni kuwa Serikali ya Japan inataka msamaha wa Kodi ya VATkwenye mradi huu, nayo haitaki. Sasa tunapewa mradi wa shilingi bilioni 100, bure, kisha tunataka na VATkwenye vifaa vinavyofumika kwenye mradi huo huo kweli! Serikali inaweza kupata mapato mengi mno ya kodi ikiwa mradi huu wa upanuzi wa bandari ya Kigoma utafanyika. Kwa nini waukwamishe kwa mapato kiduchu tu ya VAT ya sasa? Kwa nini Serikali haioni picha kubwa?

Mheshimiwa Spika, tatu, Jumuia ya Ulaya (*EU*) kupitia Benki yao ya Uwekezaji (*European Investments Bank*) wameidhinisha fedha, dola milioni 20 sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la abiria katika uwanja wa ndege wa Kigoma na kuupanua uwanja ili ndege kubwa zitue kwa ajili ya kuunganisha nchi za maziwa makuu na Mji wetu. Tangu mwaka 2018 Januari, zabuni imetangazwa, mpaka leo kazi haijaanza wakati uwanja wa ndege wa Chato ambao haukuwa kwenye Bajeti ya Serikali wala mpango wa maendeleo umejengwa na kukamilika. Serikali inataka kuwaambia nini watu wa Kigoma? Wao sio Watanzania kuliko ndugu zao wa Tabora?

Mheshimiwa Spika, nne, hata miradi ambayo fedha tayari zipo, haifanywi. Kwa mfano, Manispaa ya Kigoma Ujiji tuna mradi mkubwa wa kuweka *pavements* kwenye mitaa yetu ili kutoa maarifa ya ufundi na kisha ajira kwa vijana. Lengo la mradi huu ni kutumia shughuli za ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya kuongeza ajira kwa vijana na mzunguko wa fedha kwa wananchi kwa vijana na wanawake kupewa mafunzo ya ujenzi wa hizo barabara za mawe (*pavements*) na kisha kupitia vikundi vyao kupewa kazi hizo za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imegoma kusaini mkataba wa Mkandarasi Mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi na usanifu wa mradi huu pamoja na kuwa mfadhlili wa mradi, Serikali ya Ubelgiji iko tayari na fedha ziko tayari. Mradi huu ambaao ungehusu kata nane za Manispaa ya Kigoma Ujiji ungekuwa ni '*Game Changer*' kwa uchumi wa Kigoma. Nao unakwamishwa. Kwa nini?

Mheshimiwa Spika, watu wa Kigoma ni wavumilivu sana. Wamevumilia kwa zaidi ya miaka hii 58 ya Uhuru wa Tanganyika na 55 ya uwepo wa Tanzania bila kuunganishwa na mkoa wowote, wakatengwa kiuchumi. Uvumilivu huo una kikomo, hasa ikiwa ni kwa miradi yao ya miundombinu na uchumi inahujumiwa namna hii. Serikali isiwafikishe huko.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara hii ilipaswa ichochee ukuaji wa uchumi, kwa nini uchumi unadumaa?

Mheshimiwa Spika, mgawo wa bajeti ya maendeleo kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Tano ni ufuatao: 2016/2017 shilingi triliioni 4.8 ambayo ilikuwa 40.3 % ya bajeti yote ya maendeleo ya shilingi triliioni 11.8. Mwaka 2017/2018 shilingi tirilioni 4.9 ambayo ilikuwa 40.8 % ya bajeti yote ya maendeleo ya shilingi triliioni 11.9. Mwaka 2018/2019 shilingi triliioni 4.1 ambayo ilikuwa 34.5 % ya bajeti yote ya maendeleo ya shilingi triliioni 12.0.

Mheshimiwa Spika, mpaka mwaka huu wa fedha unaoisha 2018/2019 Bunge litakuwa limeidhinisha kwa Wizara hii jumla ya shilingi triliioni 13.8 katika miaka mitatu ya bajeti. Ni wastani wa 38.5% ya bajeti yote ya maendeleo kwa miaka hii mitatu. Tukipitisha bajeti ya 2019/2020 tutakuwa tumewekeza jumla ya shilingi triliioni 40.6 na kati ya hizo shilingi 18.7 zitakuwa zimekwenda Wizara hii ya Miundombinu. Hii ni sawa na 46% ya Bajeti yote ya maendeleo kwa miaka minne kati ya mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, ni halali kabisa kwa Wabunge kuhoji: ajira ngapi za kudumu zimetengenezwa kutokana na

uwekezaji huu? Sekta zipi nyingine za uchumi zimechochewa (*multiplier effect*) kutokana na uwekezaji huu? Kwa Mfano, viwanda vingapi vya chuma vimeanzishwa? Pato la Taifa limeongezeka kwa kiasi gani kutokana na uwekezaji huu? Watanzania wangapi wameondokana na umasikini? Mapato ya Serikali yameongezeka kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kikawaida ni Bajeti ya Wizara hii ndiyo ambayo matumizi/manunuzi yake hutumika kuchochaea shughuli za kiuchumi na kupeleka fedha kwa wananchi kupitia miradi mbalimbali ya ujenzi. Hali iko hivyo duniani kote, lakini hapa nchini kwetu hali ni tofauti, manunuzi mengi ya ujenzi yanayofanywa kupitia Wizara hii hayajachochaea ukuaji wa uchumi, bali namna yalivyofanyika yamekuwa ni sababu ya kudumaza uchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ilirithi Bajeti ya Serikali ya Awamu ya Nne ya Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 ilipoingia madarakani Novemba 5, 2015. Katika wakati husika kasi ya mzunguko wa fedha nchini (M3) ilikuwa ni 15%. Hivyo kila shilingi nchini ilibadilisha na wastani wa mikono 15 kwenye matumizi ya kiuchumi. *Ripoti ya BOT ya Mwezi Machi, 2019* (inayoelezea hali ya Februari, 2019) inaonyesha kuwa M3 kwa sasa ni 3% tu. Mzunguko wa fedha umepungua mno.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mitatu tumepitisha *Tanzania Shillings 1.5 trillion* kununua ndege. Fedha zote hizo zimekwenda nje ya nchi, hakuna hata shilingi moja kati ya hizo ambayo imerudi nchini. Hiyo ni moja ya sababu ya kupungua kwa mzunguko wa fedha nchini.

Mheshimiwa Spika, tuna ujenzi wa *SGR*. Mkataba wa Ubia Kati ya Kampuni ya Yapi Merkezi ya Uturuki na kampuni ya *Construção África SA* ya Ureno, naambiba Kampuni hii imejitoa kwenye mkataba huu na kwamba kuna Kampuni nyingine iko kwenye huu mradi. Ikumbukwe ni hiyo kampuni ya Ureno ndiyo yenye usoefu wa ujenzi wa reli. Je, mbia mpya wa Yapi Merkezi ni Nani? Uwezo wake ukoje? Tumefanya *Due Diligence* ili mambo ya *Indo Power* ya kwenye korosho yasijirudie? Taifa linapata nini?

Mheshimiwa Spika, tumerudia makosa tuliyoafanya wakati wa ujenzi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam. Mwezi Septemba, 2012, Wizara ya Fedha kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya *Exim*ya China walitiana saini makubaliano ya mkopo wa miaka 33 yenye thamani ya dola za Kimarekani bilioni 1.225 kwa riba ya 2% kwa ajili ya ujenzi wa bomba la gesi linalouganisha eneo la Msimbati na Mnazibay mpaka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kampuni zilizoshinda zabuni ya ujenzi huu ni *China Petroleum Technology and Development Corporation (CPTDC)* na *China Petroleum Pipeline Engineering Corporation (CPPEC)*, ambapo kila kitu kilichotumika kwenye ujenzi wa bomba hili kilitoka China na hakuna ushahidi wa kitaalam wa ujenzi huo ulioachwa nchini. Ndicho tunachofanya kwenye *SGR*. Mbaya zaidi kwa sasa tunatoa hela ndani kupeleka Uturuki na za nje tunazozikopa ni kutoka mabenki ya kibiashara yenye riba kubwa.

Mheshimiwa Spika, reli inahitaji chuma na chuma cha pua (*Iron and Steel*), mbao ngumu, wahandisi na mafundi mchundo wengi, vifaa vidogo kama *screws* na kadhalika. Je, Serikali imefungamanisha ajenda ya viwanda na ujenzi wa reli? Serikali inaweza kutuambia viwanda vingapi vyatugavi kwenye bidhaa za ujenzi wa reli vimejengwa?

Mheshimiwa Spika, viwanda vingapi vyatugavi mataruma vimejengwa nchini? Tunaagiza mataruma na hata *screws* za kufungia mataruma kutoka nje ya nchi. Ndiyo maana trillioni zote hizi tunazoipa Wizara kwa miaka hii mitatu hazisaidii ukuaji wa uchumi.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na afya njema. Pia, nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wenyeviti wa Bodi zote zilizoko kwenye Wizara hii na Wakurugenzi Watendaji wote wa Taasisi zote zilizopo kwenye Wizara hii kwa kazi kubwa ya kumsaidia

Mheshimiwa Rais katika kuwatumikia Watanzania. Nawaombea dua kwa Mwenyezi Mungu awape umri mrefu ili waweze kutimiza ndoto ya Mheshimiwa Rais ya kuona Tanzania mpya. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nachingwea – Liwale ni barabara muhimu sana kwa Wilaya ya Liwale, kwani ndiyo barabara pekee inayoiunganisha Wilaya ya Liwale na Makao Makuu ya Mkoa wa Lindi. Naishukuru Serikali kwa kuanza upembuzi na usanifu wa kina kwa barabara hii. Nashauri kazi hii iambatane na utafutaji wa fedha ili kuweza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nangurukuru – Liwale ni barabara ya kiuchumi kwa Wilaya ya Liwale. Usafirishaji wa mazao kutoka Liwale hadi Dar es Salaam kuititia Lindi kuna kilometra zaidi ya 750 ukillinganisha na kilometra 500 ukipitia barabara ya Liwale to Nangurukuru. Hivyo, utaona umuhimu wa barabara hii ni mkubwa sana kwa uchumi wa Wana-Liwale na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nashukuru tena kuona kwenye bajeti hii kumetengwa shilingi milioni 300 ili kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kama ilivyo barabara ya Nachingwea – Liwale. Hii pia Wizara ianze kutafuta fedha ili hatimaye nayo pia iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mawasiliano, nashukuru kwa kupatiwa mawasiliano kuititia kampuni ya *Halotel* kwa kutujengea minara kwenye kata tisa ambapo sasa kwa kiwango kikubwa upo unafuu kidogo, lakini bado kuna shida ya mawasiliano katika Vijiji vya Ndapata, Mkutano, Kikulyungu, Nahoro, Kipelele, Mtungunyu na Mtawatawa. Vijiji hivi hali ni mbaya sana katika mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Spika, Reli ya *TAZARA* bado ni reli muhimu sana kwa nchi yetu. Kwa upande wa Zambia wao kwa reli hii siyo kipaumbele chao tena pamoja na kuwa uongozi wa reli hii kwa kiasi kikubwa unamilikiwa na upande wa Zambia. Wazambia wamekuwa wakifanya vitendo vyta kuhujumu reli

hii kwa makusudi. Hivyo basi, imefika wakati Serikali yetu ifanye mapitio ya Sheria ya Uendeshaji wa Reli ya *TAZARA*. Hatua hii ni muhimu na iende sambamba na kuifutia madeni au kuipa mtaji ili iweze kujidoresha.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Mabaharia (*DMI*) ni chuo kilichosahauliwa kwa muda mrefu ndiyo maana uwepo wa chuo hiki hata kwa jamii hautambuliwi pamoja na kuwa nchi yetu imezungukwa na bahari na maziwa makuu. Sekta ya Uvubi na Usafiri wa Majini una mchango mdogo katika nchi yetu kutohana na kupuza chuo hiki muhimu kwa uchumi wa nchi yetu. Nashauri Serikali ianze sasa kuimarisha chuo hiki ikiwa ni pamoja na kikitangaza, kwani sasa chuo hiki hakitambuliwi katika jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usafirishaji (*NIT*) ni chuo muhimu sana kwa sasa, hasa kwa kuwa nchi yetu inakwenda kuimarisha Sekta ya Uchukuzi kwa kujenga reli ya kisasa, ununuzi wa ndege na ujenzi wa meli kwenye maziwa makuu. Hivyo basi, Serikali ione umuhimu wa kuimarisha chuo hiki, kwani ndiyo chuo kinachokwenda kupika wataalam katika Sekta ya Uchukuzi. Chuo hiki ni lazima kipewe fedha za kutosha ili kiweze kujiimarisha kupata wataalam.

Mheshimiwa Spika, sera ya kuunganisha mikoa yetu kwa barabara za lami ni jambo linalopaswa kupewa kipaumbele kwa mikoa yote kwani bado kuna mikoa ambayo hadi leo haijaunganishwa siyo tu kwa barabara za lami, hata kwa barabara za changarawe. Mfano, Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Lindi, mikoa hii, pamoja na kuwa mikoa jirani lakini pia ni mikoa muhimu sana kwa kukuza uchumi wa mikoa hiyo miwili. Hivyo, naiomba Serikali kufanya kila iwezavyo kutekeleza sera hii ya kuunganisha Mikoa ya Lindi na Morogoro kwa barabara ya Liwale – Mahenge (Ulanga).

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege wa Lindi, pamoja na kuwa moja ya viwanja vya zamani nchini, hakijapewa kipaumbele. Hii ni kudumaza maendeleo ya Mkoa wa Lindi sambamba na Bandari ya Lindi. Nashauri

Bandari ya Uvuvi ya Kanda ya Kusini ikajengwe Lindi ili kuinua uchumi wa Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo yote hapo juu, naunga mkono hoja hii muhimu kwa uchumi wa nchi yetu.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu kwa manufaa ya wananchi wa Mkoa wa Mara na Watanzania wote kwa ujumla. Tunaona bajeti kwa miaka mitatu zimetengwa shilingi trilioni 13, nataka Serikali itueleze tunapata ajira kiasi gani na *return* yake ni nini? Fedha nydingi zinaenda kwenye upembuzi yakinifu, sijui huu upembuzi yakinifu utaisha lini ili ujenzi kamili uweze kuanza kwa sababu Wilaya ya Ranya, *TARURA* haijapata fedha za maendeleo ya barabara kwa miaka miwili mfululizo sasa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Musoma – Busekela ni ya kilometra 42, lakini fedha zilizotolewa ni kilometra tano tu, bado kilometra 37. Zitaishaje bila fedha? Naishauri Serikali ipeleke fedha za kumalizia hizo kilometra 37 zilizobakia.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Wanyere – Kitaryo imekatika, hakuna mawasiliano sababu ya daraja. Kwa sababu Wizara hii imetengewa fedha nydingi, naishauri Serikali ifanye jitihada za haraka kuhakikisha inatengeneza barabara hii na daraja ambalo limeshaua watoto zaidi ya 20 ili kunusuru maafa mengine yasitokee.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mara una miradi viporo vingi sana kama vile Bunda – Kisorya, Makutano – Sanzate, Mugumu – Tabora B zinazohitajika fedha ili kuweza kukamilisha miradi hii viporo.

Mheshimiwa Spika, kuna *round about* ya Tarime inasababisha ajali za mara kwa mara. Naishauri Serikali iondoe hiyo *round about* badala yake ziwekwe taa za kuongozea kama vile Barabara ya Mwenge kwenda Mikocheni, Kawe, Mjini, Ubungo ili kuepusha ajali zinazotokea mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mara una uwanja wa ndege ambao unapanuliwa (unaongezwa), kitu ambacho kinaathiri wananchi wanaozunguka (waliopakana) na uwanja huo kwani wananchi hawa walishafanyiwa tathmini takribani mwaka na miezi minne, lakini wananchi hawa hadi sasa hawajui hatma yao kwani tathmini imefanyika bila wao kujua nyumba zao zimefanyiwa tathmini ya shilingi ngapi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ikarudie kufanya tathmini na suala hili liwe shirkishi kwa wananchi wenyewe na Serikali iwatengee (iwape) eneo lingine la kwenda kujenga nyumba nyingine pale ambapo watakuwa wameshalipwa fedha za kupisha uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Spika, *TBA* hawafanyiwi ushindani na makampuni binafsi ndiyo maana kazi za *TBA* ni *substandard* (kazi nyingi za Serikali zinafanywa na *TBA* matokeo yake majengo mengi hayakidhi viwango). Mfano mradi wa nyumba Bunju zinazojengwa na *TBA* haziko *competitive* hata kidogo kwani haziwezi kuingia kwenye ushindani kwa vile hazina viwango. Kwanza hazina (hakuna) *social services* kama vile zahanati, shule, barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nyumba hizi hazinunuli? Ni kwa sababu bei iko juu sana kulinganisha na ubora wa nyumba zenyewe, kwani hadi sasa nyumba zilizonunuliwa ni chache sana, nyingi hazijanunuliwa, zimekaa tu na kuendelea kuharibika. Naishauri Serikali, hizi nyumba zipangishwe badala ya zinavyokaa zenyewe bila watu.

Mheshimiwa Spika, lingine katika Sekta ya Ujenzi; kati ya wakandarasi Watanzania asilimia 80, ni wakandarasi asilimia 20 tu ndiyo wanaopata kazi. Ni aibu kwa nchi yetu ya Tanzania. Ushauri wangu ni kwamba Serikali itoe ujuzi kwa Wakandarasi wetu ili tuweze kuwatumia kuokoa pesa zinazokwenda nje.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, naomba barabara ya Kitosi – Mwampembe yenyе urefu wa kilometa 67 ambayo ni mkombozi kwa Tarafa ya Wampembe ichukuliwe na Serikali au la, iwe inapewa fedha ya kutosha toka *TANROADS*. Wizara inatoa shilingi 90,000/=, inatosha nini? Tafadhali naomba tuwe tunaipa fedha zaidi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Nkara – Kala ni ya Halmashauri/*TARURA* lakini haipewi fedha. Adha zinazowapata wananchi wa Kata ya Kala inatakiwa iondolewe na Serikali. Tafadhali ongezeni fedha *TARURA* ili iwe na uwezo wa kusaidia wananchi vijijiini.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Katongoro kwenda Ninde haipitiki kabisa, kisa hakuna fedha ya kuhudumia barabara hiyo ya kwenda Ninde na kata yote isifikasi. Tafuteni fedha kuimarisha *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu mitandao ya simu. Naomba vijiji vifuatavyo vipate mawasiliano ya simu: Kijiji cha Kasapa, Kata ya Sintali, Kijiji cha Msamba Kata ya Ninde, Kijiji cha Kisambara Kata ya Ninde, Kijiji cha Lupata Kata ya Wampembe, Kijiji cha Izinga Kata ya Wampembe na Kijiji cha Mialambo Kata ya Kizumbi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ijenge magati ya meli katika vituo vya Namansi (Kijiji), Kijiji cha Ninde, Kijiji cha Msamba na bandari katika Mji mdogo wa Wampembe. Mji huu una biashara za kutosha na wasafiri wengi. Hali ilivyo inapokuja meli ni hatari kwa wasafiri na matukio kadhaa yanatokea.

Mheshimiwa Spika, nashauri Bandari ya Wampembe na barabara toka Sumbawanga hadi Wampembe ikijengwa ni rahisi kupata soko la nafaka ya mahindi Kongo Kusini.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri,

Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara kwa kazi kubwa na ngumu wanayoifanya. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Urambo, tunashukuru sana barabara iliyokamilika katikati ya Mji wa Urambo. Ahsanteni sana kwa kuongeza uzuri wa mji. Barabara hii nzuri ni muhimu sana ikaunganishwa vizuri pale inapoungana/kuchepuka kutoka barabara inayoendelea Kigoma.

Mheshimiwa Spika, tunaomba *round about* kwanza kwa usalama wa magari na waenda kwa miguu na pili kwa mwonekano mzuri wa barabara inayoingia mjini.

Mheshimiwa Spika, tunaomba minara ya simu katika maeneo ambayo hayana mtandao wa simu; na orodha ya kata na vijiji imeletwa Wizarani.

Mheshimiwa Spika, tunaomba maombi mawili ya *round about* na minara yafikiriwe kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Ahsante sana.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambayo ni Wizara muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu kwenye maeneo tofauti ili kuinua uchumi kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, *TARURA* waongezewe fedha. Suala hili limekuwa na changamoto kubwa sana, kwani *TARURA* wana barabara nyingi za mitaa na vijiji lakini wanashindwa kumaliza kazi hizi kwa muda muafaka kwa sababu ya fedha kidogo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni usafiri wa meli kwa Ziwa Tanganyika. Kumekuwa na changamoto kubwa ya usafiri wa majini kwa wananchi wanaotumia Ziwa Tanganyika kwa usafiri na biashara. Naomba kujua Serikali imefikia wapi katika suala la Meli ya *MV Liemba*?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko ya Wakandarasi wengi kutokulipwa fedha zao kwa wakati. Kwa nini Serikali isiwalipe Wakandarasi ili kuleta ufanisi kwa kazi na miradi wanayopewa ili kuinua uchumi wa nchi?

Mheshimiwa Spika, ni vyema kufuatilia na kujua uwezo halisi wa Wakandarasi kabla ya kupewa tenda ili kuepusha hasara zinazoweza kujitokeza kwa Taifa, kwani kumekuwa na malalamiko mengi sana na kupelekeea vitendo vya rushwa na kupelekeea hasara kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa viwanja vya ndege ni vyema liangaliwe kwa umakini kwa kuangalia aina ya watu kwa maeneo ambayo wana uhitaji wa viwanja vya ndege ili kuweza kukuza uchumi kwa eneo husika na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, suala la *TBA* bado kuna changamoto; miradi mingi wanayopewa haikamiliki kwa wakati. Pia napenda kuishauri Serikali ipunguze miradi kwa *TBA* na badala yake wapewe watu wengine ambapo kukiwa na ushindani huleta ufanisi mzuri wa kazi na uharaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la watu kuwekewa X za kijani na nyekundu: kumekuwa na mkanganyiko katika utekelezaji wa suala hili pale inapotokea nyumba moja ina alama mbili ya kulipwa na kubomolewa, wanawaambia wananchi wabomoe. Je, suala hili likoje? Tunaomba ufanuzi.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Serikali kwa upana wake na Wizara kwa namna ya pekee kwa kazi kubwa na ya mfano wanayoifanya, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Tunduru Kaskazini na bajeti ya mwaka 2019/2020; nashukuru kwa miradi ifuatayo ambayo imetengewa fedha. Ukarasa wa 348, daraja F/ Mbanga – shilingi milioni 20 (ukamilishaji). Nina mashaka na

utoshelevu wa fedha hizi kukamilisha kazi iliyobaki kwani bado kazi ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 348 - matengenezo ya barabara Mjmwema – Ngapa - Tunduru/Nachingwea *Boarder* – shilingi milioni 60. Barabara hii ni muhimu saba kuunganisha Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Lindi. Tunaomba ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 348 - ujenzi wa Daraja la Ngapa katika barabara ya Mindu – Ngapa - Nachingwea/ Tunduru *Boarder* – shilingi milioni 60. Jumla ya fedha zote ni shilingi milioni 140. Kwa kulinganisha na mahitaji katika Jimbo langu, pamoja na kushukuru kwa tulichopata tunaomba yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya miradi muhimu sana. Barabara ya Mkoa – Mjmwema - Nachingwea *Boarder*. Tunaomba ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, ikiwemo Daraja la mto Lumesule.

Mheshimiwa Spika, barabara ya mchepuo (*Tunduru-By-Pass*), ni bahati mbaya haikupata umuhimu katika bajeti, tunaomba izingatiwe.

Mheshimiwa Spika, Tunduru *Round about*, hapa kuna barabara inayokwenda Songea, Mtwara na Msumbiji. Makutano ya barabara katika eneo hili, wakati wa ujenzi wa barabara za Tunduru – Matenanga – Namtumbo – NA – Tunduru – Nakapanya – Mangaka - Taaluma na umuhimu, ikiwemo usalama. Tunaomba yafanyike marekebisho ya kitaalam.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mironde – *Kalulu - Selous Game Reserve*, ni barabara ya kimkakati; katika ziara yake Waziri Mkuu akiwa Kalulu alielezea umuhimu wake na kusisitiza kwamba Serikali itaijenga.

Mheshimia Spika, nashukuru sana.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ina majukumu yanayogusa sekta kama tatu zenyenye kuwezesha maendeleo ya nchi na wananchi. Katika aya ya 26 ukurasa wa 15, Waziri ameeleza ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam – Chalinze, kilomita 144 haujaanza kutokana na maamuzi ya Serikali kusogeza mbele utelekezaji wa mradi huu ili kukamilisha kwanza miradi hii inayoendelea, ni vyema katika majamuisho Serikali ikaeleza imesogeza mbele mradi huu mpaka lini.

Mheshimiwa Spika, aidha, ni kwa nini Serikali imeamua kusogeza mbele wakati ambapo imesema mara kadhaa kwamba mwaka 2011 kwamba mradi huu ungetekelezwa kwa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (*PPP*) na ungekuwa na barabara za kulipia ili kurejesha ghamama za ujenzi ambazo zingeingiwa na sekta binafsi katika ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika aya ya 44, ukurasa wa 24, Serikali ieleze sababu ya barabaa za Kimara - Korogwe Maji Chumvi (kilomita tatu) na sehemu ya Goba - Madale (kilomita tano), ujenzi wake kwenda taratibu. Aidha, ni kwa nini Serikali imechukua kipande kidogo tu cha Mloganzila – Kisopwa (kilomita moja) kati ya kilomita 14.66 za barabara ya Kibamba – Kisopwa – Kwembe - Makondeko. Kwa kasi hii ndogo itachukua miaka takribani 14 kwa barabara hiyo kukamilika.

Mheshimiwa Spika, katika aya ya 54, ukurasa wa 30, imeelezwa kuwa ujenzi wa barabara ya juu (*interchange*) katika barabara ya Ubungo umefika asilimia 28. Hii inaonesha kwamba kasi ya ujenzi ni ndogo sana. Wizara ikumbuke kwamba mwezi Machi, 2017 wakati na uzinduzi wa ujenzi Mheshimiwa Rais aliagiza kwamba ujenzi wa barabara ya juu ya Ubungo ukamilike ndani ya miezi 30. Kwa agizo hilo ujenzi unapaswa kukamilika mwezi Agosti, 2019, hivyo kwa asilimia 28 mwezi Mei ni kiwango cha chini sana cha utekelezaji. Hivyo Wizara itoe maelezo ni mikakati gani imewekwa kuharakisha ujenzi ili ukamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwenye aya ya 60, ukurasa wa 33, Waziri ameeleza kuwa upanuzi wa barabara kwa njia nane

kwa sehemu ya Kimara - Kiluvya (kilomita 19.2) unaendelea ambao utarahisisha pia upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji. Hata hivyo, Waziri hajaeleza ujenzi wa barabara umefikia hatua gani, eneo ambalo ni vyema akalieleza katika majumuisho. Katika kipindi cha uzinduzi uliofanywa na Rais ambapo walishiriki, kasi ya ujenzi kabla na baada ilikuwa kubwa. Hata hivyo, kwa sasa kasi imepungua, hivyo ni vyema Wizara ikafuatilia kwa karibu kuwezesha ujenzi kufanywa kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba mkandarasi kama alivyofanya kwa eneo la Kibamba CCM kusawazisha eneo kwa ajili ya kituo cha muda cha daladala afanye hivyo katika eneo la Kiluvya. Eneo la kusimama daladala lilishawekwa, Wizara ihakikishe *SUMATRA* inasimamia daladala zifike Kiluvya badala ya kuishia Kibamba CCM na kufanya wananchi wa Kiluvya waingie gharama kubwa za kupanda mabasi yanayokwenda Kibaha, Mkoani Pwani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Rais kuhusu fidia ya wananchi kupisha ujenzi wa barabara hii, naomba Wizara irejee hukumu ya kesi ya wananchi wa Mbezi ambao walifungua kesi Mahakama Kuu Kitengo cha Ardhi ambapo mahakama ilitamka wananchi wanastahili fidia.

Mheshimiwa Spika, katika aya ya 73, ukurasa wa 40, kwenye hotuba ya Waziri amezungumzia kuhusu miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya pili hadi ya tano. Naomba majibu ya Serikali katika majumuisho ni awamu ipi hasa ya ujenzi itahusisha ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka kwa kipande cha kutoka Kimara mpaka Kiluvya?

Mheshimiwa Spika, ili kutoiingiza nchi kwenye gharama kama iliyotokea katika maeneo mengine ambapo lami na miundombinu mingine imelazimika kuvunjwa kuwezesha kujengwa kwa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka, ni vyema upanuzi wa sasa wa barabara ya Morogoro kutoka Kimara mpaka Kiluvya ukahuishwa pia ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wakala wa Majengo Tanzania (*TBA*) umekuwa ukikabidhiwa ujenzi wa majengo mbalimbali ya Serikali. Katika kazi ambazo *TBA* imefanya hivi sasa ni pamoja na ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya Mpya ya Ubungo. Naomba *TBA* iharakishe kukamilisha ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya. Aidha, naomba *TBA* izishauri mamlaka zinazohusika ili ujenzi huo unaofanyika katika Kata ya Kwembe, Mtaa wa Luguruni uhusishe pia ujenzi wa Ofisi ya Mbunge ambayo katika michoro ya sasa haijawekwa.

Mheshimiwa Spika, *TBA* pia ikutanishwe na Shirikia la Nyumba (*NHC*) kujadiliana kuhusu uendelezaji wa Mji wa Viungani (*Satellite Town*) wa Luguruni ili majengo ya Serikali na nyumba za viongozi katika eneo hilo *TBA* ifuatilie kwa karibu ujenzi uanze. Serikali illipaa muda mrefu fidia katika eneo hilo lakini shughuli za uendelezaji zimesimama.

Mheshimiwa Spika, juu ya kasma 4138 ya kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam (*De-congestion of Dar es Salaam Roads*) kipande cha Goba - Makongo kilomita nne kimetengewa milioni 310 tu ilihali kuna kipande cha barabara ambacho kwa muda mrefu hakijawekewa lami. Naomba kiwango cha fedha kiongezwe kuwezesha eneo lote lilllobaki kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwenye kasma 4161 kuhusu Madaraja ya Juu (*Dares Salaam Road Flyovers*) kwa upande wa *Ubungo Interchange* zimetengewa milioni 145 tu kwa upande wa fedha za ndani. Napendekeza kiwango kiongezwe kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo kwenye mkataba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kasma 4132 juu ya fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali katika kutekeleza miradi ya mkoa barabara ya Kimara – Bonyokwa – Kinyerezi yenye kilomita mbili umetengewa katika bajeti milioni 60 peke yake wakati barabara hii ina hali mbaya. Naomba *TANROADS* watembelee barabara hii na kufanya matengenezo

yanayostahili. Hali iko hivyo pia kwa barabara ya Goba - Matosa - Temboni.

Mheshimiwa Spika, katika kasma 2326 kumetengwa milioni 150 kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina (*feasibility study and design*) kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya juu (*interchange*) Mbezi mwisho kuelekea eneo kutakapojengwa kituo cha mabasi ya mikoani. Naomba mchakato huu uharakishwe ili uende sanjari na ujenzi wa kituo unaoendelea pamoja na upanuzi wa barabara kuwa njia nane.

Mheshimiwa Spika, fedha za Mfuko wa Barabara zitatumika pia kuboresha kwenda *DSD*barabara ya Kunguru - *TATEDO* (kilomita tano) ambapo kumetengwa milioni 120. Naomba hatua hiyo iende mbele zaidi kwa kujenga daraja katika eneo la Muungano, Kata ya Goba katika sehemu inayounganisha na Salasala.

Mheshimiwa Spika, katika kiambatisho namba 5(B-2), ukurasa 381, Waziri ameелеza barabara ambazo zitafanyiwa marekebisho ya muda maalum (*period maintenance*) kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Hata hivyo, katika orodha hiyo hakuna hata barabara moja ya Jimbo la Kibamba kwenye Kata sita za Kwembe, Msigani, Mbezi Luis, Goba, Saranga na Kibamba. Hivyo ni vyema Wizara ikaongeza katika orodha hiyo barabara muhimu za Jimbo la Kibamba zenye kuunganisha Mkoa wa Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani na zenye kuunganisha Wilaya ya Ubungo na Wilaya za Kinondoni na Ilala katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kati ya barabara ambazo ni muhimu *TANROADS*ikazichukua na kuzifanyia matengenezo ya haraka ni Temboni kwa Msuguri – Msingwa ambayo inaunganisha mpaka Wilaya ya Ilala. Kihistoria, barabara hii *TANROADS* iliwahi kuitengeneza lakini baadhi ya wananchi wakaenda mahakamani miaka mingi nyuma hali iliyofanya *TANROADS*kuacha kuihudumia kwa muda mrefu. Mgogoro huo umemalizika lakini *TANROADS* na *TARURA* bado wanarushiana mpira mpaka sasa kuhusu kuihudumia. Pamoja

na kuwa *TARURA* wameanza matengenezo madogo, naomba barabara hii ichukuliwe na *TARURA* ili ifanyiwe matengenezo makubwa na hatimaye ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwenye sehemu (b) juu ya barabara za mikoa za changarawe/udongo. Matengenezo ya barabara zilizopo kwenye Jimbo la Kibamba yamekuwa yakifanyika lakini sio kwenye kiwango cha kuridhisha. Barabara hizo baadhi zimetajwa kwenye ukurasa wa 390 za Kibamba Shule – Magoe Mpiji na Makabe Junction – Mbezi Msakuzi. Naomba katika majumuisho, Serikali ieleteze ni lini itafanya matengenezo yenye kiwango. Pia kwa barabara kutoka Mbezi kupitia Mpiji Magoe – Mabwepande mpaka Bunju. Barabara ina vipande kadhaa ambavyo viko kwenye hali mbaya ikiwemo kipande cha barabara kilichomo ndani ya Pori la Akiba la Pande.

Mheshimiwa Spika, Wakaguzi watembelee barabara hii na matengenezo yafanywe. Kwa upande mwingine, Serikali ieleteze ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami kama ambavyo Serikali iliahidi miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, kwenye kiambatisho namba 5(D-2) juu ya matengenezo makubwa ya madaraja na makalavati (*bridge major repair*) kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Nashukuru kwa kalavati (*box culvert*) la Msakuzi katika barabara ya Kibamba Shule – Mpiji Magohe limejumuishwa na kutengewa milioni 340. Naomba ujenzi wa *box culvert* hilo ufanyike kwa haraka. Aidha, naomba maelezo ya Serikali ya sababu za Kibwegere *box culvert* kutengewa shilingi milioni 10 tu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya uchukuzi, Serikali ihakikisha ujenzi wa reli kwa kiwango cha kisasa (*SGR*) unatumia kwa kiasi kikubwa malighafi kutoka ndani ikiwemo matumizi ya chuma kutoka Mchuchuma na Liganga ili kuhakikisha sehemu kubwa ya fedha zinabaki katika mzunguko wa ndani. Kamati za Kisikta zinazohusika zipewe nafasi ya kuangalia Mikataba mikubwa ya Ujenzi na

Uchukuzi ili kuhakikisha maslahi ya kiuchumi ya nchi yanalindwa kikamilifu.

**MHE. ZAINABU M. AMIRI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Isack Kamwelwe, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Atashasta Nditiye kwa juhudini kubwa wanazozifanya katika kusimamia miradi mbalimbali katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iweke vifaa vya uokoaji maeneo ya barabara kuu, mfano, gari la zimamoto, winchi, magari ya *breakdown* ili kuweza kusaidia uokoaji pindi ajali itokeapo na pia kuondoa msongamano barabarani wa magari endapo gari litapinduka na kuzuia magari, itachukua muda mfupi kushughullikia zoezi la kutoa gari hilo na magari kuendelea na safari.

Mheshimiwa Spika, pia naishauri Serikali ifanye ukaguzi wa mara kwa mara hususan *SUMATRA* katika magari ya mizigo (maroli) ili kuona ubora wake maana mengi ni machakavu pia ubebaji mzigo mara nyingi ni hatarishi kwa vyombo vingine vya usafiri. Mara nyingi magari haya hutazamwa uzito wa mzigo uliobeba katika mizani tu, ukilinganisha na magari ya abiria ambapo kila kituo kikubwa cha mabasi, hufanyiwa ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itoe elimu ya kutosha hasa katika magari makubwa ya mizigo kwa madereva wake, kuacha tabia ya kupaki maroli pembezoni mwa barabara mahala pasipostahiki, mfano Kibaigwa, Chalinze na kadhalika (*double parking*) na kupelekea usumbufu kwa magari yanayopita maana barabara inakuwa finyu na mara nyingine hupelekea ajali kutokea.

Mheshimiwa Spika, vile vile naishauri Serikali iweke vidhibiti mwendo katika magari ya mizigo maana yanaenda kwa mwendo wa kasi wa kupelekea kusababisha ajari kwa magari mengine, mfano mabasi ya abiria ambayo

wamewekwa vidhibiti mwendo na hatimaye kupelekea vifo kwa wananchi wasio na hatia.

Mheshimiwa Spika, naishauri pia Serikali iboreshe viwanja vyote vya ndege nchini ili viweze kufanya kazi kwa masaa 24, yaani usiku na mchana. Viwanja vingi vya ndege mfano, Kiwanja cha Ndege Dodoma wakati wa usiku ndege haiwezi kutua kutokana na ukosefu wa taa za kuongozea ndege.

Mheshimiwa Spika, naishauri vile vile Serikali iboreshe mizani iliyopo maeneo ya Mikese, Morogoro, maana kumekuwa na msongamano mkubwa wa magari na ukizingatia eneo la mizani lipo karibu kabisa na barabara kuu na hii ndiyo sababu, kumekuwa na msongamano hivyo nashauri Serikali iboreshe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawaombea Mheshimiwa Waziri na Naibu wake afya njema na maisha marefu ili wazidi kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe J. Magufuli, Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Mhandisi Isack Kamwelwe, Naibu Waziri Mheshimiwa Kwandikwa, Naibu Waziri Mheshimiwa Mhandisi Nditiye, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara husika. Mheshimiwa Waziri ameacha historia Pwani kwenye maji, nina hakika na barabara atazitendea haki, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa usimamizi mzuri na kufuata ilani kwani miradi mingi imeweza kuvuka na kupiga hatua na kuleta sura nyingine nchini. Hii ni kwa sababu Mheshimiwa Rais Magufuli ameamua kuleta maendeleo nchini. Kwani tumeona ununuzi wa ndege, ukarabati vya viwanja vya ndege na hata Wilaya yetu ya Mafia imepata fedha kwa ajili ya matengenezo ya Mafia.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ukarabati wa Bandari ya Dar es Salaam, Mtwara, Tanga pia tunaishukuru Serikali kwa ujenzi wa Bandari ya Nyamisati na ukarabati, tunaomba ukarabati Gati la Kilindoni, Mafia uende sambamba kwani ndiyo itakuwa mwanzo/mwisho wa safari zote za wananchi wa Mafia na kuinua uchumi na kuendeleza Kisiwa cha Mafia na hata idadi ya watalii itaongezeka. Naomba kupata maelezo lini kazi hiyo itaanza.

Mheshimiwa Spika, jiografia ya Mkoa wa Pwani iko katika hali ya kutegemeana na mikoa mingine nchini na pia kiungo cha safari zote za mikoani. Napenda kujua ujenzi wa barabara ambazo ni kiungo kikuu kwa wilaya nyingine na hata mikoa utaanza lini. Mfano, barabara ya Kisarawe – Maneromango – Vikumburu - Mloka, hii barabara ni muhimu sana na hasa kwa sasa ambapo kuna ujenzi wa mradi wa umeme Rufiji.

Mheshimiwa Spika, mkoa una visiwa vidogo vidogo vingi katika Wilaya ya Kibiti, Mafia, Mkuranga na Rufiji, tunaomba bajeti zinazokuja wafikirie kupeleka boti za uhakika ili wananchi wa maeneo hayo nao wawe na uhakika wa safari na kupata huduma muhimu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la mawasiliano kwenye Mkoa wa Pwani kwenye baadhi ya maeneo, kwingine mawasiliano ya simu na maeneo mengine mawasiliano ya redia hasa *Radio TBC*. Mfano, Wilaya ya Kisarawe ambako kuna minara yote/baadhi ya *TV/Radio* lakini bado kuna maeneo hawapati/kusikia chombo hicho cha Taifa, ikiwemo Wilaya ya Mafia na baadhi ya maeneo na hata mawasiliano ya simu. Hili suala linalelewaka kwenye ofisi ya Mheshimiwa Waziri, hivyo napenda kupata majibu ya ufumbuzi wa matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kupata taarifa rasmi ya lini Kisiwa cha Mafia kitapata chombo/meli/boti/feri ya uhakika kwa ajili ya wananchi wa Mafia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa ya kuchangia hoja hii muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Namshukuru Mungu kwa rehema na neema yake kwa Bunge letu na uongozi mzima. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Kamwelwe na Manaibu wake wote na watendaji kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yangu ya lleje imepata fedha za kujenga barabara kuu ya Mpemba - Isonpole kwa kiwango cha lami na tayari kaziimeanza. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa barabara hii ambayo ilikuwa ni ahadi yake na vile vile iko kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM ya 2015. Ahsante sana Mheshimiwa Rais, wana lleje wana deni kubwa kwake, wameingoja barabara hii miaka 42.

Mheshimiwa Spika, ziko barabara za *TARURA* Wilayani lleje ambazo kwa ugumu wake hazitaweza kujengwa na *TARURA*. Tulipeleka maombi ili zifikiriwe kujengwa na Wizara ya Ujenzi. Aidha, kuna barabara ambazo madaraja yalikatwa na mvua tangu 2016 na kwa hivyo wananchi wa Chitete na Mlale hawana mawasiliano kupitia llanga kitongoji kinachopakana na Wilaya ya Vwawa. Tunaomba sana watufikirie wana lleje watupatie fedha za kujenga miundombinu ya lleje, kwani ni migumu sana na hii imekuwa kikwazo kikubwa cha maendeleo ya kiuchumi kwa Wilaya ya lleje.

Mheshimiwa Spika, naambatanisha kwa barua husika maombi yetu kwa maandishi ili watufikirie.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BALOZI. DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Katika Jimbo la Nkenge, Wilaya ya Misenyi tuna ahadi tano muhimu za viongozi wetu ambazo zilitolewa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu uliopita. Naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano achukue hatua za haraka kutekeleza ahadi hizo. Ahadi hizo ni pamoja na:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuongeza kasi ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Katoma hadi Bukwali. Barabara hii ni muhimu sana na inaunganisha Tanzania na Uganda. Ni ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, pili, kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kajai hadi Hospitali Teule ya Wilaya ya Mugane. Ni ahadi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, tatu, barabara ya Mutukula hadi Minziro, kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahadi hii ilitolewa na Mheshimiwa Rais alipozindua *one boarder post* ya Mutukula.

Mheshimiwa Spika, nne, barabara ya kutoka Kituo cha Afya cha Kabyaile hadi Gera. Ahadi hii ilitolewa na Mheshimiwa Rais alipotembelea Kituo cha Afya cha Kabyaile.

Mheshimiwa Spika, tano, ujenzi wa kiwango cha lami wa kilometra tatu za lami Makao Makuu ya Wilaya (Kyaka – Bunazi). Ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, kivuko kipyka kati ya Bugorola – Ukara. Pamoja na jithada za Serikali kuanza mchakato wa utengenezaji wa kivuko kipyka baada ya ajali ya MV Nyerere, mchakato huu unaenda taratibu. Kivuko kilichopo sasa cha MVSaba Saba kina matatizo mengi hali inayoendeleza hofu kwa watumiaji wa kivuko hiki. Ombi, kivuko hiki kikikamilika mapema ili kinusuru maisha ya watu wetu. Pia uangaliwe uwezekano wa kuweka usafiri wa uhakika kwenye maeneo ya Kitale – Irugwa na Kakukuru – Gana.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa kifusi kwa ajili ya utengenezaji wa barabara. *TANROADS* wamekuwa na kawaida ya kuchimba kifusi/changarawe pembezoni mwa barabara jambo ambalo limekuwa linaacha mashimo makubwa sana na kusababisha vifo. Mfano, wiki iliyopita

tarehe 9 Mei, 2019 shimo lililochimbwa kwa ajili ya kifusi eneo la Kijiji cha Nakamwa, Kata ya Namilembe, Wilaya ya Ukerewe limesababisha vifo vya watu wawili baada ya gari kutumbukia katika shimo hilo. Hii ni moja ya matukio ya kifo na majeruhi ambayo yamekuwa yanatokea mara kwa mara Wilayani Ukerewe. Ushauri, baada ya shughuli za ujenzi wa barabara mashimo haya yamekuwa yanafukiwa.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya lami; kwa kuwa barabara ya Bukindo – Murutunguru – Bukonyo ni muhimu sana kwa uchumi wa ukerewe na sehemu ya barabara hii ilishafanyiwa upembuzi yakinifu, michoro na makadirio tayari yalishaandaliwa tayari yakisubiri upatikanaji wa fedha ili ijengwe. Naomba Wizara isaidie upatikanaji wa fedha ili barabara hii iweze kujengwa kwani ni kilometra saba tu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ujio wa Mheshimiwa Rais Visiwani Ukerewe tarehe 5 Septemba, 2018 aliahidi ujenzi wa barabara kilometra 14 kutoka Lugezi – Nansio kwa kiwango cha lami. Naomba Serikali itekeleze ahadi hii.

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Mheshimiwa Spika, miradi mbalimbali ya ujenzi wa viwanja vya ndege inaendelea katika Mikoa mbalimbali kama vile Msalato, Tabora, Kigoma, Mpanda, Mtwara, Shinyanga, Kilimanjaro, Sumbawanga, Arusha, Songwe na Mwanza. Kazi kubwa zinazofanyika katika miradi hiyo zinajumuisha ujenzi wa barabara za ndege, upanuzi na ukarabati wa maegesho ya ndege, ujenzi wa vituo vya waangalizi wa hali ya hewa, ujenzi wa barabara za kuingilia viwanja vya ndege, uboreshaji wa viwanja hivyo pamoja na ujenzi wa majengo ya abiria na mizigo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi zote hizo zinazoendelea bado kuna matatizo makubwa ya viwanja vingi kukosa uzio, tumeshuhudia Kiwanja cha Ndege cha Mwanza mtu aliyekatisha ndani ya kiwanja wakati ndege inaruka na kusababisha ajali. Lazima Serikali ihakikishe kila kiwanja cha ndege kinachojengwa na uzio unajengwa

kuepusha madhara yanayoweza kutokea kwa wanyama na binadamu wanakatisha ndani ya kiwanja hata Kamati ilipotembelea Kiwanja cha Dodoma mbwa alikatisha.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *UCSAF* ulianzishwa na Serikali kwa Sheria Na. 11 ya mwaka 2006 ukiwa na lengo la kupeleka huduma ya mawasiliano maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibashara. Mfuko huo umejitahidi kupeleka huduma hiyo lakini bado maeneo mengine yasiyo na mvuto wa kibashara hayajapata huduma hiyo. Tunaiomba Serikali ifanye kama kusudio la sheria iliyoanzisha Mfuko huo liliyo ili Watanzania wote huduma hiyo kwa ajili ya kuleta maendeleo.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Serikali nzima ya Awamu ya Tano na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa kazi kubwa inayoendelea kwenye Wizara hii. Naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kutoa pesa za kutosha kwa Wizara hii kulingana na bajeti ya 2018/2019 (*page 10 and 11*). Matumizi ya kawaida fedha iliyotoka ni asilimia 72.66 Vs asilimia 75. Miradi ya maendeleo fedha iliyotoka ni asilimia 60.98 Vs asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana miradi mikubwa ya Kitaifa kama ilivyoorodheshwa kitabuni ukurasa 53, 61, 117, 192 na kadhalika. Vile vile naipongeza sana Serikali kwa miradi mikubwa hapa Jijini na Mikoani Dodoma. Miradi hiyo ni Dodoma *outer ring roads pages 47, 176 and 271*. Ujenzi wa Ikulu ya Chamwino zikiwemo na barabara za kwenye Mji wa Chamwino. Ujenzi wa Mji ya Kiserikali pale Mtumba. Lami barabara ya Kongwa Junction – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe.

Mheshimiwa Spika, nina ombi mahsus; daraja katika Chilonwa na Nzali ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, mama Samia Suluhu Hassan. Barabara ya Chalinze Nyama – Chilonwa – Dabalo – Itiso – Chenene. Mawasiliano ya simu za mkononi katika Kata zifuatazo: Zajilwa (ina vijiji

vitatu) Segola (ina vijiji vitano) Haneti (ina vijiji vinne) Itiso (ina vijiji vinne) Dabalo (ina vijiji vitano) pia kwa sasa kuna Dabalo ni Mji mdogo na Membe (ina vijiji vitatu). Kata hizi tano zina mawasiliano hafifu tena kwa wakati fulani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi katika kuchangia mchango wangu na ushauri kwa Serikali katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, katika llani ya Uchaguzi ya CCM Serikali iliahidi kutekeleza ujenzi kwa kiwango cha lami katika barabara ya Singida – Sepuka – Ndago – Kizaga yenye urefu wa takriban kilometra 92. Barabara hii imekuwa barabara muhimu sana kwa sababu ya uzalishaji mkubwa wa mazao ya biashara kama vile alizeti, mahindi na kadhalika. Wakati wa kampeni za uchaguzi mwaka 2015 Mheshimiwa Rais alipita barabara hii na kuwaahidi wananchi kuwa barabara hii itajengwa kama ambavyo llani ya Uchaguzi wa CCM ilielekeza, lakini mpaka hapa tunapoongea utekelezaji wa llani katika ujenzi wa barabara hii bado unasuasua na hivyo kuwafanya wananchi kuendelea kupata adha katika kusafirisha mazao na hata mafuta yanayozalishwa katika viwanda ambavyo vimejengwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imekuwa ikitumia sana fedha nyingi katika matengenezo ya muda mfupi na mrefu ya barabara hii, jambo ambalo kama Serikali itaweka dhamira ya dhati katika kujenga barabara hii kwa Mwaka wa fedha 2018/19 Serikali ilitenga fedha za upembuzi yakinifu wa barabara hii lakini mpaka leo hatua za utekelzahi haueleweki.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta hii hii ya barabara, Serikali tangu mwaka 2010 imejenga madaraja katika barabara ya Sepuka – Mkandala – Mgungira tangu madaraja yakamiliike leo miaka 9 ujenzi wa tuta la barabara umeshindikana, hivi tumetumiaje pesa za umma kwa

mamilioni na kushindwa kukamilisha ujenzi wa tuta tu? Barabara hii ni muhimu sana katika kusafirisha mazao ya chakula na biashara kama vile mchele, alizeti na barabara hii ambayo inaungana na barabara ya Magereza –Mtuduru – lyumbu imekuwa ya muda mrefu sana mvua zimenyesha watu hawa wanakosa mawasiliano. Ni muda muafaka sasa kwa Serikali kutekeleza ujenzi wa barabara hii muhimu kwa wapiga kura wa Jimbo la Singida Magharibi.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, mawasiliano ya minara ya simu; jiografia ya Jimbo la Singida Magharibi iko *very complicated*. Toka nimekuja Bungeni tumekuwa tukipewa vitabu vinavyoonesha *distribution* ya minara ya simu, lakini hakuna utekelezaji wa mnara hata mmoja ambao uliahidiwa na Serikali ambao umejengwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018 wananchi wa Kata ya lyumbu walivamiwa na majambazi mchana na maduka yote kuporwa pesa, watu wetu hawakuweza kupata msaada sababu ya ubovu wa barabara na ukosefu wa minara ya simu, hakuna mawasiliano ya barabara wala ya simu na kata hizo ndizo zinaendesha halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ambapo asilimia 90 ya mapato yanatoka kule kutokana na kiwango kikubwa cha uzalishaji wa mchele ambao unauzwa Uganda, Rwanda na Burundi na kulilettea Taifa mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana vilitolewa vitabu hapa ambavyo *TTCL* wamepewa *market share* ili kufungwa minara katika maeneo hayo, lakini hakuna lolote liliofanyika katika kuwasaidia Watanzania hawa.

Mheshimiwa Spika, haya mambo yanatuweka mahali pagumu sana. Naomba minara ya mawasiliano ikafungwe Ikungi, Igholwe na maeneo yote ambayo wananchi wanapata matatizo katika Jimbo la Singida Magharibi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya CCM kwa kutumia zaidi ya bilioni mia mbili kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Daraja la Mto Sibiti ambalo litaunganisha Mkao wa Simiyu na Singida na kunufaisha kiuchumi na kijamii wananchi wa Mkao wa Simiyu hususan Wilaya ya Meatu. Naomba kusaidiwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kujenga kwa kiwango cha lami kilomita 25, ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi wa daraja. Pili, Daraja la Mto Sibiti halitakuwa na tija wakati mvua kubwa itakaponyesha mfululizo kama makorongo ya Itembe na Chombe yaliyopo barabara ya kutoka Sibiti hadi Mji wa Mwanhunzi hayatajengewa madaraja ya juu. Naomba makorongo hayo yajengewe daraja ili kuwepo na thamani ya pesa kwa daraja hilo kupitika kwa uhakika na magari ya aina zote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Kamwelwe, kwa kazi nzuri sana anayoifanya kuiongoza Wizara hii. Niwapongeze sana Manaibu Waziri Mheshimiwa John Kwandikwa na Mheshimiwa *Engineer Atashasta Nditiye* na Makatibu Wakuu wote kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kutujengea barabara ya Mwanga – Kikweni – Vuchama – Ngofi – Kiriche - Lomwe kwa kiwango cha lami. Sisi Wanamwanga tunamshukuru sana. Pia tunawashukuru sana kwa kuzipandisha barabara za Lembeni – Kilomeni - Ndorwe na barabara ya Kirby - Lang'ata Bora - Kifaru kuwa barabara za *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, suala langu la tatu ni mawasiliano, tunaishukuru sana Serikali kwa kulea uwekezaji katika mawasiliano. Hakika karibu nusu ya Watanzania wanamiliki simu ya mkononi, aidha, bei za kutumia mitandao ya simu zimeendelea kushuka. Hata hivyo, makampuni ya simu

yanatumia ujanja na *control/ya system* nzima kuwaonea na hata kuwaibia wananchi wanaotumia mitando yao. Unanunua kifurushi cha GB15 kwa Sh.20,000/=, kwa siku saba, unatumia GB 3 kwa siku zote saba, halafu GB 12 zinamezwu kwa kuwa siku saba zimekwisha. Huu ni wizi, mtumiaji wa simu akinunua kifurushi ni chake, lazima atumie mpaka kiishie ndiyo anunue kipyu. Huu ndiyo utaratibu wa kununua na kuuza mali.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENERWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wangu niliochangia katika Bunge lako Tukufu leo; nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua Waziri wa Ujenzi *Engineer Kamwelwe* ambaye natambua uchapa kazi wake, akiwa Naibu Waziri wa Mji alifanya kazi kubwa sana na kuwasaidia sana wananchi wa Jimbo langu. Pamoja na kazi kubwa aliyofanya, pamoja na mchango wangu wa kuongea Bungeni, nimwombe Waziri azingatie yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa kukubali ujenzi wa barabara ya Nyamwage – Utete kilomita 33, barabara hii ni ahadi ya Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ya tarehe 4/3/2017 kuwa itakamilika kabla ya 2020. Nimwombe Mheshimiwa Waziri sasa kwa kuwa upembuzi yakini fu umekamilika, aje sasa kuweka jiwe la msingi mwezi Juni ili wananchi wapate imani kwani barabara hii imeondoa Wabunge wengi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali inisaidie ili niweze kurudi 2020 – 2025. Nyamwage-Utete ni kiini cha anguko la kiuchumi Rufiji, ubovu wa miundombinu ni kero kubwa kwa wananchi, Mheshimiwa Waziri afike sasa Rufiji ili kuanza ujenzi wa barabara hii, pamoja na barabara ya Nyamwage Utete. Niombe Serikali ikubali ujenzi wa barabara ya Kibiti - Mloka ambayo inasaidia wakandarasi wanaojenga mradi wa umeme wa Rufiji (*Stiegler's*). Barabara hii ni chafu sana na haifai. Mradi huu wa umeme utachelewa sana iwapo barabara hii haitajengwa kwa kiwango cha lami. Ipo barabara ya Ikwiriri – Mloka ambayo ni kioo cha uchumi wa

Rufiji, tunaomba Serikali kuiweka katika mpango wa ujenzi wa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, ipo barabara ya Utete – Ngarambe, hii ni muhimu sana kufungua utalii wa Pwani ya Kusini. Ngarambe kuna Selou na pia kuna vipepeo vinavyoweza kuvutia watalii.

Mheshimiwa Spika, nyingine ni barabara ya Mloka - Kisarawe, Mloka - Kisaki, Bungu – Nyamisati – Kisiju - Mkuranga, Vikindu – Vianzi. Hizi ni barabara muhimu kwa kufungua uchumi wa Mkoa wa Pwani, ubovu wa miundombinu hii kumepelekea kudumaa kwa uchumi na ndiyo sababu kumekuwepo na wimbi kubwa la umaskini katika eneo la Pwani ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Kamwelwe, Manaibu Waziri Mheshimiwa Kwandikwa na Mheshimiwa Nditiye. Naishukuru Serikali kwa utekelezaji wa ujenzi wa Gati la Nyamisati. Gati hili ujenzi wake unakaribia kwisha na matarajio ni kufikia mwezi Juni mwaka huu. Tunashukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia naishukuru Serikali kwa kutenga fedha za kujenga kivuko kipyä katì ya Nyamisati na Kilindoni pamoja na ukweli kuwa kivuko hiki kilishatengewa fedha katika mwaka wa fedha 2018/2019 na mchakato wa kumpata mkandarasi ukaanza, lakini kwa masikitiko, kandarasi hii imefutwa kutokana na matatizo ya kisheria. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atupie macho utendaji wa Wakala wa Ufundı Umeme na Mitambo (*TEMESA*), wahakikishe mchakato wa ujenzi wa kivuko hiki cha Nyamisati na Kilindoni.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kivuko cha muda tulichopewa na Serikali kivuko kinachomilikiwa na Chuo cha Mabaharia (*DMI*), mpaka ninapoandika hapa bado

hakijaanza kazi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atie msukumo wa kuhakikisha boti hii inaanza kazi mara moja na hasa ukizingatia Gati la Nyamisati linakaribia kumalizika.

Mheshimiwa Spika, Gati la Kilindoni lipo katika hali mbaya sana, mbao zimechoka na ngazi ya kupanda na kushuka inakatikakatika mara kwa mara na kuhatarisha usalama wa abiria na mali zao. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (*TPA*) walishaahidi kufanya matengenezo makubwa ya gati hili. Kukamilika kwa Gati la Nyamisati itakuwa hakuna maana kama Gati la Kilindoni litakuwa bado bovu.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kilindoni mpaka Rasi Mkumbi kilomita 45 ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne na imo kwenye llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020. Mpaka sasa upembuzi wa kina na usanifu umeshakamillika, bado kutengewa fedha za ujenzi. Nimwombe Mheshimiwa Waziri chonde chonde ujenzi wa matengenezo ya muda wa (*periodical maintenance*) unakuwa mgumu kwani udongo wa kufanya matengenezo unakaribia kwisha. Hivyo ni bora barabara hii ikajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege wa Mafia; tunaomba uongezwe urefu sambamba na kuwekwa taa ili kuwezesha ndege kubwa za Kimataifa kutua moja kwa moja na kukuza utalii sambamba na ujenzi wa jengo la abiria (*Terminal building*)

Mheshimiwa Spika, suala la mawasiliano katika Kisiwa cha Mafia bado ni changamoto katika Vijiji vya Miburani, Banja, Kitohi na Chemchemi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hoja hii muhimu ya Wizara ya Ujenzi inayosimamia miundombinu ya barabara na mawasiliano nchini.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na uzima na kupata nafasi ya kuwa mmojawapo wa Waheshimiwa Wabunge kutoa mchango wa kuboresha kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya hii ya CCM ya Awamu ya Tatu kuititia Wizara hii ya Ujenzi. Nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa utekelezaji wa miradi mikubwa ya miundombinu ya usafiri nchini. Naipongeza Serikali kwa ujenzi wa reli ya kisasa (*SGR*) ya reli ya katika toka Dar es Salam mpaka Kigoma.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali kwa sababu reli hii ujenzi wa Awamu ya Kwanza toka Dar es Salam mpaka Morogoro unakamilika mwaka huu Desemba, 2019 na kwa kiasi kikubwa barabara hii inapita katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, Jimbo ambalo naliongoza mimi. Reli itakuwa na msaada mkubwa wa kuinua hali ya vipato na uchumi wa wananchi wa Morogoro Kusini Mashariki na Morogoro kwa ujumla kwa kuwa itapunguza gharama ya usafiri wa mazao ya wakulima wa Ngerengere, Mikese, Kinole, Tegetero, Tununguo, Mkuyuni, Kiroka, Tomondo, Mkulazi na Vijiji vya Kata zote za Morogoro kwa ujumla na kupunguza gharama za usafiri na kuongeza vipato vya wananchi wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo ya Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Joseph Magufuli kwa kuweka katika bajeti barabara ya Bingwa - Kisaki kuanza kwa ujenzi na kuanza kilometra 50 kwa kiwango cha lami. Naipongeza Serikali kwa sababu ni sikivu, baada ya kusikiliza maombi yangu ya ujenzi wa barabara kuanza ujenzi kila Bunge la bajeti tangu kuingia katika Bunge hilli.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi na shukrani hizo kwa Serikali kuiweka katika bajeti barabara ya Bingwa - Kisaki lakini kiasi kilichotengwa ni kidogo sana cha shilingi milioni mia moja arobaini na tano (145,000, 000) kwa kujenga barabara ya kilometra hamsini ni kiasi kidogo sana ambacho hakiwezi kutosha kulipa hata fidia tu kwa wananchi walipopisha ujenzi wa barabara hii ya Bingwa Kisaki. Ushauri wangu kwa Serikali kuongeza kiwango cha fedha katika

bajeti ya ujenzi wa barabara hii ya Bingwa - Kisaki ili ujenzi wake uanze mwaka ujao wa fedha unaanza mwezi Julai baada ya bajeti hii kupita.

Mheshimiwa Spika, kiasi hiki ni kidogo ambacho pia hakiwezi kutosha kulipa mkandarasi malipo ya awali ya asilimia 15 kwa mujibu wa sheria. Naomba Serikali iongeze fedha ili ujenzi uanze.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili naomba Serikali kutupatia minara ya mawasiliano katika Kata ya Tegetero, Rudewa, Seregete, Mkulazi, Tununguo, Kidugalo na Matuli na Vijiji vyote vya Kata hiyo pamoja na Vijiji vya Luholole, Mwarazi na Kibuko Kata ya Kibuko. Pia mnara katika Vijiji vya Newland Lubungo, Mhunga Mkola katika Kata ya Mikese.

Pia naomba ujenzi wa madaraja katika Mto Ruvu kuunganisha Tarafa ya Mvuha na Tununguo kuititia Mbarangwe, Tununguo mpaka Kisanga Stendi. Pia naomba daraja la kuunganisha kati ya Kata ya Matuli na Kidugalo kwenye Mto Ngerengere.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kuzungumzia barabara ya Amani – Muheza, zaidi ya kilometra 20 ambayo Serikali iliahidi kuiweka lami kwani Tarafa ya Amani yenye kata sita inategemea barabara hiyo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, kilimo, utalii na kadhalika, je, ni lini barabara ya Amani – Muheza itajengwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, barabara ya Muheza kwenda Magoroto inahitaji kuwekwa lami kwani ni barabara inayoenda kwenye mashamba ya michikichi ambayo ni maeneo yanayozalisha lakini pia Magoroto kiutalii (*Magoroto Camp*) ambayo inaingiza pato la halmashauri na nchi kwa ujumla. Je, ni lini barabara hii itajengwa kwa lami ikizingatiwa ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, Bandari Kavu Pangani na Kigombe. Kumekuwa na kuzuka kwa bandari kavu (bandari bubu), naomba kufahamu Wizara ina utaratibu gani wa kurasisimisha bandari hizi ili ziweze kuwa chachu ya maendeleo kwa Wilaya za Muheza na Pangani.

Mheshimiwa Spika, minara ya simu; kuna tatizo kubwa la mawasiliano ya simu Tarafa ya Amani, Kata za Zirai, Misalai na Bwiti.

**MHE. LUCIA M. MLLOWE:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uwanja wa ndege; kwa kuwa Kiwanja cha Ndege Njombe kiko katika hali mbaya, niombe Serikali ikarabati kiwanja hicho. Serikali imekuwa ikitisema iko kwene mchakato lakini sasa ni miaka milne Wanajombe wanajibowi kuwa kiko kwene mchakato.

Mheshimiwa Spika, Barabara za Itoni – Ludewa (Njombe) – Njombe – Makete. Hali ya barabara zile sio nzuri, hasa kipindi hiki wakati wa mvua. Naomba wakandarasi walipwe kwa wakati ili waweze kuharakisha ujenzi wa barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ya simu; maeneo mengi ya Jimbo la Lupembe hakuna mawasiliano ya simu mfano Madeke, Kanikerere na maeneo mengine. Naomba Serikali iwasaidie wananchi kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, miradi kushirikisha Sekta Binafsi; kwa kuwa miradi mingi inasuasua kwa sababu Serikali peke yake inagharamia. Ili kuharakisha maendeleo, nashauri miradi hiyo washirikishwe sekta binafsi kwani sekta hiyo wakipewa miradi hiyo wataharakisha kumaliza miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa *Engineer*.

Kamwelwe, Waziri na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutekeleza majukumu yao. Serikali kupitia ahadi ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufulsi aliahidi kutengenezwa kwa Barabara ya Nyashumo – Ngasamo – Dutwa, kilomita 45 kwa kiwango cha lami. Huu ni mwaka wa nne, ningependa kujua ni lini ujenzi wa kiwango cha lami utaanza ili kuwezesha usafirishaji wa bidhaa za kilimo pamoja na usafiri wa wananchi uweze kutekelezwa? Aidha, kumekuwepo na uimarishaji wa madaraja na baadhi ya sehemu korofii kwa kiwango si cha kuridhisha. Hivyo naomba kupata majibu ni lini sasa ujenzi huu wa barabara utaanza.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, barabara, maeneo ya uzalishaji. Pamoja na jithada za kuunganisha mikoa kwa mikoa, nashauri na kupendekeza Serikali iongeze nguvu kwenye maeneo ya uzalishaji kiuchumi ili kuchochaea shughuli za uzalishaji na hivyo kuongeza Pato la Taifa. Mfano, Wilaya ya Mufindi, Barabara ya Mafinga kwenda Mgololo ni uti wa mgongo wa uchumi kuelekea kwenye Viwanda vya Chai, Karatasi na Mazao ya Misitu. Wakati wa mvua unakuta malori yamekwama kwa wiki nzima, hii maana yake ni ku-*slow down speed* ya uzalishaji na hasa usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mufindi inachangia Pato la Taifa kwa kuwa mionganoni mwa wilaya tano bora kimapato. Pamoja na hali hii, bado inaweza kuchangia zaidi ikiwa barabara hii itapitika mwaka mzima. Hivyo, nia yangu hapa ni kuishauri Serikali kuwa itazame maeneo ya kimkakati kiuchumi hata kama maeneo haya hayaunganishi mkoa kwa mkoa.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano; Mji wa Mafinga ni mji wa kibiashara na unakuwa kwa kasi sana kutokana na uwepo wa shughuli za viwanda vya mazao ya misitu. Hata hivyo, kuna maeneo ambayo ni *just about or less than 15 kilometres from Mafinga Town*, hakuna mawasiliano.

Mawasiliano ni *component* muhimu kwenye shughuli za kiuchumi na *purchasing power* kuu, wakipata mawasiliano yatachangia uchumi kwa kununua *data* na muda wa maongezi. Hivyo naomba mawasiliano katika Vijiji vya Kisada, Bumilayinga, Ulole, Kikombo, Maduma na Itimbo.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Spika, nipende kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Jangwani; nipende kujua nini sababu ya ujaaji wa maji, baada ya matengenezo ya mwendokasi ndiyo imekuwa mbaya kuliko. Swali; je, upembuzi yakinifu haukufanyika au ilikuwaje, kila ikinyesha mvua lazima watu washindwe kupita barabara hii? Leo hii tunavyoongea Jangwani hakupitiki; je, hivi kweli wananchi wanazunguka na kupoteza muda mwingi kutafuta jinsi ya kufika kazini kwao?

Mheshimiwa Spika, barabara na fidia kwa wananchi wa Kibaha wanaopisha upanuzi wa barabara *TAMCO* – Mapinga. Wananchi wanashindwa kujua hatma ya maisha yao kufuatia tathmini iliyofanywa na malipo kukwama, hivyo kusababisha wananchi kuwa na umaskini uliokithiri. Serikali irudi kwa wananchi iwaambie wamekwama wapi kulipa fidia iliyowaahidi miaka minne iliyopita.

Mheshimiwa Spika, magari ya mwendokasi; najua kuwa *SUMATRA* ambao wanatetea pia wasafiri ambao ni idara katika Wizara hii. Usafiri wa mwendokasi ni shida sana, magari ni machache sana na wasafiri ni wengi, hivyo kupelekea wasafiri kujazana sana mpaka kukosa hewa na kusababisha wengine ku-*faint* kwa kukosa hewa. Nini maana ya kugharamia mradi huu na kuondoa mabasi ya kawaida, wananchi hawaielewi nia ya Serikali kuondoa magari ya kawaida, Serikali imewapa mateso makubwa kwa kuleta mradi huu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa majengo kwa ajili ya kuza. Ujenzi unaojengwa na *TBA* usiangalie upana wa viwanja na ubora wa majengo wanayoyajenga ambayo

inapelekea wananchi kushindwa kununua kutokana na udhaifu unaopelekea wanunuzi kuona nyumba hizi sio rafiki kwa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, *TEMESA*; matengenezo yanayotokana na *TEMESA* ukipeleka gari kutengenezwa inatengenezwa kwa muda mrefu kuliko yanayotengenezwa kwa watu binafsi. Hata barabarani taa zote zinapoharibika urekebishaji ni shida.

Mheshimiwa Spika, bandari; nishauri Serikali kujifunza utoaji huduma wa Bandari za Durban, Beira na Mombasa, vinginevyo wateja watatukimbia iwapo urasimu wetu na tozo nyingi utaendelea katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, *TTCL*, tumeimba mara nyingi sana kuwa Serikali ilippe madeni inayodalwa pia itoe uhuru wa uendeshaji ili ijiendeshe kibiashara, iwe na uwezo wa kukopa na kukopesha.

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu wa rehema kwa kunipa uhai na uzima na pia kuniwezesha kuchangia mada iliyopo hewani kwa lengo la kulipaisha Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nianze na Bandari ya Bagamoyo. Ni vyema Serikali ingefikiria zaidi kujenga Bandari ya Bagamoyo. Hii itasaidia kuimarisha uchumi wa maeneo hayo na pia kuongeza Pato la Taifa. Bandari ya Bagamoyo kama itajengwa, hata hii Reli ya Kati nayo ndiyo itaweza kufanya kazi vizuri, mizigo itapatikana kutoka nchi tofauti kuletwala hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, usajili wa simu; kwa masikitiko makubwa sana, *TCRA* haionekani kutoa mashirikiano mazuri na Zanzibar (SMZ). Kwa upande wa Zanzibar *ZAN – ID* ndiyo kila kitu, ndimo yalimo maisha ya Wazanzibari. Ni vyema basi kama *ZAN – ID* nayo ikatumika katika usajili wa simu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bandari ni masuala ya Muungano, kule Zanzibar bandari zake zimekuwa hovyo sana na zimeachwa kama hazina mwenyewe, je, Serikali ya Muungano ina mpango gani kuhusiana na maboresho ya bandari za Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, wizi wa mitandaoni; kumekuwa na wizi mkubwa wa wananchi katika miyamala ya fedha. Kwa mfano kama utamtumia fedha mdogo wako na kwa bahati mbaya usipate wakati wa kumuarifu, baada ya muda basi anapigisha simu na mtu mwingine kama yeche ndiye aliyeatumia fedha na azirejeshe na namba ya kurejeshe anatoa na hii inarudi kwa mwizi. Zikitakiwa namba zilizotumika ninazo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, nimejiwa na wazo ambalo ni kuona uwepo wa haja ya kumwenzi Dkt Salim Ahmed Salim kwa kupewa heshima ya jina la Mheshimiwa kuingia kwenye kumbukumbu ya milele nako ni kumuenzi akiwa hai na kusikia kiwa duniani kuwa Uwanja wa Ndege wa Songwe unapewa jina lake.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe Dkt. Salim ameshika nyadhifa nydingi ambazo ni: Balozi wa Zanzibar , Gairo; Balozi wa Tanzania, Cairo; Balozi wa Tanzania UN, New York; Katibu wa *OAU*; Waziri wa Nje, Ulinzi; na Waziri Mkuu, naomba hilo lizingatiwe.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua fursa hii kukushkuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii. Pili nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuandaa na kuwakilisha hotuba hii kwa umakini mkubwa sana. Katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta (*TPC*) napenda kuipongeza Serikali yetu kwa kuendeleza juhudhi kubwa za

kuendeleza na kuiimarisha Shirika hili, shirika hili ni mionganii mwa mashirika makongwe sana katika nchi hii. Shirika hili linajishughulisha na kazi ambazo ni lazima zifuatiliwe ili kufanikisha kazi hizi mfano, kazi ya posta mlangoni hii kazi inahitaji vitendea kazi vya usafiri ili kufika kwenye eneo husika. Ushauri wangu katika jambo hili ni Wizara kuzidisha juhudii ya kuwatafutia usafiri wa uhakika ili kuweza kukabiliana na ushindani mkubwa uliopo nchini.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Mawasiliano Tanzania; shirika hili ni mionganii mwa mashirika muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. Nachukua nafasi hii kuipongeza idadi ya wateja (*Active customer*) wa huduma mbalimbali, hili ni jambo jema kwa sababu wateja ndio watakaowezesha upatikanaji wa faida katika shirika hili.

Mheshimiwa Spika, kazi za mawasiliano kwa sasa zina ushindani mkubwa sana, mashirika mengi ya binafsi yamejitokeza na yanaendelea kujitokeza, hivyo ni vyema shirika likajipanga ili kukabiliana na ushindani huu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iliwezeshe shirika hili ili liweze kukabiliana na mashirika binafsi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu mwingu wa rehema kwa kunipa akili na busara ili kuweza kutoa mchango wangu wa maandishi katika hoja hii muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Mamlaka ya Mawasiliano (*TCRA*) imeamua na kupitisha usajili wa *line* za simu kwa njia ya kidole (*finger*) kuanzia 1/5/2019 jambo ambalo ni jema, Zanzibar na Wazanzibari kutoka ilipoanza kusajili simu za mkononi, Wazanzibar tulikuwa tukisajili *line* za simu kwa kupitia kitambulisho cha *ZENID* na hakukuwa na shida wala matatizo yoyote. Ni hivi karibuni tu mwezi Septemba, 2018 Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ilitumia mabilioni kubadilisha na kuboresha kitambulisho cha *ZEN ID*.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana tunaona wakati zoezi hili likiendelea Wazanzibari ambao tulisajili *line* zetu kwa kitambulisho cha *ZEN ID* sasa kitambulisho hicho kinakataliwa na kimeondolewa kabisa, kama nilivyosema sisi Wazanzibari tulisajili kutumia *ZEN ID* bila shida yoyote na vile vile SMZ kutumia mabilioni kuboresha kitambulisho hicho ni kwa nini sisi Wazanzibari ambao tulitumia kitambulisho cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tusiachiwe kuendelea na usajili wa kitambulisho hicho?

Mheshimiwa Spika, vile vile kuondolewa kwenye usajili kitambulisho cha *ZEN ID* si wazi kwamba kitambulisho hiki Serikali ya Muungano inaenda kukiondoa kabisa. Hivyo hivyo wapo Wazanzibari ambao hawana kitambulisho cha *NIDA* lakini wana kitambulisho cha *ZEN ID*.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimwombe Mheshimiwa Waziri atueleze kwa kutumia kusajili *line* za simu kwa Wazanzibari kwa kutumia *ZEN ID* tatizo ni nini? Suala hili ni muhimu wakati Mheshimiwa Waziri anafanya majumuisho ni vyema akalitolea ufanuzi kwani Zanzibar hasa wananchi wa Zanzibar wamekuwa wakijiliza na kutoafautiana sana. Ahsante sana.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Wizara hii kwa ujumla wao kwa maslahi ya wananchi wetu, ni wizara pana ndani ya utekelezaji wake, hivyo nasisitiza na kukubaliana na Kamati na kupongeza kwa kuongezewa bajeti, lakini ni bora zaidi ikiwa Hazina watazitoa zote au kwa asilimia zaidi ya 85.

Mheshimiwa Spika, kwani tunatarajia kuinua utalii ambao unatupatia mgawo wa zaidi ya asilimia tano ya pato la Taifa, pia kurahisisha mawasiliano ya barabara kwa uchumi wa nchi yetu. Tunashukuru jitihada ya Serikali ya kutuunganisha na nchi jirani kwa barabara ya kiwango cha lami, Sumbawanga – Matai – Kassanga (*DRC CONGO*), Matai

– Kasesya (Zambia). Ombi, tunaomba kasi kuongezwa kwa ukamilifu wa barabara hizi pamoja na kuwemo kwenye bajeti iliyo bainishwa ukurasa wa 257, tunasisitiza fedha za miradi ya maendeleo kutolewa zote na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hali ya barabara ya bonde la Rukwa kutoka Kibaoni hadi Kilyamatunda ina hali ngumu kutokana na maji yanayoporomoka kutoka mlimani na kuelekea Ziwa Rukwa, yanakuwa na nguvu na kukokota miti mikubwa na kuhatarisha madaraja katika barabara hiyo yote na yote yameharibika na kupelekea kila mwaka kurekebishiwa maeneo korofi na kuendelea kutumia pesa nyingi za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo na ushauri, barabara hii ni kutengenezwa kwa kiwango cha lami na ujenzi wa madaraja makubwa na madhubuti, ndiyo suluhisho lake. Pamoja na Bajeti iliopendekezwa kwa baadhi ya maeneo katika ukurasa 302, Ntendo – Muze, Ilamba – Kaoze, Kasansa – Kilyamatundu, Mtowisa – Ilembo, ni matumaini yangu, ushauri wa muda mrefu wa ujenzi wa barabara hii kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa, tuna Kiwanja cha Ndege, Sumbawanga ambacho kinafanyiwa ukarabati na kuongezwa urefu wa uwanja huo, kwa kiwango cha lami, ili nasi tupate usafiri wa Anga. Ombi, tunaomba kasi kuongezwa katika kuendeleza ukarabati huo, ambao haujaonekana ipasavyo, kwani tuna kiu kubwa na kukamilishwa mradi huo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, bado nasisitiza Wizara kuangalia uwezekano wa kuweka utaratibu wa kuzijenga barabara za mabonde ya Rukwa na Tanganyika kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Sasa tuanze kupata *feedback* ya upande wa Serikali. Tunaomba tuanze na Wizara ya Fedha, halafu na Mheshimiwa Naibu Waziri Kwandikwa ajiandae robo saa.

Wizara ya Fedha dakika 10, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tafadhali.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye mjadala huu wa bajeti ya Wizara hii muhimu sana ambayo inachukua sehemu kubwa ya keki ya bajeti ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba muungane nami kumpa pole *Secretary* wangu ambaye alfajiri hii amepotea mume wake, Mama Dionisia Mkoma, ndio maana sijakaa vizuri hata mimi mwenyewe.

**MBUNGE FULANI:** Pole sana.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Ahsante.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nitoe pongezi mahsus i kwa Mheshimiwa Rais ambaye ameendelea kutoa kipaumbele cha juu kwenye ukarabati na ujenzi wa miundombinu msingi, yaani *basic infrastructure* na hii amefanya kwa umahiri mkubwa tangu alipokuwa Waziri wa Ujenzi; na kwa kweli alitambua mapema sana kwamba miundombinu ni kichocheo na mhimili mkuu wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana Mhandisi Kamwelwe na Naibu Mawaziri Mhandisi Elias Kwandikwa, Mhandisi Atashasta Nditiye. Kwa kweli wanatekeleza majukumu yao vizuri pamoja na watendaji wao ambao wamekaa kule nyuma ya kioo wakiongozwa na Makatibu Wakuu husika. Niseme mapema kabisa kwamba naunga mkono hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, ninaunga mkono kwa sababu kwa kweli uwekezaji katika ujenzi wa miundombinu ya kisasa inachochea uchumi na maendeleo ya nchi na watu wake kwa namna nyingi ambazo Waheshimiwa Wabunge wanazifahamu. Ujenzi wa

miundombinu unatengeneza fursa nyingi sana za ajira, lakini pia kipato kwa wananchi wetu. Ujenzi na ukarabati wa miundombinu unatumia nguvu kazi yenye ujuzi na ndiyo maana *bench* pale tunaona ni Wahandisi watupu au waliowatangulia ni wanasayansi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pia miundombinu bora inapunguza sana ghamama za uwekezaji na uzalishaji na inaongeza uwezo wa kusafirisha watu, malighafi, bidhaa na kadhalika na kufanya biashara iende kwa haraka zaidi. Kwa kweli moja ya tofauti kubwa ya nchi zetu masikini na nchi zilizoendelea ni ubora wa miundombinu. Kila unaposafiri ukaenda nchi yoyote iliyoendelea, kitu cha kwanza unachoona ni tofauti ya miundombinu. Ndiyo maana katika mwaka ujao wa fedha kwa makusudi kabisa Serikali imeitengea Wizara hii shilingi bilioni 606 zaidi ya bajeti ya mwaka huu wa fedha tuliyonayo ambayo ni takribani asilimla 12.8 ya ongezeko.

Mheshimiwa Spika, mgawanyiko wa fedha kwenye Wizara hii, umezingatia maoni ya wadau mbalimbali na Waheshimiwa Wabunge na hasa kwamba tujielekeze kama Serikali kwenye ujenzi wa reli mpya ya kisasa ili barabara zetu nazo ziweze kudumu lakini pia ili tuweze kupata manufaa makubwa ya kuwa na hiyo miundombinu ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nichangie baadhi ya hoja ambazo zilijitokeza. Kwanza tulishauriwa kwamba Serikali katika ujenzi wa reli ya kati iufanye kwa kuzingatia faida za kiuchumi. Napenda nilihakikishie Bunge lako Mheshimiwa Spika na Watanzania kwa ujumla kwamba kazi hii ya kujenga reli imezingatia fursa mbalimbali za kiuchumi na kijamii ambazo zinapatikana katika ukanda mzima wa reli, fursa za kilimo, madini, mifugo na uvuvi pamoja na biashara miongoni mwa mikoa yetu, lakini pia katika nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, lilisemwa sana lile la kipande cha Tabora – Kigoma ambacho inajulikana, nami ni mmoja wa wadau wakubwa, nisisitize tu kwamba hili ni muhimu, halina

mjadala, lakini kikubwa ni kwamba tunajenga reli hii awamu kwa awamu na changamoto kubwa tuliyonayo ni upatikanaji wa fedha na tunaangalia *options* zote ikiwemo na kiasi ambacho kinaweza kugharamiwa na Serikali peke yake au kwa kushirikiana na wabia wengine na pia upande wa mikopo. Punde tutakapomalaiza upande huu wa *financing* hakuna mashaka kabisa. Napenda tujenge hata vipande vyote kwa mara moja. Kwa hiyo, hili tunalifanya kazi.

Mheshimiwa Spika, tuliambiwa pia tuangalie uwezekano wa kupata mkopo wenyewe gharama nafuu kuharakisha ujenzi wa reli nchini. Niseme tu kama nilivyotangulia kusema kwamba hili tunalifanya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Shirika letu la Reli, wameanza upembuzi yakinifu kwa miradi ya reli ambayo itatekelezwa kwa utaratibu wa *PPP*na hususan ile ya Mtwara, *Mbamba Bay* kupitia Mchuchuma na Liganga na pia ile reli yetu ya Tanga - Arusha – Musoma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa reli ya kat, naomba niliarifu Bunge lako kwamba Serikali iko katika mazungumzo na Benki ya Maendeleo ya Afrika ili watusaidie *ku-leverage private sector investment* na *PPP*na nilipokuwa Abidjan nilikuwa na mazungumzo na Dkt. Adesina kwa ajili ya hii na siyo kwa kipande tu cha kuelekea Kigali, lakini kwa vipande vingine vyote ambavyo bado tunatafuta fedha.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na swalii kuhusu deni la *TAZARA* ambalo uhakiki wake umekamilika na kwamba Serikali ilipe hilo deni lililopo upande wa nchi yetu. Tulipokea madai ya *TAZARA* bilioni 59.6 kwa ajili ya kulipa madeni ya mishahara na michango kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kama inavyojulikana madeni hayana yanatokana na changamoto mbalimbali ambazo zilikabili *TAZARA* kuanzia miaka ya 1990 ikiwemo na kushindwa kabisa kujendesha, lakini pia malimbikizo ya wastaafu. Sasa tumefanya nini kama Serikali, kuanzia 2015 tulianza kusaidia ulipaji wa mishahara ya watumishi wa *TAZARA* na tunalipa takribani shilingi bilioni 1.25 kwa mwezi na tumefanya hivyo hadi Aprili, 2019 na tumekwishalipa jumla ya bilioni 67.44.

Mheshimiwa Spika, lakini mwaka uliopita 2017/2018, tuliongeza pia mtaji wa TAZARA tukalipa bilioni 10 kwa ajili ya kukarabati vichwa na *engine* za treni za TAZARA. Kuhusu madai ya TAZARA ambayo yamepokelewa karibuni, tunayafanya uchambuzi wa kina ili tuweze kupata namna bora ya kuyalipa na kuwezesha shirika kuijendesha kwa lengo kudhibiti uzalishaji wa madeni mapya.

Mheshimiwa Spika, tuliambiwa pia hapa kwamba Serikali iharakishe kulipa madeni ya *pension* kwa wafanyakazi waliokuwa Posta chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kulipunguzia mzigo shirika. Serikali ilikwishafanya malipo kwa wastaifu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na zoezi maalum la kuwalipa wastaifu lilishafungwa na tulishawaandika hivyo toka Disemba, 2016.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tunashughulikia hoja zinazowasilishwa na wastaifu kwa kulingana na maombi au malalamiko yanayohusika na malalamiko hayo huwa yanawasilishwa kuititia taasisi ambazo walizifanya kazi hao wastaifu.

Mheshimiwa Spika, kwa wafanyakazi wa Posta wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, maombi ya madai yenye jumla ya shilingi bilioni sita yalikwishapokelewa na tumekwishalipa bilioni 2.7 kufikia Februari, 2017 na kiasi kilichosalia ambapo nyaraka zilikuwa zina utata kiliwasilishwa kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwezi Februari, 2019 kwa ajili ya uhakiki malipo yaweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba mradi wa kuboresha Bandari ya Dar es Salaam...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana bahati mbaya muda umekwisha.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makof)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Sasa naomba nimwite Naibu Waziri, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, dakika 15.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hoja hii muhimu. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja hii muhimu iliyopo mbele yetu kwa asilimia mia moja. Pia nimshukuru sana Mwenyenzi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa leo. Nimshukuru sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa utashi na dhamira yake ya kweli ya kuwajali wanyonge hususan kwa kutengeneza miundombinu bora. Hii miundo mbinu itachangia kukuza uchumi na kupunguza umaskini kwa sababu huduma itakwenda kwa wafanyabiasha, wakulima, huduma za kijamii wafanyakazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu kwa namna anavyosimamia shughuli za Bunge, Iakini niruhusu nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi Mhandisi Isack Kamwelwe, kwa ushirikiano na miongozo anayonipa ili kutimiza majukumu yangu. Aidha, namshukuru pacha wangu Mheshimiwa Nditiye kwa namna tunavyoshirikiana katika kufanya kazi. Vile vile niwashukuru watendaji, Katibu Mkuu Arch. Elias Mwakalinga na Makatibu Wakuu wengine wote Leonard Chamuriho, Dkt. Maria Sasabo, Naibu Katibu Mawasiliano, Jim Yonaz na watendaji wengine wa Wizara nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti namna mnavyotupa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yetu ya Wizara hii ya ujenzi. Pia inaishukuru Kamati yetu ya Miundombinu na Wabunge wote kwa ushirikiano wanaotupa ndani ya Bunge na hata nje ya Bunge. Tunaendelea kupokea maoni na ushauri wa Wabunge na sisi pia inatuboreshea kufanya kazi zetu. Vile vile niwashukuru wapiga kura wa Ushetu. Leo Madiwani wa Ushetu wapo hapa ni mashahidi,

Madiwani wote hawa wa Chama cha Mapinduzi tunashirikiana vizuri na mimi kwa u-busy wangu Madiwani hawa kazi nyingi wanazifanya, Ushetu inakimbia kwa speed kubwa. Mwisho, niishukuru familia yangu Dkt. Macelina yupo hapa mke wangu, namshukuru sana kwa ushirikiano anaonipa katika shughuli zangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hoja zilikuwa nyingi lakini ni uhakika kwamba sio rahisi kuzungumza mambo mengi sana hapa, lakini ni wahakikishie Waheshimiwa Wabunge ushauri wao tumeupokea na yote waliyozungumza tutayajibu na kuyawasilisha kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nizungumze mambo machache; kwanza kwa upande wa barabara; niseme tu kazi kubwa imefanyika, mtandao wa barabara nchi nzima barabara kuu za Kitalfa tuna kilometa 36,258. Kati ya hizo barabara kuu ni kilometa 12,176, barabara za mkoa ni kilometa 24,082, lakini kati ya barabara hizo kilometa 10,061 zipo sasa kwenye matandao wa lami kwa maana barabara kuu kilometa 8,870 na barabara za mkoa ni kilometa 1,756. Niseme tu kwa miradi inayoendelea hadi Aprili ni miradi 34 ambayo itakuwa na urefu wa kilometa 1,505 na hii miradi yote ikikamika ina-commit fedha nyingi kama Wabunge walivyosema trillioni 7.799, ni fedha nyingi, lakini katika bajeti hii tuliyowasilisha kutakuwa na ongezeko, tutakuwa na miradi kama 37 kwa maana tutakwenda kuhudumia barabara kwa ujenzi wa lami kilometa 1,961 na madaraja sita, hii ni achievement kubwa. Nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Rais zaidi na kumshukuru Waziri wa Fedha kwa sababu waanaendelea kutuwezesha na kazi kubwa inaendelea kufanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nizungumze juu ya ujenzi wa viwanja vyta ndege kwa ufupi. Waheshimiwa Wabunge wengi walivyokuwa wakichangia wamezungumza juu ya miradi ya fidia, lakini niseme kwamba, mwaka 2018 tulifanya uhuishaji wa uthamini ambao awali ulikuwa umefanyika mwaka 2007. Kwa hiyo, niyahakikishie tu Watanzania kwa ujumla kwamba kwenye maeneo ambayo kwamba tuna compensation kwa mujibu wa sharia, tunahuisha ili kuona

tunakwenda kulipa *compensation* na wananchi wanapata haki yao.

Mheshimiwa Spika, kwa wachangiaji tulikuwa na Uwanja pia huu wa Ndege wa Msalato ambapo wapo waathirika ambao wanapisha ujenzi wa uwanja 1,926. Niwahakikishie kwamba takribani bilioni 14 ambazo tunazifanyia kazi ili waweze kulipwa hawa na kwa vile uelekeo wa kupata fedha ili kujenga uwanja huu upo, kwa hiyo wananchi hawa wa Dodoma husasan eneo la Msalato nao tumejipanga pia pamoja na wengine wa maeneo mengine watapata fidia zao.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mengi ambao uthamini wa mali umeendelea; *Lake Manyara*, kule Simiyu, kule uwanja wa ndege wa Nyerere, Musoma na Songea. Katika maeneo haya yote Waheshimiwa Wabunge walichangia, lakini tumejipanga vizuri kuendelea kufanya malipo ya fidia, kwa sababu yapo maeneo mengi pia ambapo malipo yameshafanya, kwa hiyo, tunaendelea kufanya uhakiki tukipata fedha tuanendea kulipa.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba Waheshimiwa Wabunge pia wameuliza kwamba ni lini Serikali itaweka taa za kuongozea ndege. Kwa ufupi niseme kuwa, maeneo yote ambayo tunafanya maboresho ya viwanja vyta ndege tutazingatia hili suala la kuweka taa za kuongozea ndege. Kwa hiyo katika maeneo mbalimbali ambayo tuna mradi kwa mfano kule Mafia na kule Songwe, taratibu za manunuzi zinakamilika mwezi wa tarehe 30 Aprili kwa hiyo tunaendelea kuharakisha ili tuende kufanya maboresho lakini katika maboresho tutazingatia mahitaji na vipaumbele ili viwanja hivi viweze kuwa bora na bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, nizungumze pia kwamba uwanja wetu wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere unatarajia kukamilika mwishoni mwa mwezi huu wa Mei, 2019 na miradi ya ujenzi wa viwanja vyta ndege vingine katika maeneo mengine tuko kwenye harakati ya kufanya maboresho; Uwanja wa Ndege wa Songea, Uwanja wa Ndege wa

Mtware, ujenzi unaendelea kule Geita, Mwanza Nachingwea na kama nilivyosema pia na upande wa Uwanja wa Songwe tufanya maboresho makubwa ya jengo la abiria. Naona Mheshimiwa Mwakajoka ananiangalia hapa, kwa hiyo tunakwenda vizuri katika uwanja huu ili tuweze kuufanya maboresho makubwa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge pia wameuliza kuhusu suala la ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege vya Haydom, Kilwa Masoko, Lindi, Mafia, Manyara, Musoma, Mwanza na Tanga. Serikali inaendelea kutafuta fedha na pia inafanya mazungumzo na washirika mbalimbali wa maendeleo ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na kadhalika kwa ajili ya ujenzi na ukarabari wa viwanja vyote vya ndege hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo juu ya vivuko; ujenzi wa vivuko vipyta viwili katika mwaka 2018/2019 umekamilika kwa maana ya Kivuko cha Kigongo- Busisi, MV Mwanza imekamilika na Magogoni - Kigamboni MV Kazi na pia tunaendelea kujenga vivuko vingine, kwa mfano ukarabati wa vivuko vitatu MV Sengerema, MV Kigamboni, MV Utete, lakini pia tunajenga kivuko kipyta kitakachofanya huduma kati ya Kayenze na Benzi. Tumepanga vivuko hivi viweze pia ku-move kwenda pande nyingine, kivuko hiki kikikamilika ni cha kisasa, kitaweza kwenda maeneo ya Ukara kule Nansio kitatoa huduma katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya ujenzi wa maegesho ya Bwina kule Mkoani Geita maegesho ya kivuko kati Lindi na Kitunda, Mkoani Lindi, upanuzi wa maegesho Kigamboni pamoja na upanuzi wa jengo la kupumzika abiria. Kule ng'ambo Kigamboni tunaendelea kufanya maboresho, kuna mchangiaji mmoja hapa Mheshimiwa Mbunge alizungumza kwamba hakuna kinachoendelea, lakini tunaendelea kufanya maboresho, nafikiri labda hakuwepo muda mrefu, anaweza akajionea ye ye mwenye kwamba tumejipanga vizuri ili huduma hii iweze kuboreka.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Tizeba amezungumza juu ya Kivuko cha Kome – Nyakalilo, tutafanya itakavyokuwa imewezekana kwa sababu tuna harakati za kujenga vivuko vingi, tunaona namna nzuri ili wananchi wapate huduma ya vivuko kulingana na mahitaji. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Tizeba kwa sababu tulipata ajali ya kivuko wakati tulikuwa tumelenga tumpelekee kivuko kwa sababu ya matatizo yaliyotokea, hivyo avumilie kidogo, tutaona namna nzuri ya ku-reallocate ili tuweze kupata huduma nzuri katika eneo hili la Kome kwenda Nyakalilo.

Mheshimiwa Spika, nzungumze juu ya maboresho makubwa na taasisi yetu ya *TEMESA*, Wabunge wengi wamezungumza, tunaendelea kuboresha, kumekuwa na changamoto na huduma za *TEMESA*, nakubaliana nao, lakini kama Wizara tumejipanga kuboresha karakana hii kwa maana ya kuongeza vitendea kazi na kuweka vifaa stahiki. Hata hivyo, kuna baadhi ya maeneo kwenye Wilaya kama kule Ifakara tumepeleka huduma na maeneo mengine tunaendelea kuwasogezea huduma wananchi ambao wanapata huduma hizi hususan taasisi za Serikali ili waweze kuzipata kwa ukaribu zaidi. Tunalenga kwenda kupeleka huduma hii katika Wilaya 25.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie juu ya huduma ya majengo na nyumba za Serikali. Imetolewa hoja kwamba gharama ni kubwa katika ujenzi, lakini nilikuwa nimejaribu kufanya mapitio kwamba pamoja na changamoto nyingi ambazo zipo kwenye *TBA*, Wizara inaendelea kushughulikia ikiwepo tatizo la wafanyakazi, tunaendelea kuongeza wafanyakazi ili tuweze kuboresha huduma hizi. Tulifanya utafiti kuona kwamba zile huduma za ujenzi bado zipo chini kwa miradi kadhaa, mfano, ujenzi wa mabweni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tulijenga kwa bilioni 10, lakini wengine waliwasilisha gharama za ujenzi kwa bilioni 90. Pia gharama za ujenzi wa shule ya sekondari Ihungo wengine walituletea kwa bilioni 60 hadi 200, lakini Wakala walijenga kwa bilioni 12. Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Geita bilioni 17 ndio *TBA* wanajenga, lakini wengine walituwekea bilioni 67. Sasa utaona gharama zipo chini kati ya wastani wa 30% hadi 40%.

Mheshimiwa Spika, niseme jambo moja hapa ambalo Waheshimiwa Wabunge walizungumza juu ya kufanya uchunguzi kuhusu baadhi mikataba ambayo imehusika kwenye ujenzi wa shule kongwe, sisi Wizara tupo tayari tutaunda timu ambayo itahusisha wafanyakazi wa *AQRB*, *CRB* na *ERB* ili kuititia upya mikataba yote na tuweze kupata ushauri kupata ushauri ili tuweze kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kusema Mheshimiwa Kingu alizungumza kwa uchungu hapa kuhusu barabara za Singida. Kwanza Mheshimiwa Kingu nimpe faraja kwamba katika bajeti hii tutatengezea barabara za mzunguko kwenye Mkoa Singida, kilometra 46 kwa mapendekezo ambayo yapo mbele ya meza. Hata hivyo, nimhakishie kwamba kwenye eneo la kutoka Singida kwenda Mgungila kwamba katika bajeti ya mwaka huu inayoendelea 2018/2019, tulikuwa tumetenga zaidi ya milioni 150 kwa ajili ya kuboresha, kujenga madaraja katika maeneo ambayo ni korofi na kuweza kuanza kunyanya tuta. Kiasi cha fedha ambacho kinaonekana hapa ni kwa ajili ya kuendelea kufanya maboresho katika eneo hili na maeneo mengine, muda hautoshi, nafahamu kwamba yapo maeneo mengi ambayo kwenye Mkoa wa Singida kama alivyosema Mheshimiwa Kingu tunaendelea kufanya maboresho mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ningezungumza kidogo kwa kumalizia kuhusu ule mgawanyo wa fedha wa Mfuko wa Barabara. Niseme tu kwamba mgawanyo wa fedha upo kisheria, ni suala la kuangalia sheria lakini kwa upande wa Wizara kuititia, Bodi Mfuko wa Barabara tumeweka mshauri ili aweze kufanya mapitio tuone namna nzuri wa kufanya mgao huu wa fedha za *TARURA* na upande wa *TANROADS*. Hili zoezi linafanyika kwa sababu pale awali mgawo ulikuwa 80% kwa 20% kabla haujaenda 70% kwa 30% kwa mujibu wa sheria ilivyokuwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaendelea kukamilishia hili zoezi ili tuone urefu wa barabara, *network* nzima ili tuweze kuona matumizi ya barabara kwa sababu ndio *bases* kwamba ni vyombo vingapi, uzito upi unapita kwenye

barabara zetu ili sasa tuweze kuona namna nzuri namna nzuri ya kufanya mgawanyo wa barabara hizi, pia tutazingatia hali ya jiografia. Ili twende vizuri wenzetu Wizara ya Fedha pia wanalfanyia kazi jambo hili na tukiweza kuongea fedha za ujenzi wa barabara tutaendelea kuziboresha barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana kwa nafasi hii na nimalizie kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, tunakushukuru sana kwa kupitia hoja za Waheshimiwa Wabunge vizuri. Nawaona Waheshimiwa Madiwani wa Ushetu wapo hapa na leo posho zao zimezungumziwa hapa asubuhi, kwa hiyo hapa Dodoma tunasema mambo *mswanu*, mambo mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, basi kwa hatua hii, tutakaporudijioni ataanza Mheshimiwa Nditiye kwa robo saa, halafu atafutiwa Mheshimiwa Waziri, *by* saa kumi na moja kamili tutaanza kupitia mafungu kwa sababu ni mengi ili tuone tutakimbia kiasi gani. Naomba wale ambao wamejandardaa kwa ajili ya mambo hayo, basi waweze kuwahi na wengine wote tuwahi kufika ili tuimalize kazi hii mapema kwa pamoja.

Kwa hatua hii basi, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili jioni ya leo.

*(Saa 6.58 Mchana Bunge lilitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilitrudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Kikao chetu cha Ishirini na Sita na majadiliano yanaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na upande wa Serikali, sasa namuita Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi na Mawasiliano, Mheshimiwa *Engineer Atashasta Nditiye*. Karibu sana, una robo saa. (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi aliyotupatia kukutana mahali hapa kwa ajili ya kujadili mambo muhimu yanahu nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa majukumu mengi sana anayofanya kwa ajili ya nchi yetu. Nimpongeze vilevile kwa majukumu mengi anayoendelea nayo na nashukuru kwa kuniamini niweze kumsaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mhandisi Isack Aloyce Kamwelwe, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa *support* kubwa anayonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

Nichukue nafasi hii vilevile kumpongeza sana na kumshukuru pacha wangu Naibu Waziri wa Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano anayehusika na Ujenzi, Mheshimiwa Elias John Kwandikwa bila kuwasahau watendaji wote nikianza na Mhandisi Dkt. Chamuriho (Katibu Mkuu wa Uchukuzi), Mhandisi Dkt. Maria Sasabo (Katibu Mkuu wa Mawasiliano) na Arch. Mwakalinga (Katibu Mkuu wa Ujenzi).

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa maelekezo na misaada mbalimbali wanayoipatia Wizara yetu katika kutekeleza majukumu yake. Nichukue nafasi hii niwashukuru Wabunge wote kwa ushirikiano, urafiki na ukarimu ambao wanaitendea Wizara yetu katika kutekeleza majukumu yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Muhamwe lilioko Mkoa wa Kigoma, Wilaya ya Kibondo. Vilevile naishukuru familia yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kwa sababu ya muda nitajaribu kujieleza kwa baadhi ya hoja chache tu, kwa upande wa uchukuzi nitagusia masuala ya hali ya hewa lakini nitagusia miradi miwili mikubwa ya kimkakati ya reli ya kutoka Tanga - Musoma na Mtwara - Mbambabay. Nkipata nafasi nzuri nitagusia masuala mazima ya ATCL lakini kwenye mawasiliano nitazungumzia suala la usajili wa laini za simu pamoja na utendaji wa UCSAF.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, kwanza, nitoe pole kwa Watanzania wenzetu ambao wamepata madhara sehemu mbalimbali kutokana na mvua nyingi na kubwa zinazoendelea kunyesha maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Sasa hivi Mkoa wa Dar es Salaam na maeneo kadhaa ya Pwani yame-experience mafuriko ambayo yanaendelea, tunaona kwenye mitandao ya kijamii na sehemu mbalimbali na tunapigiwa simu hata na ndugu zetu kwamba hali si nzuri sana kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Mamlaka ya Hali ya Hewa imekuwa ikifanya kazi nzuri sana ya kuwaelimisha Watanzania juu ya athari ambazo zitatokea kwa siku zijazo kutokana na vifaa vya kisasa wanavyovitumia. Itakumbukwa kwamba tarehe 21 Aprili, 2019, Mamlaka ya Hali ya Hewa walitoa tahadhari kwamba Mikoa ya Kusini Lindi na Mtwara ingekumbwa na kimbunga cha Kenneth. Bahati nzuri tuliedelea sana kuhakikisha kwamba tunatoa tahadhari kwa wananchi lakini Mungu akatuepushia mbali kile kimbunga hakikuweza kutoa athari kubwa. Ilipofika tarehe 24 tuliwatahadharisha tena hata wenzetu wa Mikoa ya Simiyu na Shinyanga kwamba kuna kimbunga ambacho kingetokea kutokea misitu ya Congo kingeweza kuathiri maeneo ya Kahama na tulishuhudia kwamba kulikuwa na mafuriko yaliyotokea.

Mheshimiwa Spika, hili najaribu kuwaelezea baadhi ya Wabunge ambao walithubutu kusema kwamba Mamlaka ya Hali ya Hewa inafanya utabiri kama waganga wa kienyeji, hiyo sio kweli. Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania sasa hivi inafanya utabiri wake kwa asilimia 87.8. Katika hali ya kawaida tungepaswa hata kuondoa lile neno utabiri tuwe tunasema tu hali ya hewa kama mataifa yaliyoendelea yanavyofanya. Wakisema kitu kinatokea na sisi kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa tukisema kitu kinatokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mvua kubwa zinazoendelea kunyesha Mkoani Dar es Salaam na maeneo ya Pwani ni sehemu ya mvua za masika. Nitoe wito kwa Watanzania wenzetu kwamba mvua hizi ni kubwa na zitaendelea kuwepo kwa kipindi chote mpaka mwisho wa mwezi huu. Tunaomba wachukue tahadhari na waendelee kufuatilia taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa. Tumejipanga kuhakikisha kwamba tunawahabarisha Watanzania ili wachukue tahadhari mbalimbali kujiepusha na uharibifu wa mali zao lakini pia na maisha yao.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha Mamlaka ya Hali ya Hewa kutoa utabiri wa viwango vya kimataifa, Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba mamlaka ina wataalam waliobobe katika masuala ya Hali ya Hewa. Aidha, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Mamlaka inakuwa na vifaa vya kisasa vya kufanya uangazi (*observation*) na utabiri.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Serikali imeingia mkataba wa ununuzi wa rada tatu za kisasa za hali ya hewa ambazo zitafungwa katika Mikoa ya Mtwara, Mbeya na Kigoma. Rada itakayofungwa Mtwara itasaidia kufuatilia vimbunga katika bahari ya Hindi, rada itakayofungwa Mbeya itasaidia kuhudumia wakulima kwenye mikoa inayozalisha chakula kwa wingi lakini na rada itakayofungwa Kigoma itasaidia katika kufuatilia na kutoa tahadhari ya matukio ya radi na taarifa muhimu kwa wananchi wanaofanya shughuli zao katika Kanda ya Ziwa Tanganyika na mwambao wa ziwa hilo. Ununuzi wa rada hizo tatu utaifanya Tanzania kuwa na

jumlah ya rada tano ikijumuisha na rada zilizofungwa Dar es Salaam na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea kiasi fulani suala la ujenzi wa reli kati ya Tanga - Musoma. Hatua tuliyofika mpaka sasa hivi kwa upande wa Serikali ni kufanya upembuzi yakinifu lakini tumekwishafanya usanifu wa awali na wa kina, tumekwishajua gharama zinazopaswa. Hatua iliyoko sasa hivi ni kutafuta mwekezaji ambaye ataingia mkataba na Serikali kufanya mradi huo kwa njia ya *PPP*.

Mheshimiwa Spika, katika kufikia hatua hiyo kuna kitengo ambacho kiko Wizara ya Fedha ambacho ndiyo kinashughulika na mikataba hiyo. Watu wa Wizara ya Fedha wanatusaidia katika kuhakikisha kwamba mikataba itakayoingia na mwekezaji mbia inakuwa na tija kwa nchi yetu. Hatuko tayari kuona kwamba nchi yetu inaingia kwenye mikataba ambayo haina tija kwa wananchi. Sisi tumejjipanga kuhakikisha kwamba mikataba yote tutakayoingia inakuwa na tija lakini inawasaidia wananchi kwa kizazi cha sasa, cha kesho na kinachokuja.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna wabia wamekuwa wakijitokeza mara kwa mara kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kutaka kuwekeza kwa njia ya *PPP* kwa reli ya Tanga - Musoma lakini pia kwa reli ya Mtwara - Mbambabay. Hata hivyo, masharti yao wakati mwagine yanakuwa ni magumu sana kutekelezeka na tumekuwa tukiendelea na mazungumzo nao kuhakikisha kwamba mkataba kati yetu sisi Serikali na wao basi unakuwa na tija kwa nchi yetu. Tusumie lakini na wao wasiumie wapate faida kwa sababu tunategemea waingize hela zao katika shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, vipande vya reli kutoka Tanga - Musoma na kipande cha reli kutoka Mtwara - Mbambabay na matawi yake ya Mchuchuma na Liganga bado yako kwenye mazungumzo na yako mahali pazuri. Itakapofikia mahali muafaka tutawaelewesha Watanzania kwamba sasa tunaingia mkataba kwa ajili kutengeneza reli hizo.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kidogo suala la ndege zetu za *ATCL*. Serikali imenunua ndege hizo na kuwapatia *ATCL* ili wazifanyle biashara warudishe pesa kwa Serikali. Hivi karibuni kumetokea maneno ya manung'uniko kidogo kutoka kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kwamba nauli za *ATCL* zimekuwa kubwa. Ukweli ni kwamba si sahihi, nauli za *ATCL* bado zimeendelea kuwa ni nafuu kabisa na ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge wengi huwa wanakuwa na *option* namba mbili baada kukosa tiketi za *ATCL*, ni kwa sababu huduma ni nzuri na nauli zao ni nyepesi.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kawaida tunakubali kuwa na ushindani, kuna ndege nyingine za *Precision*, ziko ndege za aina mbalimbali na zenyewe zinatoa huduma kwenye njia ambazo *ATCL* wanafanya kazi. Huwa wanaanza kwa bei nafuu lakini mwisho wa siku wanaenda kuwa na gharama kubwa sana ambazo wateja wao huwa wanakimbia *ATCL*. Nakuomba sana tuwashawishi Wabunge waiunge mkono *ATCL*, ni shirika letu la ndege ili liweze kuendelea kutoa huduma nzuri na za uhakika na ndege zetu ni za uhakika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nikiri changamoto ya kuwepo kwa *delay* zetu. Nikiri changamoto ya kuwa na *cancellation* kwenye baadhi ya *route*. Hilo ni la kweli tumekwishalishuhudia na sisi kama Serikali tumeshatoa maelekezo kwa *ATCL* kwamba kuanzia sasa hivi ndege yoyote ambayo itakuwa na *delay* zaidi ya nusu saa tunahitaji tupate maelezo ya maandishi yakiambatana na vielelezo. Kama ni hali ya hewa basi tupate na taarifa ya hali ya hewa ambayo imeambatanishwa *ku-justify* maelezo ya *delay* ya safari husika. Hilo tumekwishaongea na watu wa *ATCL* na wanafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba safari zote za ndege haziwi na changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, niongelee kwa harakaharaka masuala ya mawasiliano, kuna suala la usajili wa laini za simu. Ni kweli kuanzia tarehe 1 Mei, Serikali kupitia *TCRA* imeamua Watanzania wasajili laini zao za simu kupitia alama za vidole zikiambatana na kitambulisho cha *NIDA*.

Mheshimiwa Spika, kwanza nifafanue ni laini moja kwa kila mtandao. Kama una mitandao ya Tigo, Voda, Halotel, Airtel na *TCL* unaruhusiwa kuwa na laini moja moja. Endapo utahitaji laini ya pili eleza tutakusajili.

Mheshimiwa Spika, nia ya kufanya hivyo ni kuhakikisha kwamba kwa kiasi kikubwa tunayadhibiti matumizi mabaya ya mtandao. Ukitasajili laini zako tatu za Voda tukajua kabisa ni wewe umesajili maana yake ikitumika vibaya basi tutakuchukua halafu tutakupeleka kwa upole kabisa ili uweze kwenda kuwasaidia Polisi kutoa maelezo ya hicho kilichokufanya utumie mtandao vibaya, hatuna lengo baya.

Mheshimiwa Spika, suala la vitambulisho tumeamua kuchagua kitambulisho cha *NIDA* kwa sababu moja tu kwamba ni kitambulisho ambacho kinavuka mipaka yote Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Kitambulisho cha Mkazi wa Zanzibar tunakikubali, ni halali na kizuri na hakina tatizo lakini tunachokiona ni kwamba kile kinatumika kwa Mzanzibar, kikija huku Bara hakitumiki, kwa hiyo, hakiwezi kutumika kwa Bara lakini mitandao ya simu kama Halotel, Tigo na kadhalika inatumika Bara na Visiwani. Tukichukua kitambulisho cha kule peke yake hakitatusaidia kudhibiti uhalifu.

Mheshimiwa Spika, pia leseni za magari siyo kila Mtanzania aliyetimiza miaka 18 ni lazima awe na leseni ya gari. Kuna wengine hawana leseni ya gari, wale ambao hawana leseni ya gari wanahitaji kuwa na mawasiliano ya simu. Kwa hiyo, tumeona kwamba kitambulisho cha *NIDA* kitawasaidia kwa sababu kile ni kitambulisho ambacho kinamhusu Mtanzania yejote aliyetimiza miaka 18.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi nipende kutoa taarifa kwamba kwa Zanzibar taarifa za *NIDA* zinasema zaidi ya asilimia 90 wameshapewa namba ya usajili wa vitambulisho vya *NIDA*. Masuala ya kupata kitambulisho yanaendelea taratibu lakini namba za usajili wamekwishapata. Kwa hiyo, tuna uhakika kwamba wataweza kusajili bila tatizo lolote.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania Bara tuko kwenye Watanzania milioni 16. Kwa hiyo, ukichanganya tuko mahali pazuri na bado tunaamini kwamba kwa miezi nane tulioitoa, Watanzania wengi watakuwa wameshasajili na wataweza kutumia huduma vizuri kwa usalama wao lakini kwa uchumi vilevile kuona kwamba zile *message* za tafadhali nitumie pesa kwa namba hii zinadhibitiwa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, Kuna Mheshimiwa Mbunge alizungumza kuhusu masuala ya picha za ajabu ajabu. Ni ngumu sana kama Serikali kumdhibiti mtu yuko chumbani kwake akaamua kujipiga hizo picha akaangalia mwenyewe. Huwezi kumzuia mtu kama huyo apige picha aangalia chumbani kwake afurahi kama inaweza ikamsaidia lakini anapoitoa nje ya chumba chake ikaanza kusambaa tutamkamata yule wa mwisho mpaka yule wa kwanza aliyejipiga zile picha akazituma kule. Nia na madhumuni ni kwamba mitandao ya mawasiliano itumike kwa faida kwa Watanzania wote bila kuathiri mtu mwingine ye yote ambaye hataki taarifa ambazo wewe unazo. Tumejipanga kuhakikisha kwamba tunadhibiti uhalifu wa kimtandao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kuna suala la UCSAF na minara ya mawasiliano. Niliiwahi kuzungumza kwamba tunafahamu changamoto ya minara ya mawasiliano kwa Waheshimiwa Wabunge na tumeendelea kufanya kazi kwa bidii sana kuhakikisha kwamba eneo kubwa sana la nchi yetu linapata mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi asilimia 94 ya Watanzania wanawasiliana. Tunachokiangalia ni kwamba kuna mawasiliano eneo fulani. Changamoto ndogo sana tunayoipata sasa hivi ni kwamba kama kuna mawasiliano ya Halotel kuna Watanzania wanataka Voda au Tigo lakini sisi Kiserikali tunasema eneo fulani Kongwa wana mawasiliano kwa sababu wana mtandao wa Halotel labda na TTCL. Wakiapata dharura watapiga simu, wakitaka kuza mazao watapiga simu, wikitaka kufanya miamala kutoka Benki kwenda mitandao hiyo au kutoka mtandao kwa mtandao

watafanya miamala. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba kila watu wanawasiliana na kwa hilo asilimia 94 ya Watanzania wanawasiliana na hizi asilimia 6 zilizobakia mpaka inapofika katikati ya mwaka ujao tunakwenda kutangaza mwezi huu vijiji 689 tutakavyovipelekea minara ya mawasiliano ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanaendelea kuwasiliana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, naunga mkono hoja asilimia 100, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Eng. Atashasta Nditiye. Tunakushukuru sana kwa kupitia hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ulivyofanya na umetumia muda wako *exactly*, ahsante sana.

Sasa naomba nimwite mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Isack Kamwelwe ili aweze kupitia michango yenu na kutoa majibu ya Serikali. Mheshimiwa Waziri, karibu tafadhali.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye kwa rehema zake nyingi ametujali afya njema na kutuwezesha kukutana katika Bunge hili Tukufu la Bajeti ili kuweza kukamilisha kazi tulioianza tarehe 9 Mei 2019 ambapo niliwasilisha hoja hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Katibu wa Bunge kwa kusimamia kwa ufanisi mkubwa majadiliano yote kwenye Mkutano huu wa Kumi na Tano wa Bunge hili tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda pia kumpungeza Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake anaoendelea kutuonyesha wasaidizi wake katika majukumu yetu ya kila siku Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii pia kuwashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Bunge kwa kufanya kazi kwa karibu na Wizara yangu. Kipekee nimshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Selemani Kakoso, pamoja na Wajumbe wake ambao wameiongoza Wizara vizuri katika utekelezaji wa miradi ambayo imeainishwa kwenye Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Ninaahidi kwamba Wizara ninayoiongoza itafayafanyia kazi masuala yote yaliyoshauriwa na Kamati hizo.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa maoni, ushauri na mapendekezo yake kuhusu bajeti ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika bajeti yangu. Waheshimiwa Wabunge 18 walichangia wakati wa majadiliano ya hoja ya Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge 91 wamechangia kwa kuzungumza katika bajeti hii inayoendelea na Waheshimiwa Wabunge 66 wamechangia kwa maandishi wakati wa majadiliano ya hoja ya Wizara yangu. Nawashukuru sana kwa michango yao.

Mheshimiwa Spika, hivi punde Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa Wizara yangu wameanza kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa kuzingatia maeneo ya kisekta (sekta ya ujenzi na sekta ya mawasiliano na uchukuzi). Niwashukuru sana kwa jinsi ambavyo wamejibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kujibu hoja za kisera pamoja na kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja zilizojitokeza. Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara itajibu hoja zote za Wabunge kwa maandishi na kuwapatia Waheshimiwa Wabunge wote majibu ya hoja hizo kwa njia ya kitabu kitakachoandaliwa kabla ya hitimisho la Mkutano huu wa Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo wote tunafahamu, mkataba wa miaka mitano kati ya wananchi na Serikali walioichagua ni kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 ambayo itahitimishwa mwaka 2020. Baadhi ya ahadi zilizomo kwenye Ilani ya Uchaguzi ni pamoja na ujenzi wa reli ya *SGR*, ukarabati wa reli ya kati, ukarabati wa bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga, ufufuaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*), ukamilishwaji wa barabara zinazounganisha mikoa, uboreshaji wa mawasiliano nchini na ufufuaji wa Kampuni ya Meli. Ahadi hizi zinatokana na kilio cha muda mrefu cha Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili tukufu ambao wamekuwa wakiishauri na kuitaka Serikali kuwa na miradi ya vipaumbele na kuitekeleza ili nchi iweze kupiga hatua za haraka kuelekea kwenye uchumi wa kati.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hayo, ndiyo maana sehemu kubwa ya bajeti ya maendeleo imemelekezwa kwenye Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na hata leo ameongeza zaidi ya shilingi bilioni 90 kwenye Wizara hii. Hii ni kutokana na majukumu makubwa ambayo Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imeyabeba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sasa inakaribia kukamilisha ahadi ilizozitoa kupitia Ilani yake ya Uchaguzi. Napenda kulihakikisha Bunge lako tukufu kwamba, nikiwa mwakilishi wa Mheshimiwa Rais kwenye eneo la Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa kushirikiana na Naibu Mawaziri pamoja na Wataalam wa Wizara tutaendelea kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na ahadi alizozitoa Mheshimiwa Rais zinazohusu Sekta hii ili kufikia mwisho wa mwaka 2020 ziwe zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, aidha, tutaendelea kupambana na kuzitatua kero za wananchi zitakazojitokeza wakati tukiendelea na utekelezaji wa Ilani hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu deni la makandarasi, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 madeni ya makandarasi na Wahandisi Washauri yalikuwa shilingi bilioni 833 ambayo yalivuka na kuingia mwaka wa fedha 2018/2019. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 makandarasi waliendelea kutekeleza miradi na kuzalisha hati za madai mpya, Serikali imekuwa ikiendelea kulipa madeni ya makandarasi na wahandisi elekezi ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 deni lilikuwa shilingi bilioni 962.

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba Wizara ya Fedha na Mipango hadi mwezi huu Mei itakuwa imelipa shilingi bilioni 609. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa jinsi ambavyo ameitikia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ili kuhamkisha kwamba katika mwaka huu wa fedha, tutakapoingia mwaka mpya wa fedha tena hatutavuka na deni kubwa, na kwa jinsi hiyo basi miradi yote ambayo tumeiainisha kuanza katika mwaka ujao wa fedha tutaanza kuitekeleza bila wasiwasi wowote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia sana kuhusu deni la TAZARA, lakini pia kwenye Taarifa ya Kambi ya Upinzani walizungumzia deni la TAZARA ambalo linaonekana kufikia shilingi bilioni 434. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha amejaribu kulifafanua deni hili, lakini moja tu nizungumzile kwamba, Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge deni hili unapolizungumzia ni deni la nchi mbili, ni deni la Tanzania pamoja na Zambia. Katika deni hili ukiliangalia shilingi bilioni 237 ni deni ambalo limetokana na Itifaki ya Serikali ya China, kwa hiyo, itifaki hii inahusisha pia upande wa Zambia, lakini nishukuru kwa madeni ambayo yanatuhusu sisi huku yakiwepo malipo ya wastaifu Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameyaelezea vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika michango ya Wabunge, wamezungumzia kwa uchungu sana kuhusiana na utaratibu wa majadiliano yanayoendelea kati ya Serikali na Mwekezaji wa Bandari ya Bagamoyo. Nilichojifunza kwa Waheshimiwa

Wabunge ni kwamba Serikali ifanye haraka kuhakikisha kwamba majadiliano hayo yanakamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba majadiliano yangali yanaendelea, lakini kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walisema kwamba Serikali imekataa, sina taarifa ya hilo. Na baada ya kumaliza Bunge nilijaribu kuwasiliana na Mamlaka kuulizia kama majadiliano yameshafikia ukomo lakini ni kwamba majadiliano yanaendelea. Ila ni kweli kwamba yamechelewa kutokana na masharti ambayo yanaonekana hayana manufaa kwa upande wa Serikai ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Waheshimiwa Wabunge waridhie kwamba Serikali bado inaendelea na majadiliano na Bunge lako tukufu limekuwa muda mrefu linalishauri Serikali isije ikaingia mikataba ambayo haina maslahi kwa umma. Kwa hiyo, Serikali inaendelea na pale itakapokuwa imefikia ukomo wa yale majadiliano, nikuahidi tu kwamba Serikali itatoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge ili na wao waweze kutoa mawazo yako. Kwa hiyo, niseme tu kwamba bado tunaendelea na majadiliano kuhusiana na uwekezaji wa bandari ya Bagamoyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 15 wa kitabu cha bajeti ulizungumzia kuhusu ujenzi wa barabara (*express way*) ya Dar es Salaam – Chalinze. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuititia *TANROADS* ilimwajiri Mhandisi Mwelekezo (*Transaction Adviser*) kutoka Korea. *Transaction Adviser* huyu aliajiri makampuni mengine 11 yenye uzoefu na utaalami na miradi ya *PPP* kutoka duniani kote ili kuishauri Serikali namna bora ya kutekeleza mradi wa Dar es Salaam – Chalinze (*express way*) kwa utaratibu wa *Public Private Partnership*, alimaliza kazi hiyo mwezi Desemba, 2016.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya *PPP* Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa idhini tuendelee na hatua zingine za utekelezaji tarehe 22 Mei, 2017. Aidha, wakati idhini ya Wizara ya Fedha na Mpango inatolewa tayari Serikali ilishaanza juhudzi za kupunguza msongamano katika bandari

ya Dar es Salaam, ambazo ni ujenzi wa bandari kavu ya Ruvu, ukarabati wa reli ya *meter gauge* na ujenzi wa reli ya *SGR*. Hivyo, busara ya Serikali zilipelekea kuamua kufanya mapitio upya ya taarifa ya upembezi yakinifu ili kupunguza madhara (*risk*) ambayo yaneghamia upande wa Serikali kumlipa mwelekezi ambaye angejitokeza kuwekeza katika mradi huu kwa kuwa magari ya kubeba mizigo yaneganzia Ruvu badala ya kuanzia bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa usanifu wa mradi huu wa *express way* ilikuwa ni kwamba barabara inakwenda kuanzia bandari ya Dar es Salaam na kwamba ilikuwa inategemea tozo sasa za magari ambayo yatakuwa yanabeba mizigo kuanzia bandari ya Dar es Salaam. Lakini sasa hapa katika kwa sababu *study* zote zilikuwa zinaendelea, *SGR* na baada ya kuonekana kwamba bandari ya Dar es Salaam sasa imekuwa na mizigo mingi uwezo wake utapungua ndiyo tukaamua kujenga bandari ya Kwara. Ukiangalia *study* hiyo sasa inabidi irudiwe kwa sababu kama mwekezaji alikuwa anategemea tozo zake azipate kutoka kwenye magari ni lazima hiyo iweze kurudiwa ili kuona kama bado tunaweza tukachukua mkopo kwa mwekezaji na kwamba mkopo huu utalipwa katika muda unaostahiki.

Mheshimiwa Spika, hilo ndiyo ambalo limefanya kwamba, kwa sababu tunaendelea na ujenzi wa *SGR* na ambaao tunategemea itabeba zaidi ya tani milioni 17 kwa mwaka, wakati huo huo tumejenga *dry port* ya Kwara na kwamba *SGR* ikishafika Morogoro tunatarajia kujenga tena *dry port* nyingine Morogoro kwa hiyo, ikiwa kwamba zile *parameters* ambazo zilikuwa zimetumika, wakati wa kusanifu huo mradi wa *express way* ziweze kurejewa tena ili tuweze kupata mradi ambaao utakuwa na manufaa. Sambamba na hilo, Serikali imefanya maamuzi inajenge Kilometra 19.2 barabara nane ambaao na tayari mradi umeshaanza, kwa hiyo, yote hayo inabidi yarejewe ili kuona kwamba kama mradi huo tutautekeleza utaendelea kuwa na manufaa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia pia kuhusu ujenzi wa viwanja wa ndege vya

Kigoma, Sumbawanga, Tabora na Shinyanga. Mikataba ya ujenzi wa viwanja vya ndege vya Sumbawanga, Tabora, Shinyanga na Kigoma ilisainiwa tarehe 30 Juni, 2017 kati ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*TAA*) na wakandarasi wa ujenzi chini ya ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya. Utekelezaji wa miradi hii umechelewa kuanza kwa kuwa baada ya Serikali kuhamisha miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege kupeleka Wakala wa Barabara, mambo yafuatayo yalijitokeza na ambayo yamechelewesha utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, moja, mfadhili ambaye ni Benki ya Uwekezaji ya Ulaya alitaka kujua taarifa juu ya mtekelezaji mpya wa mradi huu yaani *TANROADS*. Serikali ilielekeza kuwa *TANROADS* ni Idara ya Serikali inayoaminika Serikali na imetekeliza miradi mbalimbali ya wafadhili, pia imepata Hati safi za ukaguzi kwa miaka saba mfululizo. *TANROADS* imekuwa ikifanya manunuzi makubwa ya Taasisi nyingine kama vile *TACADS* na ujenzi wa zahanati zinazofadhiliwa na washirika mbalimbali wa maendeleo. Baada ya maelezo hayo ya Serikali, mfadhili alielewa na kukubali kwamba kazi ile sasa isimamiwe na Wakala wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, kinachoendelea sasa hivi imebidi ku-review sasa ile *Financing Agreement* ili kuondoa *TAA* na kuweka *TANROADS* ili sasa *no objection* iweze kutoka. Sasa hivi kwa mujibu wa taarifa za Hazina ni kwamba shughuli hii ya ku-draft hiyo *document* ya *Financial Agreement* kwa kuweka *TANROADS* na kuondoa *TAA* iko kwenye hatua za mwisho kwa sababu taratibu hizi za mikopo zina taasisi nyingi za kupitia ndiyo maana uchelewaji umekuwa mkubwa. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge hasa kwenye haya maeneo ambayo yamekuwa earmarked Shinyanga, Tabora, Kigoma, Sumbawanga kwamba miradi hii Waheshimiwa Wabunge itatekelezwa tuko kwenye hatua ya mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia kwamba katika miaka mitatu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetenga fedha nyingi

kwa ajili ya utekelezaji wa miundombini ya kimkakati. Wakataka kujua sasa kwanza *impact* ya utekelezaji huo, nishukuru kwamba jibu hilo amelijibu Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipopewa zile dakika zake 10. Ziko faida nyngi siwezi kuzirudia lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameshazizingumzia.

Mheshimiwa Spika, nitaomba nizungumzie kidogo kuhusu *local content*. Katika mradi wa SGR makubaliano kati ya Serikali na mkandarasi kuhusu ujenzi wa mradi huu, ni kwamba asilimia 35 ya malipo yanayolipwa kwa mkandarasi yafanyike kwa fedha za ndani. Lengo ni kuhakikisha kwamba, mkandarasi anatumia siyo chini ya asilimia 35 ya fedha zote za mradi katika matumizi ya rasilimali za ndani.

Mheshimiwa Spika, malighafi kama kokoto, mchanga, nondo na saruji anavyovitumia mkandarasi vyote ni vya ndani ya nchi. Aidha, matengenezo na uzalishaji wa mataruma ya zege unaofanyika hapa nchini katika Kambi za Soga na Kilosa unatumia malighafi za humu nchini. Kiasi cha saruji kinachotarajiwa kutumika katika kipande cha Dar es Salaam hadi Makutopora kwa mujibu wa mkataba ni mifuko ya *cement* au ya saruji 9,200,000 sawa na tani 460,000 za saruji. Kwa upande wa chuma, kiasi tani 115,000 zitatumika kutoka viwanda vya ndani. Chuma cha reli kinachotoka Japan ni asilimia 5.2 tu ya thamani ya mradi na hii ndiyo fedha ambayo tunaitoa kwenda kupeleka nje kwa hiyo ni asilimia 5.2, kwa hiyo asilimia kubwa inabaki hapa ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, mradi utatumia mataruma 1,204,000 ambayo ni asilimia 5.6 ya thamani ya mradi wote wa malighafi zake zote zinatoka hapa nchini na zinazalishwa hapa nchini maana yake zinatumia nondo za hapa nchini, zinatumia mchanga hapa nchini, *cement* hapa nchini pamoja na kokoto ni hapa hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati kadhaa za Bunge lako tukufu zimetembelea maeneo haya na kujionea uzalishaji unavyofanyika kwa kutumia malighafi zinazozalishwa ndani ya nchi. Licha ya malighafi karibu zote zinazotumika katika

mradi huu kuwa za ndani ya nchi ukitoa reli yenyewe ambayo inaagizwa kutoka Japan kwenye kiwanda pekee kinachotoa reli za viwango vya juu, asilimia 20 ya wataalam wabobezi katika mradi huu ni wazawa, na kwamba asilimia 80 ya wataalam wa kati na nguvu kazi ni Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa jumla ya wazawa 14,140 wamepatiwa ajira katika mradi huu ambapo asilimia 90 ni Watanzania. Ukiacha wananchi wengine wanaojihusisha na shughuli zisizo rasmi katika maeneo ya mradi, hii ina maana kwamba malipo ya watumishi hawa kiasi cha shilingi bilioni 5.2 kwa mwezi, sawa na shilingi bilioni 62 kwa mwaka ni fedha zinazotumika ndani ya nchi moja kwa moja kutoka kwa watu ambao wameajiriwa kwenye mradi. Aidha, wakandarasi zaidi ya 500 wadogo wadogo wa ndani wamepewa kazi katika mradi huu, baadhi ya kazi hizo ni pamoja na za ujenzi, ugavi na utoaji wa huduma mbalimbali ambapo wote hawa wanalipwa na fedha za mradi huo.

Mheshimiwa Spika, mbali ya faida zilizoanza kuonekana katika hatua ya ujenzi, manufaa makubwa ya mradi yataanza kupatikana baada ya ujenzi kukamilika. Mradi wa *SGRunatarajwa* kuhudumia tani milioni 17 za mizigo kwa mwaka, mizigo hii ni pamoja na ile ya nchi za jirani zisizo na bandari za Uganda, Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Kwa upande wa miradi ya barabara, viwanja vya ndege, majengo na vivuko katika mwaka wa fedha 2015/2016 hadi mwaka 2017/2018 jumla ya miradi 4,816 imetekelvezwa na makandarasi wazawa na miradi 116 imetekelvezwa na makandarasi wa nje. Aidha, jumla ya ajira 362,854 zilizalishwa katika sekta ya ujenzi katika miaka hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016/2017 jumla ya ajira 109,846, mwaka 2017/2018 jumla ya ajira 116,864 na mwaka 2018/2019 jumla ya ajira 136,144 zimezalishwa katika maeneo mbalimbali ya ujenzi ikiwemo miradi ya barabara, miradi ya viwanja vya ndege, miradi ya vivuko na miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*), mpaka sasa Serikali inatoa huduma kwa kutumia ndege mpya sita (6) zillizonunuliwa na Serikali kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, ndege tatu aina ya *Bombadie Q4100-8* zenye uwezo wa kubeba abiria 76 kila moja, ndege mbili (2) aina ya *Air Bus A2200-300* zenye uwezo wa kubeba abiria 132 kila moja na ndege moja aina ya *Boing 787-8 Dream Liner* zenye uwezo wa kubeba abiria 262. Aidha, *ATCL* imekabidhiwa na Mheshimiwa Rais ndege mbili zifuatazo; moja aina ya *Foker 50* yenye uwezo wa kubeba abiria 44 na ya pili aina *Foker 28* yenye uwezo wa kubeba abiria 70.

Mheshimiwa Spika, pia *ATCL* inatarajia kupokea ndege aina ya *Bombader-8* mwezi Novemba mwaka huu 2019 na *Boeing 787 Dream liner* ambayo inatarajiwa kupokelewa Januari, 2020. Ili kuendelea kuiongezea uwezo *ATCL*, Serikali imetenga fedha katika bajeti yake ya mwaka wa fedha 2019/2020 kununua ndege nyiningine moja aina ya *Bombardier Q4100-8* na ndege mbili aina ya *Airbus*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *ATCL* kwa kutumia ndege sita zinazotoa huduma kutoka Dar es Salaam kwenda katika vituo 10 ndani ya nchi vikiwemo Bukoba, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Kigoma, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Tabora, Zanzibar na vituo vitano nje ya nchi ambavyo ni Bujumbura, Entebbe, ....Harare na Lusaka. Aidha, *ATCL* inatarajia kufungua kituo cha Johannesburg mwezi Juni, 2019, Mumbai mwezi Julai, 2019 na Kituo cha Guangzhou kabla ya mwisho wa mwaka wa 2019. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kuwa na safari zinazounganisha Mji wa Dodoma na sehemu nyiningine za nchi, *ATCL* kufuatia maombi ya Waheshimiwa Wabunge imeamua kuifanya Dodoma kuwa *sub-hub*. Aidha, *ATCL* inaangalia sasa uwezekano wa kuanzisha safari za kutoka Dodoma kwenda *KIA*, kutoka Dodoma kwenda Mbeya, kutoka Dodoma kwenda Mwanza na kutoka Dodoma kwenda Zanzibar. Sambamba na vituo hivyo, *ATCL*

ipo kwenye maandalizi ya mwisho ya safari za kwenda Mkoa wa Katavi Mji wa Mpanda na kuangalia uwezekano wa kuanzisha safari kati ya Dar es Salaam na Tanga kuitia Pemba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamekuwepo na dhana kwamba ununuzi wa ndege na gharama za awali na uwekezaji katika mifumo, mitambo na miundombinu zimehamishiwa kwenye Fungu 20, yaani Ikulu. Suala hili siyo la kweli kwa sababu gharama hizo zimetengewa fedha katika Fungu 62 ambalo ni la Sekta ya Uchukuzi. Aidha, gharama za uendeshaji wa ATCL zinatokana na mapato ya ndani ya kampuni kama inavyooneshwa katika hesabu za ATCL zinazokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wote wa ndege unafanywa na Wizara yangu ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na ni Fungu 62 ambalo linapitishwa na Bunge lako Tukufu; na hata katika bajeti hii tunaomba mpitishe shilingi bilioni 500 ili tuweze kununua ndege nyingine tatu ambapo moja itakuwa ni *Bombardier* na mbili ni *Airbus*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wataalam marubani, ni kweli kwamba uwiano wa marubani wenye leseni katika nchi yetu kwa sasa ni asilimia 49:51 ambapo wazawa ni asilimia 49 na wageni ni asilimia 51. Hata hivyo, Serikali ina mikakati ya kuongeza marubani wazawa kwa kuwasomesha hapa nchini katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kuitia Mradi wa *East African Skills for Transformation and Regional Integration Program*. Mradi huu utatekelezwa kwa mkopo wa dola za Marekani milioni 21.5 kutoka Benki ya Dunia na utaanza kutekelezwa rasmi mwezi Juni, 2019. Nitoe tu taarifa kwamba fedha hizi, *financial agreement* imeshasainiwa, tayari tunazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuitia mradi huu, chuo hicho kitakuwa na uwezo wa kusomesha marubani 10 kwa mwaka. Aidha, Wizara yangu inafanya mawasiliano na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi

wa Elimu ya Juu iweze kuwakopesha wanafunzi wa kozi ya Urubani. Kwa sasa ili rubani aweze kuingia katika soko la ajira atatakiwa kusoma na kupata leseni ya biashara kwa gharama ya shilingi milioni 132.6.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ina Mfuko wa Kusomesha Marubani ambao unasimamiwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga *TCAA* ambao una uwezo wa kusomesha takriban marubani watano hadi 10 kwa mwaka kulingana na makusanyo katika mwaka husika. Mfuko huu mpaka sasa umesomesha wanafunzi watano ambao wameshahitim na kuajiriwa kwenye sekta. Aidha, wanafunzi 10 wataanza masomo mwezi Oktoba, 2019. Serikali itaendelea kuhakikisha inaongeza idadi ya marubani na wahandisi wazawa katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia Bandari ya Mtwara na hasa Kamati yangu ya Miundombinu. Serikali ilibuni mradi wa kuboresha Bandari ya Mtwara kwa lengo la kuboresha huduma zake za sasa na wakati ujao na baadaye katika ukanda wa Mtwara. Katika kutekeleza hili, kumekuwepo na hoja ya kujengwa na kuchimbwa kwa urefu wa kina cha mita 13 badala ya 15 na urefu kati ya maji yanapojaa na sakafu ya gati ya mita tano badala ya mita 5.5.

Mheshimiwa Spika, vipimo vilivyozingatiwa wakati wa kujenga na kuchimba Bandari ya Mtwara vilitokana na ushauri wa awali uliotolewa na Mtaalam Mshauri *MSURS* kutoka Uingereza ambao ni urefu wa kina wa mita 13 na urefu kati ya maji yanapojaa na sakafu ya gati ya mita tano. Aidha, uchambuzi wa kina wa kitaalam unaonesha kuwa vipimo hivyo vinavyotumika ni sahihi kwa meli na shehena tarajiwa katika bandari hiyo.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Mtwara kutoka kwenye kina ambacho ni *low tide* inajaa mpaka mita nne. Kwa hiyo, ukichimba *draft* ya mita 13 wakati maji yamejaa, yatafika mpaka mita 17. Kwa hiyo, meli ya aina yoyote ni lazima ita-dock kwenye Bandari ya Mtwara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Nditiye amezungumzia suala la usajili wa laini za simu, lakini naomba nitoe taarifa kwamba takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2018 idadi ya wananchi nchini ilikadiriwa kuwa milioni 54.2 ambapo watu 52.6 wanaishi Tanzania Bara na wananchi milioni 1.6 wanaishi Tanzania Visiwani.

Aidha, asilimia 50 ya Watanzania wana umri chini ya miaka 18. Kwa kuwa zoezi la usajili wa laini za simu linamalizika mwezi Desemba, 2019 Serikali itahakikisha wananchi wenyewe kustahili kusajiliwa na *NIDA* wanasa jiliwa ili kuwezesha wananchi kuendelea kupata huduma za mawasiliano zilizo salama. Kuna Waheshimiwa Wabunge walionesha kwamba pengine kuna baadhi ya vitambulisho ambavyo havitumiki, lakini nashukuru kwamba Mheshimiwa Eng. Nditiye amelizungumzia vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunatambua uwepo wa uhitaji wa vitambulisho vingine vyenye biometria vinavyotumika kwa sasa kusajili laini za simu ikiwa ni pamoja na pasi za kusafiria, leseni za udereva, kitambulisho cha Mpiga Kura pamoja na *Zan ID*. Hivi vyote vinatumika katika kusajili laini za simu. Sasa hivi kuna kamati maalum ambayo inafanya kazi. Kitu kinachotakiwa ni kwamba laini zote kwa kutumia vitambulisho vyote vinavyosajiliwa lazima visomane na lazima visomane pamoja na kitambulisho cha Taifa na hili litatusaidia kukwepa madhara tunayoyapata ya wananchi kuibiwa.

Mheshimiwa Spika, lengo letu tunataka kila laini ya simu, kila mtumiaji awe anafahamika. Kwa hiyo, kwa sasa ni vitambulisho vyote vinatumika na wataalam wapo wanaendelea na kuhakikisha kwamba wanafanya utafiti ili kwamba vitambulisho vyote hivi viweze kusomana pamoja na kitambulisho cha Taifa.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali kuiongezea mtaji *7TCL*. Naomba pia kutoa kutoa ufanuzi kuhusu jitihada zilizochukuliwa na Serikali katika kutoa mtaji kwa Shirika la Mawasiliano Tanzania. Serikali inaendelea

kutekeleza mikakati yake madhubuti ya kuboresha mashirika yaliyokuwa yamebinafishwa lakini yakashindwa kujiendesha kwa ufanisi. Kwa msingi huo, imetunga Sheria Na. 12 ya mwaka 2017 ya kuanzisha Shirika la *TTCL* likiwa linamiliikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeendelea na juhudzi za kuhakikisha kwamba *TTCL* sasa inapewa mtaji. *TTCL* ilipewa kibali cha kukopa jumla ya shilingi bilioni 96 na ilishakopa shilingi bilioni 66. Sasa hivi iko kwenye *process* ya kumalizia kukopa shilingi bilioni 30 ili iweze kuwekeza na *TTCL* iwe ni Taasisi ambayo inaweza ikajitegemea. Nashukuru kwamba kwa muda mchache mwaka 2019 iliweza kutoa gawio na mwaka huu tayari imeshajipanga kutoa gawio.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetengeneza *corridor* tatu; ya kwanza ni ya kutoka Dar es Salaam kuititia Tanzam *highway* kwenda mpaka Zambia, *corridor* ya pili ni ile ambayo inakwenda *Central Corridor* na ndiyo maana tunajenga *SGR*, lakini tunayo *corridor* ya tatu ambayo inatoka Mtwara kwenda mpaka Mbambabay na ninashukuru kwamba Serikali tayari imeshakamilisha barabara ya lami kutoka Mtwara kwenda mpaka Songea na kwenda mpaka Mbanga na sasa hivi tunajenga kilometra 66 zilizobaki.

Mheshimiwa Spika, *corridor* hii ikishakamiliika na kwa sababu sasa hivi tunanunua *flow meter* ili ziweze kufungwa Bandari ya Mtwara na *flow meter* zifungwe Bandari ya Dar es Salaam pamoja na Bandari ya Tanga, tunataka tuwezeshe *corridor* zote hizi ili ziweze kuhudumia nchi jirani na kujiongezea mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bandari ya Tanga tayari muda wowote mkataba utasainiwa. Nilitembelea Tanga, Tanga ilikuwa imeshakwenda chini sana, lakini tunahakikisha sasa kwamba Tanga inaanika. Kwa sababu yale magati mawili yaliyojengwa yamejengwa kwenye *draft* ambayo ni ndogo, maji ya kina cha mita tatu mpaka nne. Mikataba tutakayosaini tunataka tufanye *dredging* ili

kuongeza kina kwa sababu kwa Tanga sasa hivi meli ilikuwa ikifika inakwenda kupaki mita 1,400 halafu mizigo sasa inapakiwa na matishari kuleta kwenye magati huku ambayo yanaweza yakatembia kwenye kina kidogo. Matokeo yake ilikuwa ina-*discourage* wenye meli kuja kuleta meli zao Tanga.

Mheshimiwa Spika, hilo tunaliondoa na hiyo ndiyo ambayo Waheshimiwa Wabunge mlikuwa mnaizungumzia. Tunapambana na Bandari majirani. Tunataka tufanye *dredging* na kwa mujibu wa taarifa ambayo ninayo, *TPA* mmeipongeza, wanatarajia mpaka itakapofika mwezi wa *Tatu mwakani dredging* itakuwa imekamilika. Ikishafika mwezi wa tisa wataongeza tena magati mawili yenyе ukubwa wa mita 300, 300. Hii itawezesha sasa Bandari ya Tanga iweze ku-*compete* na bandari nyininge za jirani.

Mheshimiwa Spika, tukiwa na Bandari ya Tanga na wakati huo huo tunaendelea kukarabati Bandari ya Dar es Salaam ambayo tunafanya *dredging* kwenda mita 15 na gati Na.1 limeshakamilika, utaona kwa wale wanaopita Dar es Salaam sasa hivi hata kule meli zinaanza kupungua, lakini kwa ujumla, meli zinaongezeka kwa Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, malengo yetu ni kwamba tunataka tuboreshe bandari zetu na tunajenga gati lingine la shilingi billioni 137 kwa upande wa Mtwara. Tunataka tuhakikishe kwamba meli nyangi sasa zinakuja kupaki katika Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Tanga pamoja na Bandari ya Mtwara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutekeleza kuhakikisha kwamba inafufua usafiri kwenye maziwa. Upande wa Ziwa Nyasa tayari kuna meli tatu na zinafanya kazi. Upande wa Ziwa Victoria tumeshasaini mkataba wa meli moja kubwa itakayobeba abiria 1,200 na tani 400 pamoja na ujenzi wa chelezo, tunakarabati na zile meli za zamani; *Mv Victoria* na *Mv Butiama*. Kwa upande wa Kigoma tunatarajia kusaini tena meli moja mpya ambayo itakuwa

inabeba abiria pamoja na mizigo na kukarabati meli ya MV Liemba. Taratibu za manunuzi zimekamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunachotarajia sasa hivi ni muda wowote tutasaini mkataba kabra ya mwisho wa mwezi Juni, 2019. Malengo yetu ni kuhakikisha kwamba maziwa yote sasa yanatumika kiuchumi. Niseme tu kwamba Mkoa wa Katavi tayari tumeshapata mfanyabiashara mmoja ambaye ananunua tani 1,200 kila mwezi tutakuwa tunampelekea Congo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna madini ambayo yamepatikana upande wa Kongo ambayo yatakuwa yanapitisha tani 2,000,000 kwa mwaka. Ndiyo maana tayari tunaendelea na mazungumzo ya pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika ili tuwe na matishari ya kutosha pia katika Bandari ya Kigoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda naona unanitupa mkono, nimalizie kwa kutoa taarifa pia kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba *meter gauge* kutoka Dar es Salaam kwenda Isaka inaendelea na ukarabati, inafufuliwa. Meli yetu hii ya *meter gauge* kwenye usanifu wake ilikuwa imesanifiwa kubeba tani milioni tano kwa mwaka, lakini ilikuwa imeshuka mpaka inabeba tani 300,000. Baada ya ukarabati huo, tutarudisha sasa kwenda kwenye hizo tani zinazotakiwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa ushauri ambaao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge kwamba tuangalie namna ya kuikodisha *TRC* ili iweze kuhudumia pamoja na reli ya *TAZARA*. Nimshukuru sana na Mheshimiwa Turkey, leo kazungumza kitu ambacho nimewahi kukisikia mara ya mwisho wakati alipotembelea yule Waziri wa Ethiopia aliyejiuzulu. Nao nchi yao walipeleka vizuri kutohana na hizi *bond*. Kwa hiyo, ushauri wako Mheshimiwa Turkey nimeupokea.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya machache, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako lipitishe kifungu

kwa kifungu na lipitishe bajeti ya Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, naomba kuta hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa *Eng. Kamwelwe* kwa kuhitimisha hoja yako vizuri sana na imeungwa mkono.

### **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 68 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano**

**MWENYEKITI:** Hili ndilo Fungu lile la mshahara wa Waziri, kuna majina kadhaa hapa, tuanze na Mheshimiwa Saada Mkuya...

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN - KATIBU MEZANI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijasoma.

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza, Mheshimiwa, mpaka Katibu asome kwanza.

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management*.....Sh.1,450,664,265/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saada Mkuya, swalii la ufanuzi la kisera!

**MHE. SAADA SALUM MKUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu nilizungumzia zoezi linaloendelea la usajili wa laini za simu kwa kutumia vitambulisho vinavyotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho ya Tanzania (*NIDA*), lakini sasa kwa upande wa Zanzibar, kuna

vitambulisho hivyo, maarufu ni kama *ZAN ID*, na kwamba *TCRA* wanakataa kusajili kwa kutumia ile *ZAN ID*, lazima wapate vitambulisho vya *NIDA* na kwetu kule Zanzibar, takriban Wazanzibari laki saba tayari wanavyo vitambulisho vya *ZAN ID* na tunatumia kwa mahitaji mbalimbali, *almost* mahitaji yote kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika majibu ya Mheshimiwa Waziri sikupata ufanuzi vizuri na naomba atakapojibu hili, kama hatujaridhika nitawaomba wenzagu tusimame ili tuweze kulijadili kwa kina, nitakamata shilingi ya Mheshimiwa Waziri ili tulijadili kwa kina, ni kwa sababu gani hasa za msingi vitambulisho vinavyotolewa na *ZAN ID* havitumiki katika usajili wa laini za simu!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Kamwelwe, ufanuzi tafadhalli!

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mtandao ni suala ambalo kiasi fulani limekuwa ni hatari kwa sababu wizi ni mkubwa, kweli huko tulikotoka ilifikia mahali fulani kwamba vitambulisho visitumike vyote. Tumeshaiagiza *TCRA* kwamba sasa hivi watalam wakae, wajaribu kuainisha vitambulisho vya *ZAN ID* na nimevisoma kwenye taarifa yangu, kwamba navyo pia lazima vitumike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *TCRA* wanafanya kazi, Tanzania Zanzibar, Tanzania Bara, wote ni Watanzania, lazima wawasiliane, lazima watumiane fedha na kwamba vile ni vitambulisho vya makazi kwa upande wa Zanzibar na huku tuna hivi vitambulisho vya taifa ambavyovita-cover maeneo yote. Kama mnayo taarifa hata juzi Mheshimiwa Rais alisema, jamani msisimamishe, endeleeni kusajili. Kwa hiyo sasa ni kazi ya watalamu kuhakikisha kwamba *ZAN ID*na hivyo vilivyoko huko vya wapiga kura, leseni, *passport*, kwamba vyote viwe vinaweza vikasomwa na kitambulisho cha Taifa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Saada Mkuya naomba uache shilingi yangu tu kwamba, Serikali inalifanyia kazi na kwamba vitambulisho vyote ni lazima vitumike.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saada bado unasimama jambo lako limekubalika.

**MHE. SAADA SALUM MKUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio, leo mimi nimekwenda kusajili pale na nilijaribu tu, ninacho kitambulisho cha *NIDA*, nilijaribu tu, nikawaambia mimi sina kitambulisho cha *NIDA* nataka kusajili kwa kutumia *ZAN ID*, wamekataa moja kwa moja. Kwa hiyo, naomba kuondoa shilingi ya Mheshimiwa Waziri ili sasa tupate *firm commitment*, lini *TCRA* kwa kuainisha Makampuni ya Simu wataanza kutumia *ZAN ID* katika usajili wa laini za simu. Naomba wenzangu mniunge mkono, kwa sababu hii hatua ni hatua muhimu na *ZAN ID* ni kitambulisho ambacho kinajulikana na kimepata *certificate za quality pamoja na security of information*. Naomba wenzangu waniunge mkono ili tulijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Hasa ninyi mliosimama mmesimama kuunga mkono nini. (*Kicheko*)

**MHE. SAADA SALUM MKUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa hoja.

**MWENYEKITI:** Hpana wewe mtoa hoja sikushangai, nawashangaa wanaouna mkono. Kwa sababu Waziri amesema, sasa hivi *TCRA* wameagizwa na Waziri, wakae waangalie vitambulisho zaidi ya kitambulisho cha Taifa, *ZAN ID* itaingia, *passport* itaingia, leseni ya dereva itaingia.

Kwa hiyo, leo ukienda na leseni ya dereva kwa leo hutaandikishwa lakini hivyo vinaingia katika utaratibu. Jambo likiagizwa si linachukua muda kunanii, ameshakubali kwamba siyo tu *ZAN ID*, kama alivyotoa mtoa hoja lakini, labda hilo la Waziri la lini, lakini vimekubalika zaidi ya hicho. Tukijadili sana *ZAN ID* sijui kama tunafanya sawa.

Mheshimiwa Waziri labda la lini hilo, hiyo *process mnadhani* lini labda vitaanza kusoma vyote hivyo ulivyovitaja.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hili ni suala la kitamam, tumeshawaagiza tayari waweze kulifanyia kazi, labda niseme sasa sijui nifanyeje maana yake mpaka niwasiliane na wataalam. Haya ni masuala ya kitaalam, lakini niweke *commitment* ya mwezi mmoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Good luck Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba maelezo ya Serikali, katika hitimisho lake Mheshimiwa Waziri hajaongelea miradi mingi mikubwa ya ujenzi ambayo imekwama kwa sababu ya huu mkanganyiko wa VAT. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri asiponipa majibu ya kuridhisha nitashika shilingi.

**MWENYEKITI:** Labda chukua kama dakika mbili eleza kidogo, Waheshimiwa Wabunge wengine hawaelewii mkanganyiko huu wa VAT unahusu nini.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mwaka jana katika *Finance Bill* tuliondoa VAT katika miradi mikubwa ya ujenzi ili kurahisisha miradi hiyo ambayo inafadhiliwa na nchi marafiki, nchi washirika, wadau wa maendeleo, lakini sasa, miradi hiyo imekuwa na ucheleweshwaji mkubwa kwa wakandarasi hawa kusamehewa VAT. Kwa hiyo, imesababisha hii miradi isifanyike, mingine isimame kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, mradi wa Nyakanazi wa Mizani, wa Manyoni, wa Kidatu Ifakara, barabara yote imesimama. Kwa hiyo, ukimuuliza Waziri wa Fedha, anamtupia Waziri wa Ujenzi, Waziri wa Ujenzi anasema kikwazo Waziri wa Fedha, kwa hiyo, wamekuwa wakirushiana mipira na siku zinakwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ni kweli miradi hii imesimama kwa sababu ya hiyo?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza niseme kwamba pengine hapo nyuma kidogo tulikuwa tuna changamoto ambazo zilikwamisha baadhi ya miradi ambayo ilitakiwa ipate msamaha wa VAT, lakini nilihakikishie Bunge lako kwamba hivi sasa tumerahisisha sana na ninavyozungumza hivi sasa kwa mara mbili mfululizo, tumetoa *GN* ambayo kila mojawapo imesamehe zaidi ya miradi 380, kila moja ya hiyo *Global GN*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nilieleze tu, zamani ilikuwa kwamba, ilitakiwa kila mradi utolewe msamaha peke yake na kwa miradi ya nchi nzima kuwa *scrutinized* ilikuwa ni changamoto kubwa kweli, ile ofisi inayochambua ile miradi ilikuwa imeelemewa. Kwa hiyo, tulichofanya ni kwamba tumemtaka kila Waziri mwenye sekta, anapowasilisha ombi la msamaha wa kodi kwa miradi yake, athibitishe kwamba maombi hayo yamezingatia matakwa ya sheria ya VAT. Kwa sababu kabla ya hapo, tulikuta kwamba kuna vitu vingi ambavyo havistahili kabisa msamaha. Sasa huo mzigo anabeba Waziri mwenye dhamana ya sekta, sisi Wizara ya Fedha tutakwenda kukagua baadaye kama kweli matakwa ya sheria yamekidhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia labda niseme tu kwamba, Sheria ya VAT, kifungu cha 6 na cha 7, pamoja na aya ya 9 ya ile sehemu ya pili ya Jedwali la Sheria ya VAT, ndio inayotoa msamaha ili kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na miradi inayogharamiwa na fedha za Serikali inahusu miradi ya miundombinu ya maji, usafirishaji, gesi, nishati, majengo ya utoaji wa huduma za elimu na afya na kadhalika na hapo ndio tunatakiwa tutoe ile hati ya msamaha wa ile miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 7(b) cha Sheria ya VAT kinatoa msamaha kwa kodi katika mikataba ambayo imesainiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sasa hiyo, ndiyo ilikuwa inataka kwamba, kila anayeteketeza mradi aliye VAT kwa wale wenye mikataba yenye misamaha ya kodi, halafu aje kurejesha baada ya kuzalisha au kutekeleza mradi husika na hiki kama Waheshimiwa Wabunge mnatukumbuka, ndiyo kipengele tulichofuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko miradi ambayo imekuwa na changamoto na labda niitolee mfano, kuna mradi wa kuboresha Bandari ya Dar es Salaam, na hapa ni kuwa mradi huu haukukidhi kigezo cha kupata msamaha wa VAT na ni kwa mujibu wa kifungu cha 6(2), ambacho kwenye mkataba hakukuwa na kipengele cha msamaha wa kodi, kwa mujibu wa Sheria ya VAT. Kwa hiyo, tulichofanya mtekelezaji wa huu mradi amefanya marekebisho kwenye mkataba na hicho ndiyo kilichelewesha, alikwenda kufanya marekebisho kwenye mkataba ili kuingiza kipengele ambacho kinatoa msamaha wa VAT. Kwa hiyo, nilkwa miradi ya namna hiyo ambayo kumekuwa na ucheleweshaji, lakini hili sasa tumeshalimaliza na kama tulivyoeleza kwenye maelezo ya Mheshimiwa Waziri, Serikali iliruhusu kutolewa vifaa vya huo mradi vilivyokuwa vimekwama bandarini ili mradi uendelee kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa sana suala la uchelewaji wa kutekeleza miradi kwa sababu ya VAT limeondoka. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlinga, swali lako umeridhika.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Waziri anavyoviongea sasa hivi ni *theory*, lakini siyo *practically*, ukienda hata kwenye kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, ameandika kuwa imekwama kutohana ucheleweshaji wa hiyo misamaha! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya majibu anayotoa kila siku ndiyo anayatoa hayo hayo. Ukimuuiliza Waziri wa Ujenzi, atakwambia huyu ndiye anayechelewesha, ye ye

anakwambia tatizo liko kule, kwa hiyo, miradi imesimama, lakini ukiwa uliza hivyo hivyo wanatoa hizo sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba nitoe hoja ili Bunge Iijadili, Serikali itoe *commitments* zake hapa, lini, kwa sababu ni mwaka mmoja tangu tupitishe hiyo sheria. Naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Nilikuwa naangalia kama mmeufika kumi, lakini naona kama mmeshafika kumi. Haya, Mheshimiwa, simameni tena, Mheshimiwa Mary Nagu, Mheshimiwa, Katibu niandikie..

**MBUNGE FULANI:** Mtuka.

**MWENYEKITI:** Ahsante, mnaweza kukaa, nachukua tu baadhi, tuanze na Mheshimiwa Mary Nagu! Dakika mbilimbili.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Serikali imefanya jambo zuri kutoa VAT kwenye miradi ambayo inaongeza maendeleo yetu, lakini ile kutolewa tu haitoshi, ni pale ambapo inaponufaisha kampuni zile kubwa ambazo zinafanya miradi hiyo mikubwa, ndio tutakuwa na faraja. Sasa kama watu wanakaa wanashindwa kutekeleza kwa sababu ile VAT haitolewi kwa muda unaotakiwa. Serikali naomba ione ni kitu gani ambacho kinafanya basi *practically*, hili jambo ambalo Waziri ameonesha kwamba ameisamehe, ametoa, lakini haisaidii, kama vile VAT bado ipo. Kwa hiyo, tunaomba tupate maelezo hayo, nina hakika tutaharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yussufu Hussein!

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Shida iliyopo katika Serikali yetu na tunapata makubwa ni kwamba tunapokuwa hapa, Waheshimiwa Mawaziri wanajibu maswali vizuri ili bajeti yao ipite au suala lile lione kane limepitia, lakini ukiondoka hapa sasa, ukirudi

kwenye utekelezaji, hakuna utekelezaji, miradi inakwama, shughuli zinakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tukikaa hapa tukazungumza suala la pale Bandarini tu Dar es Salaam mizigo inayotoka Zanzibar, unapata majibu mazuri, ukirudi pale tatizo lilelile, wapiga kura wetu wanatusakama, kwa hiyo, tunataka Serikali tunaposema, ielewe kwamba tuna nia safi ya kwenda mbele kwenye nchi yetu na siyo hivyo wanavyotufanya kwamba wanajibu ili funika kombe mwana haramu apite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakasaka!

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba tu Mheshimiwa Mlinga aachie shilingi, kwa sababu kitu kinachoonekana hapa ni *miscommunication* tu kati ya Wizara ya Fedha na Ujenzi na kwa sababu tayari kwenye kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kuna hilo suala la *ku-mention* hilo suala la ucheleweshaji wa msamaha wa VAT, basi Serikali ingejji-*commit* tu kwamba hizi Wizara mbili ziweze kushirikiana vizuri ili kuondoa huu ucheleweshaji. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maghembe, profesa!

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Kwenye Muswada wa Fedha mwaka jana, jambo hili lilitokea na tulidhani tumelitatu na tuliondoa VAT kwenye miradi ya ujenzi na miradi ya maji, lakini ukaenda Arusha sasa, tumepewa msaada na ADB kujenga mradi wa maji, lakini mkandarasi amechimba visima, visima vinatoa maji, tangu mwaka jana, mabomba yako bandarini yameniyimwa *exemption* ya VAT. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unajiuliza, fedha tumepewa na Waziri amesema vizuri kwamba kama mradi unatokana na mradi wenye makubaliano kati ya *Donor* na

Serikali ya Tanzania, unasamehewa VAT, lakini tangu mwaka jana, mabomba yako bandarini, yamenyimwa VAT, wananchi wanahitaji maji, na watu wanalaumiana tu, hakuna sababu yoyote ya jambo hili kutusumbua hapa! Hakuna *complication* yoyote kwa sababu miradi hii mikubwa ama inatekelezwa na fedha za ndani za Serikali, au na *donor* ambaye ana mkataba na Serikali, kigugumizi kinatoka wapi? Waziri atupe maelezo mazuri zaidi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tizeba!

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri uwe na subira wamalize kwanza.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Alichokisema Waziri wa Fedha, *theoretically* ni sahihi kabisa, kwamba hapapaswi kuwa na sababu, kwa sababu Bunge lilikwisharidhia likamwondolea ile *burden* ambayo *otherwise* alikuwa anaibeba peke yake, lakini kinachosikitisha ni pale ambapo, hata lili *obvious* kabisa, kama anavyosema Profesa Maghembe, jambo liko wazi! *Grant*, msaada, fedha ya msaada havipaswi kulipiwa kodi. Hata hivyo, utakuta mradi umesimama mwaka mzima, miezi nane, miezi mitano, miezi mingapi *exemption* haipatikani, kuna nini? Kama liko tatizo, Wizara inalionna lipo tatizo iliweke wazi ili tulijadili tuliondoe, lakini kutujibu yaliyo kwenye sheria na maandishi, halafu utekelezaji haufanani, sidhani kama ni sahihi, tunatengeneza mambo halafu tunapiga risasi miguuni mwetu sisi wenywewe. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsate sana Mheshimiwa Dkt. Tizeba. Mheshimiwa Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nimemuelewa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ana nia njema katika kulipeleka taifa mbele lakini Mheshimiwa Mlinga hoja yake ni ya msingi. Hili nataka

niliseme, tulipofanya yale marekebisho ya sheria kumrejeshea Waziri wa Fedha mamlaka ya kusamehe kwa miradi ambayo ilikuwa imeshakwama ili tuweze kuikwamua, wanasheria watasema sheria unapoitunga inaanza kutumika kwenda mbele siyo kurudi nyuma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tatizo tumelijenga sisi wenyewe. Lengo ilikuwa ni kukwamua miradi yote hii na vigezo ambavyo vimo kwenye *GN* ile pamoja na Waraka ambaao umetolewa na Wizara ya Fedha unakaa vizuri tu, hakuna ubabaishaji kwamba utaleta vitu ambavyo haviruhusiwi kusamahewa *VAT*. Changamoto iliyopo ni ndogo sana, ni hiyo sheria kuangalia kwenda mbele, haibebi miradi ambayo ilianza kutekelezwa siku za nyuma kabla ya marekebisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotakiwa kufanya ni kesho kutwa kwenye *Finance Bill*, Serikali ifanye *commitment* tu kwamba watakuja na mapendekezo ya kufanya marekebisho ili tuibebi miradi yote ile ambayo imekwama. Tukifanya hivyo ni rahisi sana. Juzi kwenye Kamati ya Bajeti niliwaambia kama wanashindwa kuiandika hiyo mimi naweza nikajitolea kuandika *amendment*hiyo. Ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Waziri wa Maji nilikuona ulisimama.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa tu Mheshimiwa Maghembe kwamba Wizara ya Maji tulikuwa na *VAT exemption*, tulifanya maombi kwa ajili ya mradi wa Same, Mwanga na miradi ya *ADB* ya Arusha ambayo yote *VAT exemption* tumeshazipata kwa upande wetu.

**MWENYEKITI:** Mmezipata lini Mheshimwia Waziri?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata zaidi ya mwezi mmoja kwa sababu mimi mwenyewe nilikuwa nafuatilia kila siku na tayari tumeshazipata.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, kumbe Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Maghembe mnaongea lugha moja. Kama ni mwezi mmoja tu mmepata juzi maana yake mnaongea pamoja, kwamba imechelewa sana hadi kutoka. (*Makof*)

Mheshimiwa Waziri wa Fedha halafu anafuata mtoa hoja nafikiri, kama una lolote kabla sijamrudishia Mlinga.

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Senator Chenge amemaliza.

**MWENYEKITI:** Hapana, lazima Serikali ipate nafasi labda kama hawataki. (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Kama alivyoanza kusema Mheshimiwa Waziri wa Fedha kulikuwa na kutokelewana nini kilitakiwa kifanyike kabla.

Hata hivyo, kwa sasa hivi imeshawekwa vizuri kwamba kila Waziri wa sekta husika yeye anatakiwa ajiridhishe kulingana na Sheria ya VATkile anachokiomba kwa sababu yeye ndiyo kinamhusu. Tayari Mawaziri wote wa sekta wameshaandika barua za *commitment* ya kwamba watakuwa wanajiridhisha wao ili inapofika Wizara ya Fedha timu ile ya Wizara ya Fedha isianze kuititia tena ombi moja baada ya lingine baada ya Waziri mwenye sekta kujiridhisha kulingana na Sheria ya VAT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hiyo *commitment*, ndiyo hata hiyo aliyoisema Mheshimiwa Waziri wa Maji kwamba tayari miradi yake yote imeshapata VAT *exemption*. Hakuna mradi hata mmoja ambao huna shida ya VAT *exemption*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya mwezi huo mmoja tayari tumeshatoa *Global GN* mara mbili. Katika kila *GN* tumetoa miradi 380, mara mbili ni zaidi ya 700 ambapo tumeshatoa miradi hii na tutaendelea kufanya hivyo kwa sababu sasa kumekuwa na uelewa wa pamoja ndani ya Serikali ya nini tunatakiwa kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Mlinga rafiki yangu aachie shilingi ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ili tuende sasa kutekeleza miradi yote ambayo ina maombi haya ya kuombewa msamaha wa VAT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimwombe Mheshimiwa Mlinga aweze kuachia shilingi ya Mheshimiwa Waziri ili tukafanye kazi. Pia nilifahamishe Bunge lako kwamba tatizo lilikuwepo pale awali lakini kuwa na changamoto ni jambo moja bali kushughulikia kwa usahihi ni jambo nyingine. Kazi imefanyika kuhusisha Maafisa wa *TRA* na Maafisa wa kwetu upande wa *TANROADS*, tumekuwa na namba ya vikao vya kutosha angalau kuweza kupata ufanuzi ili tuweze kwenda sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu baada ya kuwa tumefika pazuri jumla ya miradi ambayo imesamehewa ni 1,019 kwa muda huu mfupi. Wakati tunaandaa taarifa hii kulikuwa na changamoto lakini sasa tunaenda vizuri na Maafisa wa *TRA* walioko wengine ngazi ya Mkoa wakati mwanzo walikuwa hawahusishwi kwenye zoezi la *exemption* nao sasa wanahusishwa ili kurahisisha zoezi la hii misamaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe tu Mheshimiwa Mlinga aachie shilingi sisi tunaendelea kulisimamia jambo hili ili miradi yetu isiendelee kukwama. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mlinga tufungie hoja yako.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa michango ya Wabunge na

*commitment ya Serikali. Hata hivyo, naiomba Wizara ya Fedha ipunguze urasimu isitake kula visivyoliwa. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, narudisha shilingi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Sasa visivyoliwa sijui vitu gani tena? Mlinga bwana!

Haya tuendelee na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilionesha mfadhaiko wa Watanzania wakiwemo wananchi wa Jimbo la Bagamoyo kuhusiana na kusitishwa mradi maalum wa uwekezaji Bagamoyo. Mradi huu kama vile miradi mingine ya uwekezaji una mchango mkubwa sana katika kutufikisha katika uchumi wa kati kama ambavyo *Vision 2025* imetuelekeza. Jambo hilo tuna kwikwi nalo sana kwa sababu nchi hii tunahitaji kufikia kiwango cha maendeleo ambacho kinawatoa wananchi katika hali duni ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri katika maelezo yake na amesema kwamba majadiliano ya uwekezaji huu bado yanaendelea. Sasa mimi nimepata mfadhaiko, nimesoma ukurasa wa 99 wa kitabu chake aya ya 136 na naomba kunukuu, anasema: "Majadiliano na wawekezaji waliokuwepo yaani Kampuni ya *China Merchant Holding International Limited* na *State General Reserve Fund* ya Serikali ya Oman yamesitishwa". (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyaandika ndani ya kitabu chake. Sasa nataka kujua ukweli, nipokee yaliyokuwa kwenye kitabu hiki cha Waziri au kauli ambayo ameisema kwamba

majadiliano bado yanaendelea? Nadhani Waziri kwa sekta hii ndiyo mwenye mamlaka na kama majadiliano yamesitishwa yeye ndiyo mtu wa kwanza anayajua na ameyaweka kwenye kitabu, hii kauli nyingine iliyokuja inanitia wasiwasi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Waziri atupe kauli muafaka ama *firm commitment* ya kwamba mradi huu unaendelea au mradi huu sasa haupo? Kama maelezo haya hayakunitosheleza, nina nia ya kukamata shilingi na kuwaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono tulijadili jambo hili lenye manufaa kwa taifa letu. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, *Engineer Kamwelwe ufanuzi tafadhali.*

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hoja ya Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo kuhusiana na ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyozungumza ni kwamba majadiliano (*negotiation committee*) kuhusiana na ujenzi wa bandari yamechukua muda mrefu sana. Tulifika mahali tukaandikiana barua na huyo mwekezaji, wakati tunaandika hotuba hii mwekezaji alikuwa ameandikiwa barua muda mrefu sana na hakuweza kujibu. Kwa hiyo, wakati tunaandika hii *speech*, hizi *speech* zinaanza kuandikwa mwezi Machi, alikuwa haja-*respond*kwamba sasa anarudi kwenye mazungumzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kwenye kitabu ikaonekana kwamba tumesitisha baada ya kuona kwamba muda ni mrefu sana. Kwa sasa ametuandikia kwamba yuko tayari kuendelea na mazungumzo. Tulimwandikia barua ya kwanza akachukua muda mrefu sana kujibu sasa amejibu kwamba tunaendelea na mazungumzo, ndiyo maana kwenye kitabu ikawa imeonekana kwamba tumesitisha lakini mazungumzo yanaendelea ili tuweze kufikia muafaka.

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Utaratibu wa nini tena?

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna taratibu za Kibunge kama kuja jambo jipya ambalo limetokea ambalo halikuwemo kwenye hotuba, Serikali au hata Mbunge analeta *amendment* ya kurekebisha eneo lile. Kwa hiyo, naomba uwape muda Serikali walete *correction* ya hicho kifungu ukurasa wa 99 ili tuweze kuwa *on record* kwamba neno yamesitishwa limefutwa. Wanawenza kuandika hata kwa mkono tu wakaweka saini hapa kwenye *record* za Bunge ikaingia kwamba neno limesitishwa limeondolewa. (*Makofii/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Hilo halikubaliki, neno jipya lipi, hii ajenda imekuwepo muda wote, imekuwa mpya mpya tangu lini tena?

Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, wewe ndiye mwenye hoja.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili lina umuhimu mkubwa kwa wawekezaji kwa maana ya nchi ya China na *China Merchant Holding* ni Shirika la Serikali ya China, Serikali yetu rafiki kwa miaka mingi na pia Serikali ya Oman. Sijaafiki maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu nikisoma katika kitabu chake *categorically* imesema kwamba majadiliano haya hayatafanyika mpaka wawekezaji wameondosha masharti na sasa hivi hajasema kwamba masharti yameondoka, kwa maana kwamba hili ambalo analisema ni jipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naondosha shilingi, naomba kutoa hoja ili Wabunge wenzangu waniunge mkono tulijadili jambo hili. Naomba kutoa hoja.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hamjafikia idadi ya kumi.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Haya, Katibu niandie wako wengi mno, nikiandika mimi watasema nimependelea. Haya tukae basi, majina niliyoandikiwa na Katibu, kwanza ataanza Mheshimiwa Mussa Mbarouk, dakika mbilimbili.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Dkt. Kawambwa lakini labda mimi nitoe masikitiko yangu tu kwamba mambo yetu haya ya kuchelewachelewa na kutafuta sababu na visingizio wakati mwingine tunapoteza fursa wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya Bandari ya Bagamoyo, kwanza ilianza Bandari ya Tanga (Bandari mpya ya Mwambani) wakaja wawekezaji kutoka Kuwait pamoja na Serikali ya Uganda yakaja maneno maneno hivi hivi ikaenda mpaka Uganda na Rwanda wakaenda kushirikiana kujenga Gati Na. 9 katika Bandari ya Kilindini, Mombasa Kenya. Bandari ni lango kuu la biashara duniani kwa nini sisi tunatafuta sababu sababu. Kumbe kama ni VAT watu walikwishazungumza kwamba iachwe. Kama ni suala la bandari kwamba inatakiwa ijengwe tungefanya haraka tukaiwahi hiyo fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi kwa taarifa Kenya wanajenga Bandari mpya ya Lamu, kuna hatari ikaja ikawa Bandari yetu hiyo ya Bagamoyo ikajengwa kwa kuchelewe kwetu ikawa haina maana. Mimi naishauri Serikali ufanyike mpango wa haraka haya mambo na visingizio na sababu zisizokuwa na msingi viishe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niseme tu kwamba mradi wa Kanda Maalum ya Uchumi ya Bagamoyo ni mradi mkubwa na wa kimkakati lakini kumekuwa na upotoshaji mkubwa sana tangu jana jioni kuitia kwenye mitandao ambapo imesababisha sintofahamu kwa wananchi na hata kwa baadhi ya viongozi. Ukweli ni kwamba mazungumzo ambayo yalikuwa yanafanyika kati ya *Government Negotiation Team* na hawa wawekezaji yalikuwa yanakwenda vizuri mpaka Oktoba, 2018 walipokutana kwenye kikao cha mwisho hawa ndugu zetu wakaja na madai tisa. Kati ya madai tisa, madai saba hayakuwa na matatizo makubwa isipokuwa madai mawili ambayo yalikuwa yanaingilia uhuru wa nchi na haya ameeleza vizuri sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwezi Desemba, *Government Negotiation Team* iliwaandikia barua ikieleza kwamba tumezungumza lakini haya hayawezi kuzungumzwa, kwa hiyo, warudi mezani watueleze kama wako tayari. Mpaka sasa hivi hatujapata majibu kwamba wako tayari kutekeleza yale ambayo yanahuusu uhuru wa nchi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu jana wame-indicatesasa wako tayari kuja kuendelea na mazungumzo, sisi tunaiagiza *Government Negotiation Team* watakapokuwa tayari wakija hapa nchini wataendelea na mazungumzo. Hili ambalo limeandikwa hapa kwenye hotuba liko sawasawa, tulisitisha kwa muda mpaka wawe tayari kuzungumza kama ambavyo sisi tunataka. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Jamani, kelele ya nini Mheshimiwa Waziri anafafanua vizuri?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Waheshimiwa, Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusimama kuunga mkono hoja ya Mbunge wa Bagamoyo, Mheshimiwa Dkt. Kawambwa kuhusiana na maelezo ambayo Serikali imeyatoa kuhusu mradi wa Bagamoyo *Special Economic Zone*. Ni dhahiri Wabunge wenye wameona hapa kwamba maelezo ambayo Waziri wa Uchukuzi ameyatoa na maelezo ambayo Waziri wa Viwanda na Biashara ambaye *Special Economic Zone* iko chini yake ameyatoa yanaonesha kuna *total confusion within Serikalini*. Ndiyo maana nilikuwa nimetoa ushauri kwamba baada ya maelezo ya Waziri wa Uchukuzi kwamba hotuba yake iliandikwa mapema kabla ya taarifa mpya kutoka ilikuwa ni kiasi cha Waziri kuleta *addendum* ya hotuba ili kurekebisha hilo tuweze kuwa na *official communication* kwamba majadiliano yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi leo umeliongea vizuri sana kwamba tunaendelea kujadiliana kwa miaka saba kwa mradi mkubwa kama huu, mradi ambao unaenda kuipaisha nchi yetu na kuiweka kwenye ramani ya dunia sisi ni watu wa namna gani? (*Makof!*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Dakika haziko kwako, Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na kimsingi naweza kuelewa Mheshimiwa Dkt. Kawambwa kama kila mmoja akijiweka kwenye *position* yake kama mtu ambaye pamoja na kuwa ni mradi wa Kitaifa utanufaisha Taifa zima lakini kwa wananchi wake ndani ya miaka saba bila shaka amewaeleza mambo mengi na neema nyingi mabazo mradi huo wataupata. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *I can understand* kama ni *frustration* ambazo Mheshimiwa Kawambwa anazo. Lakini pamoja na hayo ningemuomba na kumsihi Mheshimiwa Dkt. Kawambwa arejeshe shilingi *on the point* kwamba Mheshimiwa Waziri amesema kitabu kilipokuwa kinaandaliwa walikuwa katika huo mtanzuko waliokuwepo na nitumie fursa hii kuiomba na kuishauri Serikali, tuwe na *speed* katika kufanya *negotiation* lakini pia tuwe na tahadhari kwamba tusiwe na *speed* ambayo baadaye tukaingia katika mradi ambao tukaja kukaushwa damu kwa hiyo tuwe na *speed* lakini tuwe na umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda nimuunge mkono Mheshimiwa kawambwa na hasa tukizingatia suala la majadiliano kuchukua muda mrefu. Hapa tunazungumzia Bandari ya Bagamoyo lakini tunalo tatizo jingine la Liganga na Mchuchuma. Majadiliano chini ya *NDC*kuhusu chuma bado yanaendelea hatukuwa na sababu sisi ya kujenga *SGR* kwa kutumia chuma kutoka Japan. Tungeweza kujenga reli kwa kutumia chuma ya kutoka Liganga na Mchuchuma, ni kwa sababu ya majadiliano kuchukua miaka chungu nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na namuunga mkono zaidi hasa ukizingatia mgongano wa kauli za Mawaziri. Niliridhika zaidi na kauli ya Mheshimiwa Eng. Kamwelewe lakini alivyokuja Waziri wa Viwanda na Biashara nikachanganyikiwa kabisa hawakzungumza kabla ya kuja hapa? Ile kauli ya Waziri wa Uchukuzi ilikaa vizuri zaidi kwamba wakati anaandika hiyo taarifa walikuwa bado hawajajibu na kwamba wamejibu wataendelea na majadiliano lakini Mheshimiwa Waziri wa Viwanda anasema kauli sahihi ni ile iliyoko kwenye kitabu cha hotuba, sasa tumsikilize nani?

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa Kawambwa.

**MWENYEKITI:** Dakika mbili zimekwisha tumalizie na Mawaziri wawili. Mhehsimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Waziri wa Fedha. Mheshimiwa Kango Lugola tafadhalii.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mionganini mwa Wabunge ambao tuliambatana na wewe kwenda China na tukapata fursa ya kupata wasilisho la wale China *Merchants* kwa hiyo leo niko upande wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua umuhimu wa mradi huu lakini majibu ambayo Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ameyasema na hata yale ambayo yako kwenye ukurasa wa 99 siyo majibu hata kidogo yanayojichanganya. Yote yamejengwa kwenye msingi wa makubaliano, yote yamejengwa kwenye msingi wa maslahi mapana ya nchi. Majadiliaono ambayo Serikali inaendelea ni kwasababu ya ukubwa wa mradi na changamoto. Makubaliano haya siyo ya ununuzi wa Bajaji wa Toyo ni mradi mkubwa ambao unahitaji Serikali iwe katika hali ya utulivu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba waelewe kwamba mradi huu makubaliano yetu yatakopokuwa yameleta muafaka mradi huu Serikali itautekeleza pale ambapo masharti yale ambayo yanaminya maslahi mapana ya Taifa yataondolewa ya kujipangia tozo...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** ...masharti ya kuzuia Wawekezaji wengine...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri ahsante.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, naomba pana kelele tuendelee. Mheshimiwa Waziri wa Fedha dakika mbili.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa. Kwanza namuomba sana Ndugu yangu Mheshimiwa Dkt.Kawambwa muachie Waziri shilingi ili aweze kuendelea na hatua ambayo ameieleza vizuri.

Waheshimiwa Wabunge mradi huu ni kweli kabisa una fursa kubwa hili halina ubishi lakini ni lazima tuwe waangalifu na masharti yale ambayo tulikuwa tunajadiliana na Muwekezaji na hususani kuhakikisha kwamba maslahi ya Taifa yanazingatiwa. Hata kama tungefanya kwa mlezi miwilii, hata wiki moja kama hatukuzingatia maslahi ya Taifa Bunge hili litahukumiwa, Serikali itahukumiwa ni muhimu sana sana tuhakikishe kwamba maslahi ya Taifa yanazingatiwa, chelewa ufile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Dkt. Kawambwa unaua pia kwamba Serikali kwa sasa inatekeleza miradi mingi ya maendeleo ikiwa ni pamoa na barabara ya kutoka Bagamoyo kwenda Tanga mpaka mpakani mwa Kenya ambayo nayo itakuwa ni fursa kwa wananchi wako. Mheshimiwa Kawambwa nakusihi sana muachie Waziri shilingi yake...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** ...ili aweze kutekeleza, kuendeleza

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Kawambwa na Mwenyekiti nakuomba shilingi hiyo tafadhali irudishe Bwana tuendelee lakini nakupa nafasi ueleze kidogo. Karibu sana Mheshimiwa Kawambwa.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nilikuwa katika Serikali na sina nia na makusudio yoyote ya kuivuruga Serikali yangu. Na nina imani kubwa na Wataalam wetu wa Tanzania kwa sababu kila siku wamekuwa makini na wamekuwa makini sana katika kazi. Nilikuwa katika Wizara hii kabla nimefanya nao kazi *successful* katika miradi kadhaa kwa hivyo nina imani kwamba tunauwezo wa kusonga mbele kama tutasimamiwa kuweza kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna walivyoniomba, kwangu, ombi lako ni amri lazima nitekeleze amri ya Spika. Shilingi ya Waziri nairudisha lakini nikitaka ile kauli yake aisimamie iliyosema kwamba "majadiliano yataendelea au majadiliano yanaendelea na kwa majadiliaono haya yaza matunda ili Taifa hili liondokane na umasikini"

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nakushukuru sana. Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kuhusiana na kubadilisha muelekeo wa namna ya kuendesha miradi yetu. Hivi sasa tumekuwa tunaona fahari kama Taifa kusema tunatoa pesa mifukoni mwetu kununua ndege, kujenga reli, kujenga vitu vingine vitu ambavyo vina gharama kubwa sana. Hii ina gharama kubwa kwa sababu kama tunanunua kwa fedha zetu ina maana tunalipa fedha za kigeni nje lakini pia zinabakia huku ndani, tunalipa huku ndani. Maana yake ni nini? Maana yake tunapata matatizo kwenye kuhudumia vitu vingine kwa sababu fedha zinahama katika njia ambayo hatuwezi kutumia vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa rai yangu, nilikuwa nataka nilichukue wazo ambalo alililetta Mheshimiwa Turkey asubuhi kwamba tutengeneze miradi yetu sasa nataka

mabadiliko ya Kisera tutengeneze miradi yetu kwa kutegemea zaidi *private public partnership* iende kwa vitendo ili tupunguze na tuweze kuifanyia kazi kwa sababu sasa hivi tumeunda Wizara maalum kwa ajili ya kusimamia jambo hilo. Kwa hivyo, nataka kujua Serikali iko tayari namna gani kutekeleza miradi hiyo kwa njia ya *PPP* hasa miradi ambayo ni *grand* kama ulivyosema wewe asubuhi. Kama hatukuridhika nitaomba tujadiliane namna ambavyo tuendeshe nchi yetu kiuchumi kusogea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Uafanuzi Mheshimiwa Waziri tafadhali. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikia hoja inayojengwa na Mheshimiwa Ally Saleh ni hoja nzuri kwa sababu kwa uhalisia kutekeleza miradi ye Serikali peke yake kwa Fedha za Serikali peke yake haiwezekani. Kwa hiyo, pale ambapo pana fursa ya kutegemea *PPP* ni sahihi lakini kilicho cha msingi hebu turudi kwenye uhalisia. Tukirudi kwenye uhalisia, miradi hii lazima uwe na uwezo kwanza wa *ku-solicit good PPP's*, lazima uwe na uwezo wa *ku-negotiate good PPP's* vinginevyo huko nyuma tulishaingia mkenge mara nyingi na ndiyo maana tumeunda kitengo mahususi kabisa cha kusimamia miradi hii ya *PPP*siyo kwamba tunaiweka pembeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana pia katika maelezo yangu nilieleza hata baadhi ya miradi ambayo tunai-*fast truck* iende kwa utaratibu huo wa *PPP* ikiwemo reli ambayo tunakusudia kujenga kwenda *all the way* kuitipia Lake Nyasa mpaka Mchuchuma na Liganga. Kwa hiyo, hili sidhani kama tunahitaji kubadilisha sera yoyote iko pale tayari na tunayo Sheria ya *PPP* kwahiyo suala ni kuitaayarisha na kuandaa watalaam wa kutosha kuweza kuihakikishia kwamba nchi inaingia kwenye miradi thabiti ya *PPP*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Saleh dakika moja tu nakupa maana yake tunaingia kwenye upande mwingine.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *ok.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sijaridhika na yeye Waziri atakuwa shahidi, nilipeleka mradi wa *PPP* wa 1000 *megawatts* au zaidi Serikali *full funded* bila senti moja ya Serikali na au pia uwezekano wa *PPP* na jibu la *frustration* niliyoipata kutoka Wizara ya Nishati na Wizara yake yeye Waziri hatukufika popote hata yule mtu hakuitwa kufanya mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama upo muda naomba kutoa hoja tujadili jambo hili.

**MWENYEKITI:** Bahati mbaya muda hakuna tunaingia kwenye *guillotine* sasa. Katibu tuendelee na tumekosa watu wawili, Mheshimiwa Chegeni na Mheshimiwa Cecil Mwambe *next time*.

#### **NDG. ATHUMAN HUSSEIN -KATIBU MEZANI**

#### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 68 – Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano**

Kif. 1001- <i>Administration and Human Resources Management</i> .....	Sh.1,450,664,265/=
Kif. 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh.328,238,000/=
Kif. 1003 - <i>Policy and Planning Unit</i> .....	Sh.334,487,031/=
Kif. 1004 - <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh.113,008,000/=
Kif. 1005 - <i>Legal Service Unit</i> .....	Sh.130,642,704/=
Kif. 1006 - <i>Government Communication Unit</i> .....	Sh.232,667,000/=
Kif. 1007 - <i>Procurement Management Unit</i> ..	Sh.188,338,000/=
Kif. 1008 - <i>Management Information System Unit</i> .....	Sh.11,628,000/=
Kif. 2001 - <i>Communication Division</i> .....	Sh.595,530,000/=
Kif. 2002 - <i>Information, Communication and Technology Unit</i> .....	Sh.587,994,000/=
<i>(Vifungu vilivytotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)</i>	

**Fungu 62 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano**

Kif. 1001 - *Administration and Human Resources Management*..... Sh.3,430,964,570/=  
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*.....Sh.763,659,000/=  
Kif. 1003 - *Policy and Planning Unit*..... Sh.1,875,489,150/=  
Kif. 1006 - *Government Communication Unit*.....Sh.285,396,000/=  
Kif. 1005 - *Procurement Management Unit*..... Sh.473,751,000/=  
Kif. 1006 - *Internal Audit Unit*..... Sh.392,053,000/=  
Kif. 1007 - *Legal Services Unit*.....Sh.416,502,000/=  
Kif. 1008 - *Information, Communication and Technology Unit*.....Sh.441,048,000/=  
Kif. 2005 - *Transport Infrastructure Division*...Sh.1,479,261,150/=  
Kif. 2006 - *Transport Service Division*..... Sh.74,884,579,470/=  
Kif. 5002 - *Transport Safety and Environment Division*..... Sh.965,427,660/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 98 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano**

Kif. 1001 - *Administration and Human Resources Management*..... Sh.1,785,684,970/=  
Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*..... Sh.647,465,900/=  
Kif. 1003 - *Policy and Planning Division*..... Sh.407,162,600/=  
Kif. 1004 - *Government Communication Unit*.....Sh.144,413,600/=  
Kif. 1005 - *Procurement Management Unit*..... Sh.144,109,806/=  
Kif. 1006 - *Internal Audit Unit*..... Sh.147,732,500/=  
Kif. 1007 - *Legal Service Unit*.....Sh.124,722,500/=  
Kif. 1008 - *Information, Communication and Technology Unit*..... Sh.137,824,500/=  
Kif. 2002 - *Technical Service Division*..... Sh.14,224,090,800/=  
Kif. 2005 - *Roads Division*.....Sh.17,924,624,300/=

Kif. 5002 - *Safety and Environment Unit*..... Sh.331,040,300/=  
Kif. 6001 - *Airport Construction Unit*..... Sh.123,792,404/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **MIPANGO WA MAENDELEO**

#### **Fungu 62 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano**

Kif. 1003 – *Policy and Planning Unit*.....Sh.26,000,000,000/=  
Kif. 2005 - *Transport Infrastructure  
Division*.....Sh.2,947,722,242,895/=  
Kif. 2006 - *Transport Service Division*..... Sh.570,000,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 68 – Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano**

Kif. 1003 – *Policy and Planning Unit*.....Sh. 0  
Kif. 2001 - *Communication Division*.....Sh. 0  
Kif. 2002 – *Information, Communication and Technology*...Sh.0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 98-Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano**

Kif. 1003 - *Policy and Planning Division*.....Sh.275,000,000/=  
Kif. 2002 - *Technical Service Division*.....Sh.53,117,000,000/=  
Kif. 2005 - *Road Division*..... Sh.1,136,667,229,268/=  
Kif. 5002 - *Safety and Environment Unit*.....Sh.1,800,000,000/=  
Kif. 6001 - *Airport Construction Unit*.....Sh.102,192,375,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa naKamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilitrudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mheshimiwa Waziri taarifa tafadhali.

## T A R I F A

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila Marekebisho hivyo basi naomba Makadirio haya yakubaliwe na Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi hiyo, ahsante sana.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kukubaliwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha kwa 2019/2020 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Naomba niwashukuru sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi n.k wote katika Wizara hii na Serikali kwa ujumla kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mkiendelea kufanya na mnayoendelea kufanya, kwa niaba ya Bunge hili niwapongezeni sana, mnafanyakazi nzuri, Wizara hii ni kubwa, ni nzito, mambo yote ya ujenzi na nchi hii inejenga kila mahali, shughuli za uchukuzi ni nydingi uchukuzi wa ardhini, uchukuzi wa majini, uchukuzi wa angani na mawasiliano ndiyo kabisa, mnafanyakazi kubwa sana tunajua, tumejitahidi kama Taifa kuwapa bajeti kadri tulivyoweza. Tunajua pamoja na bajeti hii bado siyo kwamba

inatosha kihivyo lakini mtajitahidi basi kwa kutumia bajeti hii kufika mbali kadri mtakavyoweza na kama mlivyolahidi Bunge hili sisi tunawatakania kila la heri.

Mheshimiwa Waziri Mkuu tunawatakania kila la heri Serikalini huko katika utekelezaji wa Bajeti hii ya 2019/2020 katika kiwango hiki ambacho tulikubaliana. Kwa mara nyingine tunawapongezeni sana kwa kweli kazi inaonekana, viwango nya majengo yetu, barabara zetu na kadhalika vinazidi kupanda kila kukicha, tuko pamoja na ninyi. (*Makofi*)

Basi baada ya pongezi hizo naomba sasa kwa kuwa muda wenyewe unakaribia karibia. Safari hii nashangaan kidogo Waheshimiwa Wabunge futari ya safari hii hatukaribishani!! Mambo yamebana kidogo? Hata kwenye futari jamani? Ukaribu wa futari si bado uko pale pale? Maana yake Spika hajapata *card* hata mwaliko mmoja tangu hili shughuli ianze sasa nikajiliza mimi tu au na wenzangu pia!! Basi tukaribishane au labda bado kidogo siku zikisogea sogea kidogo? Nawatakania kila la heri ndugu zangu. (*Kicheko*)

Tunaahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Saa Tatuh Asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumanne,  
Tarehe 14 Mei, 2019 Saa Tatuh Asubuhi)*